# MAONO NA MA TANGAZO YA UZIMA WA MILELE

YA MUTAWA DAMASKINOS GRIGORIATIS
KILIMA TAKATIFGU
GREKIA

CENTRE DE LA MISSION ORTHODOKSE
KOLWEZI KONGO
1998

# YALIYOMO

1. Ono wa ajabu ya Mukristu moja murahimu na mweshimiwa....................................3
2. Ono ya Yoasafat, mkubwa mpadri ya Nyumba ya wenye Yosafat ya muji Karia ya Kilima Takatifu juu ya Mt. Georgie Mkubwa........................................................................4
3. Jibu matata ya Mutawa Evlogios ile saa ya lufu yake................................................ 8
4. Ono ya mwaminifu moja aliyeitwa Dimitrios toka mukini Stratonio, karibu ya Kilima Takatifu.................................................................................................................8
5. Aliona ninyi toka uzima ingine mwaminifu Konstantinos Nachopulos, toka mukini Neokastron Pierias ya Grekia........................................................................................10.
6. Mutawa moja aliyekaribia lufu, alipata hatari kujifanya chakula ya joka-shetani......11
7. Mtu mutajiri Hrisaorios alijifanya uchezo ya ma shetani kwa saa ya lufu yake.......12
8. Yule Mutawa aliyezania maungo yake mufazili, alikwenda mu gehena....................13
9. Historia wa ajabu ya Mtume Thomas, wakati alihubiri mu inchi India....................13
10. Sasa pahali ilianguka jua, ulikumbuka Mungu? ......................................................14
11. »Mutosheni huyu mbali ya hapa. . . »......................................................................14
12. Njia nani nitachakula mu uzima yangu? .................................................................15
13. Lufu ya Mtakatifu Mutawa Benediktos. .................................................................17
14. Alisema ninyi mfupa ya kichwa ya yule mwenye pagano aliyekufa kwa Mutawa Makarios. ...............................................................................................................18
15. Mtakatifu Antonio alipanda mbinguni kwa akili yake............................................18
16. Miaka tatu mugonjwa ao ma saa tatu mu gehena? ..................................................19
17. Namna gani kijana moja alitosha mama yake toka gehena.....................................20
18. Zambi ya kutosha mimba kwa mapenzi ni matata sana...........................................22
19. Ma ulimi yote ya dunia nzima hawakuweze kutangaza mateso ya gehena...............22
20. Maana miaka elfu moja machoni mwako na kama jana iliyopita. . (Zaburi 90, 4)....23
21. Miaka ma ngapi muliacha kanuni ya ma sala yenu? ...............................................24
22. Usichoke juu ya mimi, kwa sababu Bwana aliniokoa. ............................................25
23. Maono ingine ya Mutawa na mwalimu ya roho padri Yosefu wa Spileotis.............25
24. Uhamakio ya nafsi kwa ma roho ya shetani, kisha uchanisho ya nafsi toka mwili...27
25. Fazila gani ulifanya na ulikuja mu utukufu ya paradizo? ........................................36
26. Musopokeni, wa ndugu, kukumbuka ile saa ya lufu yenu........................................37
27. Ee Ndugu Akakie ulikufa? .......................................................................................38
28. Misinana utukufu ya Watawa. . . ..............................................................................39
29. Nilipata hazina ya furaha mingi mu mbingu. . . ......................................................39
30. Ole kwa wale wanafanya zambi na hawatubu..........................................................40
31. Inapaswa kumurudia huyu mukongo na mutaleta hapa mutawa Athanasios.............41
32. Juu ya ninyi unaendelea kufanya zambi? .................................................................43
33. Simama hapa kufamia matendo makubwa ya Ufikisho ya Mbili ya Bwana Yesu.....45
34. Mtakatifu Mutawa Efrosinos alikwenda mu paradiizo.............................................49
35. Historia ya ajabu juu ya yule mpadri aliyekuja toka uzima ingine kusikilizana na shemasi moja.............................................................................................................50
36. Mtoto moja alipanda pa pepo....................................................................................52
37. Mazungumuzo ya mtakatifu mutawa makarios wa m'siri na malaika moja wa Mungu.......................................................................................................................52
38. Historia ya mwanamuke moja aliyerudia toka uzima ingine...................................57
39. Ee mwenye zambi, unataka na weye kukuja hapa? .................................................61

40. Mu Hadeze hakuna toba.............................................................................62
41. Mazungumuzo ya mt. askofu Grigorio kama ukumbusho ya watu mu Matayarisho 63
42. Namna gani aliona Mutawa Averkios Bwana Yesu Kristu ..................................65
43. Malaika ya Mungu alisaidia maungamo ya mutawa moja....................................66
44. Historia toka uzima ya Mtakatifu Uaros...............................................................67
45. Faida toka ma Ibada ya Liturgia Takatifu na makumbusho ni ukubwa.................68
46. Ono na faida ya roho mingi ya Petro Mostratos................................................70
47. Historia ya ajabu juu ya kutii kwa wazazi ...........................................................72
48. Ninakushukuru sana mtoto wangu; ulinipumuzika..............................................74
49. «Kristu alifufukuka wa padri. . . ............................................................................74
50. Walikuja Mzazi-Mungu na Mtakatifu Anastasia. . . ..............................................75
51. Mutawa Stefano toka Monasteri ya Mtakatifu Grigorio.......................................75
52. Sasa nilijiuhuru, sasa nilipata kimya, sasa nilipumuzika. . . .................................75
53. Mwisho takatifu ya Mwaminifu moja...................................................................76
54. Wanakuja ma kundi yote ya watakatifu. . . ..........................................................76
55. Hawa wanaofanya utii hawakufe. . . . ...................................................................78
56. Mtoto mwanamuke Konstantina alipanda mu Paradizo. . . .................................79
57. Ee Mungu wangu, uko wapi? Mtoto yangu anapotea. . . ....................................80
58. Ah, mtoto yangu, hawa waganga tendo kibaya ninyi walinifanyisia! ...................81
59. Lufu mubaya ya mutawa moja..............................................................................81
60. Askofu Grigorio........................................................................................................81
61. Askofu mtakatifu Nikolaos.....................................................................................82
62. Mtakatifu Efimia mu nyumba ya mutawa Paisios...............................................83
63. Mpadri mkubwa Markos ya Monasteri ya Mt. Dionisios....................................83
64. Kama unaomba, mpadri wangu, inakuja hapa ulimi moja ya nuru toka Mungu. .84.
65. Jeshi ya wa malaika mu nyumba yake. . . .............................................................84
66. Muujiza ya Mtakatifu Georgie mkubwa kwa mkubwa ya inchi ya Siria...............85
67. Muujiza moja ya Mtakatifu Nikolaos....................................................................88

## 1. Ono wa ajabu ya Mukristu moja murahimu na mweshimiwa.

Mtu moja aliyekuwa mwenye ndoa zamani, alizala watoto na alikuwa na na watumishi na mali mingi mu nyumba yake. Tena alikuwa murahimu kabisa na mukaribishaji. Usiku moja alikula na alikwenda kupumzika. Asubui walimuona kularia pa kitanda na mwili yake katika baridi na alionekana kama mwenye kufa. Wajerani yake walimusimama, walimuweka pa kitanda na walipima kumurudisha mu uzima, lakini walichoka ya bure. Kisha ma siku madogo alikuja kwa maungo yake na wa jerani yake walimuuliza malari ninyi alipata na hii ma siku alikwenda wapi kama mufu. Yule alikataa kuwajibu; paka aliria bila utulivu na bila usimamisho na, mpaka lufu yake, hasikusema hata sauti moja kwa mtu moja. Wakati ilikaribia mwisho ya uzima yake, aliita karibu yake mtoto mkubwa yake na alimwambia hii ma sauti mbele ya wa jerani wote:

«Mtoto mupendwa wangu, ninakupatia sasa hii amri yangu ya mwisho. Ninataka hii amri kuitimiza, kama unaweza, kabisa mingi. Ninataka kupatia ruhuma kwa wamaskini, kuonyesha mapendo kwa wageni na wasafiri. Utawaita mu nyumba yako na mapendo mingi, utawasaidia kwa kila huitaji yao na utawapatia kila kintu wekona yo lazima, sawa vile uliniona kufanya na mimi mpaka sasa. Kwa sababu ukaribizaji ni fazila inayeipokea sana Mungu kuliko ya ma fazila ingine na, huyu mtu anayefata hii fazila, atapata malipo ya roho mingi mu ufalme ya mbingu Wake. Na kwa sababu ninataka yote mweye kufata hii fazila na onyesho ya mapendo kwa watu wenye maskini na wengine, hii siku ya mwisho yangu, nitamitangaza ono moja niliyeona, mbele ya miaka madogo, wakati muliniona pa kitanda, kama mufu ndani ya nyumba yetu.

Munajua ya kama tango kipimo ya ujana yangu nilikuwa na heshima mingi mbele ya Mtakatifu kamili Mzazi-Mungu Maria na kila siku nilisoma ma sala na wimbo yake. Kwa ajli ya hii mapendo yangu, ile nilikuwa mu uzima yango yote, Rabi wetu Yesu Kristu alinistahili na maombezi yake kunipatia ma zawadi mengi katika roho; lakini kabisa alinipatia zawadi ya kuonyesha mapendo kwa wamaskini na wageni, sawa vile na mweye munaijua, kwani nilipokea kila mtu na mapendo na niliwapatia bile bintu walikuwa na lazima.

Ile usiku ya zamani niliona ona moja, nilisikia na sauti nguvu iliniambia na jina yangu: «Lamuka toka kitanda yako na unifata». Mimi nililamuka na mkono moja ilinikamata na iliniongoza ndani ya kiwanja moja. Ile saa huyu mtu aliyeniongoza, alikimbia na mimi nilikuwa wa pekee bila kujua nitafanya ninyi. Mara moja nilisikia ma sauti ya matata na matetemeko. Nilipindula mukongo na niliona hazina ya ma shetani mengi, wenye walikuja yulu yangu juu ya kuninguruma kama ma nyama makali. Mimi, wakati niliwaona, nilikimbia na boka mingi na nilifika ndani ya nyumba moja na nilifunga mlango. Lakini hawa walinifukuza, walipasula mlango na waliingia ndani kunibamba. Lakini, juu ya kusikia kupita nzuri, sikia na hii sauti. Ilipita sasa miaka tatu, tangu ile siku nilibeba huyu mugeni hapa mu nyumba yetu, mu usiku ya Siku Kuu ya Makumbusho ya Watakatifu Wote ya Kanisa yetu, juu ya kumukaribisha. Wakati nilirudia ku mlango, nilipata na mugeni mwingine, aliyepokea mama yako, katika amri yangu, juu ya kupokea na kukaribisha kila mtu, anayekuja kwetu, kama malaika ya Bwana na kisha saa kidogo alileta na mugeni mwingine na ndugu muloko yako. Ile saa mimi nilisikia furaha mingi, kwa sababu nilistahiliwa kupokea mu nyumba yangu wageni tatu, katika mufano ya Utatu Mutakatifu. Niliwapatia chakula na bintu ingine, katika zwezo yangu.

Basi, wakati, ninarudia sasa kwa ono yangu, waliingia ndani ma shetani, nilianza kupaza sauti kuita Bwana juu ya kunisaidia kwa maombezi ya Mama wake Mtakatifu Kamili Maria. Ile saa ninaona wanaume tatu, wenye waliniambia: «Usiogope, kwa sababu sisi tulikuja akusaidia». Walifukuza ma shetani na waliniuliza mimi kama ninawajua. Mimi niliwaambia:

-Hapana, wa Bwana wangu, misimijue.

Hawa walinijibu: Sisi tuko wale wageni tatu, wenye uliwakaribisha mu nyumba yako na mapendo mingi na ukaribishaji kubwa. Sasa alitutumia Bwana Mungu ya kusaidia wewe nakuripa juu ya hii mapendo mingi ulituonyesha kwa sisi; na tazama tulikuokoa toka mikono ya shetani.

Wakati walisema, hivi walitoka.

Mimi nilishukuru Mungu na, kwani niliogopa kwenda inje juu hapana kuniuzi ma shetani, nilimbakia saa kidogo ndani ya nyumba. Kisha saa kidogo nilifanya alama ya Musalaba na nilitoka inje na kitumaini kwa ulinzi ya Bwana Mungu. Wakati nilitembea, niliona kufika mukongo yangu ma shetani mengi kunisema:

-Twende mbio kumubamba kwani haipaswe kukimbia.

Mimi niliogopa na nilikimbia kuliko mbio na niliita Mzazi-Mungu:

-Ee Mzazi-Mungu Mtakatifu kamili Maria, unisaidie.

Nilitembea vile mbio na nilifika ku mutoni moja ya moto, ile ilikuwa na ndani ma nyoka na ma nyama makali ya Hedeze. Mwili yao ilikuwa ndani ya ma ulimi ya moto na paka kinywa yao ilikuw ainje wazi, sawa walisikia njaa na walitaka kunikula. Wa Shetani, wenye walinifukuza na walinifokea kuanguka ndani ya mutoni ao, hawa wataniangusha. Mimi ile saa niliangalia pempeni kutafuta njia ingine. Mara moja niliona kilalo moja mwembamba na urefu sana, wala niliwaza ya kama ilifika mpaka mbingu. Nilikuwa na shaka, kwani misikujue kufanya ninyi: Nikusema nitaanguka ndani ya mutoni, pahali niliogopa moto na ma shetani, nitambakia kwa mamlaka ya ma shetani ao kupanda hii kilalo? Nilichakula kupanda kilalo. Ma shetani waovu walinifata mukongo. Mimi nilipanda na boka mingi na hatari kuanguka chini ndani ya ma moto. Wakati nilikuwa mu chongo ya ile kilalo, walifika ma shetani na mimi nilipaza sauti na malalamiko mingi kusema kwa Mzazi-Mungu:

-Mtakatifu kamili Mzazi-Mungu Maria, unisaidie.

Mara moja alikuja karibi yangu Mama Mupendwa-wema, Mam ya huruma na alinipatia mkono yake ya kuume mukusema kwangu:

-Usiogope, ee mutumishi mupendwa wangu, Kwa sababu wewe ulisoma mwimbo na ma sala kwa mimi na ulipendake wa maskini, wenye ni wandugu wadogo ya Kristu, Mwana wangu na Rabi wangu, kwa hivi nilikuja na mimi ya kusaidia kwa hii mambo yako.

Wakati aliniambia hii ma sauti yake, alinikamata na mkono yake na, o, muujiza wa ajabu! mara moja alinirudisha nyumbani yangu na nafsi yangu aliingia ndani ya mwili yangu, lakini mweye muliniona ya kama niliisha kufa.

Basi, mtoto wangu, usiwe muvivu na muzaifu kwa hii utumishi mbele ya Mzazi-Mungu na Mama ya Mungu Mwenyezi wetu, Bikira Maria. Kila saa utamuhimbia, utamutukuza na utamushukuru, sawa vile nilifanya na mimi baba yako mupaka sasa. Vile Yeye atakuwa Musaidizi yako mu kila huitaji yako. Hii ni amri yangu ya kwanza ile inapaswa kuifanya. Amri yangu ya mbili, sawa vile nilikuambia ni hii: Kama unaweza, penda wageni, waskini, wanawake wasipo bwana, watoto yatima na fanya nguvu kuwapatia kila kintu hawa wekona lazima. Vile utapata furah ana kwa hii dunia na utariti na Ufalme wa milele ya Mungu! .

Wakati alisema hii yote ma sauti yake kwa wale walikuwa pempeni ya kitanda yake, alitoa nafsi takatifu yake kwa Mikono ya Mungu. Mwana wake alikumbuka mu uzima yake yote ma shauri ya baba yake na alifanya uzima takatifu na wa mapendo ya watu wengine. Vile alifika na ku mwisho ya uzima yake na alistahiliwa na ufalme ya mbingu wa milele.

## 2. Ono ya Yoasafat, mkubwa mpadri ya Nyumba ya wenye Yosafat ya muji Karia ya Kilima Takatifu juu ya Mt. Georgie Mkubwa

Ku mwaka 1854 mutawa Yoasafat, aliyeishi miaka mingi mu Kilma Takatifu, alikwenda mu nyumba ya Monasteri ya Mtakatifu Paulo, ile iko mu mji Karia juu ya Siku Kuu ya Mt. Georgie. Aliikaa usiku mu kiti moja ndani ya Kanisa na aliwaza upenda-wanadamu ya Mungu.

Aliwaza juu ya ufikisho ya Kristu duniani, usulubio na ufufuo yake na upandisho yake mbinguni. Alifurahi kwa roho na alianza kusema bila kusimama sala hii: «Bwana Yesu Kristu, Mwana wa Mungu, unihurumie mimi mwenye zambi». Ile saa alizania ya kama alitoka inje ya kanisa na nafsi yake ilitoka ya mwili yake na ilikuwa ndani ya kiwanja moja kizuri sana. Ndani ya hii fasi nzuri aliona hazina ya wakijana wale walivaa mavazi mazuri kabisa. Waliangaza kama jua na walitembea pole-pole na namna upole. Alishangaa wa nani ni wale wakijana na hii shamba nzuri ilikuwa ya mtu nani? Alipita hii hazina na kisha aliona hazina ingine na wakijana mengi kabisa, wenye walivaa manguo kama wa askari na walikuwa wote wenye nguvu na wenye mwangaza pa uso yao. Basi, alisimama na aliangalia hii utukufu na neema yao. . Moja kijana katikati yao alisema: «Huyu ndugu zetu anataka kwenda kwa Mfalme wetu na inapaswa moja katikati yetu kumupeleka». Alitosha mtu moja katikati yao na alisema: «Mitapeleka mimi mwenyewe huyu ndugu kwa Mfalme, kwa sababu ananipenda na kila mchana na usiku anaita jina yangu na mimi mara mingi nilimusaidia mbele ya Mfalme wetu».

Kweli huyu kijana, mkubwa ya waskari alikaribia mutawa Yoasafat na alimwambia: «Unifate mimi na nitakupeleka mbele ya Mfalme».

-Ee ndugu, anamwambia Yoasafat, nani niko mimi na nitasimama mbele ya Mfalme na Mfalme atanifanyisia ninyi mimi? Nani eko huyu na namna gani ananifamia mimi?

-Ee ndugu, anamwambia Mtakafifu mkubwa wa askari, unafanya ya kama usijue nani eko Mfalme na unaonyesha ya kama usijue na mimi nani niko? Kwa sababu unanipenda na unakumbuka jina yangu, nilikuja mimi sasa juu ya kukupeleka kwa Mfalme na unifata sasa».

Walitembea pamoja ile kiwanja urefu na walifika ku mwisho yake na waliingia ndani ya njia moja mwebamba na urefu na kibabashi yake pembeni walikuwa marefu mingi na Mutawa Yoasafat aliogopa, kwani asikujue alikwenda wapi na nani eko huyu aliyemuongoza.

-Mwongozi yake mukuona Mutawa ya kuogopa anamwambia:

Juu ya ninyi, ee ndugu, ukona uzaifu na usisopoke na akili yako kwa mwito ya Jina ya Mungu: «Bwana Yesu Kristu, Mwana wa Mungu, unihurumie mimi mwenye zambi». Mutawa, wakati alisikia hii ma sauti, alianza kuria na, ile saa alianza kusema hii sala ya Kristu na roho yake ilijaza na kivukutu ya mapendo ya Mungu. Mara moja alikamata nguvu na boka ilitokea sana. Mara ingine mwongozi yake alimwambia: «Unaona ya kama sasa uko kupita nzuri? Kama unataka wokovu ya nafsi yako, usiache hii sala ya Kristu. Vile, utapata akili safi na roho na utaona ma fumbo ya Mungu. Halafu, sopoka kufanya maungamo safi kwa padri ya roho yako juu ya kila mambo kibaya itaonekana kwako.

Walitembea pamoja ndani ya hii njia mwebamba, pahali ma fasi ya kona walikuwa ma musalaba ma mengi. Mwongozi yake, Mt. Georgie, alifanya alama ya musalaba juu ya kumufata na kufanya hii alama na Mutawa Yoasafat. Tena mara moja aliimba: «Musalaba yako tunasujudu, ee Rabi, na Ufufuo yako tunatukuza».

Kisha mwendo ya kuenea walifika mu ya kona ya ile njia, pahali ilikuwa kilalo moja pa pepo, kwani mwisho yake moja ilikuwa pa kilima moja. Alianza kuogopa na kutetemeka Mutawa Yoasafat, kwani aliwaza namna gani atatabuka hii kilalo, iliyekuwa pa pepo. Mwongozi yake alimwambia: «Ee ndugu, unipe mkono yako na sema bila kusimama sala ya Kristu, bila kuwaza kintu na uwazo ingine». Wakati walifika mu katikati ya ile kilalo, pahali chini yake ilikuwa mutoni, mwongozi alisema kwake: «Hapa fanya musalaba yako na ita Jina ujaliwa-neema ya Mtakatifu kamili Mzazi-Mungu Bikira Maria na Yule atakupatia nguvu! ». Kweli, yule alisema: «Mtakatifu kamili, ee Mzazi-Mungu, unisaidie mimi mwenye zambi». Alikamata nguvu mingi, wala ilitokea boka iliyekuwa ndani yake.

Wakati walifika mu fasi ingine ya mwisho ya ile kilalo, walipanda na nguvu sana ile kilima. Kule ilikuwa mulango moja na, wakati walifanya mbele alama ya musalaba mara tatu, waliingia ndani. Kule waliona kuzambalishwa mbele ya ma macho yao kiwanja ingine njema kabisa iliyefanana na ragi ya mbingu. Wakati walitembea, huyu Mutawa, alishangaa kwa ajili ya

hii utukufu na ile makao. Kule aliona watu mengi, waliyevaa manguo meushi, kama watawa na waliangaza kama jua. Walipokea mwongozi yake na ubusu na furaha mingi walimwambia:

-Salamu, ee Georgie Mkubwa, mutumishi mupendwa ya Kristu!

-Salamu na mweye, Watawa, watumishi wapenzi ya Kristu!

Hawa watawa wote walipindula ma kichwa yao kwa mutawa Yoasafat na walimwambia: «Faida gani kama mutu akipata dunia nzima, na kupata hasara ya uzima yake? (Matayo 16, 26). Kama utaishi miaka 100, 200, tena na miaka 1000 ndani ya hii dunia, na utapata ma feza mengi na matukufu na ma furaha, faida gani utapata ile saa ya matata ya lufu yako? Kwa hivi, ndugu wangu, acha uvivu na rudia muzima yako ya zamani iliyekuwa wa fazila na heshima ya Mungu, utawa na unyenyekevu juu ya kukuja ndani ya hii uzima wa heri, ile ulistahiliwa kuiona sasa na saidio ya mulinzi yako, Mt. Georgie Mkubwa, mwenye anakupenda na alikuletea hapa kufurahi saa kidogo kwa hii ma fasi ya paradizo. Usichakula ma bintu ya dunia na utapotesha ma bintu ya mbingu. Usiache roho yako ya kuishi na uzaifu, usingizi na masubuko ya bure na usiache sindano ya roho, kwani katika hii sindano utapata mapendo ya milele ya Kristu.

Usitaabu Kristu na rabi wetu, aliyetukomboa na Damu Yake Takatifu, wakati iliyemwangisha pa Musalaba yake. Kama unataka sisi kuomba kwa Mungu juu ya weye na ya dunia nzima, geuza uzima yako na hivi utamufurahisha Mungu na sisi, wenye tunapenda dunia nzima na tunataka kukuja yote mweye hapa mu Ufalme ya Mungu».

Kisha walipindula na walisema kwa Mt. Georgie:

-Ee Georgie, Mushahidi ya Kristu wetu na ndugu mupendwa wetu, subuka na chunga hii nafsi ya mutawa Yoasafat na utamupeleka mbele ya Mfalme ya watu wote, kwani ukona uwezo mingi mbele Kwake». Ile saa mutawa Yoasafat alisikia nani alikuwa na mwongozi karibu yake, mara ma ngapi alimusaidia mu dunia na alimuweka musaidizi yake mbele ya Kristu kwa wokovu wake. Kwani aliisha kujaza na shukrani na mapendo mbele ya Mtakatifu Georgie, alimukaribia na ya saa mingi alimubusu na machozi ya mapendo.

Walitembea tena ndani ya ile kiwanja nzuri na huyu Mutawa aliona na watawa wengine, kuliko wenye utukufu ya wengine ya mbele, lakini walikuwa madogo. Aliuliza mwongozi yake: «Ee Mtakatifu ya Mungu Georgie, hawa watakatifu, wenye ni kuliko yulu ya watawa wengine ni wa nani na matendo yao ni ma nani? ». Mtakatifu Georgie alimujibu:

-Ee ndugu, hawa ni toka watawa ya hii jira, wenye walikombana hawa wenyewe, bila mwongozi ya roho. Walitembea pa mwenendo ya watakatifu wa padri, wenye zamani na, kwani walimushukuru Mungu, Yule aliwaripa na hii utukufu sasa unaiona.

-Lakini leo ilionekana kila alama ya fazila na namna gani iko namna kupatikana watu mu dunia na hii ma fazila?

Ile saa Mtakatifu Georgie alimwambia:

-Ee Ndugu Yoasafat, leo weko mu ndunia watu wenye fazila wadogo, lakini kama mtu moja atachoka juu ya kupata fazila kidogo, atavumilia ndugu yake na hasipende kumuhukumu, huyu atamufurahi Mungu na ataitwa mkubwa katika ufalme ya mbingu.

Walitembea mwendo yao na walifika mu Nyumba ukubwa kabisa ya Mfalme Mkubwa wa mbingu. Kule mu maingio waliwapokea na waliwasalimia na ubusu katika Kristu wanaume wakubwa na watukufu, wenye ma uso yao iliwangaziwa na waliwaongoza ndani ya chumba moja iliyejaza na nuru. Mu fasi ya kuume ya maingio ilikuwa picha ya Kristu, lakini mu fasi ya kushoto ilikuwa picha ya Mzazi-Mungu aliyeikaa pa kiti yake.

Ndani ya ile chumba waliikaa ma hazina mengi ya wa kijana, wenye walivaa manguo meushi na walikama kwa mikono yao musalaba na mawa na hii walitosha harufu nzuri. Hawa wote walikamata pa mikono yao Yoasafat na mbele ya picha ya Kristu na Mzazi-Mungu waliimba hii: «Ni wajimbu kweli. . . ». Kisha walibusu ile ma picha na walisema kwa Mutawa: «Ee ndugu, hii matendo yote unaiona wanajifanya juu ya weye; basi, anaangalia kuwa mtu muzuri na mupendwa ya ma fazila juu ya kukuja hapa mbio».

Kisha waliondoka wote na walimbakia Mt. Georgie na Mutawa. Ile saa ilifuguliwa mulango moja kubwa na ilisikiwa sauti moja utamu iliyesema: «Ee Bwana, wema yako ni kubwa, kwa watu wote». Ile saa aliona Mutawa kanisa moja nzuri kabisa, na katikati yake ilikuwa kiti moja wa moto, kupita katika mwangaza ya jua. Kule aliikaa Mfalme ya utukufu Kristu katikati ya ma hazina ya wanaume, waliovaa mavazi kama wakubwa ya wa askari na ma uso yao walijaza na mwangaza. Kristu na Rabi wetu alivaa pa kichwa yake taji na maimbwe kama diamant na aliangaza Uso yake yote kama umeme.

Ndugu Yoasafat alisimama ku mulango kuangalia ndani na ushiago na bila kushiba. Aliingia ndani Mt. Georgie, alifanya alama ya musalaba, alipika magoti mara tatu na alisujudu Mfalme. Kisha alikuwa tayari kurudia juu ya kupeleka karibu yake na Yoasafat, lakini ile saa alisikia sauti ya Mfalme, aliyemwambia hivi: «Umwache huyu, hana mustahili kuingia, kwa sababu hana nguo ya ndoa».

Mukusikia hii sauti Mutawa Yoasafat aliogopa ya kama atahukumwa na alianza kusema sala ya Kristu: «Bwana Yesu Kristu, Mwana wa Mungu, unihurumie mimi mwenye zambi». Mt. Georgie alianguka mbele ya miguu ya Mfalme na alimwabia: «Ee Bwana, kumbuka hii Damu uliimwangisha pa musalaba kwa wokovu ya watu; kwa hivi ninakuomba umusamehe nafsi hii yenye zambi na umuongoze mu njia ya wokovu. Ninajua ya kama wema wako ni bahari na urefu sana bila mupaka». Na ile saa Mfalme alimujibu:

-Ee Georgie, unajua nzuri mapendo ngapi nilionyesha kwa huyu Mutawa na nilimupatia baraka yangu kufamia hii ma fumbo yote ya mapendo yangu, kwani hii ma fumbo watu wengine walisindana miaka mingi juu ya kuiangalia na kuifamia. Huyu hasikukuwa na ndani ya nafsi yake mapendo yangu, alinizarau, aliishi mpaka sasa na uzaifu na paka juu ya bile bintu ya hii dunia, alizarau mimi na hana mustahili ya usamehe».

-Ninajue, ee Bwana, aliendelea kusema Mt. Georgio, ya kama, kama utahukumu na haki Yako, huyu kweli ni mustahili ya malipizo, lakini ninakuomba, acha wema wako kwa huyu mutumihsi yako. Unajua ya kama dunia nzima iko ndani ya matendo maovu, hali kibaya ilizambalisha ma fasi yote na hakuna mifano mazuri mengi. Umupatie, neema yako, ee Bwana, juu ya kuokolewa mutumishi wako, kwa sababu eko na matakio nzuri na paka kwa ajili ya ma zwezo mbaya yake inajikokota mu zambi».

-Georgie mupendwa wangu, ninajua hali ya dunia, manyanganyi ya hamuri yangu, mazulumi, masharati na matendo yote ya kuonekana na wasiyoonekana ya watu wote. Lakini ninaongojea hata toba ya mtu moja mwenye zambi. Ninatakia watu wote kuokolewa, kwa hii mambo nilimwanga Damu yangu pa musalaba na kila siku ninazabihu maungo yangu. Lakini huyu mutawa, kwa ajili yake unaomba neema yangu, hasisikie ma amri yangu na mupaka leo anafanya mapenzi yake. Nilikusimama kuonyesha njia ya kweli, lakini yule anaanguka mu uzaifu, anazarau na anakataa zabihu yangu».

-Ile saa Mt. Georgie, alibusu miguu Yake na unyenyekevu mingi na alimwambia: «Kumbuka, ee Bwana, damu yangu iliyemwangisha kwa mapendo yako na unipatia hii nafsi. Umusamehe, ee Bwana na umustahili kunywa kilauri ya mapendo Yako na kufanya mapenzi yako Takatifu».

-Ile saa Bwana na uso katika furaha alimujibu: « Ee Georgie, nitafanya mapenzi yako».

Alimupatia na mukono ya kuume yake kilauri moja na alimuwambia: «Kamata hii kilauri na umupatie kukuywa hii iko ndani; hii ni kilauri ya mapendo yangu. Watakatifu wote walikunywa toka hii kilauri, kwa sababu hii mu uzima ya bure inajaza na mateso, mahagaiko, maombolezo na lufu ya mwili juu ya kusafishwa nafsi na kufurahi kisha hapa mu paradizo ya milele».

Mt. Georgie alikamata hii kikombe na alimupatia kwa Yoasafat, aliyeikamata na aliikunywa. Alilewa kwa furaha na mapendo ya Kristu Arusi wa mbingu na mukuingia mu Kanisa ile, alisimama chini ya miguu ya Kristu, aliwabusu na mapendo na furaha mingi.

Kristu alipindula kichwa yake kwa Mutakatifu na alimwambia: «Beba ndugu Yoasafat na umupeleke chini duniani juu ya kukombana na kupata hivi mapendo yangu ya kwanza iliyepotesha kwa ajili ya zambi na uzaifu yake. Kama atakuwa tayari, nitamustahili kukunywa hii kilauri nilikunywa na mimi ku mwaka yangu zamani».

Kisha walibusu miguu ya Bwana Yesu na walisalimia wakubwa wote ya ile nyumba ya mbingu na walianza kushuka na kurudia duniani. Ndugu Yoasafat alisema kwa mwongozi wake: «Ee Mt. Georgie, haina namna kumbakia na mimi hapa juu ya kuwa pamoja, kwani misipende kurudia mu dunia?

-Mupendwa wangu, alimwambia Mutakatifu, hii unaniomba hakuna namna, kwa sababu mapenzi ya Bwana wetu ni ya kushuka chini na, wakati utapambwa na ma fazila yote, utakuja hapa kufurahi Utukufu yake kwa milele».

Walirudia toka njia umoja na walifika mu kati ya njia, pahali ilikuwa kilalo. Ile saa Mtakatifu alisema kwa Yoasafat: « Ufalme wa mbinguni ni tayari, haiongojee na watu wenye wanapenda kuingia ndani, inapaswa na haraka kutumika ya kuingia kwake». Basi, wema ya Mungu unaifamia, fanya nguvu kupata mapendo ya kwanza na mimi nitakusaidia». Wakati alimwambia hivi, alimuweka pa uso yake alama ya musalaba mara tatu na kisha alikimbia.

Ile saa mara moja walisikiwa ma sauti matata na makali toka ma shetani, iliyekuja toka chini ya mutoni na walisema: «Sasa, kwani alimbakia huyu mutawa wa pekee, twende kumutupa chini, mbele ya kukuja Georgie». Ndugu Yoasafat hasikuweze kwenda wala mbele wala mukongo, lakini ma shetani walinguruma kumutupa mu mutoni. Ile saa yule alilamuka mikono yake yulu na alisema: « Ee Bwana, unisaidie hii saa, kwa sababu ninapata hatari kujibomoa ya ma shetani wenye matata». Ilikuja sauti toka mbingu iliyemwambia: «Ee Ndugu wangu, usisimame kusema sala ya Kristu: «Bwana Yesu Kristu, Mwana wa Mungu, unihurumie mimi mwenye zambi», na kwa maombezi ya Mzazi-Mungu Mama Maria usitapate mambo moja».

Mara moja ndugu Yoasafat alianza kusema hii sala ya Kristu, bila kusimama na bila kusikia alirudia ndani ya mwili yake, sawa vile alikuwa pa kiti ndani ya kanisa, pahali walifanya watawa Ibada ya Siku Kuu ya Mtakatifu Georgie.

## 3. Jibu matata ya Mutawa Evlogios ile saa ya lufu yake.

Mu nyumba inayeitwa «Habari Njema ya Mzazi-Mungu» ya Skiti ya Mtakatifu Anna ya Kilima Takatifu ya Grekia, aliishi na utii kubwa na unyenyekevu mutawa Evlogios, aliyeishi uzima yake mu mwaka 1885 na kipimo yake miaka 95. Sawa vile walikikiri na Watawa wengine ya Mukini-Skiti yao, Mutawa Evlogios, mbele ya kutoa nafsi yake kwa Mungu, alipokelewa ma roho ya shetani ya nyakati ma saa 24. Wa tawa wote waliona ndugu Evlogios, mbele ya lufu yake, kutega kichwa yake hata mu fasi ya kuume, hata mu fasi ya kushoto na alijibu mbele ya ma sauti ya ma shetani, wenye walimushitake na walimukumbuka ma zambi na makosa yake ao kusema kweli ao kusema ya uwongo. Wakati Evlogios alisikia ma sauti ya ma shetani, aliwajibu kwa kila sauti yao: «Fasi wapi? Wakati gani? Fasi wapi? Wakati gani? Na mtu nani? Hii ma jibu alisemaka padri Evlogios ya ma saa 24. Wale waliyekuwa karibu yake, walipima kusimamisha kichwa yake, juu hapana kutegwa hivi ya kuendelesha, lakini haikukuwe namna. Mara mengi aliwajibu: «Hapana! haikujifanye hii tendo, munasema uwongo. Juu ya hii kazi, munanihukumu, nilitubu. Na mara ingine aliendelea: «fasi wapi? Wakati gani? ». Vile, bila kusema sauti ingine kwa Watawa wengine wenye pempeni, alitoa nafsi yake kwa Mungu, bila ujulisho ingine.

## 4. Ono ya mwaminifu moja aliyeitwa Dimitrios toka mukini Stratonio, karibu ya Kilima Takatifu.

Hii ono ilifanyika ku mwanzo ya mwaka 1520. Aliiandika Mtakatifu Mitrofanis, Mutawa mwenye jangwa ya Katunakia ya Kilima Takatifu, wakati alikwenda kwa hii Mukini juu ya maungamo ya Waminifu. Anatwaambia, basi, hii historia juu ya jamaa moja. Mwaminifu moja mweshimiwa, aliyeitwa Dimitrios alitumika ku mwaka 1520 mu societte moja, iliyetosha shamba, juu ya kusaidia jamaa yake. Alikuwa na watoto wa ine; walikufa wa tatu na alimbakia paka moja, wa mwisho, aliyempenda sana kwani alitii na aliheshimiwa wazazi wake. Lakini mapenzi na mawazo ya Mungu hakuna namna kujua watu. Kisha nyakati kidogo, kwa ajili ya malari moja, alikufa na huyu mtoto na wazazi hivi walimbakia, bila utulivu mu uzima yao. Kisha ma siku kumi na tano, toka ile siku ya lufu ya mtoto yao, baba alipotesha nguvu na mahasa yake na alionekana kama mufu. Mwili yake ilikuwa ya kufa na ilikuwa baridi na paka makao ya roho ilikuwa na kivukutu. Kwa hivi wa jerani yake walikamata mpango hapana kumumazika, mpaka kukufa mwili yake yote.

Lakini mwaminifu Dimitrios alikwenda mu uzima ingine na fasi yake na, wakati alirudia alijitulivu sana, hapana paka huyu, lakini na wa jerani yake yote, kwa ajili ya bile bintu aliona, alifurahi na alishangaa. Aliona watoto wake na tena huyu wa mwisho kuwa mu fasi moja wa furaha na shangilio, pahali na huyu alitamaa kuipata na kumbakia daima kule. Tazama namna gani anatwaambia huyu mumoja safari yake mu dunia ya mbingu.

«Wakati nilikuwa chini pa kitanda katika malari yangu, ninaona kijana moja mwenye kuvaa manguo ya mwangaza mingi na uso yake hakuna namna kusema namna gani ilikuwa na mwangaza. Nilisahau kamili uzima ya inchi yetu na matendo ya dunia na maangalio yangu ilikuwa kwake. Nilizania ya kama nilitoka toka mwili yangu na huyu kijana alikamata kwa mikono yake nafsi yangu na tulipanda pamoja kwa mbingu. Niliangalia ya kama tulipita mavirigo wa saba ya mbingu. Mukupanda yulu, tulikutana nuru pamoja na umeme, lakini kuliko yulu hii nuru ilikuwa kabisa nuru na ilizambalishwa inchi moja na mawa mazuri mbele ya ma macho yetu na hii utukufu yake hakuna namna kuisema. Kisha hii inchi wa paradizo, tulifika mbele ya milango wa wili, yenye walikuwa ya kufungwa nguvu. Mu fasi ya kuume walikuwa wa kijana wa wili na mu fasi ya kushoto ma kijana makali na ma uso yao walikuwa mbaya sana. Wakati tulikaribia mukaribibifu yangu ananisema:

-Namisha kichwa yako chini na usujudu.

Mimi, ile saa nilikuwa na kichwa yangu chini na nilisikia sauti moja toka mbali iliyeniambia:

-Juu ya ninyi ulileteа huyu mtu hapa? Misikusema kuleta huyu mtu hapa, lakini mujerani yake, anayeitwa Nikolaos. Huyu Dimitrios ekona miaka tena kuishi mu inchi chini.

Kisha hii sauti alinibeba muongozi yangu na tulienda mu fasi ya mashariki, pahali ilikuwa kiwanja moja ya kujaza na mawa mazuri ya ma namna ya kuachana. Chini mu kimvuli ya kila muti aliikaa na mtu moja. Hawa watu walikuwa na kipimo ya miaka paka umoja, lakini ma uso yao walikuwa na mwangaza kuliko mingi na ma uso ya wengine watu walikuwa kidogo ya nuru. Kwa kila mtu sisi tuliona matendo yao, bile walifanya mu uzima yao na walifamia moja kwa mwingine. Ndani ya hii kiwanja mukuangalia mu kuume na kushoto, niliona watu mengi, wenye niliwafamia mu uzima yangu, lakini waliisha kufa ya zamani. Niliona kule na mwanamuke moja nduba, mwenye toka onekano yake ya inje alijua kila mtu uzima ninyi alifanya kwa inchi hapa chini. Niliona na wanyanganyi, wenye waliisha kuhukumwa ya kutundikwa na wenye zambi wengine na watu wazuri, wenye walikuwa na matendo yao mazuri ile walionekana nguvu. Tena niliona na warafiki wengi na ma jerani yangu kuikaa ndani ya hii fasi.

Mu fasi ingine ya ile kiwanja nzuri niliona kuikaa na watoto wa ine, wenye walikuwa wazuri na wenye mwangaza pa uso na mwili yao. Mwongozi yangu aliniuliza: «Ee ndugu, unafamia hawa watoto wazuri? ». Ninakaribia tena karibu na ninaona katika ajabu ya kama hawa watoto walikuwa watoto yangu. Tena huyu wa ine aliyekufa ku mwisho, walikuwa na yo katikati yao. Ile saa nilisema kwa malaika yangu: «Ndivyo, Bwana yangu, ninawafamia; hawa ni watoto

yangu». Furaha yangu ilikuwa kabisa kubwa, kwa sababu niliwaona kuwa wenye furaha na sawa kuvaa manguo ya nuru. Niliomba toka mwongozi yangu kuniacha kuikaa pamoja nao, kusikia furaha yao na shangilio na hapana kutoka ya watoto yangu. Lakini malaika alinikokota toka ile makao mukunisema ya kama bado kukuja nyakati yangu. Mimi ile saa nilimuuliza: «Bwana wangu, hii fasi ni Paradizo na Ufalme wa mbingu? ».

-Yule aliniambia: Hii makao wala Paradizo, wala Ufalme wa Mbingu iko, lakini ni hii inatwaambia Mandiko Takatifu: «inchi ya wenye upole». Kule wanapumzika ma nafsi mupaka Ufikisho ya Mbili ya Yesu Kristu. Uhukumu ya Mwisho itajifanya, wakati Kristu atafufuka kizazi yote ya watu, juu ya kufurahi na mwili yao ku furaha ao ku malipizo ya nafsi. Ile saa wenye zambi na wasipo kutubu wataingia mu mulango ya kushoto, iliyeona, wakati tulipanda mbinguni na waliichunga wa shetani makali, lakini wenye haki wataingia mu mulango ya kuume, iliyechunga wa malaika wenye kuvaa mavazi meupe na kupe watafurahi Ufalme wa Mungu. Ma nafsi, lakini ya Watakatifu wakubwa, alisema musaidizi yangu, weko mu fasi kupita juu, kutoka ile fasi inakuja hapa nuru.

Wakati tulishuka, tulifika mu fasi moja ya kuoza na harufu ilikuwa kibaya sana. Kule waliikaa hazina ya watu, wenye walikuwa uso yao katika taabu mingi. Niliuliza wa nani ni hawa watu na malaika yangu aliniambia ya kama hawa watu ni watu wa Ebrania, wenye hawakusadiki kwa Kristu. Tulitembea tena kidogo mbali na tulikutana makao ingine kupita na uchafu na kuoza mingi, pahali watu walionekana kama wadogo kabisa kama ma bilulu na walitelemuka ndani ya matope ya uchafu. Niliuliza mwongozi yangu na aliniambia ya kama hawa ni wa Turki, wenye kufata fundisho ya uwongo na watu wenye zambi ya hii dunia». Kule nilifamia na hawa watu wanaomba hapa bintu na ma feza, kwani hii iko kazi yao na ma uso yao walikuwa na taabu mingi. Wakati tulitoka ya kule, tulizunguluka na ma fasi ingine mbaya kabisa, pahali watu ya ma ndini ingine ya kuachana, watu wasipo imani ya Mungu, wafumu, wapagano na watu wasipo imani ya kweli Orthodokse. Niliuliza mwongozi yangu:

-Bwana yangu, hii ni gehena iliyesema Evangelion ya Kristu?

-Hapana, hii mateso ni ya nyakati kidogo, nikusema mupaka Ufikisho ya Mbili ya Bwana Yesu Kristu. Inapaswa kujua ya kama gehena ni moja, lakini mateso na malipizo ndani yake ni mengi ya kuachana; sawa vile mu Ufalme ya mbingu kila mwaminifu anabeba makao yake ya kuachana, katika matendo ya toba na ma tendo ya ma fazila iliyefanya duniani.

Wakati mwongozi yangu alisema hii ma sauti, nilisikia kukuja toka chini ya mutoni sauti ya joka moja mukubwa na pamoja ilipandisha juu ya harufu kibaya. Mimi ile saa niliogopa na nilikombana kujifuchama kwa mikono ya Muchungaji malaika yangu. Nilimuuliza:

-Sauti ninyi iko hii na inakuja ya wapi? Na hii arufu kibaya, Bwana yangu, ni ninyi?

-Huyu anayepaza sauti nguvu na anajisagia hivi ni Hadeze, mwenye anapokea wasiyo imani wote, wenye ya fundisho uwongo, wenye zambi wasiyo toba na watu wabaya wote.

Na, ile nyakati sauti kibaya ya huyu joka ilikuwa ndani ya masikio yangu, nilijipata mara moja ndani ya nyumba yangu. Niliona mwili yangu kama maiti, ubaya na wa baridi na misikutake kuingia ndani yake. Mwongozi yangu, halafu, aliniweka ndani na haraka na mimi nilisikia umivu mingi na mizilo na misipa yangu na mifupa walianza kutegwa».

Ono ya mwaminifu Dimitrios ilijikikiri ya kama ilikuwa kweli, kwa sababu, kisha ma siku mbili, mujerani yake Nikolaos, hata alikuwa muzuri mu afya yake, mara moja aligonjwa na alikufa. Vile matayarisho yote waliisha kufanya ya huyu Dimitrios waliipatia kwa mufu Nikolaos. Katika hii jabo ilitimizwa na neno ya ile sauti takatifu, iliyesikia na Dimitrios: «Misikukuseme kuletea hapa huyu, lakini mujerani yake Nikolaos».

## 5. Aliona ninyi toka uzima ingine mwaminifu Konstantinos Nachopulos, toka mukini Neokastron Pierias ya Grekia.

Hii Ono ya mwaminifu mukristu Konstantinos, aliniambia mutawa Andreas Grigoriatis (toka Monasteri ya Mt. Grigorios ya Kilima Takatifu), mwenye alitumika mu shamba moja karibu ya mukini ya huyu mwaminifu. Tazama alisema ninyi padri Andreas, kisha ile mazungumuzo alifanya pamoja na mwaminifu Konstantinos:

«Ku mwaka 1945, mimi, anasema padri Andreas, nilikuwa mupisi ya Monasteri kidogo yetu, iliyekuwa karibu ya mukini Livadi ya Pieria. Mu Juma ya Matawi ya ile mwaka 1945 alikuja kwa Monasteri yetu huyu Konstantinos Nachopulos juu ya kuuza sabuni na mwana-kondoo moja juu ya Siku Kuu ya Ufufuo ya Kristu. Kwa sababu ile saa alilofa padri mwingine aliyeitwa Nestoras, mimi milimupokea, milimufanysia kafe na nilimuuliza namna gani iliisha malari yake na namna yeye aliokolewa. Yule aliniambia na mapendo mingi hivi:

«Mimi, padri Andrea, sawa vile unajua, nilikuwa askari pamoja na wakijana wengine juu ya kuchunga mukini yetu toka wa adui yetu. Ku mwanzo ya mwezi ya Tisa ya mwaka 1944 tuliondoka ya Mukini yetu pamoja na wa aksari toka Mukini Meliki na pamoja na mukubwa yetu Georgie Kukiotis tulikwenda mu mukini Kukos. Toka kule ku mwanzo ya mwezi ya kumi, tuliondoka na tulikwenda mu njimbo Kilkis na kisha ilijifanya nvita na wa adui wetu. Wa adui wetu walituharabisha na walitukamata watumwa. Katikati ya wale watumwa nilikuwa na mimi. Walitufunga mu fasi moja ya wa askari ya muji Thesaloniki.

Wakati nilikuwa kule, padri Andrea, nilikuwa na muchoko mingi na nilianguka chini na malari na nilikuwa pa kitanda kama mufu. Kisha walifanya waganga ninyi na mwili yangu, mimi misijue. Paka ninajua ya kama nilienda na nafsi yangu ndani ya makao mnene, pahali walikuwa ma chumba mengi na walikuwa nuru nguvu, kupita ya nutu ya jua. Mimi misikujue ilikujaka wapi ile nuru. Mimi nilipita toka chumba moja kwa ingine, kwani walikuwa milango katikati yao na nilifika inje ya lupago moja na kule nuru na mwangaza waliisha kuniajabu sana. Ilikuwa nuru moja kupita nguvu ya jua, lakini hii nuru haikulugua, sawa hii nuru ya jua yetu.

Ndani ya ile lupago walikuwa watu mengi na nilifamia mengi, wenye walikuwa toka mukini yangu na waliisha kufa, mbele ya miaka madogo. Walivaa manguo ile walivaa na hapa mu inchi yetu; niliwasalimia na nilisema kwa maungo yangu, ya kama hawa wamekufa, namna gani sasa mimi niko pamoja nao? Nilikufa na mimi na bado kuisikia? Ile saa, hawa waliniambia ya kama: «hapa utakuja na weye».

Kisha nilienda mu kibabashi ya ile lupago, pahali walikuwa ma nguzo ya mbau na mu ngambo ingine mbali niliona kuanja ingine kuzambalishwa iliyekuwa na mawa ya kuachana. Ndani ya ile kiwanja walikuwa ma njia na walitembea watoto ya kipimo yao na miaka 10-12. Hawa watoto walikuja toka fasi ingine na waliingia ndani ya ile kiwanja ya mawa na sisi tiliikaa ndani ya ile kibabashi na tulifurahi kwa ajili ya mawa mazuri.

Nilimbakia kule ma siku makumi mbili na nisikuwa na uwazo ya chakula, lakini nilifurahi wakati niliona mawa na wale watoto, waliyekuwa kama wa malaika wadogo na walitembea kule ndani.

Mara moja nilijipata pa kitanda yangu ndani ya obitalo na, wakati nilifungua ma macho yangu, nililamika hivi: Aaaa! Ile saa mara moja dada moja ya ile obitalo alikuja kwangu na alitangaza waganga mukusema kwao: «Lazaro alifufuka. . . . » Waganga walinipatia maziwa, juu ya kuzombelea chakula mwili yangu na kisha ma siku madogo, walinituma nyumbani yangu na mu jamaa yangu.

## 6. Mutawa moja aliyekaribia lufu, alipata hatari kujifanya chakula ya joka-shetani.

Wakati moja aliishi kijana mwanaume moja, aliyeitwa Theodoros. Alikuwa mtu, bila matangenezo mu uzima yake na bila matakio mu uzima ya utawa. Lakini alifata ndugu yake kwa

Monasteri moja. Kama mtu moja alimushauria ma sauti ya wokovu, yeye hakuna namna kuifata na kuimaliza hii ma shauria. Wala alipokea kufanyika mutawa.

Basi, ilifika nyakati na kwake kuja ku mwisho ya uzima yake, kwa ajili ya malari moja, iliyemuleta karibu ya lufu. Karibu yake walisanyikwa wa ndugu ya Monasteri yake na waliomba Mungu kumwema, ile saa ya kutoka nafsi yake mbinguni.

Mara moja, wakati wa ndugu waliomba, Theodoros alianza kupaza sauti nguvu na kusema hivi: «Mutokeni ya karibu yangu, kwa sababu mimi nilijitoa kwa joka-shetani juu ya kuninguruma. Lakini hasiweze kunikula kamili, kwa ajili ya ufikisho na ma sala yenu. Mutokeni sasa mweye juu ya kutenda kazi yake, kwani alikamata mpango kunikula. Juu ya ninyi mimi sasa nitavumilia hii mateso ya kuchelewa kunikula?

Wa ndugu waliogopa sana na walimwambia: Fanya, ndugu wetu, alama ya musalaba pa mwili yako.

-Ninataka kufanya alama ya musalaba, lakini misiweze, kwa sababu tema ya joka, inanilekea mukono yangu.

Kisha hii jibu ya Theodoros, watawa walianguka chini na ma sala mengi na machozi waliomba kwa Mungu juu ya kumuokoa toka kinywa ya joka-shetani. Kisha saa ya kuenea, alisimama mara moja huyu Theodoros na alisema na nguvu mingi:

-Wa ndugu wangu, mumushukuruni Mungu, kwa sababu joka, aliyetaka kuninguruma, alikimbia kwa ma sala yenu na hasikuweze kusimama hapa hata kidogo. Sasa, basi, ninamiomba, mumuombe kwa Mungu kunisamehe zambi yangu na kisha hii jabo yangu wa matata, nitaepuka uzima yangu wa dunia.

Kweli, wakati alisikia nzuri na alipata ma nguvu yake, alirudia na roho yake yote kwa Mungu na aligeuza mawazo na uzima. Alijifunda mingi kwa ajili ya hii malipizo iliyemutuma Mungu, juu ya kuishi na toba na kutumika ya wokovu yake. Kisha aliishi miaka ya kuenea, alifurahi Mungu na alitoka nafsi yake toka mwili na alipumzika kwa mikono ya Mungu.

## 7. Mtu mutajiri Hrisaorios alijifanya uchezo ya ma shetani kwa saa ya lufu yake.

Anatwaambia Mtakatifu Grigorios wa Dialogos ya kama wakati moja aliishi mtu moja aliyeitwa Hrisaorios, mutajiri na mkubwa ya dunia ile wakati. Wala aliongeza mali, mafeza na ma nyumba yake, wala alitajiri na ma zambi ya mwili, ya upenda-feza, ya utukufu ya bure na ujivuno. Ilikua saa na alianguka na malari moja nguvu pa kitanda ya lufu. Alikuwa ma macho yake wazi na aliangalia kusimama mbele yake ma roho mbaya na makali kabisa na walimukokota mu mulango ya hadeze. Huyu alianza kutetemeka, kugeuza ragi ya uso yake na kujazwa na jashu mingi. Alilalamika bila kitumaini kujipatia saa kidogo juu ya kutubu. Kisha aliita na mtoto yake mukusema: «Ee Maksimos, mtoto yangu, kuja mbio kwangu na uniokoe na uwezo ya sala yako na imani yako».

Basi, alikuja mtoto yake karibu yake na wajerani wengine, lakini hawakuweze kuona ma roho mbya ya shetani, wenye walisirika na walitaka kuongoza Hrisaorios mu gehena. Walisikia hii jabo kwa ajili ya boka na ugeuzo ya ragi mu uso ya huyu mtu na kwani alipindula mwili yake pa kitanda. Saa ingine alipindula mwili yake mu fasi ya kushoto ya kitanda juu hapana kuona maroho mbaya ya shetani, lakini ma shetani walikuja mbele yake na walimuogopesha na wakati ingine alirudia mu fasi na kuume na mara ingine ma shetani walikuja mbele yake na walimuogopesha. Alipotesha kila kitumaini, kwa sababu hasikuweze kuokolewa, na kisha alianza kupaza sauti: «munipatia nyakati mpaka asubui. . . . . » na hivi nafsi yake ilitoka ya mwili yake bila kupata nyakati kutubu! ! !

Hii yote mambo ya matata aliiona Hrisaorios juu ya kusikia sisi na kutengeneza uzima yetu. Kwa sababu faida gani alipata huyu mtu, kwani aliona ma roho wa giza ya shetani na aliomba nyakati ya kutubu, lakini hakuna toba mu roho yake?

## 8. Yule Mutawa aliyezania maungo yake mufazili, alikwenda mu gehena.

Na hii jabo anatwaambia Mt. Grigorio wa Dialogos.

Mu mji Ikonio ya Azia Kidogo aliishi zamani mutawa moja ndani ya Monasteri moja, iliyeitwa wa Galatia. Huyu mutawa walimusadiki watawa wengine ya kama alikuwa mufazili na mufano nzuri na upole. Lakini, sawa vile, ilionyesha mwisho yake, huyu alikuwa mbali ya ma fazila mazuri na ya kweli. Nikusema alionekana ya kama aliishi kama mtakatifu na alikula chakula kidogo, lakini kwa siri alikula chakula kuliko mingi.

Siku moja alisikia ya kama mwisho ya uzima yake ikaribia. Aliita karibu yake wa ndugu ya Monasteri yake. Wa ndugu yake walikuja na wlaiongolea kusikia sauti moja kubwa toka kinywa yake, kwa sdababu walimuzania ya kama alikuwa mutawa mukubwa na mtakatifu. Ile saa yule na boka na tetemeko mingi aliwaambia:

Mulisadiki ya kama mimi nilikula kidogo, lakini kwa sisi nilikula mingi. Tazama sasa nilijitoa kwa joka mwenye matata kunikula. Huyu joka-shetani alifunga na mukila yake miguu na magoti yangu, na kichwa yangu ni ndani ya kinywa yake na pole-pole inatosha na nafsi yangu.

Wakati alisema hii ma sauti yake, alifariki, bila kupata nyakati uhuru juu ya kutubu.

## 9. Historia wa ajabu ya Mtume Thomas, wakati alihubiri mu inchi India.

Mtume Thomas, katika mapenzi ya Bwana Yesu Kristu, alijiuzisha kwa mtu ya biashara aliyeitwa Amvanis kama mutumwa na muyengaji mkubwa. Amvanis alipeleka mutumwa yake Thomas mu inchi yake India na alimuletea mbele ya mfalme ya inchi kama mukubwa muyengaji. Yule mfalme alimupokelea na alimupatia makuta mengi juu ya kumuyenga ma nyumba yake mapya.

Mtume ya Kristu, wakati alibeba makuta ya mfalme, aliwakaburia kwa watu wamaskini na wagonjwa na hasikuyenga ma nyumba yake.

Kisha wakati kidogo alituma mfalme wasaidizi yake kuangalia namna gani wanatembea ma nyumba yake mapya. Walikuja kule na, wakati waliona ya kama hata masingi hawakukuwa tayari, na tena, walisikia ya kama ma feza Thomas alikaburia kwa watu wenye malari na wamaskini, walisirika na walikwenda mbio kwa mfalme yao kumwambia hii mambo. Yule alihamuru kufunga Mtume na mikono yake mukongo na kumuletea mbele yake. Wakati alikuja mbele yake, alimuuliza na kisilani:

-Uliniyenga nyumba yangu?

-Ndivyo, alimujibu Thomas na upole na ni nzuri kabisa.

-Twende, basi, alimuwambia mfalme, twende kuiona na mimi.

-Ee mfalme, haina namna kuiona hii nyumba yako mu hii uzima. Kisha ondoko yako ya hii uzima, utaiona na utaifurahi na nafsi yako.

Ma sauti ya Mtume alisikia mfalme Gundaforos, kama matusi na uchekeleo. Na, kwa sababu alisikia ya kama huyu mtu (Thomas) alikuwa mtu masikini na hasikukuwa namna kumurudisha makuta yake, aliwaza ya kama paka lufu yake atamusimamisha kidogo kisilani na hasira yake. Kwa hivi alihamuru kumutosha ngozi yake na mwili yake muzima na kisha kumutupa pa moto.

Lakini Mungu Mwenyezi alifanya ninyi? Ndugu ya mfalme alisirika sana kupingana ya Mtume Thomas na alimwambia nguvu kwa mfalme ndugu yake kumulipiza. Lakini mara moja

alifariki na naziri ya kufa na Mtume Thomas ilisimamisha. Watu wote, basi, walitengeneza matendo juu ya maziko na Khirio ya ndugu ya mfalme.

Lakini, Mungu, ambaye asipende lufu ya mwenye zambi, alifanya na hapa muujiza yake wa ajabu. Wakati alifariki ndugu ya mfalme aliyeitwa Gadi, walikamata nafsi yake wa malaika na waliionyesha ma nyumba wa milele na wale watu waliokolewa toka zambi ao walitubu. Nafsi ya Gadi alishangaa kwa utukufu ya ile nyumba ya mbingu, iliyekuwa kuliko nzuri ya ma nyumba ingine na aliomba wa malaika, wasaidizi yake kumwacha kuikaa ndani ya chumba moja ya ile nyumba wa mbinguni. Lakini wa malaika hawakupokelea maombi yake mukusema ya kama hii nyumba ya paradizo iko ya ndugu yake mfalme Gundaforos na hii nyumba aliiyenga mtu moja mugeni aliyeitwa Thomas

Wakati alisikia hii sauti ya wa malaika Gadi, aliomba wa malaika wake juu ya kumwacha kurudia mu inchi mara ingine juu ya kuuza ile nyumba ya utukufu toka ndugu yake.

Basi, na mapenzi ya Mungu, alirudia nafsi ya Gadi kwa mwili yake juu ya kuokolewa hivi na Mtume Thomas toka lufu na watu mengi kusikia kuhubiri ya Mungu wa kweli na kuokolewa kwa ajili ya hii ufufuo ya Gadi.

Wakati wajerani walitayarisha maiti ya Gadi juu ya maziko, mara moja mwili yake ilianza kupumuzi. Watu wote walishangaa na walimwita mfalme, ndugu ya Gadi, ya kama ndugu yake alifufuka.

Wakati ndugu yake alifufuka alisema kwa ndugu yake:

-Ee Ndugu wangu, kama unanipenda, ninataka kuniuzisha hii nyumba nzuri iliyejenga mukristu Thomas mu mbingu.

Mfale, wakati alisikia hii ma sauti, aliangaziwa akili yake na nuru ya Roho Mtakatifu ya kama Thomas ni ya kweli Mtume ya Mungu na katika nuru ya roho yake alimwambia kwa ndugu yake:

-Ee Ndugu wangu, misiweze kuuzisha hii nyumba kwa sababu haina kazi teketeke ya kuiyenga. Ninazania kuliko nzuri ya kuonyesha nani eko muyengaji, mwenye anaishi tena, na yule kwa mapendo yako, atayenga nyumba moja kwako.

Mara moja alihamuru kumutosha Thomas toka kifungo na kumuletea mbele yake. wakati alikuja mbele yao Mtume, wale wa ndugu walipika magoti yao chini na waliomba hurumia kwa sababu bila kujua, walifanya matendo mbaya kwake. Walimuomba kuhubiri Mungu wa kweli na ma fundisho Yake, juu ya watu wote kupata ma furaha ya milele, kama wataenda mu paradizo na kuangalia bile ma nyumba aliona na Gadi.

Mtume ya Mungu Thomas alisikia hii ma sauti yao na ajabu na alishukuru ya roho yake chini kabisa Mungu juu ya ile matendo yake ya ajabu na maangalizo yake. Mara moja aliwafundisha na aliwabatiza watu wote na ma taifa ingine mengi aliwabatiza kwa Jina ya Baba na ya Mwana na ya Roho Mutakatifu.

## 10. Sasa pahali ilianguka jua, ulikumbuka Mungu? . . . . .

Wakati moja, mutawa moja ya jangwa alitoka ya jangwa na alikwenda mu muji moja juu ya kuuzisha ma bintu yake. Aliikaa inje ya mulango ya nyumba moja, pahali ndani mtu mutajiri, mkubwa ya ile nyumba, ile saa alikuwa karibu ku mwisho ya uzima yake. Ile saa huyu mutawa aliona kufika pa punda yao watu wenye makali kabisa na walikamata pa mikono yao ma goma. Waliacha ma nyama ya punda yao inje na waliingia ndani. Wakati aliwaona yule mugonjwa, alianza kupaza sauti na malalamiko kusema: «Ee Bwana unihurumie na unisaidie». Ile saa wale waliyekuja walimuuliza: «Sasa, pahali ilianguka jua, ulikumbuka Mungu? . . . Juu ya ninyi, wakati ilikuwa muchana usikumutafuta? Sasa hakuna kwako kitumaini ya wokovu, wala utulivu. Na mara moja walitosha mbio nafsi ya mwili yake na waliondoka.

## 11. «Mutosheni huyu mbali ya hapa. . . »

Mutawa moja aliyeishi mu jangwa alitwaambia hii Historia: «Ndugu moja alitakia kufanyika mutawa juu ya kuokoa nafsi yake, lakini mama yake alimuzibiria. lakini, kisha maombi mingi, alimwacha na huyu aliondoka. Alifanyika mutawa, lakini alipita uzima yake na uzaifu na uvivu. Ile wakati alifariki na mama yake.

Kisha miaka ya kuenea, alipata malari na huyu ndugu na ilifika karibu ya lufu yake. Mara moja nafsi yake iliachanwa toka mwili yake na ilipanda mbinguni juu ya kuhukumwa. Katikati ya wale walikuwa mu gehena alikuwa na mama yake, aliyemwambia: «Na weye, mtoto yangu, ulihukumwa mu makao ya wenye gehena? Iko wapi ma neno yako, ile uliniambia ya kama: «Uniacha mama yangu kuokoa nafsi yangu? ». Yule alisimama na haya na taabu mu roho yake kwa ajili ya hii sauti ya mama yake, bila kujibu kwa mama yake. Kisha alisikia sauti moja alimwambia: «Mutosheni huyu mbali ya hapa. . ». Mara moja ile saa alisikia ya kama aliona maono. Alisimama na aliambia kwa watu wengine aliona ninyi. Alitukuza Mungu, ambaye anakombana na namna mingi juu ya kuongoza vyumbe vyake kwa wokovu.

Wakati alikuwa nzuri sana mu afya yake, alifungwa mu chumba yake na machozi mingi aliomba kwa Mungu kumusamehe na alikangamana kupata wokovu yake. Umivu juu ya makosa yake ilikuwa hata mingi, na wa ndugu wengine walimwambia kusimamisha hii muchoko na sala kidogo, juu hapana kuharabisha afya yake. Lakini yule aliwaambia: «Kama misikuweze kuvumilia ma sauti ya mama yangu, namna gani nitavumilia haya ile siku ya Uhukumu mbele ya Kristu, wa malaika  na Ulimwengu mzima?

## 12. Njia nani nitachakula mu uzima yangu?

Mutawa moja wa jangwa alisema hi Historia:

«Wakati moja aliishi mutawa moja mwanamuke, aliyepanda juu mu  fazila ya Kristu na utawa. Wakati nilimuuliza, juu ya maneno gani aliondoka toka dunia juu ya kuwa mutawa, huyu aliniambia historia ya uzima yake:

«Wakati nilikuwa mtoto mdogo, ninakumbuka ya kama baba yangu alikuwa mtu mzuri na mupole. Alitumika ma shamba yetu, alileta mu nyumba yetu matunda kwa muchoko yake. Alisuburia kidogo na ninyi wote waliyemufamia, walizania ya kama alikuwa bubu.

Uzima ya mama yangu ilikuwa ya kuachana kabisa. Alipenda kusimanga ma kazi na watu wengine, kusimanga na kujulisha ma tangazo  watu wengine. Alisema ma sauti mengi, hata mingi na watu hawakumuona kuishi hata siku moja na kinywa yake ya kuifungwa. Wakati ingine alikombana na watu na wakati ingine alisema ma sauti mbaya ya zambi na bila upole na haya. Wakati mingi kabisa ya uzima yake alipitisha ya kulewa na kuishi pamoja na wanaume wenye zambi. Aliharabisha makuta ya baba yangu yote. Alifanya uzima moja ya zambi, lakini mu uzima yake yote hasikupata hata malari moja, wala kusikia umivu moja; Mwili yake ilifuraha na ilikuwa na afya nguvu.

Ilikuja wakati na baba yangu alifariki, kisha malari mengi ya kuachana na wakati mingi. Lakini jabo ya matata nani ilikuwa ile siku alikufa baba yangu? Ilisimamishwa pepo moja nguvu, na umeme na kogoloma nguvu sawa dunia nzima ilitetemeka. Ilianza kunyesha nvula mingi na sisi tusikuweze kutoka inje ya nyumba yetu. Vile ya ma siku tatu tulikwa na maiti ya baba yetu ndani ya nyumba yetu bila kuimazika. Watu ya mukini yangu, wakati waliona hii mambo, walianza kushitaki bnaba yangu na walisema hivi: «Ole, Ole kwake! Mambo kimbaya ilikuja katikati yetu na sisi bado kuisikia! Huyu mtu alikuwa adui mkubwa ya Mungu na joo vile Mungu anakataa kutuwacha ya kumazika maiti yake.

Lakini sisi, mbele ya kuanza kuoza maiti yake, tulikamata mpango ndani ya nvula mingi kutembea pamoja na maiti na tulifika mu fasi ya maziko. Na kule tulimumazika.

Kisha lufu ya baba yangu, mama yangu alikuwa na uhuru mingi na alitembea mu fasi pahali alipenda na kuishi uzima ya zambi. Alipotesha hata mingi haya ya uzima yake, mpaka alifanya nyumba yetu nyumba ya zambi katika mwili na aliharabisha mali na uriti yetu yote. Ilikuja wakati na alikufa na yeye bila toba juu ya ma zambi na makosa yake. Wa jerani yangu walimufanysia Khirio nzuri katika utukufu, mataji mingi na muchezo na watu mengi. Tena na ile muchana ilikuwa nzuri na kivukutu mingi.

Kisha lufu ya mama yangu, mimi nilikuwa na kipimo miaka kumi na tano. Usiku moja ilikuja ndani ya akili yangu uwazo mija: Njia nani nitachakula mu uzima yangu? Nitachakula maisha ya baba yangu na nitaisha na uzima ubikira, upole na wema? Lakini huyu, aliishi na ma fazila ya Kristu, lakini hapa hasikufurahi hata furaha moja ya hii dunia. Walimuteswa magonjwa mengi, na watu walimuzarau mupaka maziko yake! Kama uzima yake ilikuwa nzuri mbele ya Mungu, juu ya ninyi alipima mateso mengi? Nani ilikuwa maisha ya mama yangu? Aliishi na afya nguvu, lakini alifanya zambi ya mwili na wanaume wengine, lakini afya yake ilikuwa nguvu sana mpaka mwisho yake. Basi, na mimi nitafata hii uzima yake. Kwani ni kuliko nzuri kusadiki kwa macho yangu, na hapana kusadiki ma sauti ya watu wengine.

Vile nilikamata naziri na nililarisha kupumzika. Usiku alikuja kwa ndoto yangu mtu moja murefu na mkubwa sana. Uso yake ilikuwa ukali sana na aliniuliza na gazabu: «Nani iko uwazo ya roho yako?» Mimi niliogopa sana na wala uso yangu misikuweza kupindula juu ya kumuona. Lakini yule aliniangalia na aliniuliza mara ingine:

-Uniambie, basi, unakamata naziri nani?

-Wakati aliona kulekea kwa ajili ya boka yangu na kupata hatari kuwa mazimu, alinikumbuka huyu mumoja ile mawazo usiku nilifanya, mbele ya usingizi yangu.

Mimi, wakati nilisikia kidogo nzuri kwa ajili ya boka mingi, misikuweze kukataa, ninyi ma sauti yote aliniambia na nilianza kuomba hurumia na usamehe.

Yule alikuwa sasa kidogo mupole, alinibeba na mukono yangu na a liniambia:

-Kuja kuangalia eko wapi baba yako na mama yako na kisha chakula weye wa pekee njia nani unataka kufata mu uzima yako.

Basi, wakati alinitosha ya ile makao nilikuwa, aliniongoza ndani shamba moja nzuri sana, pahali walikuwa miti na matunda iliyejaza na kuachana, lakini hakuna namna kusema na ulimi yangu. Nilitembea na muongozi yangu na mara moja alinikutana baba yangu, alinibatia. Alinibusu utamu na alinisema: Mtoto wangu mupendwa.

Mimi ile saa nilimubatia na nilimuomba kumbakia karibu yake. Ile saa yeye alinisema na utamu na mapendo:

-Sasa, mtoto yangu, hakuna namna kumbakia hapa. Lakini, kama unataka kufata namna ua uzima yangu, haitapita wakati minmgi na weye utakuja karibu yangu.

Mimi nilimuwambia kunichunga karibu yake, lakini malaika aliyenisidikiza, alinikokota ya mukono yangu mukusema:

-Kuja, sasa kuangalia na mama yako juu ya kujulishwa ya hii matendo ya matata, njia nani iko lazima kuichakula.

Aliniongoza mu makao moja katika giza, pahali walisikiwa maombolezo, malalamiko na makelele. Kule alinionyesha tanuru moja ya kuwakisha, pahali pempeni yake walisimama watu wenye mbaya na wenye matata kwa uso yao.

Wakati niliangalia ile makao ya matata, ninaona na mama yangu kuwa ya kulobekwa ndani ya ile kisima ya moto mpaka sigo yake na mabilulu mengi walimukula ma fasi yote pempeni yake. Kwa ajili na umivu na matata alitetemeka, lakini meno yake walipigwa na mwili yake muzima ilitetemekwa. Wakati alilamuka ma macho yake na aliniona, alianza kuria na maombolezo na malalamiko mingi na aliniambia: «Ole kwangu, mtoto yangu! Maumivu yangu misiweze kuivumilia na mateso yangu ni bila mwisho! Ole kwangu, mwenye zambi ma mwenye taabu. Kwa ajili ya furaha kidogo ya usharati, angalia sasa mateso ngapi nilipata na malipizo ya

matata kabisa. Kwa mafuraha ya dunia, sasa ninateswa kwa milele. Mtoto wangu, hurumia mama yako, ambaye, sawa vile unaniona, ninajilugua ya moto na ninalekea sana. Kumbuka, mtoto yangu, ile wakati nilikunyonya na nilikukomea. Unipe mukono yako na unitosha ya hapa ndani. Misiweze kuvumilia saa ingine».

Mimi misikuweze kuwaza nitafanya ninyi na misikuweze kukaribia mama yangu, kwani walikuwa karibu wale wenye makali ma shetani. Lakini huyu mama yangu aliniambia na machozi mingi:

-Mtoto yangu, unisaidia, usizarau mataabu na malalamiko ya mama yako. Usinizarau mimi mwenye taabu, ambaye anateswa kabisa ndani ya gehena na anajikula daima ya bilulu isiyokulala.

-Mimi ile saa, kwa ajili ya wema, nilifungula mkono yangu juu ya kumutosha toka hii gehena, lakini, wakati ulimi ya moto iligusha mukono yangu, niliuma sana na nilianza kupaza sauti na kuria na maombolezo. Kwa ajili ya maombolezo yangu walilamuka ninyi wote walilala nyumbani, na walikuja mbio ku kitanda yangu na waliniuliza juu ya ninyi niliria na niliomboleza. Ile saa, mimi, wakati nilisikia kidogo nzuri, nilianza kuwaambia maono yangu. Tangu ile saa nilikamata naziri, bila shaka, kuishi sawa vile aliishi na baba yangu. Ninatakia Mungu anistahili kupata upatanisho pamoja na baba yangu juu ya kuishi pamoja na neema ya Mungu, kwa sababu bile matendo ya milele walinijulisha matukufu ngapi na ma sifu walitayarishwa kwa wale watu walichakula utawa na fazila na, kupindua, ma ngapi malipizo na ma gehena mingi wanaongojea ninyi wote wanaharabisha uzima yao mu zambi na ma furaha ya usharati.

## 13. Lufu ya Mtakatifu Mutawa Benediktos.

Anatuwambia Mt. Grigorio wa Dialogos, ya kama mu jira, pahali ilikuja juu ya kutoka ya hii uzima mt. Mutawa Benediktos, yeye alijua ya mbele siku na lufu yake katika Neema ya Mungu na alijulisha wanafunzi wake yote na wa ndugu yake kuwa karibu yake ile saa. Tena aliwaambia ya kama, kwa ile siku ya lufu yake, itajifanya na muujiza moja juu ya kujulishwa watu wote ya kama nafsi yake inatoka ya mwili yake.

Ma siku sita, mbele ya lufu yake, alihamuru wanafunzi wake kuchibula kaburi yake. Mara moja ile saa ilianguka pa kitanda na kivukutu mingi pa mwili yake ya ma siku sita. Siku ya sita alihamuru wanafunzi wake kumusimamisha na kumupeleka mu kanisa.

Wakati kule na saidio ya wanafunzi wake, alipewa Mwili na Damu ya Kristu, alinyanyua mikono yake yulu mbinguni na aliomba na mapendo mingi kwa Mungu. Ile saa alitoa na nafsi yake kwa mikono Yake.

Ile saa wa ndugu wa wili, moja aliikaa mu chumba yake, lakini mwingine aliikaa kidogo mbali waliona waote wa wilipamoja maono umoja. Waliona kila mumoja ya kuachana njia moja iliyeongoza mu chumba ya Mutakatifu Benediktos; na hii njia ilitoka ya mashariki mupaka mbinguni. Hii njia ilikuwa na chini manguo matukufu sana. Kwa hii njia walipanda na wanaume watukufu na wenye nuru, wenye walikamata na ma taa ya kuwakisha kwa mikono yao na walitembea na upole. Mara moja ndani ya hii picha ya maono alionekana na mwanaume moja mwenye kuvaa manguo meupe, aliyeangazwa. Alisimama karibu ya wengine na walitembea pamoja ile njia. Aliwauliza:

Munajua, basi, ya mtu nani, hii njia munaiona iko chini yake manguo wa mwangaza na matukufu na mweye munaona hii njia na ajabu?

-Hapana, hatujue, walijibu wale wa kijana.

-Huu njia ni njia pahali alitembea mupendwa ya Mungu Benediktos na atapanda mbinguni.

Wakati walisikia hii mambo wa wili, kisha hii maono wa ajabu, walisikia ya kama ilikuwa ujulisho juu ya lufu ya Mutawa Benediktos.

## 14. Alisema ninyi mfupa ya kichwa ya yule mtu mwenye pagano aliyekufa kwa Mutawa Makarios.

Mutawa Makarios wa Misiri alijulisha kwa wanafunzi wake hii hadisi: «Wakati moja zamani, nilitembea mu jangwa na nilipata mfupa ya kichwa ya mtu moja chini ya inchi. Niliitega kidogo na bakora yangu na nilishangaa, wakati nilisikia sauti ya huu kichwa:

-Juu ya ninyi unanipiga na bakora yako? Zamani nilikuwa na mimi mtu na nilitembea sawa vile weye.

-Nani uko weye?

-Mimi nilikuwa askofu ya ma sanamu na wale watu wenye pagano, wenye walimbakai zamani hapa. Weye uko Makarios mubebaji ya Mungu; sikia, basi, ya kama kila saa utaomba juu ya wenye kuwa mu gehena, wanasikia kidogo utulivu.

-Utulivu ninyi na gehena ninyi wanasikia wale watu ni kule chini?

- Hata urefu ni mbingu toka inchi yetu, hata chini ni moto inayeiko chini yetu; ndani ya hii moto sisi tunasimama na tuko ndani kabisa. Tuko vile ya kusimama moja nikusema mtu hasiweze kuona uso ya mwenzake, lakini paka mbavu yake. Basi, wakati weye unaomba kwa ajili ya mapendo yetu, sisi hapa tunasikia kidogo utulivu.

-Utulivu ninyi munasikia, kama sisi tunaomba kwa Mungu?

-Tunaweza mtu moja kuona uso ya mwenzake na hii maangalio inatupatia kidogo utulivu.

Wakati alisikia hii ma sauti padri Makarios, aliomboleza chini ya roho yake na alisema: Ole, ole, taabu na sikitiko ngapi ilileta kwa kila mtu ile siku ya uzalio yake! Ilikuwa kuliko nzuri hapana kuzaliwa mtu, sawa vile alisema na Bwana Yesu juu ya Yuda mutoaji yake. Kisha hii mazungumuzo aliuliza mara ingine mfupa ya kichwa ya yule askofu pagano:

-Mu gehena ni na mateso ingine kupita nguvu ya matata?

-Chini yetu iko gehena ingine kuliko kibaya na matata sana.

-Na wa nani wanateswa kule? Alimuuliza Mpadri mkubwa Makarios.

-Sisi, hata kidogo, tunajirehema ya Mungu, kwani tusikumufamia mu uzima yetu. Lakini wale walimufamia nzuri Mungu na kisha walimukana, ni chini yetu na wanateswa kuliko mbaya ya sisi.

Wakati aliisha hii zungumuzo, mpadri mukubwa alikamata mfupa ya hii kichwa na alizibiria ndani ya bulongo.

Wa ndugu wapenzi wangu, hii hadisi inapaswa kuisikia nzuri, kwa sababu hawa wanakana Mungu, kisha wanatwswa kuliko mingi ya wenye pagano mu gehena. Basi, inapaswa kusopoka tusiepuka ya Kanisa yetu ya kweli, Kanisa Orthodokse na tusikana MUngu wetu katika matendo yetu wa giza. Anakana Mungu hapana paka huyu anayemukana na ma neno yake, lakini na yule anayefanya matendo ya zambi na anasadiki kwa Mungu paka ya bure, bila faida ya roho yake, kwani anakataa kutubu.

Mushuhuda ya hii ma sauti yangu ni Mtume Paulo, anayetuwaambia: «Wanakiri ya kwamba wanajua Mungu, lakini kwa matendo yao wanamukataa; » (Kwa Tito 1, 16).

## 15. Mtakatifu Antonio alipanda mbinguni kwa akili yake.

Wakati moja, Mt. Antonio alilamuka kufanya sala na kukula, katika saa ya zwezo yake, kwani ilikuja saa ya tatu magaribi. Lakini ile alipanda yulu pa pepo nafsi yake, pahali walionekana wa shetani wenye giza na wakali, wenye walimuzibiria kupanda kupita yulu.

Wafwasi ya nafsi yake walianza kukelele pamoja na ma shetani, wenye waliomba jibu ya hiinafsi, nikusema kama ekona deni moja ya zambi mbele yao. Wa malaika waliwaambia ya kama, ninyi wote makosa aliifanya Antonios toka uzalio yake, Bwana Kristu aliizimisha daima. Lakini tangu ile wakati alijifanya Mutawa na alitoa maungo yake kwa Mungu, muweze kuhamakia matendo yake.

Wa shetani walimushitaki Antonios, lakini hawakuweze kuonyesha kweli ma sauti yao ya uwongo, na hivi njia yake ilikuwa uhuru, bila mazibirio. Ile wakati Antonios aliona maungo yake kurudia ku mwili yake na alikuwa sawa vile alikuwa mbele.

Lakini tetemeko yake ilikuwa hara mingi, na alisahabu kukula ile sikui na alimbakia ile siku na usiku ya kuomba kwa Mungu na maombolezo. Alishangaa, wakati aliwaza majaribu ma ngapi tukona kukombana na machoko ma ngapi inapaswa kutabuka ma roho mbaya ya pepo. Kwa hivi alishauria kuvaa sisi nguvu ya Mungu, sawa vile anatwaambia Mtume Paulo: «Kwa hivi twaeni silaha zote za Mungu, mupate kuweza kushindana katika siku ya uovu, na mukikwisha kutimiza yote, kusimama» (Wa Efeso 6, 13).

Kisha hii maono walimutembelea watu wengine na walianza kusuburia juu ya matokeo ya nafsi toka mwili yake na makao ni nani, pahali itakwenda. Usiku ingine alisikia sauti moja kumuita:

-Ee Antonie, lamuka, toka inje ya chumba yako na ona.

-Kweli, Mutawa Antonios alitoka inje, alinyanyua richo yake yulu mbinguni na aliona hii maono.

Mtu moja mwenye matata sana kwa uso yake na murefu kabisa, kwani urefu yake ilifika mupaka mawingu, alisimama, lakini wengine, sawa walikuwa mabawa waliluka pempeni na mbele yake. Yule alifungula mikono yake na alizibiria wengine ya kuluka, lakini wengine waliweza kupita na kuluka kupita juu na waliendelea njia yao, bila mazibirio.

Huyu shetani mkubwa alipiga meno yake, kwa sababu ma nafsi ingine walipita na huyu hasikuweze kuwakamata na kuwangusha chini.

Mara moja ilisikiwa sauti moja:

-Ee Antonie, fanya nguvu kusikia hii maono onaiona sasa. Mara moja ilisafisha akili yake na alisikia ya kama hii maono aliiona ilikuwa mapito ya ma nafsi kwa mbingu na ya kama yule mtu makali na murefu kabisa, alikuwa shetani, anayechukia waminifu. Ninyi ya wale waminifu walifanya zambi, bila kutubu, huyu shetani anawababamba na anawazibiria ya kupita yulu; ninyi wote, lakini, hawakupokea ma shauria yake, hasiweze kuwazibiria, na kwa hivi wanaluka yulu yake na wanatembea mbinguni.

Wakati Mt. Antonios aliona hii maono, alikumbuka na ingine ya mbele na alishindana kila siku kuendelea ku mbele mu uzima wa fazila ya Kristu.

## 16. Miaka tatu mugonjwa ao ma saa tatu mu gehena?

Mu Skiti (Mukini) ya Mtakatifu Andreas ya muji Karies ya Kilima Takatifu, inayeitwa na Serayo, ku mwanzo ya hii miaka mia makumi mbili, ilijifanya hii jabo:

Mutawa moja aliyekuwa toka Rusia na aliishi mu Kilima Takatifu, aligonjwa sana na alikuwa na maumivi mingi pa kitanda; aliomba Mungu kumuponyesha. Ile saa alikuja mbele yake malaika moja ya Mungu na alimuwambia:

-Unachakula ninyi? Kumbakia miaka tatu pa hii kitanda na mateso kwa ajili ya hii malari yako ao unataka kumbakia ma saa tatu mu gehena na kisha utatunzwa?

-Huyu mugonjwa, aliwaza mbele mingi, na kisha alimujibu: Ninachakula ma saa tatu kwenda ndani ya gehena.

Malaika, basi, alimubeba na alimuletea na nafsi yake mu gehena. Alikuja, basi, ndani ya mateso matata, pahali wenye zambi na wasipokutubu waliteswa sana, bila kuweza kuomba ya fasi

fulani saidio. Pamoja nao aliteswa na mutawa huyu, aliye omba saidio takatifu na utembeleo ya malaika. Basi, Mungu alituma malaika yake na alimuuliza:

-Ee padri, ukona mambo gani na unaniita? Sisi tulifanya sikilizano kuikaa ndani ya gehena ma saa tatu.

-Walipita mpaka sasa miaka tatu mia na kupita ndani ya hii mateso matata na sasa ilikuja waakti ya kunitosha ya hapa.

-Ee ndugu, bado kupita wala saa kipande na namna gani unasema weye ya kama walipita miaka 300?

-Ninakuomba, alimuwambia mutawa kwa Malaika, unipeleke pa kitanda ya umivu yangu miaka tatu na hapana kuteswa hapa ma saa tatu.

Kweli malaika alimupeleka mara ingine mu dunia na, wakati alimbakia pa kitanda yake mugonjwa nyakati kidogo tena, alimubeba na alimupumzika mu Ufalme ya mbingu.

## 17. Namna gani kijana moja alitosha mama yake toka gehena.

Askofu ya muji Kiru Theodoritos aliandika mu kitabu yake ya kama alimutembelea siku moja ndugumoja aliyekuja toka mbali, Alimukaribisha na alimupatia kukula. Huyu, wakati alianza kula, alitumia paka mukono ya kushoto yake, lakini mkono ya kuume alikuwa na yo ya kufunga na nguo moja. Askofu alimuuliza, juu ya ninyi ekona hivi mukono yake ya kufunga na nguo na yule alikataa kumjibu. Askofu na namna upole alikokota kidogo ile nguo iliyefunga mukono yake na ilitoka harufu kibaya ya kuoza sana; nma hii harufu kibaya ilijaza nyumba ya askofu nzima. Alimuuliza mara ingine juu ya ninyi inatosha harufu kibaya mukono yake, na ile saa huyu mugeni alimuelejea hivi:

-Mimi, Mweshimiwa, nilikuwa mama muzuri mu uso yake kabisa, lakini alikufa baba yangu na huyu alimbakia mbalaka, bila bwana tangu kipimo ujana yake na mimi ile mwaka nilikuwa mtoto mudogo. Kwa sababu tulikwa watu wamaskini, mama yangu alifata uzima ya zambi na usharati na ile makuta alibeba ya hii kazi yake, kama mwanamuke ya zambi, tuliishi mu uzima yetu. wakati nilifika mu kipimo ya ujana, alikufa mama yangu na aliniacha makuta mengi. Mimi, kwa sababu nilisikia ya kama hii maisha ni ya bure, mali na mafuraha na utukufu ya hii dunia ya ya bure, nilikabula makuta ile kwa maskini na wenye malari na ma kanisa na nilitoka mu jangwa, pahali niliomba kwa Munmgu kupata wokovu yangu, wokovu ya wazazi na watu wote ya dunia.

Niliomba kwa Mungu daima kunijulisha, kama alipokelea mafeza iliyekaburia kwa saidio ya mama yangu kama huruma ao kila tendo nilifanya, ilijifanya ya bure?

Nilienda mu Yerusalema na nilitangaza hii yote kwa Patriarhi. Yule aliniambia:

-Mtoto yangu, ulifanya nzuri na ulikaburia bile bintu na mali juu ya saidio ya wazazi yako. Lakini juu ya mama yako alikwenda wapi, kisha lufu yake, hakuna hapa mtu moja mumebaji ya Mungu juu ya kutujulisha mama yako alikwenda wapi.

Mimi nilibeba baraka yake na niliondoka kwa Skiti-Mukini ya Thivaida ya Misiri. Kule, kweli nilitafuta wa padri ya jangwa watakatifu, wenye waliniambia ya kama eko mtu moja wa jangwa na kwake inapaswa kwenda. Na baraka yao niliondoka juu ya kumukutana ndani ya jangwa. Nilitembea na miguu ma siku 30. Kisha upatanisho na ufamio yetu, mimi nilimwambia uwazo ya ufikisho uangu kwake na yule, mbele alinitulivu, na aliniambia na unyenyekevu mingi:

-Mtoto wangu, hii tendo uliyeniomba ni kubwa sana. Lakini kwa muchoko uliyefanya kuja mpaka hapa, tutaomba pamoja mbele ya Munfu juu ya kupata tatanuo ya ulizo yako na kupata ujulisho ilikwenda wapi nafsi ya mama yako.

Alitoka huyu mumoja inje na bakora yake alifanya muviringo moja chini ya inchi na aliniambia:

-Hapa ndani ya hii muviringo utasimama weye ma siku saba na usiku. Usitakula hata kintu kimoja, wala utaikaa na utaomba Mungu na machozi. Hii kazi umoja nitafanya na mimi ndani ya pango-chumba yangu na Bwana Mungu Mwema atafanya mapenzi yake.

Wakati ilifika usiku ya saba, akili yangu ilipanda mbinguni na niliona mu fasi ya kushoto kizipa moja mnene ya kujaza machafu, matope ya uchafu na arufu kibaya. Ndani ya hii kizipa niliona ma kichwa, mikono na miguu na waliyepanda na walishusha, sawa vile anafanya maji, wakati inajipika. Wakati hii uchafu ya kizipa inajipika na ilipanda na ilishusha, mara moja niliona na mama yangu, mwenye alinifamia na alianza kuniita na malalamiko:

-Mtoto yangu, mtoto mupendwa wangu, unisaidia na uniokoe. Na, wakati alisema hii ma sauti yake, hii matope ya uchafu alimuzibiria mara moja. Mara ya mbili ilimupanda matope ya uchafu mpaka kilari yake na huyu mama yangu alipata saa kuniomba mara ingine: «Mtoto mupendwa wangu, unisaidie! . . . na hii matope uchafu ilimupanda mara ya tatu na huyu aliniambia: «Uniwema mtoto wangu, usiniache ndani ya hii uchafu na mateso ya gehena wa milele».

Ile saa mimi, kwani nilikuwa na umivu mingi juu ya mateso ya mama yangu, nilifungula mukono yangu na nilimukamata na ma nywele yake. Wakati huyu alikwenda kujilobeka mara ingine, nililobeka na mimi mukono yangu ndani ya uchafu na nguvu mingi nilimutosha inje ya ile kizipa. Ile saa niliona mu fasi ya kuume yangu sahani moja mnene, pahli ilikuwa maji safi. Nilimunawa ndani na nilimuweka kusimama katikati ya wakijana wenye kuvaa ma nguo meupe, na wenye walisimama pempeni yangu.

Mama yangu alishukuru na machozi mingi Bwana ya Utukufu na alibusu na heshima wale wa malaika wenye mwangaza. Tena alishukuru na mimi.

Asubui, wakati ilikuja mchana, alikuja mutawa wa jangwa na aliniuliza:

-Ee ndugu, hii usiku uliona maono moja kwa sala yako?

-Padri mtakatifu, niliona maono moja ya ajabu kabisa na misitaweza kuisahabu mu uzima yangu yote.

Nilimwambia yoyote matendo ile niliona. Ile saa yule alinikikiri ya kama aliona na huyu hii maono umoja na alimushukuru Mungu na Mwokozi wetu na machozi mingi kwa ajili ya wema mingi Yake, kwani aliacha kutoka nafsi moja toka gehena mu Paradizo. Mukono yangu, lakini, ile niliweka ndani na ile kizipa juu ya kukokota mama yangu, ilichunga hii harufu kibaya na nilimuuliza mpadri:

-Mpadri mweshimiwa, ninakuomba nguvu, fanya sala kwa Mungu juu ya kufukuza hii harufu kibaya inatoka ya mukono yangu. na yule aminisema:

-Usisikitike juu ya hii mambo, mtoto yangu. Vile Mungu alipenda kumbakia hii alama bila kutoka juu ya kusadiki na wenye wanakataa Mungu, wavivu na wazaifu watu, kwani hawa wanashaka ya kama ni mateso ya gehena na bintu mazuri mu paradizo.

-Iko vile, mpadri mweshimiwe, lakini misiweze kuvumilia hii harufu kibaya, wala watu wenye wananikaribia hawaweze kuvumilia. Ile saa huyu mpadri mtakatifu alikata kipande moja ya nguo meushi yake, alifunga mukono yango na aliniambia ya kama itambakia vile mpaka mwisho ya uzima yangu.

Ee ndugu, kwa sababu ulichoka kukuja mpaka hapa, nitaomba kwa Mungu juu ya kusaidiaya kurudia nzuri. Na, wakati alisema hivi, ilipuliza pepo nguvu na mawingu moja ilifika karibu yake na alimwambia:

Kwa jina ya Bwana wetu Yesu Kristu, kamata huyu ndugu na utamupeleka mu makao yake na kule atatangaza kwa watu wengine mtendo wa ajabu ya Mungu na rehema yake kubwa.

Wakati aliisha hii ma sauti yake huyu mpadri, mawingo moja alinibeba, alininyanyua pa pepona, sawa vile alipeleka wa Mitume mu Getesimani juu ya Khirio ya Mzazi-Mungu, vile alileta na mimi inje ya nyumba yangu, iliyekuwa karibu ya Konstantinopoli.

Hii, askofu Mtakatifu, ilikuwa historia ya mukono yangu na sababu gani nilimufunga na hii nguo ya mpadri yule ya jangwa.

## 18. Zambi ya kutosha mimba kwa mapenzi ni matata sana.

Hii maono aliona Mutawa padri Paisios toka Kilima Takatifu, aliyekufa mu mwaka 1994. Tazama alitwaambia ninyi:

«Hii mwaka 1984, siku mukazi mbili, kisha mu Juma ya ufufuo ya Kristu, saa 12 kati ya usiku ya mwezi ya Ine (Aprilie), niliona maono moja ya matata sana! NImekwakisha ma taa mbili, wakati nilifanya sala juu ya wale ma nafsi wanateswa ao mu hii dunia ao mu gehena, niliona maono moja.

Niliona shaba moja iliyeota ngano, lakini ngano bado kukauka kamili. Mimi nilikuwa inje ya kikabashi ya ile shamba pahali walikuwa ndani hawa watu wenye kufa.

Mu fasi ya kushoto ya ile kibabashi, ilikuwa kiwanja moja, iliyekuwa fasi kibaya na bila kuwa kurima. Hii fasi ilijitetemeka toka sauti moja nguvu kabisa. Hii sauti ilikuja toka ma kinywa na malalamiko ya ma elfu. Kila mtu, kama alisikia hii malalamiko yao, iko namna kutetemeka kwa boka na sikitiko na taabu.

Niliteswa toka hii malalamiko yao, lakini misikuweze kuelejea maono. Mara moja nilisikia sauti moja kusema: «Hii shamba na ngano ya kukomea nzuri ni fasi ya wale watu wenye kufa na watafufuka. Lakini ile makao inayetetemeka toka malalamiko mingi ni fasi, pahali wanateswa wale watoto waliwatosha wa mama yao na mapenzi yao.

Wakati nilirudia kwa maungo yangu toka hii maono, misikuweze kupata kimya kwa ajili ya umivu mingi. Misikuweze hata kupumzika kidogo, kwani nilikuwa muchoko mingi toka siku ya jana.

## 19. Ma ulimi yote ya dunia nzima hawakuweze kutangaza mateso ya gehena.

Kitabu moja, inayeitwa Gerondikon, nikusema historia ya watawa, inatwaambia ya kama wakati fulani walikuwa wa ndugu wa wili, wenye walikuwa na mpadri ya roho moja, aliyewashauria juu ya mateso ya gehena mara mengi. Ndugu moja katikati wa wili alisikia na aliogopa, wakati alisikia hii mateso ya gehena na juu ya kuokolewa alikamata naziri kufanyika mutawa. Ndugu yake mwingine, kwani hasikusadiki hii ma tangazo juu ya mateso mu gehena, alimbakia ndani ya dunia mukufanya ma zambi mengi ya kuachana. Kisha miaka madogo ilikaribia mwisho ya uzima yake. Basi, ndugu yake, aliyekuwa mutawa, alimuwambia kwa ndugu yake, kama atakufa, kisha lufu yake, kukuja kwa ndugu mutawa kumwambia namna gani iko hali mu uzima ingine na kama kweli ni mateso, sawa vile aliwaambia mpadri ya roho yao ya zamani.

Kisha wakati fulani, usiku moja, aliisha kufa ndugu yake aliyekuwa mu ndunia, alikuja kwa ndugu yake mutawa kwa ndoto yake. Ile saa mutawa ndugu yake alimuuliza:

-Ninakuomba, ndugu wangu, uniambie kweli, mu Hadeze ni ya kweli mateso, ile wanatwaambia ma kitabu ya Kanisa yetu na alitwaambia na mpadri ya roho yetu ao waliandikwa juu ya kuogopa watu ya dunia?

-Ile saa ndugu yake alimujibu: Mateso ya Hadeze ni kuliko matata mingi na hakuna ulimi ya watu juu ya kuweza kuandika matata na mateso yao.

-Mutawa, ndugu yake alimuuliza mara ingine: Iko namna kupima na mimi hata kidogo toka ile mateso ya Hadeze juu ya kusadiki kuliko nguvu?

-Ndugu yake alimujibu: Na mahasa nani unataka kuipima?

Na Mutawa alimujibu: Mimi ni mtu mudogo kwa nguvu ya nafsi yangu na ninaogopa ya kama nitakufa, kama nitaangalia ao nitasikia na mikono yangu; kwa hivi, kama iko namna, kununka hata kidogo.

Ile saa ndugu yake, aliyeisha kufa zamani, alimupatia kidogo nguo yake na ilitoka arufu kibaya sana, hata mingi na watawa ya ile Monasteri yake hawakuweze kuvumilia na mengi walikimbia kama wazimu mbali ya Monasteri yao.

## 20. Maana miaka elfu moja machoni mwako na kama jana iliyopita. . . (Zaburi 90, 4).

Ndani ya Monasteri moja ya zamani, inatwaambia kitabu Gerondikon, aliishi mutawa moja mweshimiwa, aliyesikia toka Zaburi 90 hii mstari ya yulu hasikuweze kuisikia.

Na, kwani ndani ya hii Monasteri, hasikukuwe hata mutawa moja mwalimu ya roho juu ya kumusaidia, yule mutawa alifanya sala kwa Bwana juu ya kumusaidia na kumufafanusha maana ya hii mstari: «Maana miaka elfu moja machoni mwako na kama jana iliyopita. . . ». Kweli, Bwana alisikia sala yake na siku moja, kisha asubui, wakati watawa wote walirudia ma nyumba yao, huyu alimbakia kuomba, katika zwezo yake, ndani ya kanisa. Ile saa aliona mara moja ndege moja Kipepeo-kuku, muzuri kabisa, aliyeluka pempeni na yulu ya kichwa yake ndani ya kanisa. Alifurahi sana kwa ajili ya yatakuwa nzuri yake na alipima kumukaribia na kumukamata kwa mikono yake. lakini huyu ndege alichofa pole-pole na mutawa alimufata. lakini huu ndege hasikuluke kabisa yulu, lakini kidogo yulu. Mutawa alimufata na alitoka inje ya Monasteri na walifika ndani ya pori moja. Kule kipepeo-kuku alisimama mu fasi moja ya pori na alianza kuimba nzuri sana. Mutawa kwa ajili ya wimbo nzuri na utamu ya yule ndege, alisahabu ma bintu yote ya dunia na alikuwa na akili na mawazo yake ndani ya paradizo. Na neema ya Mungu hasikusikie machoko, wala njaa, wala baridi ao ma huitaji ingine ya mwili yake. Alisikia ndani yake furaha moja ya ajabu na alisikia hii wimbo ya ndege ya wakati miaka 300. Huyu ndege alikuwa malaika ya Mungu, aliyeonekana kama kipepeo-kuku na aliimba hata utamu sana!

Kisha malaika alipanda mbinguni, lakini mutawa kisha hii maono, alirudia kwa Monasteri yake mukuzania ya kama ilipita paka saa moja tangu ile saa alitoka ya Monasteri yake.

-Wakati alifika mbele ya mulango, mukubwa ya mulango alimuuliza: Weye ya makao nani ulikuja?

-Huyu mutawa alishangaa, kwa sababu asikujue huyu mutawa, aliyekuwa ku mulango nani alikuwa na alimwambia: Mimi ni mutawa fulani, usinijue?

-Mukubwa ya mulango alizanai ya kama huyu mutawa aliopotesha akili yake na alimwambia: Uende nzuri, ndugu wangu, mu njia yako, kwa sababu sisi hatunana ndugu na hii jina yako hapa. Mimi misikuona weye hata mara ingine, ninakuona mara ya kwanza na misikuona kuingia mara ingine mu Monasteri yetu.

-Ile saa huyu mutawa alistajabu na alitetemeka. Alimwambia ma desturi ya Monasteri yote, tena na ma jina ya watawa wote. Kisha aliingia ndani na aliomba kukutana na padri mukubwa ya hii Monasteri. Padri mkubwa aliita watawa wote, lakini hata moja katikati yao hasikumujue huyu mutawa mugeni. Basi, huyu mutawa mwenye ajabu, aliwaambia na ajabu na boka:

-Ninashangaa na misijue mitasema ninyi, namna gani ilifanyiwa hii mageuzo ndani ya saa moja. Mimi nililofa ya Monasteri yetu paka saa moja na namna gani waligeuza ma uso yenu na sasa misijue hata mutawa moja, wala na mweye musinijue! Mushuhuda yangu ni Mungu, ya kama haikupitisha hata saa moja tangu ile dakika nilitoka ya Monasteri yetu. Mbele ya saa kidogo tulisoma pamoja Ibada ya Asubui. Padri mukubwa yetu alikuwa huyu na jina fulani na watawa walikuwa wa fulani na jina yao. . .

Ile saa Padri mkubwa alileta kitabu ya ma jina ya Watawa wenye zamani na alisoma mbele ya yule mutawa nma jina yao. Ile saa huyu mutawa alisikia ya kama padri mukubwa yake alikuwa yule na jina fulani na waliisha kupitisha miaka 300. Padri mkubwa alianza kuuliza huyu mutawa mutu nani eko, namna gani aliishi mu uzima yake na namna gani alistahiliwa toka Mungu kuangalia hii maono ya ajabu. Huyu mutawa alimujibu:

-Misijue hata fazila moja mu uzima yangu; paka nilifanya utii kwa mukubwa yangu na nilikuwa mapendo kwa wapadri wote na misikusikia kwazo moja, kwa ajili ya makosa ya wa ndugu yangu. Nilikuwa kabisa heshima mingi na maopendo kwa Mzazi-Mungu Bikira maria na kila siku nilisoma mbele ya Ikona-Picha yake Kanuni na Wimbo Akathiste yake.

Kisha aliwaambia onekanao ya ndege kipepeo-kuku na historia yote namna gani ilifanyika mu pori. Watawa wote waliria sana na walimubusu na furaha. Walimuona hapana kama mtu ya hii dunia, lakini kama mutu ya mbingu, kwa sababu ma neno yake walikuwa wa mbingu na takatifu. Ile saa padri mkubwa alimuwambia:

-Tukuza Mungu Mwenyezi, aliyekustahili kuona hii maono ya ajabu, iliye haikumuone mtu mwingine ya hii dunia. Tena uliishi furaha moja na utamu ile wanaishi paka wenye wanaingia mu paradizo. Lakini inapaswa kujua, ndugu wangu, ya kama walipita miaka 300 na hapana saa moja sawa vile weye ulizania.

Wakati alisikia sauti hii ya padri mkubwa alitukuza Mungu, aliria kwa furaha na aliomba kupewa Komonyo Takatifu. Alipewa Mwili na Damu ya Kristu na alisema:

-Sasa Bwana umwache mjutumishi mwako. . . » na mara moja alitoa nafsi yake kwa mikono ya Mungu.

## 21. Miaka ma ngapi muliacha kanuni ya ma sala yenu?

Ma miaka ile alikuwa patriarhi ya Yerusalema mtakatifu na mwenye akili mkubwa Sofronios ilifanyika hii jabo ya ajabu kwa faida ya roho kwa watu mengi. Basi, aliishi kule mutawa moja, mukubwa na mufazili mu uzima yake, aliyeitwa Eftropios. Ilikuja wakati na alikufa huyu mtu ya Mungu na alienda mu fasi ya wenya haki watu ya Mungu. Patriarhi alitayarisha mambo yote juu ya maziko yake na alihamuru watawa filani kuchibula kaburi yake mu ile fasi walimazikwa na waminifu yote. Kule waliisha kumazikwa zamani wa ndugu makumi mbili, wenye lakini walikuwa tena bila kulekea na kuoza ma miili yao. Kwa sababu hawakujua wa nani walikuwa hawa wa ndugu, patriarhi aliita taifa yote ya waminifu na walifanya ibada ya usiku: magaribi, sala ya asubui na Litrurgia na kuomba kwa Mungu kuwajulisha sababu gani wale wafu walimbaki bila kuoza na kuharabisha ma miili yao.

Mungu Mwema kamili, basi, ambaye anamaliza mapenzi ya hawa wanamutii na wanamuogopa, alibariki mufu moja katikati ya hawa wa makumi mbili na alifufuka. Alifungula kinywa yake na alisema:

-Sisi, ee Mweshimiwa Mkubwa askofu yetu, tuko wapadri na watawa na, kwa sababu tulichanga na masubuko ya hii dunia, na utukufu ya bure, upenda-feza na ma kosa ingine, tuliacha ma kanuni ya ma sala yetu. Kwa hii mambo sasa tuko ya kufungwa na ma miili yetu hakuna baraka ya Mungu ya kulekea na kufanyika bulongo.

-Patriarhi Mkubwa alimuuliza: Miaka ma ngapi muliacha makuni yenu?

-Na huyu mufu alimujibu: Miaka makumi mbili.

Ile saa Patriarhi alisema kwa watawa wengine kufanya ma sala ya wale wafu na hivi watafunguliwa toka monyororo ya kosa yao. Na kweli, kisha miaka makumi mbili, nikusema, wakati walitimiza watawa wengine ma sala yao, wa ndugu hawa walifunguliwa toka mafigo yao na ma nafsi yao walipata pumziko.

Basi, wa ndugu wangu, wenye padri na watawa na wakubwa ya ma kanisa na ma Monasteri yetu, lakini na mweye waminifu wapenzi watoto ya roho yetu, tusizarau ma Ibada na ma sala

yetu. Huyu anayeacha sala na kanisa yake, bila sababu na maneno ya malari ao sababu ingine na eko inje ya Kanisa, analipizwa na mafigo toka wa Padri wakubwa wetu. Hii ma Ibada ni hii: sala ya magaribi, sala ya Apodipno Kidogo, Sala ya kati ya usiku, sala ya asubui, Saa ya kwanza, Saa ya tatu, Saa ya Sita na Saa ya Tisa na Kanuni ya kusema sala ya Bwana Yesu na kupika magoti.

Hii matendo ya sala inapaswa kuifanya yote na mapendo mbele ya Mungu na mukaribifu yetu, kwa sababu huyu anayechukia ndugu yake, aipaswe kuingia mu Misa, sawa vile anasema na Mtume Petros, kwa sababu hii sala inaleta mafigo kwa maungo umoja yake na pa kichwa yake.

Ssisi, wa ndugu wangu, tuendelea kuomba kwa Mungu juu ya kutufungula milango ya Ufalme ya mbingu katika neema ya Yesu Kristu, kwa mwenye tunatoa utukufu, sifa na usujudu kwa milele ya milele. Amina.

## 22. Usichoke juu ya mimi, kwa sababu Bwana aliniokoa. . .

Mu Monasteri ya Mt. Dionisios ya Kilima Takatifu aliishi na aliisha uzima yake na ma fazila mingi mutawa Ignatios ku mwaka 1953. Padri mukubwa Gabrieli, aliyekuwa ile ma siku mu shamba, mbali ya Monasteri yao, alisikia jabo moja ya ajabu na, wakati alirudia ku Monasteri yake, alisema hii hadisi kwa mutawa Lazaro na yeye aliiandika mu kitabu moja. Hivi aliandika hii hadisi mutawa Lazaro katika kinywa ya mpadri Gabrieli:

Wakati, mbele ya ma siku mbili, niliondoka ya shamba yetu, ile iko mu fasi Monoksilitis, ndani ya Kilima Takatifu, mu njia nilikutana mutawa Serapioni, ambaye ni toka inchi Russia na aliishi mu Skiti-Mukini Hromicha ya Kilima Takatifu. Kwa ile mazungumuzo tulifanya pamoja, tulisuburia juu ya lufu ya mutawa yetu padri Ignatios, aliyekuwa toka Monasteri yetu. Kisha mutawa Serapioni alisema kwa padri Gabrieli, mkubwa ya Monasteri ya Mt. Dionisios: «Mimi, ee padri mtakatifu, kwa mutawa Ignatios nilikuwa ushukuru na shukrani mingi, kwa sababu, wakati yeye alitumika mu shamba yenu, hapa karibu ya fasi Monoksilitis, alinisaidia ya kila huitaji na mambo yangu. Alinipatia manguo na bintu ya chakula ya kuachana. Alikuwa huyu murahimu na mwema mutawa. Basi, wakati nilijulisha ya kama alikufa, kwa ajili ya mapendo na shukrani yangu mbele kwake, niliomba na Komboshini yangu na niliomba kwa Mungu kumusamehe mutumishi wake padri Ignatios na kumuweka ndani ya paradizo. Kila usiku nilifanya komboshini moja na buchanga mia moja. Wakati nilifanya sala ya siku kumi na tano na nilisema kwa Mungu juu ya kumuokoa, mara moja niliona ndasni ya chumba yangu mwangaza nguvu moja na katikati ya hii nuru niliona padri Ignatios muzima na mwenye furaha. Alinikaribia, alinamia kichwa yake mbele yangu na mapendo mingi na heshima alinisema: «Ninakushukuru sana, padri Serapioni, ninakushukuru juu ya mapendo yako na ninakuomba, usichoke kuendelea sala juu ya wokovu yangu, kwa sababu Mungu Mwema aliniokoa na niko mu fasi nzuri sana. Mimi ni mwenye heri na niko pamoja na wale watakatifu waliokolewa». Hii ma sauti yeye aliniambia na alikimbia mara moja.

Na mimi, ee Padri mkubwa yangu, nikona kitumaini kwa ajili ya hii maono yangu, ya kama ndugu wetu Ignatios, hapana paka aliokolewa, lakini alikataswa.

## 23. Maono ingine ya Mutawa na mwalimu ya roho padri Yosefu wa Spileotis.

Mutawa na padri ya roho Yosefu aliishi mu Kilila takatifu na alikufa ku mwaka 1965. Huyu alichoka sana juu ya kupata neema ya Mungu mu uzima na roho yake. Monatseri ya Mt. Filotheos aliandika kitabu moja, pahali ni fundisho na uzima ya huyu mutawa mukuwa Yosefu. Tazama aliandika ninyi huyu padri Yosefu juu ya maungo yake:

«Basi, usiku moja, wakati niliomba, akili yangu ilitoka na ilikwenda mu kiwanja moja. Kule walikuwa watawa wengi, wenye walisimama kwa mustari moja, sawa kufanya bukomvi.

Mukubwa moja ya wa askari alikuja karibu yangu na aliniambia: «Unataka kukombana na weye mu fasi ya kwanza? ». Na mimi nilimujibu ya kama ninapenda sana kukombana pamoja na wa adui yangu, waliokuwa ma shetani, wenye walikunguruma kama maimbwa na, kama waliwaona watu wengine, waliogopa sana. Lakini kwa roho yangu haikukuwe boka, kwa sababu nilikuwa na hata chuki mingi na nilitaka, kama ilikuwa namna, kuwalumiza na meno yangu. Ni kweli ya kama, wakati niliishi na mu dunia, nilikuwa mutu mwenye nguvu sana. Ile saa, basi, aliniachana yule mukumbwa ya wa askari toka ile mustari waliokuwa watawa wengine. Pamoja tulipita mistari tatu ao ine, pahali walikuwa tena wa wili ao wa tatu watawa wengine na waliongojea kukombana kupingana na ma shetani. Ile saa ma shetani walikuwa tayari kunipingana, lakini mimi nilikuwa chuki mingi ndani yangu juu ya kukombana na wao. Kule yulu mukubwa aliniacha na aliniambia: «Huyu anayetaka kukombana na hawa ma shetani, mimi misimuzibiria, lakini ninamusaidia».

. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

Ku mwisho usiku ingine niliona mara ingine maono ingine. Niliona makao moja mnene, pahali katikati ilikuwa bahari. Ndani ya ile makao walikuwa chini mateko mingi ya kufuchama na haikuonekana. Mimi nilikuwa mu fasi moja ya yulu na niliona hii yote mambo. Mu fasi ya bahari alikuwa shetani moja wa matata na toka ma macho yake ilitoka moto. Alikuwa na kisilani na makali sana. Alitosha inje kichwa yake na aliona, kama watawa walijibamba ndani ya mateko. Waliyopita toka ile fasi Watawa, bila kusopoka, wengine walijibamba toka sigo, wengine toka mikono, wengine toka miguu na wengine toka kifuno. Wakati aliona hii mambo, shetani mukubwa, alifurahi na alipika mikono yake. Mimi ile saa nilitaabu sana na niliria. Ah, nilisema, ee shetani mwovu, unatufanyisia ninyi na unatulanda namna gani! Ile saa nilirudia kwa maungo yangu na mu nyumba pahali nilikuwa, nikusema ndani ya chumba pahali niliendelea sala yangu. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

Wakati ingine nilikwenda usiku kwa padri mkubwa yangu juu ya kuungama na kupewa Komonyo Takatifu. Niliikaa kidogo pa riimbwe moja ya njia na mara moja nilisikia sauti moja utamu na ilikuwa ndege moja, iliyeimba nzuri sana. akili yangu ilinyanyua toka hii sauti ya ndege na nilifata hii sauti juu ya kuitafuta huu ndege eko wapi. Niliangalia ma fasi ya kuume na kushoto na nilizania ya kama niliangia ndani ya kiwanja moja toka njia moja iliyekuwa meupe sana na ma kibabashi yake kama makalasi. Ndani ya ma kibabashi walikuwa mawa ya kuachana, ile saa akili yangu ilisahabu sauti ya yule ndege na niliangalia utukufu ya paradizo.

Nilitembea ndani na niliona nyumba urefu moja na wa ajabu na akili yangu alistajabu, Mu mulango ya ile nyumba kabaila, ilikuwa Mtakatifu kamili Mzazi-Mungu na alikamata kwa mikono yake Yesu. Mzazi-Mungu alionekana na mavazi mweupe kabisa na aliangaza kama teluji. Wakati mimi nilikaribia, yule alinibatia na alinisema sauti moja. Misisahabu ile mapendo alinionyesha, kama Mama wa kweli. Ile saa mimi, bila boka, nilikuja karibu yake, wakati nilikaribia picha yake. Na hii kazi anafanya mtoto moja mudogo, kama ataona mama yake, vile nilifanya na mimi. Namna gani nilitoka ya karibu yake, misiweze kijua. Kisha na njia ingine nilikuja mu kiwanja, pahali ilikuwa nyumba moja kizuri. Hawa walimbakia kule, walinipatia baraki kimoja na waliniambia, ya kama huyu anayependa kupita ya hapa, pahli ni ubatio ya Abrahamu, tunamupatia baraka kimoja. Vile nilitoka na nilikuja mara ingine mu maungo yangu na niliikaa pa riimbwe moja, pahali nilisimama kupumzika kidogo.

. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

Wakati moja nilikuwa na taabu mingi na uzima yangu ilikuwa paka mateso moja nguvu sana. Mara mengi kupita niliteswa kwa ajili ya watu wengine, wenye mimi nilitaka kuwasaidia juu ya kuokolewa, lakini wale walinichekelea na majaribu waliwateswa.

Kwani, basi, nilikuwa mu taabu na umivu hii, nilikuja kwa maono moja. Na, ile wakati nilitembea, nilijipata ndani ya kiwanja moja, pahali bulongo yake ilikuwa meupa kama teluji. Nilishangaa sana na nilisemaka mu maungo yangu: «namna gani nilijipata ndani ya hii makao

nzuri? ». Na nilitafuta kutoka, kwani niliogopa kama mtu moja atanikutana, atanifokea, kwani niliingia kule, bila ruhusa ya mutu moja. Niliangalia ma fasi kuume na kushoto juu ya kupata mulango ya kutoka inje. Niliona mulango kimoja na niliingia ndani. Kule ndani ilikuwa kanisa ya Mtakatifu Mzazi-Mungu Maria. Kule waliikaa wakijana wengi, wenye walivaa mavazi ya mwangaza. Walikuwa na musalaba moja nyekunda pa kilari yao na mbele ya uso yao. Moja katikati yao alisimama ya kiti yake; alikuwa mukubwa ya wa askari na aliniambia:

-Kuja ndani, kwani tunakuongojea weye.

-Nilimwambia; unihurumie, kwani misina mustahili kuikaa karibu yenu, paka inenea kusimama mbele ya miguu yenu.

Yule, alicheka na aliniacha kusimama mbele ya Ikonostasi, pahali ilikuwa picha ya Mzazi-Mungu, na aliniambia:

-Ee Mama na Malkiaya dunia mzima, Mfalme Mama ua wa malaika. Mzazi-Mungu Mwenye Safi Bikira, onyesha neema yako kwa mutumishi yako, mwenye anateswa hata mingi, kwa ajili ya mapendo yako, kwani iko hatari kulekea kwa taabu mingi.

Mara moja ilitoka mwangaza mingi toka Picha takatifu yake na alionekana Mzazi-Mungu maria kama muzima na mwenye muzuri kabisa, na mimi nilianguka chini kwa miguu yake na misikuweza kumuangalia na paka niliria mukusema:

-Unihurumie, Mama mupendwa wangu, kwa sababu bila kusikia, ninakutaabu!

Vile na macho yangu ya kujaza na machozi na kujana kwa furaha, nilirudia kwa maungo yangu».

## 24. Uhamakio ya nafsi kwa ma roho ya shetani, kisha uchanisho ya nafsi toka mwili.

Hii maono aliona Mutyawa Grigorio, aliyekuwa mwanafunzi ya Mtakatifu Basile wa Mupya, makumbusho yake anafanya Kanisa yetu mu tarehe 26 ya Mwezi ya tatu kila mwaka.

Huyu mutawa, ambaye ni na mwandishi ya hii maono, aliishi, ku mwisho ya wakati mia ya tisa mu muji Konstantinopoli na aliona hivi hii maono.

Ile wakati aliishi mu mji mukubwa Padri mkubwa yake, mt. Basile, na ile nyakati mwanafunzi yake mwingine mwanamuke, aliyeitwa Theodora, aliisha kufa. basi, Grigorio, basi, alisikitika kwa sababu alikufa dada ya roho yake Theodora na aliuliza maungo yake: «Nafsi yake alienda wapi? Aliokolewa ao hapana? » Juu ya hii mambo aliuliza padri mukumbwa yake Basile kumwambia sauti kimoja. Kweli, padri ya roho yake siku moja alimwambia na mucheko kidogo:

-Unataka, mtoto yangu, kuona Thehodora, eko wapi?

-Namna gani, ee padri yangu, iko namna kuona mimi Theodora, aliyekufa ya zamani na sasa eko mu uzima ingine?

-Hii usiku utamuona, alimujibu padri ya roho yake, mt. Basile.

Hii usiku, basi, wakati nililala, anasema mutawa Grigorio, ninaona kijana moja kuniambia:

-Kuja na kwenda sasa pamoja na padri ya roho yako kuona Theodora.

Mimi ile saa, nilizania ya kama nililamuka na nilienda mu chumba ya padri ya roho yangu; misikumupate kule na nilitoka inje. Nilitembea mbio kuingina mu Kanisa ya Blahernes ya muji Konstnatinupoli. Mara moja nilijipata mbele na makao moja mwembaba na ya kilima, pahali nilipanda na nilifika mbele ya mulango kimoja, iliyekuwa ya kufungwa. Toka mlango kidogo niliona ndani mwanawake wa wili, wenye walisuburia na mimi niliwauliza:

-Hii nyumba ya mtu nani iko?

-Moja mwanamuke aliniambia ya kama hii ni ya mt. Mutawa na padri ya roho yangu basile, ambaye mbele ya saa kidogo alikuja hapa juu ya kutembelea watoto ya roho yake.

Mimi, wakati nilisikia hii ma sauti, nilifurahi na nilimwmabia, ya kama na mimi ni mtoto ya roho yake na nilimwambia kufungula juu ya kuingin na mimi ndani.

-Yule alinisema: «Wewe usikukuje ya hapa mara ingine na tusikujue; kwa hivi toka ya hapa, kwa sababu, bila ruhusa ya mama Theodora, hasiweze hata mtu moja kuingina hapa ndani. Bile ma nyumba yenye mwangaza ni ya mt. Mutawa baba yetu Basile na alipatia hii yote kwa mtoto ya roho yake Theodora.

Mimi, wakati nilisikia jina Theodora, nilikamata nguvu na nilianza kukokola mulango na kuita nguvu. Ile saa alinisikia ya ndani Theodora na alisema kwa wanawake wengine wa wili kunifungula. Wakati niliingina mimi ndani, huyu alinibatia na aliniuliza:

-Nani alikuletea hapa, ee bwana Grigorio? Ulikufa na ulistahiliwa kuja ndani ya hii makao wa heri na uzima wa milele?

-Mimi, bila kusikia ya kama ninaona maono, nilimujibu: «Ee Mama Theodora, bado kufa, lakini niko tena mu uzima ya inchi yetu; lakini kwa baraka ya mutawa Baba yetu Grigorio nilifika hapa juu ya kufunda hali ya roho yenu, namna gani ulipita ma kundi ya ma shetani ya pepo na namna gani ulivumilia mambo matata ya lufu».

-Huyu alinijibu: Mtoto wangu mupendwa, ee Grigorio, ninakuwambia ya kama maumivu na machanisho ya nafsi yangu toka mwili yangu ninakusema ya kama inafanana sawa mtu moja atajitupa ndani ya moto mutupu na atalungua pole-pole mupaka kutoka nafsi toka mwili. Wakati nafsi yangu ilitoka ya mwili, niliona pempeni yangu watu wenye makali na mbaya, wenye walipiga meno yao kupingana yangu na waligeuza ma sauti yao na waliria sawa ma nyama. Kama nilitaka kupindula macho yangu mu fasi ya kuume ao kushoto, kwa mufano, ma shetani walisimama mbele yangu na maono ya ma uso yao ilikuwa kuliko kibaya ya gehena.

Mara moja, katikati ya hii sikitiko na uchungu yangu, ninaona wa wili wa kijana, wenye walisimama mu fasi ya kuhume ya kitanda yangu na namna ukali na matata walisema kwa wale ma shetani:

-Ee wazulumu na wenye uchafu ma shetani, juu ya ninyi munakuja ile saa kwa lufu ya waminifu wetu na munawapatia boka na tetemeko kwa ma sauti yenu ya makali? Lakini musifurahi, kwa sababu mbio-mbio mutakimbia.

-Ma shetani walileta mbele ya  uso yangu matendo yanbgu yoyote ile nilifanya tangu kipimo ujana yangu, wala walikuwa zambi kwa ma neno, wale walikuwa matendo mbaya na walisema ya kama mimi misikutubu. Kisha alikuja muzulumu moja munene na mukafiri, aliyekuwa uso ya simba na, wakati mimi nilimuona, nilipta boka mingi. Wa Malaika wa wili waliniambia:

-Epuka nafsi toka mwili yake, lakini usipatia umivu mingi kwa huyu mtu, kwa sababu hasikufanya zambi manene na matendo mbaya mengi.

Yule alijeza kilauri moja ya kintu moja ya kunywa, alinipatia na mimi, bila kutaka, niliikunywa. Ilikuwa hata buchungu, na mimi misikuweze kuivumilia. Nafsi yangu ilitoka inje ya mwili yangu na wa malaika walimbeba na walimpanda mbinguni. Ile saa mimi niliona mwili yangu kuwa chini mu inchi na nilistajabu. Nilishangaa, kwa sababu misikujua hii mamabo yote wanajifanya mu saa ya lufu ya mtu moja.

Wa malaika walinikamata na tulipanda mbinguni. Mara moja ma shetani wenye makali walinizunguka pempeni yangu na walisema na ma sauti nguvu: Huu nafsi alifanya ma zambi mengi na inapaswa kutujiba ya kila zambi yake.

Ile saa wa malaika waliangalia tendo nani nilifanya nzuri mu uzima yangu, kwa sababu na mimi niliisha kutumika juu ya wokovu ya nafsi yangu. Ma shetani, wakati walisikia kila tendo kizuri yangu walisikitika na walikombana pamoja na wa malaika juu ya kunikamata kwa mikono yao.

Kisha niliona mpadri mkubwa wetu, mutawa mt. Basile, aliyesema kwa wamalaika: «Ee wa bwana wangu, huu nafsi alifanya matumishi mingi juu ya mimi na alinifurahi sana ile wakati ya uzee yangu. Kwa hivi niliomba toka Mungu na alinipatia huu nafsi wema Wake. Wakati mutaisha hii mambo ya kuhamakia, ninamiomba kumuleta huu nafsi mu nyumba wa mbingu, pahali alinitayarisha Mungu juu ya kuikaa mimi pamoja na watoto wa roho yangu.

Vile yule aliondokana wa malaika waliluka yulu na mabawa yao na walinikamata na mimi tulipanda yulu mu fasi ya mashariki. Mu njia yetu tulikutana ma kundi ya ma shetani ya kuachana, pahali kila nafsi inapaswa kupitisha juu ya kuhukumwa matendo na maneno yake: Hii ma kundi ya ma shetani ni:

1. Kundi ya uhukumu

Tulikutana kundi moja ya ma shetani wenye makali na katikati yao alisimama na mkubwa yao. Unisadiki, mtoto yangu Grigorie, mushuhuda ni Mungu wetu, ya kama hawa watu nilihukumu mu uzima yote yangu, ma shetani walinisema ma jina yao yote, ile saa na fasi niliwahukumu na kinywa yangu, ile maneno niliwaambia kupingana yao na walitaka ma shetani kunihukumu. Ni kweli ya kama walisema na mauti mengi ya uwongo kupingana yangu kwa ajili ya uwovu yao. Kama, kwa mfano, nilisema sauti moja juu ya kusaidia mtu moja kwa mapendo, ma shetani walisema ya kama kwa ajili ya masimango nilisema hii ma neno na walitafuta kunihukumu na waliomba jibu ya wa malaika. Wa Malaika waliwajibu sauti kweli na kwa maombezi ya mpadri mukumbwa yetu mt. Basile, tuliondoka ya hii kundi.

2. Kundi ya matusi

Kwa hii kundi tulipita bila kutuuzi ma shetani kwa maombezi ya mpadri na Baba ya rogo yetu mt. Basile. Wa Malaika walipanda na walisema na katikati yao «ya kama huu nafsi alipata neema mingi toka mutumishi ya Mungu mt. Basile»; joo vile sisi hatukuwana masikitiko ya hii kundi ya ma shetani.

3. Kundi ya uwongo

Ndani ya hii kundi ilikuwa hazina moja ya ma shetani na ma uso yao walikuwa mbaya sana na mastahili ya kuichukia. Wakati walituona, walifokea na walileta tetemeko mingi, ya kama mara mingi, kabisa ma miaka ya kipimo udogo yangu, nilisema ma sauti ya uwongo mingi na nilifuchama kusema sauti ya kweli. Tena walinionekana kila nyakati, kila fasi na ile ma sauti nilisema na pamoja na watu filani nilisuburia. Lakini wa malaika walisema sauti kweli juu ya matendo ya uzima yangu, juu ya toba yangu, juu ya machozi na maombi iliyefanya na vile kwa maombezi ya mt. mpadri yetu Basile tulipita toka hii kundi.

4. Kundi ya gazabu na hasira

Hapa ilikuwa makutano moja na ma shetani mengi, pahali mukubwa yao aliikaa katikati yao na kisilani mingi na aliwahamuru ma shetani wengine na ma sauti makali,

bila sisi kusikia ma sauti yake. Basi, walinihamakia hapana, paka, wakati nilikelele na nilikuwa makari ao paka na richo makari kupingana ya mtu moja, lakini tena na, wakati nilipiza na nilikuwa gazabu kupingana na watoto yangu na ma sauti ninyi niliwaambia. Tena, kama nilikuwa  na chuki ao sikitiko mbele ya mtu moja. Hii matendo yangu yote, waliniambia na makelele. Kwa kila namna nilisuburia na watu wengine na ma alama filani nilifanya mbele yao, vile na ma shetani walifanya na walinichekelea. Tena walisema na ma jina ya wale watu mimi niliwafanya huzuni ya roho katika ma neno yangu makali, hasira na kisilani yangu; tena na ile nyakati nilisema hivi na hivi. . . Lakini na toka hapa tuliondoka na maombezi ya mtawa baba yetu mt. Basile.

5. Kundi ya majivuno

Tuliendela kupanda yulu na tulikutana shetani ya majivuno, lakini wale ma shetani hawakupate hata zambi moja juu ya kunishitaki, kwa sababu mimi nilikuwa mtu masikini na misikukuwana kintu juu ya kujivuna.

6. Kundi ya chabulana

Wakati tulifika hapa, katika neema ya Kristu, hawakukuwa na wale wa shetani hata sauti moja juu ya kunishitaki na joo vile tuliondoka katika furaha. Lakini, kwa ondoko yetu wale walipiga ma meno yao na gazabu na chuki mingi na walitaka, kama ilikuwa namna kunikula.

8. Kundi ya masimango na kusema ma sauti ya bure.

Ma shetani makubwa ya hii kundi walitaka kuwajibu mimi kwa yoyote ma sauti ya bure na masimango niliisha kusema mu uzima yangu tangu kipimo ya ujana yangu. Tena na wimbo ya dunia waliniambia ya kama walikuwa mastahili ya malipizo. Mimi misikujue nitawajibu ninyi na nilishangaa, namna gani wanakumbuka hii matendo na ma sauti yangu yote, kwa sababu mimi niliisha kuisahabu. Lakini na toka hapa kwa maombezi ya mpadri na baba yetu mt. Basile, tuliondoka.

9. Kundi ya kulanda

Hii kundi ya ma shetani anahamakia wale watu wanalanda wa ndugu wao na wanawabeba mali na mariti yao na ma cheo yangu na namna kibaya. Basi, walianza kunihamakia, kama nililanda mtu fulani na nilimubeba makuta yake, sifa yake ao utumishi yake. Lakini, kwa sababu hawakuweze kunionyesha matendo mbaya yangu, walipiga meno yao na walinitetemeka; lakini sisi tuliondoka ya hapa bila kutuuzi.

10. Kundi ya uzaifu na usingizi

Hapa ma shetani walinihamakia, kama nililala na nilikuwa muzaifu na nilikataa kwenda mu Kanisa ao kwa ajili ya uzaifu yangu misikufanya tendo kizuri, ile ilipaswa kuifanya kwa nafsi yangu na saidi ya watu wengine. lakini na hapa, kwani hawakupata kosa yangu, waliniacha na tulipanda mu kundi ingine.

11. Kundi ya upenda-feza

Kwa hii kundi ilikuwa umeme na giza mingi. Na hapa walihamakia hawa wenye makali na, kwani hawakupate kintu kimoja juu ya kunilipiza, kwa sababu mu uzima yangu yote nilikuwa msikini, tuliondoka ya hapa, bila kutuuzi.

12. Kundi ya ulevi.

Tulipanda yulu na tulifika mu kundi ya ulevi. Ma shetani waliniongojea kama ma simba juu ya kunikula. Lakini, kwa sababu hawakuwa na mamlaka ya Mungu kuhamakia ma nafsi yote, walikuja wa malaika, wenye walinisidikiza na walihesabu hii vinyo yote nilikunywa mu uzima yangu yote. Ile saa ma shetani na namna ukali, walifokea na walisema hivi: Weye usikukunywe ma kilaruri filani kwa Siku Kuu fulani, pahli walikuwa na watu filani na filani? Usikukuwe mulevi ile siku fulani? Usikukunywe, wakati ulikwenda mu nyumba ya yule mtu fulani na ulikunwa ma kilauri filani? Hii ma sauti waliniambia na ma sauti ingine, waliokuwa ya kweli. Ile sa wa malaika walileta katikati matendo mazuri yangu na namna gani nilitubu juu ya hii ma kosa yangu. Kwa maombezi ya mpadri ya roho yangu tuliondoka ya hapa. Mu njia walinisema wa malaika: «Unaona, nafsi yangu, hatari ngapi iko na nafsi moja, juu ya kupitisha hii yote ma kundi ya ma shetani?

-Mimi niliwajibu: Ndivyo, wa bwana wangu, hatari ni ukubwa juu ya ma nafsi wenye zambi na ninasadiki ya kama hata nafsi moja haiweze kupitisha bila kumuuzi. Ninazania tena ya kama hata mtu moja ya wale wanaishi mu dunia, mambo gani na tetemeko ninyi ikona nafsi moja, kisha lufu yake. Ole, ole kwake! ! Boka na tetemeko ninyi inaongojea kila nafsi iliyetoka ya mwili yake na hii dunia ya bure. Na sisi tunazaifu na tunakataa kutumika ma sheria ya Mungu juu ya kupata wokovu ya ma nafsi yetu.

-Ile saa wa malaika waliniambia: Iko Maandiko Takatifu na Mafundisho ya Watakatifu wetu, lakini uzima ya furaha na utamu, ma chakula mengi ya kuachana, ma furaha ya zambi wanafunga ma macho ya watu na hawaione, wala hawaiwaza, lakini wanaishi sawa hawatakufa ya milele. Wanazaifu kumaliza matendo mazuri, kabisa wanazarau fazila ha huruma na mapendo, ile inayeweza kusaidia nafsi kuliko mingi ya matendo ingine na kupitisha makundi ya ma shetani, bila kuuzi. Lakini hawa watu ni wadogo kabisa. Ole kwao, wasiyeofanya matendo mazuri. Kwa sababu inakuja mara moja lufu na inawabamba, lakini wakati wanapita ya hapa ma shetani wanawabamba na mara moja wanawatupa ma fasi wa giza na uchafu ya Hadeze, mpaka Ufikisho ya Mbili ya Bwana Yesu Kristu. Hii mambo ilikuwa namna kupata na weye, kama haikukuwe wema ya Mungu na huruma (sala) ya mutumishi Wake mt. Basile.

13. Kundi ya chuki

Hii kundi inahamakia hawa watu wenyewekona chuki mbele ya ma jerani yao na kila mwenzake yao na hawataka kumusamehe, katika amri ya Kristu. Wakati ma shetani walituangalia, walipanda yulu yangu na walitafuta hata kosa kimoja, lakini katika neema ya Kristu, hawakupate na walikimbia na haya na kufokea hivi: «Tulisahabu kuandika na makosa ingine. . . Lakini sisi tuliondoka.

Ile saa nilipata nguvu ni nuliuliza wa malaika: «Namna gani hawa wazulumu wanajua makosa ya kila mtu? »

-Malaika moja alinijubu: Usijue, ya kama, kila mwaminifu muorthodokse, kisha ubatizo yake, Mungu anamutupa na malaika moja kama muchungaji na musaidizi yake na huyu malaika anaandika matendo yake yote ya kila siku? Tena anamufata na shetani moja, ambaye anaandika matendo mbaya yake yote. Basi, wakati atafanya kosa moja mtu moja, mara moja shetani anayemufata, anaandika hii kosa ao zambi yake. Kama kwa mfano mwaminifu moja alifanya kosa moja ya kuiba kintu kimoja. Mara moja anajulisha kundi ya wizi. Lakini, kama matendo mazuri ni kuliko mengi, malaika anailetea mbele ya ma shetani na hivi nafsi ya huyu mtu inatoka na uhuru. Hii mambo yote ya kuhamakia inajifanya paka kwa waminifu waorthodoksi, kwani paka hawa wekona ubatizo ya kweli na fundisho ya kweli. Juu ya watu wengine, wenye wanafata ma ndini ingine ya kuachana hakuna ma karatasi (papier), wala uchunga ya ma shetani, kwa sababu wanafata hawa watu makosa na mafundisho ya uwongo yao.

14. Kundi ya ufumu

Hii kundi inahamakia wafumu na walozi. Hawa ma sjhetani walikuwa na ma uso kama ma nyama makari ao ma nyoka, ao kama maimbwa, mangombe makali na ma nyama ingine makali. Lakini sisi, katika neema ya Kristu, kwa sababu hawakupate kintu kimoja kimbaya kutuhamakia, tuliondoka. Tulipanda yulu na mimi niliuliza wa Malaika:

-Namna gani iko namna kusamehewa zambi ya waminifu, wenye wanaishi duniani na kusafishwa toka ma kitabu ya ma shetani?

Na wa Malaika walinijibu: Iko namna kusamehewa na kusafishwa, kama watatubu na wataungama ma zambi ya makosa yao kwa mpadri moja ya roho; hivi watabeba usamehe ya zambi yao. Lakini kama mtu moja atasikia haya kuungama safi na kweli na atazania ya kama inenea paka kuepuka toka zambi yake na atafanya maungamo paka mbele ya Mungu, huyu hakuna namna kubeba usamehe ya zambi yake. Bwana Yesu alipatia neema kwa Mitume Yake juu ya kufugula na kufuga zambi ya watu na katika wapadri ya roho iko mpaka sasa Fumbo ya Maungamo. Kama wa shetani wataangalia ya kama walisafishwa ma zambi yetu, wanatetemeka na wanakombana kutupa sisi mara ingine mu zambi moja ao ingine kuliko mbaya. Waminifu wengine wanafanya ninyi. Kwa sababu wanaogopa malipizo ya wa padri, wanasema zambi fulani kwa mpadri moja na zambi ingine mpadri mwingine, lakini hawa waminifu walijilanda toka shetani, kwani hii haina maungamo na kitubio, lakini ni uwovu. Watu inapaswa kuchakula mpadri moja juu ya uzima yao yote, kama iko namna, na aipaswe kumugeuza, bila lazima. Kama hawafanya hivi hakuna namna kuokolewa toka ma shetani waovu.

15. Kundi ya kula mingi

Hawa wa shetani walikuwa wanene kama wangurumbe, wenye makali na wenye nguvu kupita ya ma shetani wengine. Wakati walituona, walikuja yulu yetu kutukamata na walitaka kutuonyesha ma siku gani nilikula chakula mingi na kwa siri tangu kipimo udogo yangu na kabisa mu wakati ya kwarezima ya Kanisa yetu. Walinishitaki ya kama nilikanyanga malako iliyepatia mbelee ya Ubatizo yangu. Nikusema nililaka kukana matendo mbaya ya shetani na mimi nilifanya matendo na mapenzi yao. Lakini ya ngambo ingine wa Malaika walikombana kuonyesha matendo yangu mazuri na hivi tuliondoka ya wale washetani mbaya kabisa.

16. Kundi ya upagano

Mbio-mbio tulifika mu kundi hii ya upagano na ma ndini ingine ya mafundisho ya uwongo, lakini hata neno moja hawakuweze kutusema. Na sisi tuliondoka mara moja.

17. Kundi ya zambi na wanaume katikati yao (Pederastie)

Mkubwa ya hawa wa shetani aliikaa mu kiti moja juu pia na alikuwa na kwa mamlaka yake ma shetani wengine elfu moja na huyu mkubwa aligeuza uso yake mara mingi. Wakati ingine alionekana kama joka, wakati ingine kama panya, nyakati ingine ya ngurumbe ya pori makali na wakati ingine kama samaki mkubwa ya bahari. Pempeni yake ilikuwa uchafu na ilitosha arufu kibaya sana na watumishi yake walisimama na uso ukali na walikuwa tayari kunikamata. Wakati waliona ya kama niko mwanamuke, hawakuwa na kintu kunishitaki, wala kusema ya kama nililala pamoja na mwanamuke mwingine na nilifanya zambi na ye. Vile, katika neema ya Kristu, tuliuhurwa toka hii uchafu. Ile saa wa malaika waliniambia hii sauti yao: «Ma nafsi mengi wanafika mpaka hapa bila kizibirio, lakini hii kundi ya zambi ya pederastie inawatupa mu hadeze, kwa sababu hii zambi inaleta hasira na gazabu mingi kwa Mungu wetu, kuliko ya zambi ingine.

18. Kundi ya wale watu wanapakala ma miili na ma uso yao na ragi ya kuachana

Hii kundi ya shetani inahamakia wanaume na wanawake, wenye wanaweka mapambo na bintu na ragi ya kuachana pa miili na ma uso yao na harufu na wanapakala na ma nywele yao na ragi ingine, kwa sababu hii uso iliyewapatia Mungu haiwapendeze na wanataka kuonekana mbele ya watu wengine na ma uso ingine na ma ragi ingine. Ile saa wa shetani walisema kwa mimi: «Huu nafsi mara ya mbili alianguka kwa hii zambi na ni haki sisi kumukamata». Wa Malaika walionyesha matendo mazuri yangu yote na muchoko mingi na kwa maombezi ya baba yetu mt. Basile sisi tuliweza kuondoka.

19. Kundi ya usharati

Huu kundi inahamakia hawa watu waliondowa, lakini kisha ndoa yao wanafanya zambi na watu wengine. Nikusema bibi anafanya zambi na mwanaume mwingine na bwana anafanya zambi na bibi ya bwana mwingine. Lakini hivi wanajaza taji ya ndoa yao na uchafu. Lakini, mimi, katika neema ya Mungu, misikufanya hii zambi, kwani misikukuwa na ndoa na hivi tuliondoka ya kwenda mu kundi ingine.

20. Kundi ya uuaji

Hii kundi inahamakia hawa watu wenye waliuua na hawa watu kwa ajili ya kisilani yao, walipiga mtu mwingine. Tena hii kundi inahamakia kila uzulumu alifanya nafsi mbele ya wa ndugu yake. Lakini na toka hii kundi sisi tuliondoka bila mambo.

21. Kundi ya wizi

Hawa ma shetani walihamakia matendo yangu yote ya wizi na uwovu. Lakini na toka hapa, kwa maombezi ya mpadri ya roho yangu mt. Basile, tulipita na tuliondoka.

22. Kundi ya uzini

Mukubwa ya hii kundi alivaa nguo moja iliyejaza na ma pofu na ma damu na alifurahi na alitukuzwa sawa alikuwa kupambwa na vazi ya ufalme. Wa malaika waliniambia ya kama hii mavazi yake ilijifanya hivi kwa zambi ya machafu na ma uzina ya watu. Wakati, walituona, walikuruka yulu yetu na walishangaa namna gani tulitabuka ma kundi ingine na tulifika kwa wao. Vile walianza kutuhamakia ya kila zambi yengu. Na hawakusema paka ma zambi na matendo yangu ya kweli, lakini walisema na ma sauti ya uwongo na walitaka kunitosha toka mikono ya wa malaika na kunitupa mu gehena. Wa malaika waliwaambia ya kama hii zambi yote, mbele ya wakati mingi aliisimamisha na alitubu kweli. Wale walisema:

-Na sisi tunajua ya kama aliisha kuacha hii zambi yake, lakini alitupenda na alichunga ndani ya akili na roho yake mawazo mbaya na maovu na hasikufanya maungamo juu ya hii mawazo mbaya yake kwa mpadri moja ya roho, wala alifanya kanuni ya sala, wala usamehe alibeba ya mpadri ya roho yake na namna gani huyu alibeba neema mingi na sasa anangaza kama jua?

Wa malaika, halafu, walinisaidia na walinikamata kwa mikono yao na tunatembea. Ma shetani walipiga meno yao, kwani nilitoka kwao, bila kitumaini. Mu njia wa Malaika

waliniambia: «Inapaswa kujua ya kama toka hii kundi ma nafsi madogo sana iko namna kupita, bila hasara mnene. Wa mengi ya watu, kabisa, wenye hawajue Maandiko Takatifu, kwani wanakula mingi, inawakisha ndani ya mwili yao mataki ya zambi katika mwili; hivi wanakuja kwa hii kundi ya uzini, wanajihamakia nguvu ya ma shetani na kisha wanatupwa ndani ya hadeze. Lakini weye na saidio ya mpadri ya roho yako, uliokowa toka mikono ya hi kundi; na kutoka hapa hakuna boka ingine.

23. Kundi ya wale wasiyowema

Wa malaika mukusema kwa mimi hii ma sauti yao, tulifika pamoja mbele ya kundi ya usiyowema na wale wekona roho kibaya na bila mapendo. . Hii kundi inahamakia na namna kibaya hawa watu wanayechukia watu wengine na hawawapende na hawawaonyesha wema. Mkubwa ya hii kundi alionekana ya kama aliteswa ya malari moja fulani, ya kama aliria na udanganyifu, aliomboleza na alifanya ma alama sawa vile wanafanya wamaskini na wenye mateso na wanaomba saidio na huruma. Lakini saa ingine huyu mkubwa alikuwa makali pamoja na watumishi ya kundi yake yote. Walihamakia, lakini hawakuweze kunipata ya kama nilikuwa bila wema, kwani nilikuwa murahimu sana. Nilisaidia wamaskini na wenye malari, katika nguvu yangu na wa shetani walismama na haya mbele yangu. Kisha wa malaika walinibeba na tuliondoka. Mu njia waliniaambia wa malaika: «Watu wenye mengi sana, walichunga ma amri ya Mungu, lakini, kwani hawakuonyesha wema kwa wenye mateso na malari, na maskini, wakati walifika hapa, walijianguka mu hadeze».

Mulango ya mbingu

Mukupanda yulu tuliangalia na furaha mingi mulango ya mbingu, iliyeangaza kama rikalashi wa nuru na akili ya mtu haiweze kuelejea hii maono. Mtu ya ile mulango alikuwa kijana moja aliyekuwa uso ya kujaza na mwangaza na musipi na ma nywele ya zahabu, aliyetupokea na furaha mingi, kwa sababu nafsi moja alifika ku mulango ya mbingu. Mukuingia ndani ya mbingu, tulifika ndani ya pepo wa matata, iliyekuwa ma fasi yote kama mufuko ma fasi yote. Chini ya hii pepo iliyekuwa kama nguo, ilikuwa hazina moja ya wa kijana, wenye waliangaza kama jua. Wakati walituona, walifurahi kwa ajili ya wokovu yangu, walinisalimia, na waliimba hata utamu mingi na ulimi ya mtu moja hakuna namna kuisema. Mimi nilijaza na furaha na nilitembea na wasimamiziyangu juu ya kusujudu Mfalme Yesu Kristu aliyeikaa pa Kiti yake ya matata. Mukupanda yulu tuliona mawingu, lakini haina kama hii mawingu yetu, lakini walikuwa kama mawa na walikuwa mazuri kuliko ya bile yetu. Kisha tuliona kukuja mawingu moja meupe na kisha ilionekana moja ingine na ragi kama zahabu na toka yake walitoshwa maumeme na moto. Kisha tulitembea tena na tuliona mu fasi yulu sana Kiti ya Mungu iliyeangazwa sana. Pempeni ya hii Kiti walisimama wakijana ma elfu mengi, wenye walivaa manguo ya zahabu na ya nuru mingi. Hii bintu yote niliona kule, ndugu, wangu Grigorie, misiweze kukuelejea, wala akili yako aiweze kuisikia.

Tulifika mu ngambo ingine ya Kiti ya Mungu, pahali tuliona utukufu wa ajabu Yake. Ile saa wa malaika, wenye waliniongoza, waliimba mara tatu na walitukuza Mungu na boka na heshima mingi. Kisha tulisujudu Mungu ya Utatu Mutakatifu mara tatu na pamoja na sisi hazina yote na wa malaika na wote walifurahi juu ya wokovu yangu.

Ile saa nilisikia sauti moja ya utamu sana iliyesema kwa Wamalaika wangu: «Muongoze huu nafsi ndani ya ma fasi ya paradizo na mu fasi ya gehena, sawa vile munafanya na ya ma nafsi yote na kisha mutapeleka huu nafsi mu makao ya mutumishi yangu padri Basile, kwa sababu kule yeye aliniomba kupumzika huu Theodora».

Tuliondoka toka kule na furaha mingi na tulitembelea ma nyumba ya Watakatifu, wenye walikuwa bila kuhesabu na waliangaza sawa vile mwangaza ya jua. Hii makao ya paradizo walikuwa ndani ya shamba moja urefu na upana sana na pahali walikuwa mawa na arufu mingi ya kuachana. Nikusema mu fasi moja walikuwa wa Mitume, mu fasi ingine wa Nabii, Washahindi,

wa Askofu, Watawa ya jangwa na makao ya kila mtakatifu ilikuwa na nzuri sana. Basi, hawa Watakatifu walitoka inje ya ma nyumba yao, na walitupokea na walifuraha kwa wokovu yangu.

wakati tuliingia ndani ya fasi ya Abrahamu, tulimuona na utukufu mingi na shangilio ya mbingu. Kule walikuwa na ma nyumba ya Isaka na Yakobo, wenye waliangaza na neema takatifu. Kule walipumzika na watoto ya wa Kristiani, wenye waliishi mu dunia, bila zambi. Kule walipumzika pa kiti kumi na mbili kama mwangaza ya jua wa Askofu kumi na mbili, toka yao walizaliwa ma kabila kumi na mbili ya taifa wa Yuda. Ma nafsi ya Watakatifu walionekana kama miili, lakini hakuna namna mtu moja kuwagusha na mukono, sawa vile, nikusema iko namna kubamba mtu moja na mukono yake mwangaza ya jua?

Kisha tulikwenda mu ile fasi ilikuwa ma gehena ya wenye zambi. Mtoto yangu Grigorie, niliona mafungo wa giza kuwa ya kujaza, sawa vile ni buchanga ya bahari, na ma nafsi ya watu wenye zambi tangu mwanzo ya dunia na walikuwa ndani ya umeme ya lufu. Kule aikusikiwa hata sauti ingine, paka «Ole kwetu, ole kwetu», lakini ombolezo na malalamiko yao hakuna namna kuelejea. Tulishuka chini ndani ya ile fasi ni gehena. Malaika moja aliniambia: « Ulitoka ya hii ma nyumba ya giza, kwa sababu ulitubu na ulisimama zambi yako na kwa ajli ya matendo yako madogo uliyefanya ao kusema kuliko nzuri kwa maombezi ya mpadri ya roho yako mt. Basile».

Wakati tulitembela makao yote ya gehena, malaika moja aliniambia: «Ee Theodora, unajua ya kama leo mpadri ya roho yako mt. Basile anafanya ukubusho ya lufu yako, kisha ma siku makumi ine? na, wakati alisema hivi, waliniacha ndani ya ile nyumba ya mpadri yangu mt. Basile na waliondoka. Ile saa mini nilisikia ya kama, kisha ma siku makumi ine tangu lufu yangu, nilifika mu nyumba hii unaiona na ile haina yangu, sawa vile unaiona, lakini ni ya baba ya roho yetu mt. Basile, mutumishi ya Mungu. Watoto ya roho yake, wenye anawafundisha na anawaongoza mu toba, kisha lufu yao, wanaikaa ndani ya hii nyumba ya nuru yake mu paradizo.

-Sasa kuja kuona na ma chumba yetu, hahali alikuja mbele ya saa kidogo mpadri yetu mt. Basile.

Mimi nilifata mama Theodora na tuliingia ndani ya lupago moja, ilioyekuwa chini maimbwe kama nuru na katikati yao walikuwa miti ya kuachana na wenye nzuri sana. Mama Tjheodora alivaa nguo moja meupe na pa kichwa yake alileta kitambala moja nyekunda, lakini toka uso yake ilitelemusha chini kama jashu manukato takatifu, iliyekuwa na harufu nzuri sana. Mukuona mu fasi ya mashariki niliona ma nyumba ya ufalme wenye ajabu, pahali tuliingia ndani na tuliona ma mungazi mazuri na meza takatifu na machakula ya kuachana mazuri, tena walikuwa makitambala na mawa ya harufu ya kuachana. Kiti ya Mungu ilikuwa maesombe, laki i wa ajabu na iliangaza kupita ya jua na wale waliokuwa ndani, walikula matunda na walifurahi.

Wale waliyekula, walionekana watu wenye kamili, hawakuwa ya kunenepa, lakini walikuwa kama ma ulimi ya jua na ma uso yao walikuwa vema na ya kujaza neema ya Mungu na hakuna uchanisho katikati ya wanaume na wanawake. Na, wakati walikula toka hii chakula ya roho, hii chakula hakuna namna ya kuishi, kwani ilikuwa chakula ya mbingu na ya roho. Katikati yao walisuburia na ma sauti utamu na mucheko ya furaha. Wa kijana wengine waliwapatia kukunywa ndani ya kilauri kama makalasi na wote walishiba toka utamu ya Roho Mtakatifu. Mimi niliwajabu saa ya kuenea, kwani ma uso yao waliangaza sana.

Mama Theodora alikuwa mbele yangu na alikaribia mpadri ya roho yetu na alimwambia juu ya mimi; huyu aliniangalia, alicheka kidogo na alinifanyisia alama kumukaribia. Mimi mukaribia, nilipika magoti mbele yake na niliomba baraka yake. Yule aliniambia: «Mtoto yangu, Mungu ninakutakia kuonyesha wema Yake kwako, akubariki na akustahili ya Ufalme wake wa mbingu». Na, wakati nilikuwa chini mbele yake, huyu alinilamuka na mukono yake na aliniambia: «Angalia, mtoto yangu Grigorie, eko wapi Theodora, kwani mara mingi uliniomba kufunda huyu eko wapi na anaikaa wapi. Basi, tangu sasa simama na kimya na usiniuzi mara ingine juu ya huyu mama Theodora».

Yule mwenye heri na mubarikiwa Theodora wakati aliniona na richo upole, aliniambia: «Mtoto yangu Grigorio, ninatakia kwa Mungu aripe muchoko yako juu ya hii mapendo yako uliyekuwa nayo juu ya nafsi yangu na Huyu katika matakio yako, na kwa maombezi ya mpadri ya roho yetu mt. Basile, alikustahili kukuja hapa, pahali sasa unaniona».

Kisha mt. Basile alisema kwa Theodora: «Uende mtoto yangu, na onyesha kwa Grigorio, ngapi mazuri ni hapa miti ya shamba yetu». Theodora alinibeba na aliniongoza mu fasi ya kuume, pahali ilikuwa mulango moja wa ajabu na katika zahabu na pempeni yake walikuwa ma kibabashi marefu na ya zahabu. Tulifungula na tuliingia ndani na tuyliona hii shamba iliyepambwa na ma miti na mawa ya kuachana na harufu yao ilikuwa nguvu na bila kuweza kuisema. Hii miti na mawa, walikuwa hivi daima, kwani na wasiyokufa na  wa mbingu na mimi niliwaangalia na ajabu mingi. Ile saa Theodora aliniambia:

-Kama, mtoto yangu, unashangaa juu ya ile bintu unaona hapa, utashangaa ngapi kuliko mingi, kama utaona Paradizo, pahali Bwana aliiweka mu fasi ya mashariki!

Mimi nilimuomba kunionyesha bile ma fasi ya ajabu ya yulu na yule aliniambia:

-Mtoto yangu, hakuna namna, kuona hii ma fumbo wa ajabu na ya siri, kwani uko tena ku uzima katika mwili yako mu dunia. Hii yote ma fasi ya ajabu uliiona hapa, aliparta mpadri ya roho mt. Basile, ambaye toka kipimo udogo yake alikombana na ma sala ya usiku na kufunga chakula na mateso mpaka miaka ya uzee yake juu ya kuikaa pamoja na watoto ya roho yake, waliyekombana na wlaichunga ma amri ya Mungu. Fanya na weye nguvu, ile wakati uko tena mu dunia, kukombana juu ya kuja hapa na tutafurahi pamoja mpaka Ufikisho ya Mbili ya Bwana Yesu Kristu wetu. Kwa sababu, kishas Ufikisho ya Mbili ya Bwana Yesu, Huyu Mungu wetu atatupatia kuliko furaha na ma fasi ya shangilio, sawa vile anasema na Mtume Paulo, ya kama hata risikio haikusikie, wala richo haikuone na akili ya mtu hasikusikie ninyi wote bintu aliyetayarisha Mungu kwa wale wanamupenda».

Mimi, wakati nilisikia ya kama misikukuwa kule na mwili yangu, lakini paka na nafsi yangu, nilishangaa na nilikombana kugusha mwili yangu juu ya kusikia ya kama nikona mifupa na nyama, lakini nilizania ya kama nilikamata nuru ya jua.

Basi, ndani ya musingizi yangu, niliona hii maono kubwa na nilikuwa na akili yangu na nilishangaa juu ya hii yote bintu niliona. Kisha ninakumbuka ya kama tulikuja mu lupago, tuliona meza tayari na ma chakula ya kuachana na watu pempeni ya hii meza. Ile saa nilikuja kwa maungo yangu na niliuhurwa toka ile bintu wenye ajabu kabisa.

Nilianza kuangalia maungo yangu na bile bintu niliona. Niliwaza na nilisema: Hii bintu ya ajabu niliona ni toka Mungu ao toka shetani? Nilienda  kwa mpadri ya roho yangu, mt. Basile juu ya kubeba baraka yake na kumuuliza. Wakati nilibeba baraka yake, huyu aliniuliza:

-Unajua, mtoto yangu Grigorio, ya kama hii usiku tulikuwa pamoja na tulifurahi ma bintu wa milele ya paradizo?

-Mimi nilimuonyesha ya kama misijue hata kintu komoja na nilimwambia: Mpadri ya roho yangu, nilikuwa mimi mu chumba yangu na nililala hii usiku.

-Ndivyo, mtoto yangu, ninajua na mimi hii mambo nzuri ya kama ulikuwa na mwili yako mu chumba ya nyumba yako, lakini na roho yako na akili yako ulitembea ma fasi ingine. Ninyi yote bintu nilikuonyesha hii usiku, usizanie ya kama ni ma ndoto, lakini maono ya kweli. Hii usiku usikwende kwa mama Theodora? Usikufike mu nyumba yangu wa mbingu? Usikukimbie juu ya kunitaguria na ulifika mbele ya mulango moja mnene, pahali alikuja mama Theodora na alikupokea na furaha kubwa? Huyu mama hasikukuseme kwako ile uhamakio aliipima toka ma kundi ya ma shetani? Wewe usikuingie mu lupago pamoja na mama Theodora katika amri yangu na uliona ile meza wa ajabu na bintu ya chakula na matunda, na mawa ya harufu na hawa wakijana, wenye walimisaidia? Usikusimame mbele yangu na mimi nilikuonyesha mama Theodora na uniombe toka mimi kujua mu hali gani eko mu paradizo? Na huyu mama

asikukuongoze katika amri yangu ndani ya ile shamba ya ajabu na uliona miti ya kuachana na mawa yao?

Wakati nilisikia toka kinywa ya mpadri ya roho yangu hii ma sauti yote, nilishangaa na nililekea. Kisha machozi mingi walitelemusha toka ma macho yangu na niliwaza urefu ya utakaso na miujiza ya mpadri ya roho yangu, ya kama ni malaika wa inchi na, anaikaa hapa na mwili yake, lakini katika roho na nafsi yake ni mbinguni.

Mtakatifu Basile kisha aliniambia: «Kama, mtoto yangu, utapita hii uzima yako, katika ma amri ya Mungu, unaepuka kila tendo kimbaya na unatumika kila fazila, paka vile mimi nitakupokea kule, kisha lufu yako, mu fasi ile alinipatia Bwana kwa mapendo yake mingi. Mimi, kisha nyakati kidogo, nitaondoka toka hii uzima ya dunia na weye utanifata na uzima ufazili na matendo mazuri, sawa vile Bwana Yesu alinifunua.

Sopoka, mtoto yangu, usiseme hata sauti moja toka hii ma sauti mimi nilikuwambia, ile wakati mimi nitakuwa ndani ya hii dunia. Kisha lufu yangu, utaweza, kama unataka, kuandika uzima na matendo yangu juu ya kupata faida ya roho na watu wengine.

Na, wakati alisema hii ma sauti yote, mpadri ya roho yangu, alinihamuru kwenda mu nyumba yangu na kuendelea kutumika juu ya wokovu yangu.

## 25. Fazila gani ulifanya na ulikuja na utukufu ya paradizo?

Wakati moja, inatuwambia kitabu moja, inayeitwa Gerontiko, alikuwa mutawa moja, aliyejaza roho yake na taabu na uzaifu; joo vile alikwenda kwa mpadri ya roho moja juu ya kungama na kusikia sauti ya faida ya roho. Yule mwenye ajabu na mumebaji-Mungu mpadri, alimushauria nzuri na kisha alimwambia hii hadisi ya ajabu:

-Wakati moja, ilikuwa nyakati ya Kwarezima Mkubwa na mimi nililamuka mbele ya saa kidogo ya kuanza ibada ya asubui mu kanisa. Nilinyanyua mikono na ma macho yangu mbinguni na niliomba ma saa mingi kwa Mungu katika machozi. Ile saa, akili yangu ilitoka na ilipita hii mbingu inayeonekana na ilienda kwa muji moja na watu mengi. Hii muji ilikuwa nzuri sana na haiweze akili ya mtu moja kusema ao kuiandika.

Hazina ya watu ilikuwa mingi sana, bila hesabu na walivaa ma vazi mazuri sana ya kuachana na pa kichwa yao walikuwa na ma taji ya diamant. Ma taji ingine walikuwa ma safi na matukufu kama makalashi, ingine walikuwa kama zahabu na mapambo ya maimbwe.

Mukuona mimi hii bintu ya ajabu yote, nilisikia lazima kuuliza wale waliyevaa ile ma taji, ma fazila ninyi walifanya mu uzima yao na walistahiliwa kuishi ndani ya hii muji wa ajabu na ustahili ya wivu na kuwa na hata mingi utukufu na sifa?

Nilikaribia, basi, mtu moja aliyevaa ma nguo na ma pambo mingi na taji yake ilikuwa na nuru ya jua na nilimuuliza: Fazila gani ulifanya na ulikuja mu utukufu ya paradizo?

-Mimi, ndugu yangu, alinijibu yule, nilikuwa maskini na mwenye uhagaiko, mugonjwa na muvivu, mtu ya kilema na mwenye katika malari mu kipimo udogo yangu. Lakini, kwa sababu, nilivumilia na shukrani hii sikitiko na moto ya usikini na uhagaiko ya malari yangu, bila kupotesha kitumaini yangu, nilistahiliwa toka Mungu mupenda-wanadamu, kisha lufu yangu, kuikaa ndani ya hii utukufu na furaha unaniona sasa.

Nilimwacha huyu mtu na nilifika kwa mtu mwingine na uso yake ilikuwa na mwangaza kama mwezi, mavazi na taji yake walikuwa toka maimbwe ya kuachana ya kupambwa nzuri. Nilimufanyisia na kwa huyu ulizo umoja na yeye alinijibu:

-Mimi, ndugu, nilikuwa mutawa mu uzima yangu na nilitumika na muchoko mingi kwa matendo ya uzima utawa na nilifanya uvumilia kwa majaribu na ma taabu ya hii uzima. Kwa miaka ya uzee yangu, nilishindwa toka mawazo ya utukufu na nilikwenda inje na nilifanyika askofu. Nilitembesha kundi ya waminifu yangu katika boka ya Mungu na nilimaliza makazi

yangu ya kupaswa nzuri na neema ya Mungunilikuja hapa kwa hii furaha unaniona. Lakini, kama misikutoke ya Monasteri yangu na kama niliisha kuzarau hii utukufu ya dunia, sasa ilikuwa namna kuwa na mimi ya kujaza nuru kama jua, sawa yule ndugu uliyemuona mbele na ulisuburia naye.

Kisha ya huyu mpadri nilikwenda kwa mtu mwingine aliyevaa pa kichwa yake taji moja toka argint; uso yake ilikuwa na furaha na mavazi yake ilikuwa meupe kama teluji. Nilimuuliza fazila gani alitumika duniani na alifika hapa. Na yeye alinijibu:

-Mimi, ndugu yangu, nilikuwa mtu ya bure mu uzima yangu na nilitumika kutafuta makuta juu ya uzima yangu, sawa vile na Mungu anatwaambia. Wakati nilifika mu kipimo kizuri, nilindowa bibi na nilizala watoto, ninyi wote Mungu alinipatia na mu uzima yangu yote misikujua mwanamuke mwingine, paka bibi yangu. Niliisha mu maisha yangu, bila kuuzi mtu mwingine, wala nilichunga mtutu mwingine, waala nilishitaki, wala nilizulumu. Nilifanya, kama niliweza, huruma na saidio; misikulofe toka Kanisa na Ma Fumbo takatifu na katika boka na mapendop ya Mungu nuiliishi uzima yangu. Kwa hivi, kisha uchanisho nafsi ya mwili yangu, nafsi yangu ilikuja na inapumzikakwa hii makao, unaniona sasa pamoja na wenye haki.

Nilimwacha na huyu na nilienda kwa wengine wa wili; moja alikuwa na taji pa kichwa yake kwa chuma na mwingine kwa shamba na ma uso yao walikuwa sawa ma uso ya watu wa dunia. Ma vazi yao walikuwa safi bila mwangaza. Niliwauliza walifanya ninyi mu uzima yao na hawa walinijibu:

-Sisi, ndugu wetu, tulikuwa watu wa zambi mu uzima yetu; tusikuacha hata zambi moja, bila kuifanya. Kwa sababu tusikupende kuacha zambi yetu na mapenzi yetu, ilikuja lufu na amri ya Mungu kutukata kama miti wasipo matunda na kututupa mu gehena. Lakini kwa ile saa ya lufu ya mwili yetu, tuliwaza na akili yetu wema ya Mungu na hii ma sauti yeye alisema ya kama hasipenda lufu ya mtu mwenye zambi mpaka kurudia na kuishi; hivi tulitubu sana na roho ya kuvunjika na maungamo na hivi tulipata tunzo ya nafsi yetu. Ile saa, tulipatia malako kwa Mungu ya kama na nguvu yote ya nafsi yetu, tutasimama kamili zambi yetu na tutawachukia.

Vile tulionyesha kitubio yetu kwa Mungu na tuliomba Mtakatifu kamili Mzazi-Mungu Maria na Watakatifu wote juu ya kutusaidia na tusirudie mukongo. Namna gani nitakuambia, ee ndugu wangu, wema ya Mungu wa mbingu, aliyeonyesha kwa sisi, lakini na kwa watu wenye zambi yote? Mpaka saa ya mwisho Yeye anatuita kutubu, sawa vile alifanya na kwa munyanganyi, wakati alikuwa pa Musalaba!

-Hii ma sauti ya utulivu waliniambia hawa wa ndugu, wenye, walikuwa zamani wenye zambi, lakini, kwa sababu waliogopa gehena na walitumainia kwa rehema takatifu, walisafishwa na machozi ya toba na waliingia kwa makao ya pumziko wa milele.

Hii ma sauti aliniambia huyu muzee mpadri na kisha alinamisha kichwa yake chini, na aliomboleza toka roho yake. Mimi niliwaza hivi: Ole kwangu na wa ndugu wengine wenye zambi pamoja na mimi! Kama huyu mpadri muzee anaria na anaomboleza nguvu, aliyestahiliwa kuona matendo ya ajabu mengi ya ile dunia ya milele, ngapi mimi inapaswa kuomboleza na kuria kila siku kwa ajli ya zambi yangu?

## 26. Musopokeni, wa ndugu, kukumbuka ile saa ya lufu yenu

Hii hadisi nitamiambia sasa, nilipata mu kitabu moja inayeiko kwa Monasteri moja ya Kilima Takatifu. Aliisema hii hadisi mutawa Kirillo, aliyetumika mu kazi ya kusaidia wapadri wazee.

«Ku mwaka 1918 nilisaidia mu nyumba ya wa padri wazee ya Monasteri yetu mutawa moja muzee, aliyeitwa muzee padri Isihios, aliyezaliwa mu mukini moja ya njimbo Ipiros ya Grekia na aliyekufa mu kipimo yake miaka 58. Wakati ilikaribia saa ya lufu yake na walikuwa wa ndugu wengine pempeni ya kitanda yake na walimutulivu, yule aliomboleza toka chini ya roho yake na

alisema hivi na taabu mingi na machozi: «Musopokeni, wa ndugu, kukumbuka ile saa ya lufu yenu, kwa sababu hii ukumbuko inamiletea boka na, kama mulikosana kama watu wenye zambi, munaweza kutubu na kuungama na kusamehewa. Mimi mwenye zambi misikuwa na ukumbusho ya lufu na nilifanya na zambi mingi, bila kutubu, sawa vile nilipaswa na kusamehewa. Tazama, basi, sasa nilijitoa kwa joka-shetani na huyu pole-pole ananikunywa; tazama sasa alinikula mpaka kati ya mwili yangu. . . » Na mukusema hivi na maombolezo na taabu mingi, alitoa roho yake kwa mikono ya shetani.

Huyu padri Kirillo, musaidizi ya wapadri wazee ya Monasteri yake, ananiambia na hadisi ingine, hivi: «Na ndugu mutawa mwingine, aliyeitwa Antonio, wakati ilikaribia saa ya lufu yake, alikuwa na boka na tetemeko mingi, na hasikuweze kupata kimya hata kidogo; joo vile alikaruka chini ya kitanda yake na alijifuchana chini ya kitanda ya kona moja, kwa sababu alizania ya kama ataokolewa, kama atajifuchama toka ufukuzo ya ma shetani. Kule, basi, chini ya kitanda, tulimupata kutoa nafsi yake, bila sisi kujua kama alibeba Mungu ao shetani nafsi yake, mu mwaka 1916.

## 27. Ee Ndugu Akakios ulikufa?

Hii hadisi inajitangaza mt. Yoane wa Savaitis kwa mtakatifu Mutawa Yoane, mwandishi ya kitabu inayeitwa «Mugazi», padri mkubwa ya Monasteri ya Sinaya na sisi toka hii kitabu tuliiandika kama deni. Hadisi ni hii:

« Mu Monasteri yangu alikuwa mutawa muzee moja, aliyekuwa muzaifu sana na mwenye zambi. Hii ninasema hapana juu ya kumuhukumu, lakini juu ya kuonyesha kweli hii hadisi. Huyu, basi, misijue, namna gani alikuwa na mwanafunzi ya roho moja, aliyeitwa Akakios. Huyu alikuwa mtu mupole na mwenye akili. Alivumilia mateso mingi toka mpadri ya roho yake. Huyu mpadri ya roho yake alimupiga, alimuchekelea, alimutema, alimuchabula kila siku. Lakini Akakios, mwanafunzi ya roho yake alivumilia. Hii uvumilia yake ilionekana kama bunya, lakini haikukuwe bunya, Ilikuwa na uhodari na kadiri yake.

Wakati nilimuona mimi kuteswa hivi kila siku, kama mutumwa, nilimuuliza mara mingi, wakati nilimukutana: «namna gani uko, ee ndugu Akakie? Namna gani ulipita leo? na huyu mara moja alinionyesha siku moja richo yake ilikuwa ya kuvimba, kwani mpadri ya roho yake alimupika na kofi, siku ingine sigo yake ilikuwa na kilonda, siku ingine kichwa yake iliisha kuvimba. . . Mimi, kwani nilijua ya kama yeye eko mutumishi ya ma fazila ya kristu, nilimwambia: «Fanya uvumilia. Unatebea nzuri! Utapata faida ya roho mnene. Fanya uvumilia? .

Ilipita wakati ya miaka tisa na huyu mutawa Akakios alikufa. Kisha ma siku tano, toka lufu yake, mutawa mkubwa na baba ya roho ya Akakios, alikwenda kwa mutawa mwingine aliyeishi kule karibu na alimwambia:

Ee mpadri, mutawa Akakios, mtoto ya roho yangu, alikufa.

Yule, wakati alisikia hii tangazo, alimujibu:

Ee Muzee mpadri yangu, unisadiki ya kama mimi misisadiki hii tangazo yako.

Huyu basi, alimwambia: Kuja kuona.

Alilamuka mbio na pamoja na mpadri ya roho ya Akakios walitembea mbio na walifika mu fasi ile walimumazika mutawa Akakios. Alikaribia yule mutawa ya jangwa kaburi ya Akakios na alimuuliza:

-Ee Ndugu Akakie, ulikufa?

Yule mufwasi muzuri alionyesha uitii na sasa, na kisha lufu yake, na alijibu kwa huiyu mpadri:

-Namna gani iko namna kukufa, ee mpadri, mtu moja, mwenye ni mutumihsi ya utii?

Ile saa yule mutawa aliyekuwa mpadri ya roho ya Akakios, alipata boka na alianguka na uso yake chini ya inchi na alitosha machozi mingi. Kisha alisema kwa mpadri mkubwa ya ile

Monasteri kuyenga chumba moja karibu ya kaburi ya mtoto ya roho yake. Kule aliishi na toba na uzima safi uzima yake ingine mpaka mwisho ya uzima yake.

**28. Misinana utukufu ya Watawa. . .**

Mu Kitabu ya uzima ya Mtakatifu Mutawa Mkubwa Paisios, aliyemushangilia Kanisa yetu mu tarehe 19, ya mwezi sita, ndani ya hii historia ya uzima yetu tunasoma hii zungumuzo aliifanya mt. Paisios pamoja na Mt. Mfalme Konstatinos, aliyeshuka kwa inchi yetu na alisuburia na mt. Paisios. Zungumuzo yao katikati yao ni hii:

-Mweye muko mwenye heri kwani mulistahiliwa kufata uzima ya utawa, kwa sababu kweli hii sauti ya Heri ni kwa mweye.

-Na nani uko weye, alimujibu Mutawa Paisios, unasema hii ma sauti na unatukuza hata mingi sisi watawa?

-Mimi ni Konstantinos, mfalme mukubwa, ambaye nilikuja chini toka ma mbingu juu ya kukuonyesha utukufu, ile wanapata Watawa kwa mbingu na ile uwezo wekona yo karibu ya Kristu. Ninatukuza wewe, ee Paisios, kwani unashauria hawa wa kijana kwa hii uzima ya utawa na ninahukumu maungo yangu, kwa sababu misikuweze kufata hii uzima ya watawa na misiweze sasa kuvumilia hii hasara nilipata hapa, kwani misikufate hi uzima ya Watawa.

-Juu ya ninyi, ee Mfalme mweye ajabu, unahukumu maungo yako? Wewe usikupate ile utukufu na mwangaza ya paradizo?

-Ndivyo, niliipata, lakini misina na hii uwezo na utukufu wekona Watawa, wala kipande sifa yao, kwani niliona ma nafsi ya Watawa wengine, kisha uchanisho ya mwili yao kwa lufu yao, ya kama waliluka kama ma ndege kipepeo-kuku na uwezo mingi, walipanda mbinguni. Na kundi ya ma shetani hasikuweze hata kuwakaribia ma nafsi ya wale Watawa. Kisha, niliona ya kama walifungula milango ya mbingu, watawa waliingia ndani, walisimama mbele ya Mfalme na walikuwa na uwezo mingi mbele ya Kiti Yake. Kwa ajili ya hii uwezo na utukufu yao, ninashangaa mweye Watawa, ninamisema wa heri na ninahukumu maungo yangu, kwa sababu nisikustahiliwa kupata hata uwezo kidogo. Ilikuwa namna kuwa mwenye heri, kama niliacha hii ufalme yangu ya dunia na taji yangu, na kisha nilitoka kwa Monasteri moja juu ya kuvaa nguo ya watawa na kufanya kila tendo kizuri juu ya kufurahi.

-Hii ma sauti uliniambia, ee Mfalme, ni mazuri na unatulivu sana; lakini hivi ni na ma naziri ya Mungu, kwani Muhukumu mwenye Haki anapatia katika haki yake na katika machoko ya kila mtu anapatia na malipo ya roho, kwa sababu na uzima yako haikukuwa na machoko mingi sawa uzima ya watawa, wala ilikuwa umoja na uzima Wa watawa. Kwa sababu weye ulikuwa na bibi kama musaidizi yako, ulikuwa na watoto, watumwa wako na ma furaha na matendo yote. Lakini watawa walizarau ma bintu ya furaha yote ya hii uzima; walibeba mu uzima yao paka Mungu na Huyu alikuwa furaha na mali na kitumaini yao. Basi, hakuna namna kubeba wewe, ee mfalme, malipo umoja na malipo ya Watawa. . .

Hii mazungumuzo yao, ilisimamisha utembeleo ya ndugu moja, aliyekuja mu chumba ya mutawa Paisios, na mt. Mfalme Konstantinos alipanda mbinguni.

## 29. Nilipata hazina ya furaha mingi mu mbingu. . .

Mu Kitabu ya Uzima ya Watakatifu wetu iko historia moja ya askofu Sinesios ya muji Kirini juu ya murafiki moja yake aliyeitwa Evagrios. hii historia iko hivi:

Ma siku, pahali alikuwa Patriarhi ya Aleksandria ya Misiri mtu moja aliyeitwa Theofilos ( ku mwaka 411), alifanyika askofu ya muji Kirini mtu moja mwenye akili aliyeitwa Sinesios. Huyu, wakati alikuja mu njimbo yake kama askofu alileta naye na mrafiki yake Evagrios. Askofu

Sinesios alifanya nguvu juu ya kusaidia Evagrios kusadiki wa Imani ya Kristu, lakini huyu alikataa kufata ma sauti yake.

Siku moja Evagrios alisema kwa Askofu Sinesios:

-Ninakuambia kweli, ee askofu Sinesios, ya kama misiweze kusikia hii ma sauti mweye wa Kristiani munasema ya kama itajifanya mwisho ya dunia na ya kama watu wote watafufuliwa na mwili yaoumoja, na hii mwili yao itambakia kwa milele bila uharibifu na bila lufu na ile siku ya mwisho watu watabeba malipo ya roho katika matendo yao. Tena ainipendeze hii sauti munasema ya kama huyu anayesaidia mtu maskini iko sawa kupatia deni kwa Mungu na huyu anayepatia makuta yake kwa wamaskini, atapata ma hazina mingi mbinguni na kwa ile siku ya Ufufuo ya watu wote na atapata furaha mingi kwa milele. Hii ma sauti mweye munasema ni kama ma neno ya uwongo na ya bure.

-Mwenye heri askofu Sinesios, alimukikiri ya kama hii ma sauti yote ni ya kweli na kisha wakati kidogo alimusaidia yeye kusadiki na kubatizwa pamoja na watu ya nyumba yake. Basi, wakati alibatizwa Evagrios, alipatia kwa askofu Sinesios mia tatu litre ya zahabu juu ya kuikabula kwa maskini mukusema kwake hivi:

-Kamata hii ma feza na uwakaburia kwa wamaskini na uniandika barua yako moja na mukono yako ya kama Bwana Yesu Kristu atanipatia kwa mimi, kwa uzima ya milele.

Askofu Sinesios, aliandika na mapendi hii barua, iliyeomba Evagrios na aliimupatia. Kisha wakati kidogo alipata malari Evagrios na alifika ku mwisho ya uzima yake. Alipatia hii barua kwa watoto wake na aliwaambia kuweka hii barua ndani ya sanduku na karibu ya mwili yake, bila kujua mtu mwingine hii mambo.

Kisha ma siku tatu, tangu lufu yake, alionekana Evagrios usiku kwa ndoto kwa Askofu Suinesios na alimwambia:

-Fugula kaburi yangu na beba hii barua yako, kwa sababu nilipata hii deni yangu na misitake kuomba hii denia toka weye na tazama, angalia ya kama niliandika na mimi na jina yangu hii barua na mukono yangu.

-Askofu hasikujue ya kama pamoja na maiti ya Evagrios waliweka watoto yake na hii barua yake. Asubui, basi, aliita watoto ya Evagrios na aliwauliza, kama waliweka barua moja mu kaburi ya baba wao na wale watoto walimwambia:

-Ndivyo, ee Askofu, wakati baba yetu alikuwa karibu ya kufa, alituita na alitupatia hii barua na amari yake sisi tuliiweka ndani ya sanduku yake, bila kusema hii mambo kwa mtu mwingine fulani. Ile saa Sinesios alionyesha maono yake iliyeona ile usiku ilipita.

Basi, alibeba watoto ya Evagrios, watu wengi na waKristiani na walikwenda kufugula kaburi na walipata maiti ya Evagrios kuchunga kwa mukono yake hii barua ya askofu. waliifungula na waliona na ajabu mingi ya kama Evagrios aliisha kuandika na mukono yake maneno yake ingine na jina yake ku mwisho; Aliandika hivi: «Mimi Evagrios, mwenye akili, ninasema kwa weye Askofu Bwana Sinesios kufurahi. Nilifurahi sana toka Bwana wetu Yesu Kristu hii deni, iliyeandikwa ndani ya hii barua yako na nilipata furaha kuliko mingi ya mara mia kwa mbingu na uzima wa milele, sawa vile ulinilaka. Kwa hivi sasa ninatukuza Mungu na ninashukuru weye, kwani uliniongoza kwa nuru ya milele?

Ile saa, ninyi wote walikuwa kule karibu ya kaburi, walishangaa. Waliona ma sauti ya kuandikwa ndani ya ile barua na walitukuza Mungu. Kisha waliimba pamoja: Bwana hurumia» mara mingi.

## 30. Ole kwa wale wanafanya zambi na hawatubu. . .

Hii Historia niliibeba toka Kitabu ya Watakatifu ya Mwezi Ine mu tarehe 24. Ni hii:

Ku miaka ya mfalme ya Konstantinopoli, aliyeitwa Iraklios na minister ya kwanza alikuwa Nikitas ku mwaka 625 aliishi mu muji Karthageni ya Afrika ya kaskazini muaskari moja toka

kundi ya mfalme na, kwa sababu ndani ya muji ilizambalishwa malari moja epidimie, huyu alibeba bibi yake na alienda mu fasi ingine, inje ya muji juu ya kuokolewa toka epidimie. Kule shetani alimuwambia kufanya zambi na huyu maskari alianguka mu zambi pamoja na mwanamuke mwingine, aliyekuwa bibi ya mulimanzi yake. Kisha alipata hii malari na alikufa. Kisha ma saa tatu, tangu maziko yake, alianza kupaza sauti toka kaburi yake na kusema: «Munihurumie». Wakati walifugula kaburi yake, walimupata muzima, lakini hasikuweze kusuburia. Kisha ma siku tatu alisuburia na alisema hivi: «wakati nafsi yangu ilikuja saa kutoka toka mwili yangu, niliona ma shetani wenye makali na wenye matata ku uso yao, wenye walikuja kunikamata na walinikombana. Kisha niliona wa kijana wa wili wenye nzuri sana na nafsi yangu ilifurahi. Wenye walinibeba na tulipanda pamoja mbinguni. Mu njia ma kundi ya ma shetani walihamakia kila zambi yangu; walikuwa ma kundi ya uwongo, ya chuki, ya upenda-feza na ma kundi ingine. Pempeni ya hii zambi niliisha kufanya mimi, wa malaika walijibu kwa shetani na matendo mazuri niliisha kufanya. Wakati tulifika kwa mulango ya mbingu, alitukutana sisi kundi ya usharati, na huyu shetani alisema juu ya hii zambi ya usharati niliofanya na yule mwanamuke mugeni, mbele ya lufu yangu. Ile saa ma shetani walinishinda na walinishuka mu fasi chini sana ya gehena, pahali ni ma nafsi ya wenye zambi na wanapima umivu na ombolezo mingi, na hii umivu na mateso mimi misiweze kusema ao kuiandika.

Mimi, wakati nilishuka kule, niliomboleza na niliria. Ile saa walionekana mara ingine hawa wakijana wenye mwangaza, kwa wenye niliwaambia na machozi kunipatia nyakati ya kutubu. Ile saa wale walisema katikati yao:

Unaichika juu ya huyu muaskari, ambaye anasema ya kama atatubu? .

Mwingine alimujibu: ninaichika.

Basi, walipanda nafsi yangu na walimuletea mu kaburi. Mukuona, basi, mimi mwili yangu kuwa sawa uchafu na matope, misikutake kuingia ndani yake. Ile saa hawa wakijana waliniambia:

-Hakuna namna kutubu, kama usitaingia mara ingine ndani ya mwili yako na katika saidio yake utasindana na utatubu, kwani pamoja na hii mwili ulifanya hii zambi ya usharati.

Basi, mimi niliingia ndani ya mwili yangu na, wakati mwili yangu ilikuwa muzima, nilianza kufokea nguvu:

Hawa watu walinisikia kupaza sauti toka kaburi yangu na kusema: «Munihurumie», walipata faida ya roho mingi na walitaabu kila mtu juu ya ma zambi yake. Nilisikia muzima mu afya yangu na watu wengine walinipatia chakula, lakini misikuweze kula. Niliwaambia kwenda mu Kanisa. Ndani ya kanisa, basi, nilianguka chini na nilisema na sauti nguvu: «Ole kwa wale watu, wenye wanafanya zambi na hawatubu. . . Inawaongojea gehena ya matata na uhukumu ukali kabisa! . . . »

Huyu mutu aliishi, kisha ufufuo yake ma siku makumi ine. Alisema muujiza yake na kwa watu wengine mengi, wenye walipata faida ya roho mingi na walitubu. Mbele ya kufa ma siku kumi na mbili, alikamata ujulisho ya kama atakufa na hivi alitayarisha nafsi yake na kifungo ya chakula, sala na toba na hivi alienda mu paradizo.

## 31. Inapaswa kumurudia huyu mukongo na mutanileta hapa mutawa Athanasios. . . .

Hii maono alistahiliwa kuiona mpadri mkubwa Kosmas, aliyekuwa mpadri mkubwa ya Monasteri moja ya muji Konstantinopoli, ku mwaka 932.

Mwaka fulani aligonjwa sana na alimbakia pa kitanda huyu mpadri Kosmas ya mwezi tano. Basi, siku moja, alikuwa sawa mazimu; ya ma saa sita ma macho yake walikuwa ya kupindwa na kuangalia mufuniko ya nyumba yake. Vile aliangalia na alisuburia na enye fulani na alisuburia na ma sauti bila kusikia sisi alisemaka ninyi. Wakati, kisha saa kidogo, alirudia mu akili yake, alisema kwa watawa waliyekuwa pempeni yake: «Munipatie ma kipande wa wili ya mukate, ile

nilibeba mbele ya saa kidogo toka Mpadri mkubwa». Wa ndugu, walisikia ya kama aliona maono moja ya ajabu; walimwambia kuwalejea ma fumbo ninyi aliona. Asubui, basi, walikuja watawa wote ya Monasteri mu chumba moja na mpadri mukubwa yao aliwamabia hivi: «Wa ndugu na wapadri wangu, ninataka kumielejea niliona ninyi, lakini hakuna namna kusema na ulimi ya mtu; nitamiambia paka ninyi wote ninakumbuka na ninaweza kumielejea. Niliikaa pa kitanda yangu na wa ndugu wengine walinikamata juu hapana kuanguka chini. Mu fasi ya kushoto yangu nilkiona watu wadogo wenye makali na mbaya. Ragi ya ma macho yao ilikuwa nyekunda na waliniangalia kama ma nyama makali na wauaji.

Basi, walikuja karibu ya kitanda yangu na walikuwa tayari kunibeba. Kwani nilikuwa kitumaini kwa mweye, wenye mulisimama pempeni yangu, misikuwaogopa sana; lakini kisha nilisikia ya kama nilikuwa wa pekee, bila mweye, na nilikuwa kwa mamlaka yao. Wa shetani wengine walinikokota na wengine walinisukuma mupaka walinipeleka ku mutoni moja, pahali walinishuka. Mu ngambo ingine ilikuwa njia moja mwembaba na ilikuwa namna kupitisha hata muguu moja ya mtu moja. Toka hii njia mwembaba walinishuka chini na mimi, kwani niliogopa ya kama ilikuwa namna kutelemuka chini, nilitembea mu fasi kabisa ya kuume. Chini alitembea mutoni moja iliyefanya bikelele mingi.

Kisha hii njia ilikuwa mulango moja, iliyekuwa ya kufugula na alisimama kule shetani moja mukubwa, mwenye matata kwa uso yake na toka kinywa na ma macho yake walitosha ma ulimi ya moto, lakini toka pua yake ilitoka simoko; ulimi yake ilikuwa inje na kipimo yake ilikuwa karibu metre moja; mukono ya kuume yake ilikuwa na buzito na baridi sana na mukono ya kushoto ilikuwa utupe kama nguzo na urefu sana. Na hii mukono alikamata wenye zambi na aliwatupa ndani ya hii mutoni, pahali ilikuwa namna kusikia paka» «ole kwetu, ole kwetu. . . »

Wakati tulikaribia kule, huyu shetani mkubwa alisema: «Huyu ni mrafiki yangu» na pamoja na ma neno yake alifugula mukono yake kunikamata. Mimi nilipata boka mingi na nilitetemeka. Mara moja walionekana mbele yangu wa Padri weshimiwa wa wili na mimi nilizania ya kama walikuwa wa Mitume Andreas na Yoane. akati aliwaona shetani mkubwa, aliogopa na alijifuchama. Watakatifu wa Mitume walinibeba na toka mulang moja mwembaba walinileteа mu kiwanja moja, iliyekuwa ma mukini mazuri sana. Kisha hii kiwanja tulikutana fasi moja ingine na mayani maesombe ya nzuri sana na furaha mingi na neema ya hii fasi hakuna namna mutu ya kuisema na kutuelejea. Katikati ya hii fasi alikuwa mpadri muzee moja mweshimiwa na pempeni yake walikuwa hazina ya watoto wadogo na hesabu yao ilikuwa kuliko mingi ya hesabu ya buchanga mu bahari.

Nilitosha mimi boka ya roho yangu na niliwauliza ni nani huyu mpadri muzee na hawa watoto wenye wanaikaa pempeni yake? Wafwasi wangu walinijibu: « Huyu muzee ni Abrahamu na fasi yake». Ile saa mimi nilienda na sauria ya Wasimamizi yangu, kumusujudu na nilimubusu na heshima mingi.

Nilitembea kidogo ku mbele na tulifika mu kiwanja moja, pahali walikuwa miti ya mizeituni, sawa ma nyota ya mbingu. Chini ya kila muti ilikuwa hema moja na ndani yake kitanda moja na yulu ya hii kitanda alikuwa mtu moja. Ndani ya wale ma hema niliona watu wengi, wenye niliwafamia toka dunia yetu na watawa toka Monasteri yetu, waliyekufa zamani.

Wakati niliwaza kuuliza wasimamizi yangu ni ninyi hii shamba ya mizeituni, walinitaguria wale na waliniambia:

-Unawaza ninyi na unashangaa juu ya hii shamba ya mizeituni na ma nani ni bile bintu unaona ndani yake? Hii ni bile bintu inatwaambia Mandiko Takatifu na Wapadri Watakatifu wetu, ya kama watakuwa mu Ufalme ya Mungu ma nyumba mengi, pahali wataikaa wenye stahili.

Kisha hii kiwanja ilikuwa muji moja na ilikuwa nzuri sana na hakuna namna kusema mtu mwingine. Mu kibabashi ya ile muji walikuwa milango ya kupambwa na zahabu na argint na muskingi chini ilikuwa na zahabu na hii muji ilikuwa na ma nyumba na ma kiti na ma meza ya

zahabu. Muji muzima ilikuwa ndani ya mwangaza, ilitosha ma fasi yote arufu na walikuwa ma furaha mingi ya kuachana. Tulitembea ndani ya muji, lakini hatukuone ndani hata mtu moja, wala nyama, wala ndege, wala nyama ingine ao kintu toka bile bintu ni hapa mu dunia yetu. Mu yakona ya muji walikuwa ma nyumba ya ufalme ya ajabu kabisa, pahali mu ingio yao ilikuwa meza moja ya kuyengwa na riimbwe ya muji Roma na pempeni yake waliikaa hazina ya watu na walifurahi.

Mu yakona ya hii chumba ilikuwa kibabashi na chumba ingine urefu na karibu yake fasi moja ya jua, pahali waliingia ndani wakijana wa wili, wenye walikuwa ma uso yao kama jua, na hawa walisema kwa Wasimamizi waazee yangu: «Mumuwambie kuikaa na huyu pa hii meza».

Pamoja na neno yao walinionyesha na kilole yao na makao pahali waliniambia kuikaa. Kisha waliondoka ya fasi ingine ya ile nyumba wa nuru. Lakini mimi niliangalia na ajabu hii nyumba na ma bintu ya chakula ya ile meza, tena niliangalia na watu mengi, wenye niliwafamia ya hii uzima yetu. Ilipita ma saa ya kuenea na kisha walikuja kwa sisi hawa wakijana wa wili na walisema kwa Wapadri wazee wetu: «Inapaswa kumurudia huyu mukongo na mutaleta hapa mutawa Athanasios toka Monasteri ya Trayanos. Hii ugeuzo inajifanya, kwa sababu Kristu Rabi wetu aliwema watoto ya roho yake, wenye wanataabu na wanaomboleza kwa ajili ya ondoko yake».

Vile, basi, hawa waPadri wazee walinibeba na tulirudia mukongo toka njia ingine ya mbio-mbio. Mu hii njia yetu, tulikutana ma ziwa saba pahali walikuwa ma namna ya gehena ya kuachana, kwa sababu ziwa moja ilijaza na giza mingi, ingine ziwa ilikuwa na moto, ziwa ingine ilijaza na uchafu, ingine na ma bilulu na ingine ma bintu beingine ya kuachana. Ma ziwa yote walikuwa na ma hazina bila kuhesabu ya watu, wenye waliria na waliomboleza na machozi na taabu mingi.

wakati tulipita hii ma ziwa, tulipata mbele yetu Mpadri mweshimiwa Abrahamu, nilimusujudu mbele na nilimubusu. Yule alinipatia kikombe moja wa zahabu ya kujaza vinyo na asali. Kisha alinipatia ma kipanda tatu ya mukate na nilizania mimi ya kama nilikula kipande moja na nilikunywa vinyo yote. Ma kipande wa wili ingine, nilizania ya kama niliiweka ndani ya rikwapa yangu na kwa hivi jana nilimiambia iko wapi ma kipande wa wili ya mukate? Kisha saa kidogo tulipita toka yule joka-shetani mkubwa na mwenye giza, mwenye, wakati alituona, alipiga meno yake mukusema na kisilani na uchungu:

-Sasa uliokolewa toka mikono yangu, lakini kisha mu uzima yako, misitasimama kuleta kwazo na bintu mbaya mu uzima yako na kupingana ya Monasteri yako.

Hii mambo weko, ninyi wote nilikumbuka, wapadri na wa ndugu yangu. Namna gani sasa nilikuja kwa maungo yangu, misijue hata kidogo!

Wakati alisema hii ma sauti yake mpadri mkubwa Kosmas, alikwenda mutawa moja kwa Monasteri ya Trayanos na alipata mutawa Athanasios ya kuisha kufa na walimupeleka pa kitanda yake juu ya kumumazika. Wakati aliuliza, saa gani alikufa Athanasios, walimwambia ya kama alikufa jana saa ya tisa, nikusema kwa ile saa Mkubwa padri yetu Kosmas aliona hii ono na alirudia kwa maungo yake.

## 32. Juu ya ninyi unaendelea kufanya zambi? . . .

Mu wakati ya mfalme Konstantinos Mukubwa, aliishi mu muji Konstantinopoli mwaminifu moja, mwenye kwa ajili ya fundi yake alimufamia mfalme Konstantinos. Huyu alipita uzima yake na kila zambi na uzulumu, bila kuwaza hata siku moja ya kama iko gehena. Lakini Mungu, ambaye anapenda kiumbe Yake na anafanya kila kintu kizuri juu ya wokovu ya kila mtu, alionekana Huyu mumoja kwa maono moja na aligeuza uzima kibaya yake.

Siku moja, basi, huyu mwaminifu anaona mu ndoto yake ya kama alitoa kwa Konstantinos mfalme tendo moja ya fundi yake na alisuburia naye na uwezp na alifurahi. Kisha aliona mfalme,

mwenye alitosha upanga moja na alimukamata na ma nywele yake, alikuwa tayari kukata kichwa yake. Yoane, hii ilikuwa jina yake, alinamie chini kichwa yake, kwa sababu alizania ya kama mfalme anacheza pamoja naye. Lakini huyu mfalme alimuona na uso ukali na alimwambia:

-Wakati upanga itakata ma nywele yako, mara moja sigo yako itajaza na ma damu yako.

Basi, ilimuonekana ya kama kweli ilijikata kichwa yake na, wakati upanga ya mfalme iliisha kufika mupaka kilari yake, ile saa kwa ajili ya boka yake aliomba saidio. Basi, alilamuka mara moja na alishangaa juu ya hii ndoto aliiona na alifanya musalaba yake pa kilari yake, kwa sababu hii haikukuwe jabo ya kweli, lakini ilikuwa paka ndoto moja. Lakini hasikuweze kusikia maana ninyi ilikuwa hii alama juu ya uzima yake na alimbakia mara ingine bila kugeuza uzima yake.

Kisha wakati ya kuenea, alilaria pa kitanda kwa ajili ya ugonjwa moja nguvu sana. Pa kitanda alikuwa sasa na aliomba saidio ya Mungu. Ile saa, basi, anaona, lakini hapana kwa ndoto yake, lakini katika maono ya kama alisimama mbele ya kiti ya uhukumu moja kama mtu mukosefu mbele ya watu wengi. Pa Kiti wa matata aliikaa Muhukumu na Mfalme, mwenye alivaa nguo wa ufalme na wa askofu na mu fasi ya kuume alikuwa na wa kijana wengine, na kushoto kijana moja kuliko munyenyekevu na mupole, lakini pempeni yao waliikaa watu weshimiwa na watakatifu. Mukongo ya Mfalme ilikuwa zimu moja urefu na wa giza na ono yake ilitupatia boka na uchungu mingi.

Wakati, basi, alisimama huyu mwaminifu na boka na haya, anasema kwake Mfalme:

Ee Kijana, usijue nani niko Mimi?

-Yoane alimujibu: Ninajua, ee Rabi ya kama Weye uko Mwana wa Mungu na Mungu uliyekuwa mutu sawa sisi, bila zambi na ulikuja duniani, katika mafundisho ya Maandiko Takatifu yetu.

-Na Mfalme alimwambia: Kama weye unanifamia toka Mandiko Takatifu, sawa vile unasema, tena unajua na wale wanaikaa pempeni yangu, namna gani ulisahabu hii kitisho iliyekutuma kwako, mbele ya miaka madogo, mfalme Konstantinos, ao usisikie ninakuwambia ninyi?

-Ninasikia, ee Rabi, alimujibu Yoane na makumbusho toka ile boka nikona ndani ya roho yangu.

-Bwana alimwambia: Kama makumbusho ya ile boka ukona tena mu roho yako, juu ya ninyi unaendelea kufanya ma zambi yako? Basi, sikia sasa, ya kama nilikuwa Mimi, mwenye nilikupatia ile boka juu ya kuogopa mateso ya gehena na kugeuza uzima yako.

Na, wakati alisema ma sauti yake, aliwaambia na alama ya macho yake kutupa Yoane ndani ya ile zimu iliyekuwa mukongo Yake. Wakati, basi, wale wa kijana walimusukuma Yoane ya kumutupa ndani ya ile zimu urefu, yule Yoane aliomba mara moja saidio ya Mzazi-Mungu Bikira Maria. Basi, alionekana katikati yao Mzazi-Mungu Maria na ile saa Mfalme alisema kwa wenye kuvaa manguo meupe: « Mumuache kutoka inje kwa ajili ya maombi ya mama yangu».

Mupaka hapa ni maono ya Yoane, mwenye, wakati alirudia kwa maungo yake, alikwenda kwa Mutawa mweshimiwa moja na alimwambia hii ono. Mutawa alimujibu:

-Tukuza Mungu, ndugu wangu, kwa sababu ulistahiliwa kubeba hii fundisho ya ajabu. Basi, lamuka toka uvivu na uzaifu yako juu ya hapana kupata hii mateso alipata mtu mwingine na historia yake sasa nitakuwambia. Maono umoja aliona na mwaminifu mwingine juu ya murafiki yake moja aliyeitwa Georgio, aliyekuwa mutumishi ya Uhukumu watu mu nyumba ya mfalme. Yule mwaminifu aliona, basi Georgio kupelekwa toka ma shetani wenye makali sana ndani ya zimu urefu sana. Ile saa, mtu moja aliyekuwa na mapendo ya mfalme, alifukuza ma shetani, wenye walimupeleka kumutupa na aliwaambia ya kama huyu Georgio atageuza uzima yake, kisha ma siku makumi mbili. Paka kwa hii zamini aliuhurwa Georgio na huyu aliyeona ono alikimbia kwa mrafiki yake Georgio kumufunua hii ono yote. Huyu, wakati alisikia, hasikupatie hata pasopo kidogo na alimbakia bila kugeuza uzima yake. Wakati ilipita nyakati ya ma siku makumi

mbili, alitoka, ole kwake, toka hii uzima, bila kuripa deni yake, sawa vile aliisha kumwabia yule mwaminifu muzuri.

Yoane, wakati alisikia hii ma sauti yote na mukuchunga mu akili yake hii matendo yote aliona, alikimbia mbio, bila haya na aliungama makosa na zambi yake yote na kisha aliishi na amani na hivi aliisha maisha yake na aliingia mu nyumba ya milele.

## 33. Simama hapa kufamia matendo makubwa ya Ufikisho ya Mbili ya Bwana Yesu

Mu mukini moja, karibu ya Konstantinopoli, inayeiywa Avidos, aliishi mwaminifu moja muorthodokse pamoja na bibi yake, anayitwa Sofiani, mufazili na mupendwa ya Mungu, ku mwaka 1607.

Siku moja aligonjwa Sofiani na alimbakia pa kitanda ma siku makumi mbili, bila kuweza kulamuka. Wakati ilifanyika magaribi ya siku 3 ya Mwezi ya Mnane, huyu mama alifugula mikono yake mbinguni na alionekana ya kama alikufa. Wajerani yake yote walitayarisha ma bintu yote ya maziko, bile kutulifu hata kidogo. Lakini waliangalia ya kama chini ya mazimba yake ya kushoto hii fasi ilikuwa kivukutu, na walimwacha mupaka kukufa kamili.

Ile wakati alikuja na dada yake na, kwani alikuwa na umivu na sikitiko, alibeba maji na alitupa pa mwili yake. Mara moja Sofiani alipata nguvu ya mwili yake na alisema kwa dada yake Anna: «Ilikuwa kupita nzuri usikufike hapa, dada yangu, kwa sababu ulinipatia hasara na lufu kuliko, kwani ma sauti na malalamiko yako walinitosha toka ile fasi ya Paradizo na ile utukufu ya Mungu nilipata, na ile misiweze kuisema na ma neno yangu. Ilipaswa, ee mumbafu, wakati uliniona mufu, kufurahi na kushukuru Mungu na usifurahi sasa, kwani niliishi mara ingine».

Wakati alisema hii ma sauti yake na ingine, wa jerani yake walimuuliza kuwaambia ma fumbo ya Mungu, ile aliona mu uzima ingine. Yule aliomba mpadri ya roho juu ya kuungama na, kama yeye anazania ya kama iko nzuri kusikia na watu wengine, iko namna kusikia na mweye. Basi, alikuja mpadri ya roho aliyeitwa Ierotheos Kukuzelis, ambaye na amri ya patriarhi alikuja kuungama mama Sofiani. Huyu alimuwambia hivi:

Wakati nililamuka na niliikaaa pa kitanda yangu, nilipotesha nguvu yangu na niniona mbele yangu kijana moja na uso yake kujaza na nuru. Huyu alikamata kwa mikono yake kikombe moja ya kujaza maji na aliniambia:

-Ee Sofiani, ninajua ya kama ukona kihu mnene na roho yako inauma kwa ajili ya malari yako. Lakini, kama utakunywa toka hii maji inayeleta uzima, utatunzwa kwa nafsi na mwili yako na utakuwa daima furaha ya milele.

Mimi, wakati nilisikia hii ma sauti yake, nilifurahi sana na misikupende kintu ingine paka kuangalia uso ya yule kijana wa ajabu. Wakati nilikamata hii kikombe toka mikono yake juu ya kuikunywa, misijue, namna gani, nilitoka ya hii uzima na ma siku tatu na usiku nililofa toka mwili yangu na nafsi yangi alifata yule kigana na tulipanda mbinguni. Tulipita mavirigo saba ya mbingu ndani ya giza mingi na kisha tulifika mu fasi moja yenye arufu na mwangaza na mbele yake walikuwa milango makubwa wa wili. Mulango ile ya kuume ilikuwa toka zahabu na maimbwe, lakini mulango wya kushoto ilikuwa toka shamba na chuma na inaonekana kama makala ya moto. Pempeni yake walisimamama hazina ya wakubwa wa askari na ma bunduki yao, wenye walichunga hii mulango na mimi ile saa niliogopa sana.

-Aliniambia mwongozi yangu: Ee dada, unaona bile milango? Hii ni milango ya haki na ile mulango ya zahabu ni mulango ya ufalme ya Mbingu na ile mulango ya chuma ni ya gehena ya wenye zambi.

Tuliacha hii milango na tulipanda tena yulu mu fasi ingine ya nuru mingi, pahali walisimama ma hazina mengi na wanaume na ma fasi yao walikuwa ya kuachana, nikusema wanaume wengine waliikaa yulu na wengine waliikaa chini.

Ile saa mwongozi yangu aliniweka katikati ya wa malaika na aliniambia: «Ee Sofiani, hapa namisha kichwa yako na usujudu». Mara moja mimi nilinamisha kichwa yangu na nilisujudu na boka mingi, lakini nani nilisujudu misikuone. Yule mara ingine alinilamuka na aliniambia: «Simama hapa kufamia matendo makubwa ya Ufikisho ya Mbili ya Bwana Yesu». Na kisha niliona Kiti moja wa moto na ya utukufu na chini yake ilikuwa mukono moja, iliyekamata kipimo moja.

Pempeni ya yule Kiti walisimama ma hazina mengi ya wa malaika, wenye walipanda toka ile njia nilipanda na mimi na walipeleka ma nafsi ya watu, wanaume na wanawake na watoto na, wakati waliipanda hapa, walisema: «Musujudu» na wale ma nafsi walisujudu, sawa vile nikusema nilifanya na mimi. Pa ile Kiti ya matata, katikati ya mawingo wa nuru, aliikaa Rabi Kristu wetu, aliyevaa nguo moja na ragi ya nyakati na  kama ragi ya bahari. Mimi kwa ajili ya mwangaza mingi ya Uso yake, misikuweze kumuangalia. Hawa wa malaika, waliyesimama pempeni Yake waliimba: «Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu Bwana Savaothi, mbingu na inchi zimejazwa kwa utukufu wako». Waale waliyekuwa pamoja na sisi waliimba hii: «Utukufu kwa Mungu juu pia. maana utukufu wako ni mukumbwa», wengine waliimba hivi: Alliluia mara tatu, lakini wengine waliimba: Amina, amina, amina» na hata kidogo hawakusimame wimbo yao.

Mu fasi ya kuume ya Kristu aliikaa Mzazi-Mungu na ya kushoto Mt. Yoane Mutangulizi na Mubatizaji, sawa vile wanamuonyesha ma picha (Ikona) yake. Wa malaika, wakati waliisha wimbo yao, walisujudu Mungu ya kunamisha ma kichwa yao, lakini Bwana alinyanyua mikono Takatifu Yake na aliwabariki. Toka bilole ya mikono ya Kristu walianguka ya kuendelea kama mutoni maimbwe mazuri, na hii kintu mimi, wakati niliiona, nilishangaa na niliuliza mwongozi yangu, ni ninyi hii ma fumbo? Na Malaika yangu alinijibu:

-Unaona, ee Sofiani, hii maimbwe mazuri ya kuachana yenye wananguka toka mikono ya Kristu na wanakuja mu inchi? Hii ni maana ya rehema na mapendo ya Mungu wetu, ambaye anatuma mapendo na kila baraka yake kwa kizazi ya wa Kristiani waOrthodoksi na hivi anatuma baraka yake ndani ya ma nyumba ya WaKristiani waOrthodoksi, **wenye wanachunga Imani Kwake bila kuiharabisha na kupotesha** na tena kwa wale wanaungama safi ma zambi yao, wanachunga ma amri takatifu na wanachukia mapenzi ya shetani; hawa waKristiani Mungu anawabariki na anawaokoa toka kintu kibaya. Hawa wanayerehema na wanasaidia mukaribifu yao, wanapata,  wakati tena wanaishi, hii mabaraka na kisha lufu yao wanariti uzima wa heri ya Paradizo.

Hii ulimi ya moto, yenye wanaanguka toka mukono ya kushoto yake ni maana ya gazabu, hasira na kisilani Yake kwa ajili ya wale watu wanafanya uzima ya zambi na wazulumu mukaribifu yao. Hawa wanapotea hapana paka hii uzima ya dunia, lakini wataingia daima mu moto ya gehena kuteswa daima pamoja na ma shetani wenye uchafu.

Mu fasi ya kushoto ya Kiti na kipimo, sawa vile tulisema, ilionekana mutoni moja murefu na toka hii fasi ilikuja yulu arufu kibaya kama pepo ya simoko na malalamiko toka ma kinywa mengi ya watu, wenye walipaza sauti na walisema: «Ole kwetu, elo kwetu. . . »

Wa malaika walileta ma nafsi ya watu toka inchi na, wakati walisujudu, waliwaongoza juu ya kuhamakia matendo yao yote, ile walifanya mu inchi yetu na matendo yao ya mazuri waliweka mu fasi ya kuume ya kipimo, lakini ile matendo mabaya waliweka mu fasi ya kushoto yake. Kisha Kristu alihamuru hawa ma nafsi waliokolewa wa malaika waliwapeleka mu makao, pahali ilikuwa mulango wa zahabu, lakini ma nafsi waliyelipizwa kwa ajili ya zambi na hawakutubu, wa malaika waliwatupa ndani ya ile mutoni ya gehena. Ile saa wa malaika walifurahi na walishangilia juu ya wale ma nafsi waliokolewa, lakini walitaabu na walisikitika juu ya wale ma nafsi walienda mu gehena.

Ile saa wa malaika walileta nafsi moja, lakini makosa na zambi yake walikuwa kuliko mingi ya matendo mazuri yake na ilikuja saa kusema na alama ya macho yake Bwana Yesu kutupa wa malaika huu nafsi mu gehena. Lakini ile dakika, alionekana mara moja Mzazi-Mungu na Mt.

Yoane Mutangulizi na waliomba kwa Bwana Yesu hivi: «Ma wema yako, ee Mwema, wanashinda gazabu na kisilani Yako; huu nafsi kweli ni mwenye zambi, lakini hasikusimame kuchunga imani ukweli mbele Kwako na kwa hii tunakuomba kumusamehe». Wakati hawa walimuomba Kristu, walikuja na wa malaika na walionyesha ma saidio ngapi alifanya kwa watu wamaskini, ma Liturgia ngapi alifanya, ma taa, mafuta na ma Prosforo na makumbusho ile alifanya ndani ya kanisa. Tena walipanda na ma sala ya wapadri, wenye walifanya Liturgia Takatifu kwa jina yake, tena na ma rehema ya wazazi na wajerani yake, ile walitoa kwa maskini na wenye malari kwa jina yake juu ya kupumzika nafsi yake. Tena walijisikia maombi ya wenye maskini, wenye walibeba ma huruma toka ma jerani yake na walisema: Mungu kusamehe nafsi yake».

Ile saa ilisikiwa sauti ya Rabi kusema: «Tazama kwa ajili ya maombi ya wapadri yangu na wa ndugu wangu wamaskini, ninasamehe huu nafsi». Basi, wakati alipenda Kristu na alama ya mukono yake ya kuume kuonyesha kwa wa malaika yake juu ya kuweka huu nafsi pamoja na wenye haki, walifika mu Kiti Yake maombolezo, malalamiko na ma kisilani na wazazi yake na machabulana yao kupingana ya Mungu, kwa sababu alikufa mtoto yao, lakini hivi walionyesha ya kama hawasadiki mu fundisho hii ya uzima ya milele: «Natumaini ufufuo wa wafu na uzima wa milele mbele utakayokuja». Wakati walijifanya hii mambo, Bwana Yesu alisirika sana na alisema: «Kwa sababu hawakuenee kwa maombi ya wa padri yangu, lakini wanakombana kupingana yangu, mutoshe hu nafsi na mwende kumutupa mu gehena ya milele». Wa malaika ile saa walitaabu, lakini walitii kwa amri ya Kristu; walibeba huu nafsi na walimupeleka ndani ya hii mutoni ya moto. Ile saa nilipata nguvu kuuliza na mimi mwenye zambi malaika musimamizi yangu:

-Juu ya ninyi, Bwana yangu, wanataabu hata mingi wa malaika, wakati nafsi moja, anajitupa ndani ya gehena?

-Yule alinijubu: Hii shimo ni ile inaachana wenye haki na wenye zambi na wanaanguka ndani hawa watariti gehena ya milele. Kama, sisi tukona furaha wa malaika wote juu ya wokovu ya nafsi moja, kuliko taabu tukona juu ya hawa wanakwenda mu gehena.

Wakati aliniambia hii ma sauti malaika yangu, ninasikia mara moja bikelele nguvu, kwa sababu walikuja wa malaika na walileta nafsi moja katika wimbo, kufukiza na chetezo, pamoja na ma taa na furaha mingi. Huu nafsi alikuja na furaha mingi na uwezo na ma nafsi ya wenye haki walikuja kumupokea. Huu nafsi wa heri alikuwa na nguo yake safi na meupe kama jua na hasikulete hata uchafu moja ao alama ya zambi moja. Hii nguo yake meupe, mimi ninazania, ilikuwa nguo ya Ubatizo Takatifu, ile aliichunga safi na kwa hivi aliangaza kama jua. Basi, alikuja huu nafsi na alisujudu, sawa walifanya na ma nafsi wengine katika zwezo yao. Ile saa wa malaika wote walipaza sauti na walisema: «Tunakushukuru, ee Rabi Mwenyezi, kwa sababu tuliona nafsi ya mtu mwenye haki safi na bila uchafu na bila hata zambi moja». Kisha ilisikiwa sauti ya Rabi kusema hivi: «Mubebe huu nafsi na mutamupeleka mu makao ya watakatifu». Kisha alipindula sauti yake na mukono Yake kwa mimi na aliniambia: «Mubebe kupeleka na nafsi ya Sofiani ma nyumba na ma fasi ya watakatifu yangu, juu ya kuiona; lakini, kwa sababu wanamuomba watu mengi duniani, mumurudishe nafsi yake kwa mwili yake juu ya kuokolewa watu mengi, wakati watasikia hii maono yake. Kama atashindana na atapata ma fazila ingine mengi, atastahiliwa, kisha miaka tatu, kufika hapa na atapata furaha na shangilio kuliko mingi».

Kisha hii sauti ya Rabi yetu, malaika alinakamata na tulifata huu nafsi wa heri na tuliunganwa pamoja na ma nafsi ingine. Tulifika mbele ya mulango ya Paradizo wa zahabu. Mara moja niliona mbele yangu Mzazi-Mungu Maria na utukufu mingi kabisa na pamona naye alikuwa Mtume Petro, ambaye alikamata kwa mikono yake ma fugulo. Alifugula hii mulango muzuri na aliingia ya kwanza ndani Mzazi-Mungu Maria, kisha Mtume Petro na kisha wa malaika pamoja na ma nafsi yao, waliopeleka. Pamoja na hawa nilienda na mimi na walinisukuma kutembea karibu ya Mzazi-Mungu. Hii makao ilikuwa ya kujaza nuru na arufu

sana na mimi nilishangaa na nilifurahi bila kuweza kusema. Ile inchi haikukuwe sawa inchi yetu, pahli ni ma fasi ya kupanda na kushuka, maimbwe, ma mutoni na bile bintu sisi tunaona hapa, lakini ile fasi ilikuwa chini meupe kama upamba safi ao nguo ya zahabu na ilipambwa na maimbwe ya kuachana. Tena niliona miti marefu na katika arufu mingi na mawa na matunda mengi. Chini ya ile ma miti walikuwa matelo na yulu yao waliikaa wanaume, wanawake na watoto na katikati yao nilifamia wengi toka inchi na muji yangu Abidos, wenye waliisha kufa zamani.

Kule niliona baba yangu, aliyekuwa mpadri, mama yangu Anastasia na dada yangu, lakini misikuweze kuwakaribia na kusuburia na wao. Ma fasi yao hawakukuwa umoja, kwa sababu na ma fazila na matendo mazuri yao hawakukuwe umoja hapa mu inchi yetu. Nilitembea tena ku mbele niliona na Watakatifu, wenye walikuwa mu fasi kuliko yulu na walitembea wote na mavazi wa nuru. Mimi ile saa niliuliza maungo yango: Hawa watu ni wa nani? Alipindula kichwa yake Mzazi-Mungu Maria na alinijibu:

Ee Sofiani, unaona ma nyumba ya Watakatifu? Tembea mbio juu yab kutaguria na kusujudu Abrahamu mwenye haki, kwa sababu usitamuone sawa vile weye unapenda.

Ile saa mimi nilikimbia na niliona toka mbali Abrahamu kuikaa pa Kiti moja vema nzuri na pempeni yake waliikaa ma nafsi mengi, bila kuihesabu, na furaha na shangilio mingi. Mimi nilikimbia kumukaribia juu ya kumuona na kufurahi kwa ajili ya ono yake; na yule aliniona na alinifanyisia alama kukaribia kwake. Nilikamata uwezo mingi na nilitembea mbio kumukaribia, lakini ile saa nilisikia malalamiko ya dada yangu na hii maji ya baridi iliyetupa pa mwili yangu na nililamuka. Nafsi yangu ilirudia kwa mwili yangu, lakini mimi nilisikia baridi sana ndani ya mwili yangu, kwa sababu misikupende kurudia nafsi yangu mara ingine ndani ya mwili yangu.

Wakati alisikia hii ma sauti ya ajabu yote huyu mpadri ya roho alimuuliza:

-Uliona tendo ya ajabu ingine mtoto yangu Sofiani? Uliona ma kundi ya ma shetani, ma fasi ya kuachana ya gehena, sawa vile wanaona watu wengine?

-Sofiani alimujibu: Misikuone tendo ingine, mpadri wangu.

-Unajua, kama ulifanya tendo kimoja kizuri mu uzima yako? Alimuuliza mpadri.

-Tendo kizuri ninyi unaona kwa mimi mwenye zambi, mpadri wangu? Lakini, kwani unaniuliza, nitakuambia hii moja ninaijua. Mbele ya miaka tatu, ile saa nilitumika mu nyumba ya baba yangu, ilikuwa saa ya muchana, nilisikia bikelle na tetemeko, sawa ilijifanya kweli tetemeko na ile saa niliona mara moja wanaaume wa tatu wa askofu na manguo ya askofu yao, wenye, sawa vile nilisikia, walikuwa wa askofu wa tatu: Basile Mkuu, Grigorio Mutheologo na Yoane Krisostomos. Mimi nililekea kwa ajili ya boka yangu. Nilifanya alama ya musalaba na niliwasujudu na boka na heshima mingi. Wale waliniambia:

-Usiogope, ee Sofiani, sisi tuko wa askofu wa tatu na tunataka kupatia nyumba yako kwa sisi juu ya kufanyika kanisa kwa jina yetu na sisi tutaomba kwa Mungu juu ya wokovu wako.

-Mimi nilipata nguvu kuwauliza paka hii: Wa Rabi Watakatifu wangu, hii nyumba ni kizuri juu ya kutukuzwa Mungu na kuwa nyumba yenu? Kwa sababu na sisi tuko watu maskini na tusiko na fasi kujenga kanisa moja, sawa vile munaniambia. Tena misijue na uwazo ya bwana yangu, tena kama tutaweza kubeba ruhusa toka mfalme ya inchi yetu juu ya kujenga hii kanisa yenu.

-Wale waliniambia: Usisikitike kwani hii makao iko na uchafu na maivi, wala kuogopa ruhusa ya mfalme, paka weye fanya nguvu kutupatia kwa sisi na sisi mambo ingine yote tutaitengeneza. Kwa sababu zamani hii fasi pahali sasa mukona mayani ya kukauka juu ya ma nyama yenu, ilikuwa kanisa yetu. Usionyeshe uzaifu na uvivu na fanya katika amri yetu na kama utakataa kutii, tutaomba kwa Mungu kutosha weye toka hii uzima kwa sababu ulikataa kutii.

Wakati walisema hii ma sauti watakatifu wa tatu, walikimbia. Wakati usiku alikuja bwana yangu, nilimuwambia hii mambo yote. Kisha ma siku tatu, kisha sala ya usiku yetu, walikuja watakatifu wa tatu mara ingine na tetemeko na walitwambia na sauti nguvu:

-Sofiani, juu ya ninyi usikufanye hii kazi sisi tulikuwambia na sasa utakufa na lufu mara moja?

-Mimi nilisema ile saa kwa bwana yangu: Unasikia wanasema ninyi Watakatifu wetu?

Huyu bwana yangu aliwajibu:

-Wa Rabi watakatifu wangu, hii ma jabo yote aliniambia bibi yangu, lakini tuko watu wamaskini na tusiko ma bintu ya kujenga hii kanisa. Tena tunaogopa na mamlaka ya inchi yetu, kwa hivi tusikufanye kinti kimoja. Lakini, kwa sababu munatwaambia kumipatia hii nyumba kuwa kanisa kwa jina yenu, tangu leo hii makao itakuwa yenu.

-Watakatifu walimujibu: Kesho asubui utachibula ndani ya ile fasi ukona mayani ya kukauka na utapata ma musalaba, mwamba tena na Meza takatifu na utasadiki kwa ma sauti yetu. Uende na kwa mkubwa ya inchi yenu na umuomba ruhusa na sisi tutamuwambia kumipatia ruhusa.

Wakati walisema hii ma sauti yao Watakatifu, waliondoka. Sisi ile usiku yote tuliipita na wimbo na matukuzo ya Mungu na asubui tulitangaza hii jabo na kwa watu wengine ya mukini yetu. Kisha watu wote walikuja na ma piki na posholo juu ya kutusaidia ya kuchibula ile fasi. Kweli, tulipata Meza Takatifu iliyekuwa toka maimbwe ya marmbre na ma bintu ya kanisa ingine waliyekuwa ndani ya bulongo. Tulibeba ruhusa toka mukubwa ya inchi yetu, bila mambo na ilianza kazi ya kujenga kanisa yao. Sisi tulikwa na ma shamba ingine na tuliuzisha juu ya kupata makuta na tuliuza ma bintu ya kuachana juu ya upambo ya Kanisa, na, wakati iliisha kazi, alikuja askofu yetu na baraka ya Patriarhi yetu na tulifanya Ibada ya mwanzo juu ya kufanya Liturgia na ma Ibada ingine. Sisi kisha tuliondoka toka mukini yetu na tuliikaa mu muji Konstantinopoli, pahali tuliripa nyumba na makuta. Lakini ninakuomba, ee mpadri ya roho yangu, kusema kwa bwana yangu, kuniacha juu ya kufanyika mimi mutawa juu ya kuria ma zambi yangu hii ma miaka tatu, Mungu alinilaka yakama mitaishi tena ndani ya hii uzima. Mpadri ya roho, wakati alisikia matakio yake, alisema kwa bwana yake juu ya kuwacha kufanya mutawa. Yule alimwambia ya kama, kisha miaka wa mbili wataenda ma Fasi Takatifu ya Bwana Yesu Kristu mu Yerusalema na kule watafata kila moja uzima yake ya utawa.

Na kweli, wakati waliuzisha ma bintu yao, waliondoka na walikwenda mu Yerusalema na kule walijiungama uzima yao na matakio ya kwa patriarhi Sofronios. Kisha walipewa Komonyo Takatifu na Sofiani alikwenda mu Monasteri moja ya wanawake na alifanyika mutawa na jina Sofronia, na bwana wake alikwenda mu Monasteri ya wanaume na alifanyika mutawa na toka jina Xristos, mu jina ya utawa Xariton.

## 34. Mtakatifu Mutawa Efrosinos alikwenda mu paradiizo

Mtakatifu Mutawa Efrosinos alizaliwa ya wazazi, wenye waklikuwa watu bila fundisho na akili nguvu; joo vile na mtoto yao alikomea bila fundisho na hekima. Wakati alikomea, alitakia uzima ya watawa na alifanyika mutawa mu Monasteri moja. Kwa ajili ya upole na kwani alikuwa mutu bila masomo, alitumika kwa pisi ya Monasteri yake na alivumilia matusi na mazarau ya watawa wengine bila kusirika ao kuwachabula. Ndani ya hii Monasteri aliishi na mpadri moja mweshimiwa sana, aliyeomba toka Mungu kumufunua mafuraha ya Watakatifu wenye milele.

Usiku moja, basi, aliona mu ndoto yake huyu mpadri ya kama alikuwa ndani ya shamba moja na aliona ma bintu wa furaha na ajabu. Kule aliona na mupisi ya Monasteri yake Efrosinos, aliyesimama katikati ya ile shamba na alifurahi ma bintu ya paradizo. Alimukaribia, basi, na alimuuliza ni nani hii shamba na namna gani alikuwa huyu kule. Efrosinos alimwambia:

-Hii shamba ni nyumba ya watumishi ya Mungu na mimi kwa ajili ya wema mingi ya Mungu, alinipatia baraka, kusimama hapa.

-Na unafanya ninyi hapa ndani ya hii shamba? Alimuuliza mpadri.

-Mimi niko mukubwa ya bile bintu unaona hapa; ninafurahi na ninashangilia kwani ninaona na macho ya roho bile bintu ya milele hapa.

-Unaweza kunipatia na mimi hata kidogo toka bile bintu unafuraha ndani ya hii fasi ya mbingu? Alimuuliza mpadri.

-Ndivyo, utafurahi toka bile bintu yote, alimuwambia Efrosinos.

Ile saa mpadri aliona matunda madogo ya muzuri sana na aliomba kumuapatia.

Efrosinos alibeba hii ma tunda ya pomme na aliweka chini ya nguo ya mpadri mukusema kwake: Tazama, matunda ya pomme uliniomba.

Lakini, kwa sababu ilipigwa kengele juu ya kushuka wa padri mu kanisa, alilamuka na huyu mpadri. Kwani alizania ya kama hii yote aliona walikuwa ndoto na hapana maono, hasikuangalia nzuri sana. Lakini, wakati alipata ma pomme, cchini ya nguo yake, alishangaa juu ya hii jabo ya ajabu na ya saa mingi alisimama na mushiago.

Kisha alikwenda mu Kanisa na aliona kuwa kule mutawa Efrosinos. Alimukokota, basi, mu fasi moja ya kona na alimulaka kumwambia alikuwa wapi ile usiku. Efrosinos alimuwambia:

-Unihurumie, ee mpadri, misikwenda mu fasi ingine hii usiku; paka sasa nilikuja mu Kanisa.

-Kwa hivi mimi nilikulaka na nilikufunga katika roho juu ya kuonekana kwa watu wengine matendo makubwa ya Mungu na weye usitake kusema na sauti ya kweli?

-Ile saa Efrosinos munyenyekevu, alimujibu: Padri, nilikuwa kule pahali walikuwa bintu ya furaha, bile watawariti, ninyi wote wanamupenda Mungu na bile uliomba miaka mingi kwa sala yako kuiona. Kule uliona na mimi, kwa sababu Mungu alibariki akufunua kwako bile bintu ya milele toka mimi mwenye zambi.

-Na ulinipatia ninyi, mpadri Efrosine, toka bile bintu ya paradizo?

-Efrosinos alimwambia: Bile matunda ma pomme ya mazuri sana, yenye sasa uliweka ndani ya kitanda yako. Lakini, ee padri, unihurumie, kwa sababu mimi ni bilulu na hapana mtu.

Ile saa mpadri alitangaza kwa watawa wote hii maono ya Efrosinos na alisauria wote kufata wivu na mapendo ya ma fazila ya yule Mutawa Efrosinos.

Mwenye heri Efrosinos, kwani alitaka kutoka utukufu ya watu, aliondoka kwa siri toka Monasteri yake na mupaka lufu yake alimbakia bila kufamia alikwenda wapi na namna gani aliishi. Watu wengi wenye walikula vipande ya bile matunda ya pomme, walitunzwa ya magonjwa yao.

## 35. Historia ya ajabu juu ya yule mpadri aliyekuja toka uzima ingine kusikilizana na shemasi moja

Waliishi mu muji Konstantinopoli mpadri moja na shemasi moja. Ku mwanzo walikuwa na mapendo mingi, lakini kisha katikati yao ilizaliwa chuki na vile walimbakia mupaka alikufa mpadri.

Shemasi, basi, kisha lufu ya mpadri alitaabu mingi, kwa sababu hasikutagurie kuharabisha ile chuki ilionekana katikati yao na alikwenda mbio kuungama kwa wapadri wakubwa hii mambo yake. Hawa wpadri walimwambia kutembelea mutawa moja mkubwa ya jangwa. Huyu alimwambia hivi:

-Huyu anayeomba kintu kimoja na imani ataipata na huyu anayekokola mulango itamufuuguliwa, katika neno ya Rabi wetu. basi, uende sasa nyumbani yako na usiku uendw mu kanisa mkubwa ya Mtakatifu Sofia (Hekima ya Mungu). Huyu anayekuja ya kwanza kule, umusalimie toka mimi na umupe hii barua yangu na utabeba matengenezo ya mambo yako.

Basi, shemasi alikwenda usiku mu Kanisa na alisimama inje yake. Basi, alikuja usiku mtu moja, na shemasi alimusalimia na alimupatia hii barua ya mutawa wa jangwa. Yule aliisoma na alianza kuria mukusema na unyenyekevu: Nani ni mimi mwenye zambi na mtu mudogo na

mitaweza kuomba hii mambo? Lakini ninatumainia kwa maombi ya yule mtu aliyekutuma kwangu na mitafanya hii kazi, lakini ninajua ya kama hii kazi ni yulu ya ma nguvu yangu.

Basi, wakati alisimama mbele ya milango ya kufungwa ya kanisa, alipika magoti na alinyanyua mikono na akili yake mbinguni na aliomba na kimya. Kisha saa kidogo alilamuka na alisema:

-Ee Bwana, fugula kwa sisi mulango ya rehema yako» na mara moja, o muujiza ya ajabu, milango walifuguliwa hii wenyewe na waliingia ndani pamoja na shemasi mu kipande ya kwanza ya kanisa. Walisimama mbele ya milango ya kipande mbili ya kanisa, huyu mtu wa ajabu alifanya sala yake na milangu walifunguliwa hii wenyewe. Aliingia huyu ndani ya kanisa, lakini shemasi alimbakia mu kipande ya kwanza ya kanisa inayeitwa Narthikas, na aliona maono moja ya ajabu. Toka mufuniko ya Kanisa ilishuka ulimi ya moto moja pa kichwa ya yule mtu ya ajabu na ndani ya kanisa nzima na kwa kila fasi alikwenda yule mtu alimufata na hii ulimi ya moto. Wakati alifika mu Altari Takatifu huyu mtu ya ajabu, alipika magoti na aliomba kwa Mungu. Kisha alitoka inje, mu ile fasi alikuwa shemasi, mwenye aliisha kustaajabu mukuona bile bintu ya ajabu na hasikuweze kukaribia huyu mtu mtakatifu, kwani na uso yake iliangazwa kama uso ya malaika. Tena aliuliza maungo yake: «Huyu ni ninyi: Ni mtu ao malaika ya Mungu? Alisikia na richo ya roho yake yule mtu wa ajabu mawazo ya shemasi na alimwambia:

-Juu ya ninyi unakombanishwa toka mawazo yako na unauliza juu ya mimi, ee mtu wangu? UNisadiki ya kama na mimi niko mtu toka hii inchi, toka mwili na nafsi, sawa vile ni na watu wote. Kazi yangu ni secreteur mu jamaa moja ya utajiri na toka hii kazi yangu ninauza ma bintu ya maisha yangu; Lakini Maongozi Takatifu, anayetembesha dunia muzima kamili, anazombelea mara mingi na katika watu wa bure kumaliza na bintu ya ajabu. Lakini, ee ndugu wangu, twenda sasa kutengeneza hii mambo yako.

Walitembea pamoja mu soko na walifika mu kanisa ya Mzazi-Mungu ya Vlahernes. Aliomba mara ingine na milango walifuguliwa hii wenyewe. Huyu aliingia ndani, lakini shemasi alimwacha inje kusimama mbele ya milango ya kanisa na alimwambia kusopoka wale watu wanaingia ndani ya kanisa. Yule alisimama ya kupika magoti katikati ya kanisa na aliomba na kivukutu ya roho yake nguvu. Ile saa aliangalia shemasi mu fasi ya kuume toka mbali, aliona shemasi moja aliyekuja toka Altari Takatifu na alifukiza kanisa nzima. Kisha aliona na wapadri wengine, wenye walivaa mavazi ya kuangaza mingi na kisha yao ilifika kundi ingine ya wapadri, wenye walisimama ma fasi ya ma kundi ya waimbaji na waliimba wimbo moja ya utamu sana. Toka hii wimbo hasikuweze kusikia neno moja, paka hii: «Alliluia».

Wakati aliishi sala yake yule mtakatifu alikuja kwa shemasi na alimwambia:

Ee ndugu, ingia bila boka mu kanisa na mukuona wapadri mu fasi ya kushoto, fanya nguvu kufamia yule mpadri ulimbakia mpaka lufu yake, bila kusikilizana naye.

Shemasi aliingia na boka ndani ya kanisa na mukuona mu fasi ya kushoto, alikuja inje na alisema kwa mtu ya Mungu:

-Misikuweze kufamia kule yule mpadri nilikuwa na chuki naye.

Ile saa mtu ya Mungu alimwambia:

-Ingia sasa mara ingine ndani ya kanisa na angalia mu fasi ya kuume.

-Alifata amri yake huyu shemasi na aliangalia sasa paka mu fasi ya kuume ya kanisa juu ya kutafuta yule mpadri. Alitoka inje ya Narthikas na alimutangaza kwa huyu mtu ya Mungu, na mwenye alimwambia:

-Kama ulimufamia nzuri ya kama huyu ni unamutafuta, uende kumwambia ya kama Nikitas Secreteur anasimama inje na anakuita.

Shemasi, basi, aliingia ndani ya kanisa, alibeba na mukono yake yule mpadri na alimuletea inje. Ile saa huyu mwenye ajabu mtu ya Mungu Nikitas na sauti upole alimwambia:

-Ee mpadri, fanya mapendo pamoja na huyu ndugu yako, kwa sababu usikutaguria kusikilizana naye, wakati ulikuwa tena mu zima yako.

Ile saa mpadri na shemasi walipika magoti moja kwa mwingine na waliomba hurumia na walibusu moja kwa mwingine na vile iliharabisha hii chuki ilikuwa katikati yao. Kisha mpadri aliingia mara ingine ndani ya kanisa na alisimama mu fasi yake, lakini huyun mtu ya Mungu Nikitas alibeba shemasi na walitoka inje, lakini milango ya Kanisa walifungwa hii wenyewe.

Walitembea njia kidogo pamoja na kisha alisema mtakatifu Nikitas kwa shemasi:

-Ee Ndugu yangu, kombana daima kuokoa nafsi yako na uende kwa mpadri ya roho yako na umuwambia ya kama sala safi yake na uwezo yake kwa Mungu walifufuka na huyu mpadri aliyekuwa mufu juu ya kufanyika masikilizano na weye. Mimi misikusaidie hata kidogo kwa hii tendo.

Wakati alisema hii ma sauti yake mtakatifu Nikitas, alikimbia toka macho ya shemasi, mwenye alibusu ile fasi alisimama huyu mtu ya Mungu. Kisha alikwenda kwa mutawa yule wa jangwa na alimwambia hii matendo yote.

## 36. Mtoto moja alipanda pa pepo

Ku miaka ya mufalme ya Konstantinopoli Theodosios wa Mudogo, aliyeishi ku mwaka 410, Mungu mwema kamili alitaka, katika mapenzi yake, kujulisha watu mambo ya kwanza juu ya ufufuo ya watu wote iliyetajifanya ku mwisho ya hii uzima na mambo ya mbili ya kama inapaswa kuhimidi Mungu bila kosa. Kwa hivi katika mapenzi yake ilijifanya tetemeko. Taifa ya Konstantinopoli, kisha hii tetemeko, aliogopa sana na alitoka inje ya mababashi pamoja na mfalme na patrishi Proklos na wa padri wote na walifanya sala mu njia. Na, kwa sababu ile wakati ilikuwa fundisho ya uwongo ya watu filani, wenye walisadiki ya kama Bwana wetu Yesu Kristu, aliteswa hapana paka kwa mwili Yake, lakini na kwa hali ya kimungu Yake, lakini hii fundisho yao ni chabulana. Tena hawa watu waliisha kuongeza mu wimbo: «Mungu Mutakatifu, mweza Mutakatifu, Musiyekufa Mutakatifu, utuhurumie», lakini wale waliongeza hii neno: «. . . Musiyekufa Mutakatifu, uliyesulubiwa kwa sisi, utuhurumie». Kwa ajili ya fundisho ya uwongo ya kundi moja ya waKristiani, mtoto moja alinyanyuliwa na nguvu ya Mungu mbele ya ma macho yao pa pepo ya mbingu. Watu wote ile saa waliona hii mambo ya ajabu na boka mingi na ajabu waliimba «Bwana hurumia». isha saa kidogo alishuka mtoto ndani ya mawingu moja mara ingine mu inchi na alifunua mbele ya watu wote na kama majeshi ya wa malaika mbinguni wanaimba Mungu hii Wimbo Trisagio, bila kuongeza hii sauti «Uliyesulubiwa kwa sisi», nikusema waliimba hivi: «Mungu Mutakatifu, mweza Mutakatifu, Musiyekufa Mutakatifu, utuhurumie».

Kisha hii ma sauti iliyesema mtoto alitoa nafsi yake kwa mikono ya Mungu, lakini tetemeko alisimama na taifa ya wa Kristiani wote alirudia mu muji yao.

## 37. Mazungumuzo ya mtakatifu mutawa makarios Wa m’siri na malaika moja wa mungu.-

Siku moja Mtakatifu Mutawa MAKARIOS alitembea mu jangwa. Malaika wa Mungu alikuja akimufwata nyuma yake, akamwambia: «Himidi, Padri Mtakatifu.»

Padri MAKARIOS aliwaza ya kama ule mutu anaweza kuwa Mutawa wa jangwa, akimujibu : «Mungu akusamehe, mutoto yangu.»

Walitembea pamoja na Padri MAKARIOS aliona uso ya ule kijana Mutawa, ilikuwa mzuri sana kupita, alishangaa na alimuuliza:

« Mutoto yangu, ninapokuona ninashangaa juu ya nini uso wako ni wa ajabu na inangaa sana? Sijaona hata mara moja uso ya watu wengine sawa hii yako. Naapa kwa Mungu wa mbinguni nataka uniambie kweli.»

Basi Malaika alipita magoti mbele ya Padri MAKARIOS na akamwambia :

«Himidi, ewe Padri, Mimi sawa unaniona, niko Malaika wa Mungu na nilikuja ku kufundisha ile Mafumbo (Mystere) haujui na unapenda kufunza. Padri naye akapiga na magoti mbele ya Malaika na akamwambia :

Ewe Bwana, nakushukuru, kwa sababu ulinitumia Muongozi wa kunifundisha Mafundisho yote yale mimi sijue na yale Mafumbo ninatamainia kusikia.

Malaika akamujibu mara ingine: «unaniambia mimi unataka kufunza nini ?

-Padri alimujibu:

Ewe Malaika, uniambie wale watu walikufa, wanafahamia mutu mwingine ?

Malaika alimujibu hivi:

Sikia, ewe Padri. Sawa vile mu hii dunia watu wote wanalala na kesho yake asubui wanaamuka na wanajua wale watu wengine waliona jana, vilevile inafanyika mu dunia ingine ya mbinguni. Nikusema, anafahamia ndugu yake. Wanazungumuza tene wanafurahi katikati yao. Hii mambo inafanyika paka kwa watu wenye haki. Watu wenye zambi hawaoni hii furaha na hii Mapatano na shangwe.

- Padri aliuliza ule Malaika mara ingine :

Mambo gani inafwata kama mutu mmoja anakufa. Nafsi na mwili wake itaenda wapi? Tena juu ya nini sisi Waorthodoksi tunafanya sala ya wafu ?

- Malaika alimujibu hivi:

Sikia, ewe Padri wangu. Kisha machanisho ya nafsi (roho) na mwili Malaika Watabeba nafsi yake wataitembeze mbinguni, juu ya kubusu Bwana Yesu Kristu.

Hii kazi inafanyika katika siku ya tatu, kisha kufa kwake. Pakutoka mu dunia kwenda mbinguni kuna mungazi murefu sana na kwa kila daraja ya mungazi kunakaa kundi moja ya mashetani, wanaitwa dogani (frontiere) kila kundi ya mashetani inakamata ku mikono yao kartasi (papier) moja penye kwandikwa Matendo yote ya kila mutu; na ile wakati kama nafsi (roho) yetu inapenda kupita mashetani watatukumbusha Matendo yetu yote mbaya. Na watatuonyesha hivi : Siku fulani uliiba vitu fulani, siku fulani ulitenda zambi ya usharati ao ulitenda zambi fulani na fulani …..

Halafu, Malaika Wetu wachungaji watafunua matendo yetu mazuri. Kwa mfano kama tulifanya sala, tulihurumia, tulisaidia masikini, tulifunga, tulisharikia Liturgia ku Kanisa, kama tulilia kwa ajili ya zambi zetu na kwa ajili ya matendo yetu yote mema. Basi, Malaika na mashetani watapima matendo yetu yote mazuri na mabaya. Kama matendo yetu ni mazuri kabisa halafu Malaika watakamata nafsi (roho) yetu wataipeleka pa daraje ya yulu ya mungazi.

Na kule watapata kundi ingine mashetani wakali kupita. Nikusema kila kundi itaonyesha zambi moja.

Na hapa panafanyika ugomvi mingi juu ya kujua nani atabeba ile nafsi (roho). Mashetani wanatazamia tena wanaogopesha ile nafsi (roho) na wanasema : Wewe unaenda wapi ? Haukuzini na haukuharibu ubatizo wako? Sasa unapenda kwenda wapi? Rudia ku mukongo. Rudia chini ku Hadeze ya giza. Rudia ku moto ya milele. Rudia kwa vidudu wasipolala. Basi, kama ile nafsi ni ya kuhukumiwa, mashetani wataibeba, wataipeleka ku ile inchi, ku fasi moja ya giza. Ole, ole kwa ile nafsi. Ole kwa ile saa ule mutu alizaliwa. Ewe Padri wangu, nani ataweza kuonyesha mateso ngapi watateseka ku ile fasi ya gehena wale watu ambao roho yao itaenda kule?

Kama nafsi (roho) moja itakuwa safi itapanda kwa furaha mingi mbinguni, makundi ya Malaika Wataipokea na mishumaa (bougies) ya kuwakisha na chetezo ya ubani. Kisha wataipeleka ku kiti kubwa cha Bwana Yesu Mungu Wetu kubusu mukono Wake. Huko itaona makundi ya Mitume Watakatifu, makundi ya Mashahidi Watakatifu, makundi ya Mapadri Watakatifu, makundi tisa ya Malaika, atasikia nyimbo zao za mbinguni na atafurahi sana sasa.

Kisha Mutawa MAKARIOS alimuuliza Malaika juu ya nini tunafanye sala ya makumbusho kwa ajili ya wale watu walikufa.

Malaika alimujibu hivi :

Sikia ewe, Padri Mtakatifu.  Ile siku ya tatu kisha lufu ya mutu mmoja. Kanisa Orthodoksi inafanya makumbusho, kwani, sawa tulisema, ile roho haijaenda bado kwa Bwana Yesu.

Kanisa inafanya sala na inamuombe Mungu apokee na Mapendo mingi ile roho itafika ile siku ya tatu kubusu mukono kwa kupokea baraka yake.

Kisha kubusu Malaika Watapeleka ile nafsi (roho) ku dunia, ku ile fasi aliishi, kule wataanza kumuonyesha mafasi yake alitembea, na zambi zake alitenda. Nikusema watamuonyesha hivi: «Hapa, ee Nafsi (roho) uliiba vitu fulani, kule ulizini, hapa ulihukumu mutu fulani, hapa ulisema uwongo kule ulilewa, hapa ulifanya makelele, kule ulifanya machukizo» na zingine zambi.

Kisha Malaika wataanza kumukumbusha yale matendo yake mema. Kwa mufano: «Hapa ulisaidia, kule ulifunga, hapa ulitubu, kule ulisharikia  Liturgia ulifanya sala kwa Mzazi-Mungu. Sala ya usiku muzima,» na ingine. Kwa hivi hii matezamio wataifanya mupaka siku ya tisa. Ile siku ya tisa watarudi mara ingine mu mbinguni juu roho kubusu Bwana Yesu Kristu mara ya pili ..

Hapa waaminifu ya kanisa watafanya sala ya makumbusho juu Mungu apokee na huruma na macho yake ya Mapendo ya ile roho. Ndio vile iko mandiko ya Kanisa yetu ya kama ile waka ya makumbusho inaleta faida ku roho. Tena inasaidia Matendo ya huruma na kufanya Ibada Takatifu (Litrugia).

Kisha kubusu mara ya pili Malaika wataleta mara ingine ile roho ku ile fasi ya Paradiso. Kule wataionyesha kutazama Paradizo, iliyo fasi ya huruma ya Mungu, fasi ya Abrahamu, tena fasi ya watu wenye haki. Na wakati itaona ile furaha pasipo kusema, itafurahi itasihiina itaomba kwa Malaika ikae mule pamoja na watu wenye haki.

Kisha Malaika Watapeleka ile nafsi (roho) ku Gehena? Kule nafsi itaona namna wanateswa wale watu wenye zambi. Malaika wataionyesha hivi: «Tazama, hii ni mutoni ya moto, huyu ni kidudu wasipo kulala, hii ni giza ya inja na ya ndani, kule kunakaa wale watu wenye kusoga memo yao juu ya mateso mengi. Hivi polepole nafsi (roho) itaona mateso yote ya wenye zambi.

Padri wangu, alivyosema Malaika, hakuna mateso ya nguvu kupita mateso ingine sawa ile mateso ya musharati (kahaba ) na ya mnyanganyi. Kabisa- kabisa mateso itakuwa mingi kwa ule mutawa, mwanaume ao mwanamuke alizini, na ile mateso wataipata. Padri na bibi yake, kama walizini pasipo kutubu.

Kama itaisha hii safari, nafsi (roho) Malaika Wataipeleka nafsi (roho) mara ingine siku ya makumi ine (40 jours) mu mbinguni kubusu Bwana Yesu Kristu mara ya tatu. Basi waaminifu wanafanya sala ya makumbusho juu ya kumuomba Mungu akumbuke katika mapendo na huruma yake ile nafsi. Ile siku ya makumi ine iko siku ya hukumu, siku ya mwisho. Nikusema tangu ile siku nafsi (roho) itaenda ku ile fasi anataka Mungu Mpenda wanadamu kadiri ya matendo yake mtu alitenda mu dunia. Ni hivi ile nafsi (roho) itakaa mu fasi yake ya milele. Ni kule itabakia mupaka ile siku ya ufufuo wa mwili wake wakati atakapokuja mara ya pili Bwana Yesu Kristu. Kisha Ufufuo wa mwili wetu, nafsi (roho) itaungana na mwili na watasikia ao furaha, kama weko mu Paradizo, ao sakitiko na mateso mingi, kama wataenda mu Gehena.

Halafu, Mtakatifu MAKARIOS, alilia na alitosha machozi mengi na akasema : Ole kwa ile siku alizaliwa ule mutu !.

Malaika alimujibu:  Ndivyo, Padri mtukufu, hii mambo ni kweli paka kwa wote watu walitenda zambi, pasipo kutubu. Lakini kwa ule mutu mwenye haki sisi inapaswa kusema hivi : «Heri ile siku na saa, ule mutu alizaliwa».

Padri aliuliza Malaika mara ingine.

Ninakuomba kunionyesha tena na hii kitu: ule mutu mwenye zambi atakufa na ataenda mu gehena atakuwa na furaha ao mateso yake haitaisha?

Malaika alijibu hivi :

Hapana, ewe Padri Mtakatifu, hata ufalme wa wenye haki uko na mwisho, hata gehena ya wenye zambi iko na mwisho. Mufano, kama mutu mmoja atabeba mu bahari fungu ya mchanga mara moja katika miaka elfu (1000) kuipeleka fasi ingine itafika wakati moja atatamainia kubeba mchanga yote. Lakini wakati ya gehena na ya watu wenye zambi haitaisha hata kidogo. Vivyo hivyo na wakati ya Paradizo na ya wale watu wataingiamo haitaisha hata mara moja.

Padri aliuliza Malaika mara ingine- Ninakuomba uniambia na hii kitu, ewe Malaika wa Mungu: Watakatifu wake na huruma mingi kwa watu wote, juu ya kujua kama kile anaweza kuwa na Mapendo ya kumuomba msaada wao katika maisha yake?

Malaika alimujibu hivi;

Watakatifu wote wanawapenda watu wote na wanataka kuwasaidia. Lakini ninyi watu muko wabaya, watakatifu wanasikitika kwa ajili ya zambi zenu. Na wanasirika kwa sababu ninyi Munakataa kuwapigia «Aksanti», Kuwashukuru. Na Malaika Watakatifu weko na huruma mingi kwa watu wote, kwa sababu na wao waliona yale matendo ya ajabu alitenda Mungu juu ya wokovu wa wanadamu. Tena Malkia Mzazi- Mungu Mama Maria anasaidia sana kizazi ya Wanadamu.

Ilipaswa, Padri Mtakatifu, kila mutu kuchunga kinywani mwake jina la Mama Maria kwa kumuomba na kumutukuza. Lakini shetani alimudanganya na aliharibisha akili yake juu ya kusahau Jina na mapendo yake.

Leo, kama anaishi duniani, anaishi juu ya mapendo na sala ya Mama Maria kwa Mungu. Kwa sababu watu walizarau Mungu na Watakatifu Wetu.

Padri MAKARIOS aliuliza Malaika mara ingine : Uniambie, Malaika Mtakatifu, katikati ya zambi zote ni zambi gani iliyo kubwa zaidi ?

Malaika alimujibu : Kila zambi, ewe Padri Msifiwa, inatenganisha mutu kwa Mungu. Lakini chuki na matusi ni yulu ya zambi zote. Kwa sababu paka hii mbili zinaweza kuangusha mutu chini ya Hadeze.

Na tena Padri alimuuliza: Zambi gani Mungu anachukia kupita zambi zingine?

Malaika alimujibu: Majivuno. Ni paka hii zambi iliharibu dunia nzima. Kwa ajili ya hii Adamu aliyeumbwa wa kwanza alipoteza Paradizo. Kwa ajili hii Mkubwa wa kundi la Malaika wa Kwanza, alipoteza baraka na neema ya Mungu na kisha aligeuzwa akawa Malaika wa shetani. Kwa ajili ya hii Mufarisayo alipoteza uwezo wake kwa Mungu. Kama mutu atanguka kwa hii zambi ni nguvu sna kutubu na kuamuka.

Mara ingine Padri alimuuliza : Watu gani wanateswa. Mu gehena kuliko wengine ?

Malaika alimujibu hivi : Ninakuonyesha ni musharati na mwenye kuchambulana. Lakini nakuambia tena ya kama katika gehena ni fasi moja ya matata na yasipo rehema ya Mungu. Maana yake ni fasi yasipo kuonekana. Kule wanalipizwa na mateso mengi wale Mapadri, watawa wanaume na wanawake walizini pasipo kutubu mbele ya kufa kwao.

Ile kundi ya kwanza ya Malaika ilianguka ndio sasa kundi ya mashetani. Mapadri na Watawa waliishi hapa duniani muzuri wataokolewa na sifa yao itakuwa kubwa sana.

Halafu, Watawa Wabaya na wenye kuvunja amri Mungu atawatuma bila sifa, ku fasi, ya malipizi. Tena, kama Mapadri sababu ya uzaifu wao, wanaacha kufanya sala yao ya kila siku (asubui, manparibi, usiku) ao Liturgia ya siku ya Mungu na ya Watakatifu wetu nao pia watalipizwa sana kwa Mungu. Lakini nitasema nini juu ya Mapadri walevi? Ole wao kwa sababu malipizi ya ngubu kabisa inawaongojea.

Basi Padri MAKARIOS aliuliza tena Malaika:

Nakuomba unionyeshe hii mambo: Wale watu wanazarau siku ya Mungu watakuwa na faida na furaha hata kidogo kule mbinguni ?

Malaika alimujibu hivi: Ole wao, ewe Padri mukubwa, kwa sababu malipizi ya nguvu inawaongojea. Ule mutu anazarau ile siku ya Mungu, anazarau Bwana Yesu Kristu na Yesu atamuzarau kwa sababu siku ya yenga ni siku ya Bwana Yesu.

Ule mutu anasifu siku ya yenga, anasifu Bwana Yesu Kristu. Ule mutu makumbusho ya Watakatifu na anashangilia siku za Makumbusho yao, Watakatifu watamusaidi, kwa sababu weko na uwezo kubwa kwa Mungu na wakimuomba kila kitu, Bwana Yesu atawapatia. Lakini watu walifukuza woga wa Mungu rohoni mwao, na sasa hawana Mungu rafiki yao, ao Mtakatifu fulani akili yao na roho yao vitawatawaliwa paka kwa vitu vya bure vya hii uzima, pasipo kuwaza ya kama vitu hivi vitatoweka na vitapotea.

Sikia. Muzuri, Padri muheshimiwa, kila mutu akiwa Padri, ao Mutawa ao Laiki akikataa kusifu na kwenda ku Misa kila siku ya Mungu hataona uso wa Mungu, na hatapata matumaini ya wokovu wake.

Na sasa, Padri mtukufu, kama unataka kuniuliza kitu ingine, uniulize, kwa sababu sasa ni wakati kutoka mbinguni kwa Bwana Mungu wangu kwa kumutukuza.

Basi, Padri MAKARIOS alilia, na alisema: Ole kwa sisi «Tazama, huyu mutumishi muzuri wa Mungu ni Malaika wasipo Mwili na zambi, na anajiharikisha kwenda kumutukuza Bwana Yesu Kristu. Lakini sisi watu wenye zambi na wa bure hatuna na hii baraka ya kumutukuza Mungu lakini tunazarau wokovu wetu.

Na tena alimuuliza ule Malaika wa Mungu:

Ninakuomba uniambie, sala gani Watawa wa waaminifu wetu wanapaswa kufanye? Ule Malaika alijibu hivi: Kama mutu mmoja ni mwenye elimu, nikusema mutu wa akili ni vizuri kusoma zaburi ya Daudi.  Kama hana mutu wa elimu, anaweza kusema hivi : «Bwana Yesu Kristu, Mwana wa Mungu, unihurumie mimi mwenye zambi». Hii sala iko nguvu kabisa na teketeke kabisa, kwa hii maneno, watu wa akili mingi waliacha vitu vyote vya dunia wakaishi na uzima takatifu walitumika hii sala.

Hii sala watu wote wanaweza kuisema hata watu wa bure wasipo akili mingi kilamutu mwenye kutaka kuokolewa, ataweka kinywani mwake na mu akili yake hii sala pahali popote, mchana na usiku, njiani, kama anaikaa ao anatembea, ao anatumika, na hii sala iko na nguvu kusaidia ule mutu anataka kuokolewa.

Na tena Padri mukubwa alimuuliza Malaika:

Kwa sababu, ewe Malaika wa Mungu, ulifika kunifundisha mimi mwenye zambi nakuombe unioyeshe na hii kitu : Kama mutu mmoja eko mwenye zambi na atafundisha mutu mwingine kwa kuacha njia ya zambi na kufwata njia ya wokovu, yeye atapata malipo fulani ya roho yake ao hapana ?

Malaika alimujibu hivi :

Ule mutu atafundisha mutu mwingine na kumutosha mu njia ya zambi kwa kumwonyesha njia ya Mungu, huyu aliokoa nafsi (roho) yake na nafsi ya ndugu yake mu gehena. Lakini ule mutu alishauria ndugu yake kufawata njia mubaya, atamuharibu ule ndugu yake, na nafsi yake ataitoa mikononi mwa shetani. Halafu, hakuna zambi ingine kubwa zaidi kuliko hii anatenda mutu ya kuondoa ndugu yake mu njia ya Mungu na kumupeleka mu njia ya shetani. Na hakuna kazi ingine kubwa zaidi, sana ile anafanya mutu kwa kumushauria ndugu yake kwa kufwata uzima wa roho, uzima wa Mungu ….

Kisha kusema hii maneno ule Malaika aliinamisha kichwa chake kwa Padri, akamwambia

Unihimidi, Padri Mtakatifu na unisamehe.

Basi Padri MAKARIOS alipiga magoti yake chini, alimubusu Malaika na alimwambia :

« Wende na amani ku Utatu Mtakatifu na uniombee.

Wakati Malaika aliondoka na alipanda mbinguni, Mtakatifu MAKARIOS alimushukuru Mungu, alienda nyumbani mwake, na kule alionyesha mazungumuzo yote kwa rafiki yake mmoja

Mutawa mwingine aliyeishi pamoja naye, hivi vyote viwili vilitukuza na kuhimidi Mungu wa milele.Amin.

Mwisho, Utukufu kwa Mungu .-

## 38. Historia ya mwanamuke moja aliyerudia toka uzima ingine

Niliishi bila imani ya Mungu na nilichabula matata Mungu. Niliishi ndani ya haya na uzini na usharati na nilikuwa mu hii inchi kama maiti moja. Lakini Mungu Murahimu hasikuniache kujipotea, lakini aliniongoza mu toba.

KU mwaka 1962 nilipata malari ya cancer na nilikuwa mugonjwa miaka tatu. Misikuikaa pa kitanda, lakini nilitumika na nilifanya tunza kwa waganga kila wakati na nilitumainia ya kama nitapata tunzo. Ma mwezi ya sita ile ya mwisho ya uzima yangu, nilikonda sana na misikuweze kukunywa hata maji kidogo. kama nilikunywa mara moja niliitapika. Ile nyakati walinipeleka mu Obitalo na, kwani nilikuwa tena nguvu, waliita muganga moja toka kapitala muji Moska na walikamata mpango kunifanyisia operation. Wakati walinifugula tumbo yangu, mara moja nilikufa. Nafsi yangu ilitoka ya mwili yangu na ilisimama katikati ya waganga wa wili na mimi na boka mingi niliangalia malari yangu. Tumbo yangu yote na matumbo yote waliisha kujaza na cancer. Nilisimama na niliwaza juu ya ninyi tuko wa wili? Misikujue ya kama mtu eko na na nafsi. Wakubwa ya inchi yetu, wenye walikuwa wa Komuniste, walitufundisha ya kama Mungu na nafsi hakuna na hi fundisho juu ya Mungu ni uwazo na fundisho ya wapadri juu ya kulanda na kulogofya taifa na kumuchunga kwa boka. Basi, ninaona maungo yangu kusimama na tena ninamuona kuikaa pa kitanda na pempeni waganga. Walinitosha matumbo yote na walitaka kuisafisha ya cancer. klakini ndani ilikuwa paka buchafu na matumbo yote waliisha kuharabika na kuoza, hata kidogo toka matumbo ilikuwa na afya. Waganga walisema ya kama «huyu mwanamuke hakuna kintu na afya juu ya kuishi». Mimi niliona hii ma kazi yao na boka mingi na niliwaza mara ingine: « namna gani sasa wa wili? » Waganga ile saa walirudisha matumbo yangu ndani ya mwili yangu na walisema ya kama mwili yangu inapaswa kuipatia kwa waganga wengine juu ya kufanya kipimo ya mafundisho wanafunzi ya medicine. Lakini na mimi nilikwenda karibu yao na nafsi yangu na nilistaajabu namna gani tuko wa wili? Kule waliniacha pa kitanda moja, mutupu na yulu yangu waliweka paka sanda moja meupe. Kisha niliona ya kama alikuja ndugu yangu na alileta na mtoto yangu mwanaume. Ile mwaka mtoto alikuwa na kipimo miaka sita na aliitwa Andreas. Mtoto yangu alikaribia mwili yangu, alinibusu pa kichwa. Alianza kisha kuria na kusema: « Mama, mama, juu ya ninyi ulikufa? Mimi niko mtoto mudogo tena na namna gani nitaishi bila weye? Baba misinana na weye ulikufa? ». Mimi ile saa nilimubatia, nilimubusu, lakini huyu mtoto hasikusikie hii tendo yangu, wale aliniona, wala alisopoka, paka aliangalia mwili yangu iliyekuwa maiti pa kitanda. Tena niliona ya kama aliria na ndugu yangu. Kisha mimi mara moja nilikuja mu nyumba yangu. Alikuja muke yangu toka ndoa yangu ya kwanza, mama yangu na dada yangu. Bwana yangu ya kwanza nilimwacha, kwa sababu alisadiki kwa Mungu. Ile saa walianza kukaburia ma bintu yangu. Mimi niliishi na mali mingi na bile bintu yangu nilibadilisha na uzulumu na usharati. dada yangu alianza kuvaa ma nguo yangu ile walikuwa ya nzuri kabisa, lakini muke yangu alipenda kuacha na bintu kidogo kwa mtoto yangu. Dada yangu hasikutake kuacha hata kintu kimoja na alianza kuchekelea muke yangu na kusema kwake: «Huyu mtoto hana toka mwana wako na weye usiwe kintu kimoja». Kisha, hawa walitoka inje na walifunga nyumba yangu. Dada yangu alibeba pamoja naye muzigo moja na ma bintu yangu. Wakati wale walijikombana katikati yao juu ya ma bintu yangu, niliona ma shetani kucheza na kufurahi pempeni yao.

Mara moja nilikuja pa pepo na niliona kuluka na avion moja. Ninasikia ya kama mtu moja ananikamata na ninanyanyua kuliko yulu. Nilikuwa yulu ya muji Barnauli. Kisha niliona ya kama

muji haikuonekane. Ilikuja giza. Kisha giza ilikuja nuru nguvu sana na mimi misikuweze kuvumilia hii nuru nguvu. Waliniweka pa fasi moja.

Niliona miti na makanda ya mnene na mayani mazuri ya kuachana. Katikati ya miti walikuwa na ma nyumba mapya yote kabisa, lakini misikuone wa nani walikuwa ndani. Ndani ya hii kiwanja niliona mayani mingi ya mwesobe na niliuliza maungo yangu: sasa niko wapi? Kama niko mu inchi yetu, juu ya ninyi hakuna ma ma njia na ma motokaa na bintu ingine ya inchi yetu? Kidogo mbali niliona kutembea mwanamuke moja muzuri na murefu sana na mavazi ya ufalme na chini ya hii manguo walionekana ma bilole ya miguu yake. Alitembea hata teketeke na mayani haikuhabishwa toka utembeleo yake. Pempeni yake alitembea na kijana moja mwanaume na kipimo ya urefu yake ilikuwa mupaka mbavu ya yule mwanamuke. Aliisha kuzibiria uso na mikono yake, aliria na uchungu na aliomba kintu kimoja toka yule Mwanamuke, lakini misikuwe kusikia aliomba ninyi. Niliwaza ya kama alikuwa mwana wake na ndani yangu niliwaza juu ya ninyi anakataa kumwambia mapendo na kutimiza matakio yake? *(Toka hii historia yote inaonekana ya kama huyu kijana alikuwa malaika muchungaji ya huyu mwanamuke aliyeisha kufa. Tena inaonekana hapa ngapi mapendo wanaonyesha wa malaika watakatifu juu ya sisi na ya ma nafsi yetu, lakini sisi tusiweze kuiona. Tena inaonekana ya kama, kama sisi tutakufa ndani ya zambi, Mungu na Mama wake hawapende kusikia na kutimiza matakio ya wa malaika wachungazi wetu).*

Huyu kijana alianguka mbele ya miguu ya Yule Mwanamuke na alianza kumwambia nguvu na kuomba kintu kimoja. Yule alimujibu sauti moja, lakini misikuweze kusikia alimujibu ninyi.

*(Nilikuwa na wakati ingine kujua namna gani anaria sana Malaika Mtakatifu na muchungazi yetu, wakati huyu mutu aliyemupatia Mungu kwa Malaika moja juu ya kumuchunga, lakini huyu mtu hasipende kumbakia kwa Imani ya Kristu ukweli na anapotea nafsi yake kwa ajili ya zambi na mafundisho ya uwongo).*

Wakati hawa walinikaribia, nilitaka mimi kumuuliza: «Niko wapi? ». Ile saa huyu mwanamuke aliweka kama alama ya musalaba mikono yake pa kilari yake, alinyanyua ma macho yake mbinguni na alisema: «Ee Bwana, huyu ataenda wapi na hii hali ya nafsi yake? ». Mimi nilitetemeka na sasa nilisikia ya kama niliisha kufa, ya kama nafsi yangu ilikuwa mbinguni na mwili yangu ilikuwa mu inchi. Ile saa nilianza kuria na kuomboleza na nilisikia sauti moja: «Mumurudisheni hiinafsi mu inchi mara ingine kwa ajili ya matendo mazuri ya baba yake». Kisha sauti ingine nilisikia: «Nilichoka kuona hii uzima yake katika usharati na zambi. Mimi nilitaka kumuepuka toka uso ya inchi, bila kitubio, lakini aliniomba juu ya huyu baba yake. Mumuonyeshe ile fasi ilipaswa kwenda».

Mara moja nilienda mu gehena. Ile saa walianza kukuja mpaka mimi ma nyoka ya moto na ma ulimi yao walitosha moto na machafu. Arufu ya uchafu yao hakuna namna kuivumilia. Hii ma nyoka walikuja pempeni yangu na mara moja walikuja na ma bilulu ya munene sawa kilole moja. Hawa ma bilulu waliingia ndani yangu na waliniteswa na mimi nililalamika lakini hapana na sauti ya kinywa yangu, nililalamika na namna ingine. Lakini kule haikukuwe saidio, hata toka fasi fulani, wala rehema ya mtu moja. Kule niliona na huyu mwanamuke aliyekufa kwa ajili ya kutosha mimba na mapenzi yake na alianza kuomba kwa Bwana juu ya kumurehema. Huyu alimwambia: «Weye mu inchi usikunifamie, uliuwa watoto yako ndani ya tumbo yako na ulisemaka kwa watu wengine: «musizale watoto, kwa sababu watoto ni bintu ya bure». Lakini kwa Mimi hakuna watoto ya bure. Kwa Mimi na ma bintu yote ya muzuri.

Kwa mimi Bwana alisema: Mimi nilikupatia ugonjwa juu ya kutubu, lakini weye ulinichabula mupaka mwisho ya uzima yako na usikunifamie na kwa hii neno na mimi misitakufamia. Sawa vile mu inchi uliishi bila Mungu, hivi na sasa utaishi bila Mungu! ».

Mara moja waligeuza ma bintu yote na mimi nililuka mu fasi moja mbali. Uchafu na arufu kibaya yake ilitoka na ombolezo ilisimamisha na mimi mara moja niliona kanisa yangu,

iliyechokoza. Ilifugula mulango na toka yake alikuja inje mpadri moja na mavazi meupe. Huyu alisimama na kichwa yake chini na sauti moja ananiuliza:

-Nani iko huyu?

-Mini nilijibu: Ni mpadri wetu.

WEye ulisema ya kama ni mtu mubaya, lakini hana mubaya, ni muchungazi ya kweli na anatumika hapana ya makuta, lakini juu ya wokovu ya waminifu yake. Sikia hii sauti yangu, ya kama huyu mpadri anatumika mu kazi yangu. Kama, kwa mufano, yeye hasitasoma kwako sala ya usamehe, hata na mimi misitakusamehe.

Ile saa nilianza kuomba kwa Mungu: ee Bwana, unirudishe mu inchi, kwani nikona mwana moja mudogo.

Bwana aliniambia: Ninajua ya kama ukona mwana moja mudogo, ni sikitiko kwani yeye nu wa pekee.

-Kweli ni mambo ya sikitiko, nilisema mimi mwake.

-Ile saa Yule alinijibu: Mimi ninamitaabu wote na mara tatu ninamitaabu. Ninamiongojea yote mweye wakati gani mutalamuka toka ndoto wa zambi ya uzima yenu juu ya kutubu na kukuja karibu Yangu.

Hapa sasa alionekana mara ingine Mama ya Mungu, Mzazi-Mungu, mwenye nilimuita mbele mwanamuke na nilibeba nguvu kumuuliza:

-Iko hapa kwa mweye paradizo?

Misikubebe jibu, lakini mara ingine niliingia mu gehena, mu Hadeze. Sasa hali yangu ilikuwa kabisa kibaya ya zamani. walikuja pembeni yangu ma shetani na ma karatasi kwa mikono yao na walinionyehsa ma zambi na makosa yangu na walisema:

Weye ulitumika kwa sisi, wakati ulikuwa mu inchi.

Walianza kusoma ma zambi yangu; matendo yangu yote walikuwa kuandikwa na ma herufi manene na nilisikia boka. Toka ma kinywa yao ilitoka moto. Ma shetani walinipiga pa kichwa yangu. Yulu yangu walianguka makala ya moto na walinilugua. Pempeni yangu walisikiwa maombolezo na malalamiko ya watu mengi sana.

Wakati moto ilikuwa nguvu, niliona ma bintu bote pempeni yangu. Ma nafsi ya watu walikuwa uso kibaya sana; ma macho yao walikuwa ya kuvimba sana na waliniambia: «weye uko dada yetu *(Nikusema hawa watu walikuwa mu uzima yao mu parti ya Komuniste)* na inapaswa kuishi pamoja na sisi hapa. Sawa vile weye, vile na sisi, wakati tulikuwa mu inchi tulikataa Mungu, tulimuchabula na tulifanya kila tendo kibaya, uzini, usharati, majivuno na tusikutubu hata siku moja juu ya makosa na zambi yetu.

Ninyi wote walifanya zambi, lakini walitubu, walikwenda mu Kanisa, waliomba kwa Mungu, walisaidia wamaskini na ninyi wote walikuwa  na huitaji ya saidio.

Mimi niliogopa, wakati nilisika hii ma sauti yao na nilizania ya kama nilikuwa mu gehena yoyote uzima yangu na hawa waliniambia ya kama nitaishi pamoja na wao kwa milele.

Kisha hii mambo alionekana Mzazi-Mungu mara ingine  na ilikuja nuru; ma shetani walikimbia na ma nafsi waliyekuwa mu gehena na waliteswa, walianza kuomba huruma na saidio hivi:

-Mfalme Mama wa mbingu, usituache. Ee Mzazi-Mungu Mama Maria tunalugua na hakuna hata tone  moja ya maji ya kusikia kidogo baridi.

Yule Mama Maria aliria na ndani ya machozi yake alisemaka: «Ile wakati mulikuwa mu inchi, mulikataa kunifamia na hamukutubu juu ya ma zambi yenu ile mulifanya mbele ya Mwana wangu na Mungu wenu na mimi sasa misiweze kumisaidia, misiweze kukanyanga matakio ya Mwana wangu na Huyu hasiweze kukanyanga matakio ya Baba wake. Ninasaidia paka hawa watu waliwasaidia waajerani yao na juu ya wale anaomba Kanisa». Kisha sisi tulinyanyua tena yulu na chini ilitoshwa arufu kibaya na malalamiko ya ma nafsi: «Mama Mzazi-Mungu, usitwache».

Mara ingine ilijaza giza na mimi niliikaa mu fasi moja. Mzazi-Mungu aliungana mikono yake pa kilari yake, kama alama ya musalaba, alinyanyua ma macho yake mbinguni na alianza kuomba mukusema hivi: «Nitafanya ninyi juu ya huyu nafsi? Nitamuweka wapi? na sauti moja alimujibu: «Umuache toka ma nywele yake». Ile saa Mzazi-Mungu aliondoka na kimya. Kisha alirudia na alikamata ma nywele yangu pa mikono yake na mara moja walionekana ma motokaa kumi na mbili, bila ma mupeto; walitembea pole-pole na mimi niliwafata. Mzazi-Mungu alinipatia ma nywele yangu, lakini misikusikie mimi ya kama Mzazi-Mungu alinigusha. Nilisikia paka, wakati alisema ya kama motokaa ya kumi na mbili haina muskingi. Niliogopa kuikaa pa hii motokaa, lakini Mzazi-Mungu alinisukuma.

Kisha hii mambo mimi nilirudia kwa akili yangu na katika mioyo yangu niliangalia. Ilikuwa saa moja na kipande ya muchana. Kisha ile nuru niliyeona, bile bintu ya inchi yetu walinionekana mbaya sana na hainikupendeze kwani nilikuwa mu inchi, lakini nitafanya ninyi? Sasa nilisema mimi kwa nafasi yangu: «Uende kwa mwili yako». Ile saa nilirudia mara ingine mu obitalo na niliende mu fasi ya baridi, pahali walichunga ma maiti ya wafu. Hii refrigerateur ilikuwa kufunga, lakini mimi niliingia ndani, bila kizibirio na niliona mwili yangu ya kufa. Kichwa yangu ilikuwa kupindula kidogo mu fasi moja, lakini kifuno yangu iliteswa kwa ajili ya maiti ingine. Wakati nafsi yangu iliingia ndani ya mwili yangu, mara moja nilisikia baridi nguvu. Niliuhuru kifuno yangu na nililokota miguu na mikono yangu. Ile saa waliweka ndani ya hii nyumba ya baridi maiti ya mtu moja mufu na, wakati walifugula moto, waliona mwili yangu na fasi ingine. Wakati waganga waliiona mwili yangu na namna ingine, walishangaa na walikimbia. Walirudia kisha pamoja na waganga wa wili, wenye walisema kuweka moto karibu ya kichwa yangu. Pa mwili yangu waliisha kufanya bilonda mnane, kwa sababu pa mwili yangu wanafunzi walifanya mafundisho na kipimo. Ma saa mbili kisha ile moto waliiweka pa kichwa yangu juu ya kuwa kivukutu, nilifuguyla ma macho yangu na kisha ma siku kumi na mbili nilisuburia.

Asubui waliniletea kidogo chakula bitubula na mateka na kafe. Ile siku ilikuwa siku ya kwarezima. Joo vile misikukule. Na niliwaambia ya kama misitakula. Wasaidizi ya waganga waliondoka na watu wote ya obitalo walianza kunisopoka. Walikuja waganga na waliniuliza juu ya ninyi misipenda kula. Niliwajibu: «Muikaa na nitamiangaza nafsi yangu aliona ninyi. Leo misitakula na ma siku yote ya kifungo ya chakula misitakula. Waganga walishangaa na saa ingine waligeuza ragi na walionekana na ragi nyekunda, saa ingine walionekana na ragi majano na wenye malari walinisikia na pasopo mingi. Kisha walisanyikwa waganga wengi na mimi niliwaambia ya kama misisikie hata umivu kidogo. Ile saa alianza kukuja kwangu watu mingi na mimi niliwaambia niliona ninyi na niliwaonyesha ma bilonda pa mwili yangu. Police alianza kufukuza watu na mimi walinipeleka mu obitalo ingine. Kule nilipata afya kamili na niliomba ya waganga kunitunza ma bilonda yangu, kama iko namna na haraka. Ile saa waliniweka mara ingine ndani ya nyumba ya operation, na wakati waganga walifugula tumbo yangu, walisema: Juu ya ninyi walifugula huyu mtu, ambaye ni mwenye afya kabisa? Mimi ile saa niliwauliza: «Ni nani malari yangu? Matumbo yako ni safi na katika afya, sawa ma tumbo ya mtoto mudogo». Niliwaambia ya kama ma macho yangu ile saa ya operation walikuwa ya kufunga, lakini niliona hali ya tumbo yangu ndani mu rikalashi ya hii nyumba.

Walikuja na wale waganga, wenye walifanya operation na, wakati walikaribia, waliuliza:

Iko wapi malari yake? Matumbo yake walikuwa ya kuharabika sana kwa ajili ya cancer na sasa ni katika afya kabisa.

Niliwajibu: Bwana na Mungu wetu alionyesha rehema Yake kwa mimi mwenye zambi juu ya kuishi tena na kushuhuda na kwa watu wengine kila niktu niliona na mambo ninyi ilinifata. Yule Bwana na Mungu alibeba kila kintu iliyeisha kuharabika ndani ya tumbo yangu na alinirudisha katika afya kabisa. Hii muujiza nitaisema mupaka lufu yangu. Kisha nilisema kwa muganga: «Unaona namna gani mulijilogofya? ».

Na  huyu alinijibu «ya kama hakuna hata kintu kimoja iliyekuwa na afya ndani ya tumbo yako.

Mimi nilimuuliza: Sasa munasema ninyi?

Huyu alinijibu: Mungu Mweneyzi alikutunza.

Ile saa mimi nilimujibu: Kama munasadiki Kwake, mufanye alama ya musalaba na mufanye ndoa yenu mu Kanisa».

Muganga alisikia haya aligeuza ragi kwa nyekunda, kwani alikuwa toka kizazi ya wa Ebrania. Nilimwambia tena: «fanya nguvu ya kupendezwa kwa Bwana na Mungu».

Kisha niliacha obitalo, niliita mpadri, mwenye zamani nilimuchekelea na nilimuchabula. Nilimwambia matendo hii yote, kisha niliungama na nilipewa Komonyo Takatifu. Nilimuita na alibariki nyumba yangu, kwa sababu mpaka sasa ilitawala  ndani zambi ya kuachana, ulevi, uchekeleo na funjo.

Sasa mini mwenye zambi Klavdia, kwani hii ni jina yangu, niko sasa miaka kwa kipimo yangu 40 na saidio ya Mungu na Mama Mfalme wa mbingu Maria, ninaishi katika fundisho ya Mungu, ninaenda mu kanisa ya Mungu na Bwana ananisaidia. Wanakuja watu toka ma fasi yote ya dunia kunitembelea na mimi ninawambia hii matendo yote walinijifanya kwangu, kisha lufu yangu ya kwanza. Na saidio ya Mungu ninawapokea wote, ninawatangaza mtu nani nilikuwa zamani, ilinijifanya kintu ninyi na sasa juu ya ninyi niko mwaminifu ya Mungu mu Kanisa yake Ortodokse.

Iwe Jina ya Bwana na Mungu wetu utukuzwa kwa milele! Sasa ninawashauria watu wote kusopoka namna gani wanaishi, kwa sababu iko dunia ingine na uzima ingine ya milele na kila mtu atapatia jibu juu ya matendo yake ya hii dunia na katika hii matendo yake atabeba na malipo ya roho kwa uzima ya milele.

Basi, wa ndugu wangu, mumbakieni mu kanisa ya Mungu, mu Kanisa Orthodokse na muishi katika sheria ya Mungu. Amina.

## 39. Ee mwenye zambi, unataka na weye kukuja hapa?

Wakati nilikuwa duniani, lakini nilianza kusimamisha kila urafiki na watu ya dunia, nilisimama kutembelea ma nyumba ya watu na kila wakati nilitembelea paka ma nyumba mbili-tatu. Jamaa moja, pahali mimi nilimutembelea ilikuwa na mama moja na mtoto mwanamuke yake na mukana moja mwanamuke. Siku moja tuliikaa pa meza kukunywa chai na huyu mama muzee alisema hii historia:

Mbele ya miaka madogo, wakati nilipotea bwana yangu, nilikuwa na sikitiko mingi na tabu. Uzima iliisha kupotesha kwa mimi kila maana na uhodari na uwazo ya kutundikwa ilikuja ndani ya akili yangu mara mingi. Misitaweze kusahabu ile siku ya Ufufuo ya Kristu. Ile tarehe ilikuwa tarehe ya matata na kabaila pamoja. Kwa saidio ya mama yangu bile bintu ya hii Siku Kuu kubwa walikuwa tayari; nyumba yetu iliisha kubeba uso ya shangilio na Siku Kuu. Lakini ndani ya nafsi yangu misikusikie Paska! Kupindua, ilikuwa ndani yangu giza ya taabu. Mama yangu, halafu, aliyejua hali ya nafsi yangu, hasikuniache kufanya hata mwendo moja mimi wa pekee na mbali yake, bila kuniangalia. na ile saa mimi, nilipata nyakati nzuri juu ya kutimiza uwazo yangu, ile usiku ya Ufufuo ya Kristu. Mama  yangu alikwenda mu Kanisa ya aubui mapema. Vile, niliwaza, hakuna mutu mwingine mu nyumba juu ya kunizibiria; paka alikuwa mtoto mudogo yangu mwanamuke, lakini hakuna mambo toka huyu mtoto! Nilisema, basi, kwa mama yangu ya kama mimi nitachelewa kidogo, kwa sababu iliniuma kichwa yangu. Lakini nilisema uwongo. Mama yangu alinijibu: Muzuri, uikaa kidogo na, wakati itapita umivu ya kichwa yako, tutaenda pamoja mu Misa».

Mimi juu ya kusimamisha mazungumuzo naye, nililaria pa kitanda. Na bila kusikia, nililala. na mara moja niliona ndoto moja ya ajabu kabisa. Niliona ya kama nilikuwa ndani ya nyumba

moja wa giza na matata. Hii chumba ya nyumba ilikuwa chini ya bulongo ya inchi. Ndani ya hii fasi ya matata alikuwa mtoto moja mwanamuke, aliyekuwa zamani mwanafunzi pamoja na mimi ku masomo.

Nilimuona na nilimuita: Ee Olga, Olga, unafanya ninyi hapa?

Na huyu alinijibu: Ee mwenye zambi, unataka na weye kukuja hapa?

Na mara moja nilisikia kengele ya kanisa kuria.

Nilifugula ma macho yangu na boka na tetemeko mingi. Niliona ya kama nilikuwa ndani ya chumba yangu. Nilipata kimya. Hii saa aliingia na mama yangu mu chumba yangu.

-Ee binti yangu, ulilamuka? Namna gani iko kichwa yako?

-Ilipita umivu, mama yangu; saa tutaenda mu Misa.

Alifurahi na alisema: Ee Bwana utukufu kwako. Na nilikuwa na sikitiko ya kama leo utambakia bila kusikia ibada ya asubui ya Ufufuo ya Kristu!

Kisha Ibada ya Ufufuo ya Kristu, wakati mama yangu alinikulamukia kwa ajili ya hii Siku Kuu na alinisema: Kristu alifufuka- kweli alifufuka», tulianza kusuburia na namna ya mapendo. Na ile saa mimi nilimwambia hii mambo niliyeona kwa ndoto yangu. Juu ya yule murafiki yangu Olga misikujue hata kintu kimoja; wala aliishi wapi na wala mambo ninyi ilimufata. Lakini pole-pole nilipata adressa ya kambo mwanaume yake. Nilimuandika barua. Nilimuuliza anafanya ninyi Olga na huyu alinijibu hii ujulisho ya taabu, ya kama mbele ya mwaka moja, mukana yake Olga aliisha kutundikwa. Ile saa na mimi nilisikia maana ya ndoto yangu.

Bwana Mungu alifundisha huyu binti, mwaminifu yake katika hii ndoto. Mimi misisopoke sana kwa ma ndoto, lakini ma ndoto ingine ni ya kweli.

## 40. Mu Hadeze hakuna toba

Askofu Grigorio: Bwana yesu anatwaambia mu Evangelion yake: Mutembee mpaka mukona moto ya kuona. Tena kinywa ya Nabii inatwaambia: «ile nyakati ilipaswa kukusikia nilikusikia na, wakati uliweza kuokolewa, nilikusaidia». Na Nabii Solomono tena anasema: Kila tendo unaweza kufanya na mikonbo yako, uifanye. Kwani, kama utaenda mu Hadeze, kule wala kazi, wala hekima, na wala ujulisho moja iko».

Basi, toka hii mashuhuda inaonekana ya kama, namna gani uko, wakati unaondoka ya hii dunia yetu, vile utasimama na mbele ya Mungu ile siku ya Uhukumu ya mwisho. Lakini inapaswa kujua ya kama wafu wanaokolewa toka makosa madogo yao na saidio ya ma huruma, Ma Ibada ya Liturgia Takatifu na maombi ile tunafanya sisi wenye zambi kwa wenye kufa. Tena matendo ya watu wenye fazila wanasadidia ma nafsi ya wafu. Na, iko namna kwa ajili ya matendo ya watu wa fazili, na hawa ma nafsi kupata faida moja na usamehe ya zambi yao.

Mwanafunzi yake Petro Ninataka na ninakuomba kuniambia na hii mambo. Nikusema wale walihukumwa mara moja na walijitupa ndani ya gehena, sisi inapaswa kusadiki ya kama hawa watalungua na watateswa kwa moto ya milele?

Askofu Grigorio: Hii ni hivi na aipaswe kushaka hata kidogo. Kwa sababu sawa vile hakuna mwisho kwa furaha ya wenye haki, vile hakuna mwisho kwa mateso ya wenye zambi. Na hii sauti alisema kinywa ya Bwana Yesu, ya kama wenye zambi wataenda mu gehena ya milele na wenye haki na wazuri mu uzima ya milele. Kama ni kweli hii sauti Yake iliyesema juu ya wenye haki, vile itakuwa kweli na sauti iliyesema juu ya wenye zambi. Na kama mtu moja atasema ya kama Mungu ni Mwema kamili na hasitatimiza sauti Yake, inapaswa kujua ya kama, kama anamuona Mungu kama mwema na mupendwa-wema, inapaswa kumuona Mungu kama mungu ya uwongo, lakini hii sauti ni ya hatari hata kama mtu moja anataka kuiwaza.

Mwanafunzi yake Petro Ninataka kunielejea juu ya kusikia nzuri namna gani inaunganishwa haki ya Mungu na namna gani ni ya kweli kulipizwa mtu moja ya milele juu ya

moja zambi yake iliyefanya mbele ya miaka mingi, kama tutawaza ya kama zambi ya dunia itasimamisha nyakati moja?

Askofu Grigorio: Mungu ambaye ni mwema kamili, hasifuraha kuona kiumbe yake ya kuteswa ndani ya gehena; lakini, kwa sababu ni mwenye haki inapaswa kulipiza wenye zambi na wazulumu. Na hawa wenye zambi na wazulumu, wenye walienda mu gehena walienda kule na mapenzi yao na kwa ajili ya matendo mbaya yao. Lakini hawa wenye haki, wenye ni karibu ya Mungu, wekona ndanbi yao furaha bila kuisema iliyetoka ya Mungu. Na mukuona mateso ya wenye zambi mu gehena, wanamushukuru Mungu, kwa sababu aliwaokoa toka bile mateso.

Mwanafunzi yake Petro Uniambie ninakuomba, hawa watakatifu, wenye ni warafiki ya Mungu, juu ya ninyi hawaombe kwa Mungu juu ya wale waliingia mu gehena?

Askofu Grigorio: Watakatifu, ee Petro, wanaomba kwa Mungu juu ya wenye watu mbaya; tena wanaomba juu ya wa adui yao, sawa vile anasema na kinywa ya Kristu, nikusema kuomba kwa wa adui wetu juu ya kuokolewa toka mateko ya shetani na wanatumika mapenzi yake kibaya. Lakini, kama haweze ao hawapende kurudia kwa matendo ya fazila ya Kristu na haki, faida gani sisi tutawapatia, kama tunaomba kwa ajili yao?

Kama tunaomba kwahawa watu wenye zambi, iko sawa kuomba juu ya wokovu ya shetani na watumishi wake, wenye walihukumuwa kwa milele mu gehena. Kwa hivi watakatifu wetu hawaombe kwa wale watu wasipo imani ya Mungu, wala juu ya wafu, waliyeishi ndani ya kibego na ma ndini ingine, kwa sababu wanajua yakama walihukumwa mu gehena ya milele na kila maombi yao mbele ya Mungu ni ya bure.

Mwanafunzi yake Petro: Juu ya ninyi wanasema ya kama nafsi ya mtu anakufa ndani ya nmoto wa milele, lakini sisi tunajua ya kama nafsi ni usiyekufa?

Askofu Grigorio Uzima yetu ikona ma kipande wa wili; ni uzima ya mwili na uzima ya roho. KIntu ingine ni kama uzima yetu ni katika sheria ya Mungu na kintu ingine ni kama uzima yetu ni katika ma sheria ya dunia na zambi. Hivi na nafsi ya kila mtu, kama huyu anaishi katika sheria ya Mungu nafsi yake ni ya milele ndani ya furaha na shangilio ya paradizo, lakini kama aliishi, mu uzima yake katika zambi, nafsi yake ataishi ndani ya lufu yake kwa milele, nikusema ataishi bila Mungu na furaha, lakini kwa milele.

## 41. Mazungumuzo ya mt. askofu Grigorio kama ukumbusho ya watu mu Matayarisho Takatifu (Proskomidi), mbele ya Liturgia Takatifu inasaidia watu ya kweli.

Mwanafunzi yake Petro: Namna gani iko namna kupata faida moja ya roho ma nafsi ya wale watu waliisha kufa?

Askofu Grigorio Kama sisi tunakufa, bila kufanya maungamo ya zambi yetu, iko namna kusaidia na fsi yetu, kisha lufu ya mwili yetu makumbusho mu Proskomidi na mu Ibada ya Liturgia Takatifu. Joo vile ma nafsi wengi walikuja na waliomba sala mu Proskomidi. Vile iko lazima kufanya na juu ya wenye muzima.

Nilisikia ya kama nyakati fulani walibamba maskari moja wa adui na walimutupa mu buloko. Bibi yake ku mulango alifanya makumbusho yake mu Proskomidi na mi Liturgia Takatifu. Bile ma siku alimukumbuka bibi yake, bwana yake alifuguliwa toka monyororo yake ndani ya kifungo.

Tena mtu mwingine aliyetumika mu chombo moja, alinitangaza hii mambo ya ajabu yake. Alisafiri siku moja mu Roma pamoja na askofu ya muji Panormo, aliyeitwa Agathon. Na huyu alikuwa ndani ya mutumbwi, iliyekokota chombo munene. Lakini mara moja ilijikata kamba iliyemukokota na huyu kijana pamoja na mutumbwi walipoteshwa ndani ya tufani ya bahari.

Askofu, basi, aliendelea safari yake ndani ya chombo munene na alifika mu kisanga ya Ustiva. Walimbakia kule ma siku na usiku tatu na haikuonekana mutumbwi pamoja na huyu

mutumishi ya chombo; alihamuru askofu kufanya Liturgia na makumbusho yake, sawa vile tunafanya kwa wafu.

Basi, kisha ya wakati fulani, huyu askofu alisafiri mu Italia na mu kikavu ya muji moja alikutana huyu kijana mutumishi aliyeisha kupotea. Askofu alifurahi sana na alimuuliza namna gani aliweza kuokolewa toka hii hatari hata mnene.

Na huyu alimuwaambia ya kama alikombana ndani ya maji ya bahari ma siku mengi. Kisha aliingia maji ndani ya mutumbwi yake na kisha alijipindula mutumbwi ndani ya bahari. Basi, kisha alichoka sana na alipotesha kila kitumaini yake kwa ajili ya njaa, muchoko na baridi; tena alimukuja kizingu-zingu. Wakati alikuwa mu hii hali yake, alikuja moja katikati ya bahari, aliyemukaribia; Alimupatia kipande moja ya mukate juu ya kula. Aliikamata huyu askari na aliikula na alikamata nguvu. Haikupite saa mingi na alipita toka fasi yake chombo ingine; walimuona na walimukokota mu kikavu. Vile aliokolewa toka hatari.

Askofu alitafuta, basi, ile siku alionekana huyu mtu mugeni ndani ya bahari na alimupatia mukate na alipata ya kama ilikuwa ile siku umoja, walifanya makubusho yake mu Liturgia Takatifu, mu kisanga Ustiva.

Mwanafunzi yake Petro: Hii tangazo ulinionyesha weye nilisikia na mimi, wakati nilipita mu Kisanga Sikelia.

Askofu Grigorio: Ni kweli, mtoto yangu ya kama hii sala inajifanya mu Proskomidi inasaidia na wenye muzima na wenye kufa. Lakini kama wafu walifanya ma zambi mnene, hakuna namna kusamehewa katika hii sala ya Proskomidi. Nitakukumbuka sasa na historia ya huyu mtu aliyeitwa Yustos juu ya kujua weye faida ngapi wanabeba hawa watu wanaomba mu Proskomidi juu ya wandugu wao.

Huyu mutawa, sawa vile na weye unajua aliishi pamoja na mimi mu Monasteri yetu, mbele ya kufanyika mimi askofu. Na, bila baraka yangu *(yeye alikuwa mpadri mukubwa)* alikamata mu nyumba yake makuta ya tatu. Hii tendo yake ilionekana, wakati alikufa. Kwa hivi walichelewa kumumazika, lakini yeye alitaguria kutubu mbele ya kufa. Wa ndugu wake na baraka yangu walimutupa ndani ya maivi pamoja na ma feza wa tatu yake. Wa ndugu wote walimufiga katika amri yangu.

Lakini, , kisha mwezi, moja kwa ajli ya wema alihamuru kufanya Liturgia kila siku na kukumbuka jina yake juu ya kuokolewa. Wakati iliisha wakati ya ma siku makumi tatu alikuja huyu mwenye kufa kwa ndoto ya ndugu yake katika mwili aliyeitwa Kopiosos.

Huyu ndugu yake alimuuliza: «namna gani unapita?

-Mupaka sasa nilipita mubaya na katika baridi; lakini tangu leo niko mu makao ya furaha na ninaishi muzuri.

Alikuja ndugu yake Kopiosos na alitwaambia jibu yake. Tulibalula ma siku na tuliona ya kama yule ndugu Yustos alisikia kupita nzuri kisha ma Liturgia makumi tatu, tuliyefanya juu ya pumziko ya nafsi yake. Na hii tendo inatuonyesha, bila shaka, yaka huyu ndugu zetu mufu aliokolewa toka mateso yake, kwa ajili ya ma Liturgia Takatifu tuliofanya kwa wokovu yake.

Mwanafunzi yake Petro: Kweli bile ma sauti ninasikia ni wa ajabu na wananipatia furaha mnene.

Askofu Grigorio: Ma sauti ya wafu wanasaidia kwa sindano yao hawa wenye muzima juu ya tusianguke mu uzima ya zambi na kupotesha kitumaini yetu ya wokovu.

Na mtakatifu na askofu Yoane Murahimu alishauria waminifu yake kufanya mara mengi ma Ibada ya Liturgia takatifu na makumbusho juu ya wenye kufa, kwa sababu hii ukumbusho inapumzika na inaleta faida kwa nafsi yao. Juu ya kuwafundisha kuliko nzuri aliwaambia hii historia:

Wakati moja, aliwaambia, mwaminifu moja walimubamba watu ya Persia na walimupeleka mu inchi yao. Basi, walimutupa ya kufungwa ndani ya buloko, iliyeitwa Lithi na walimuchunga

na wa zamu. Hii buloko iliitwa hivi kwa sababu kila mtu aliyeingia ndai hakuna namna kutosha inje muzima.

Lakini wafugwa wengine walikombana na walitoka inje na walifika mu Kisanga Kipros. Hawa walitangaza ya kama yule mutumwa mwaminifu alikufa ndani ya buloko. Wakati walisikia hii jabo wa ndugu wakewalimuria sana na mara tatu kila mwaka walifanya Liturgia Takatifu na makumbusho. Na hii sala walifanya ma miaka ya ine. Siku moja alikombvana na alikimbia na huyu mutumwa na alifika mu nyumba yake. Wazazi wake walimuona hapana kama mutumwa, lakini kama mwenye ufufuo. Walimuangalia na ajabu na walifurahi sana na walimubusu na ma sauti butamu.

Basi, walimuwambia ya kama walimufanysia makumbusho kwa Siku Kuu ya Epifanie ya kristu, kwa Ufufuo yake kwa kila Pentekoste. Na huyu, wakati alisikia hii sauti yao, alikumbuka na aliwaambia ya kama bile ma siku alikujaka kijana moja na mavazi ya mwangaza na alimufugula toka monyororo yake. Na, wakati hii ma siku walipita huyu alikuwa mara ingine ndani ya monyororo yake.

## 42. Namna gani aliona Mutawa Averkios Bwana Yesu Kristu

Mutawa muzee Averkios alikuwa mutawa moja mupole, bila roho ugumu na haikukuwe uwovu ndani ya roho yake. Alizaliwa mu kisanga Naksos ya Grekia mu Ianuarie ya mwaka 1852. Jina yake wakati alibatizwa ilikuwa Konstatinos na alifanyika mutawa mu Skiti (Mukini) Mupya ya Kilima Takatifu ku mwaka 1898. Huyu aliishi na usikini mingi. Alimbakia ndani ya pango moja mu jangwa na mu kinywa yake aliweka mayani ya miti. . . Alifanya ma kituga na simbala na aliwapatia kwa watawa wengine na hivi alipata chakula yake. Alifanya ma kituga mengi na aliipatia kwa Monasteri na wa ndugu ya ma Monasteri walimupatia mukate ya kukauka na hivi alipita maisha yake, nikusema na mingi mateso, uvumilia na usikini. Wakati ingine walimupatia makuta juu ya ma kituga yake, lakini yeye aliikaburia kwa maskini na hasikuuze hata kintu moja na hii ma feza.

Kwa kila Siku Kuu na mu Juma alikwenda mu Kanisa ya Skiti Mupya na aliikaa mu fasi moja mukongo ya watawa wengine. Wakati alikuwa ndani ya Ibada moja ya usiku na walikuwa na Siku Kuu ukubwa watawa wengine walimuona huyu Averkios kutoka ya fasi yake, pahali aliikaa mukongo na aliingia ndani ya katikati ya Kanisa, bila sababu. Alikaribia Altari Takatifu na aliingia ndani na alienda karibu ya Meza Takatifu. Ile saa watawa wengine walimuona kupika magoti na kusujudu kwa fulani, bila kuona kwa mtu nani na averkios alimujibu na furaha: «Ndivyo, ee Rabi, ninaona. Mutawa Aberkios. Aksanti, aksanti». Kisha alimusujudu mara ingine, alitoka inje ya Meza takatifu na aliikaa mu fasi yake. Ninyi wote walimuona kuingia ndani, walizania ya kama alikwenda kusema sauti moja kwa mpadri ya kanisa, lakini huyu mpadri aliyekuwa karibu ya Averkios alizania ya kama padri Averkios ni mazimu ao mupole kabisa. Ile saa mpadri ya Ibada hasikumwambia hata sauti moja, lakini siku ingine, alimukutana na alimuuliza:

Ee Muzee Averkios, mambo ninyi ulipata jana na ulisuburia na mtu gani ndani ya Altari Takatifu?

Muzee Aberkios alishangaa na alimujibu: Ee weye padri-Yoane usikumuone Rabi wetu Yesu Kristu, aliyesimama mbeleya Mulango ukubwa na aliniita kwenda karibu yake? Aliniuliza jina yangu. Mini nilimuwambia na Huyu aliiandika mu karatasi moja ile tukona yo mu fasi moja na alinionyesha na mimi nilisoma jina yangu ndani ya hii karatasi.

Wakati walisikia hii jabo, watawa wengine walifuraha sana nawalikwenda kumuuliza juu ya hii maono. Mutawa Averkios, kwani alikuwa mtu mupole na bila roho ugumu, alizania ya kama waliona hii ono watawa wote na joo vile alishangaa juu ya ninyi walimuuliza. Hii karatasi iliyeona Averkios ya kama iliandikwa jina yake, haikukuwe karatasi, lakini Kitabu ya Uzima ya

milele, pahali Rabi mupenda-wanadamu alimuandika kama mwenye safi kwa roho yake, ambaye anastahiliwa kuiona Mungu, katika Heri ya Bwana Yesu Kristu: «Heri wenye moyo safi, masana wao wataona Mungu» (Matayo 5, 8).

Wakati ingine alisema kwa watawa wengine, wenye walimukaribia kusikia sauti moja yake ya kama aliona Neema Takatifu kufunika Skiti yao kama mawingu moja wa nuru na ilizambalishwa yulu ya wa padri, wenye walikuwa ndani na waliomba kwa Mungu. Tena mpadri Averkios aliwaambia ya kama alijua, ile wakati wapadri wote walikwenda kupumunika, nani alikuwa mustahili na nani hasikukuwe stahili kupewa Komonyo Takatifu.

Huyu mtakatifu Mutawa Averkios alikufa ku mwaka 1934.

Mwanafunzi ya roho yake aliyeitwa Yoakimu, wakati alikufa mpadri Averkios, huyu alilofa mu muji Athina. Alirudia ku mulango na alitaabu mingi, kwani hasikukuwe kule. Lakini alifanya kila siku ya wakati ma siku makumi ine Liturgia na alikumbuka Mtawa Averkios. Kisha ma siku makumi ine aliona padri Yoakimu maono moja ya ajabu. Alimuona mtawa Averkios kuikaa mu paradizo ndaninya moja nyumba iliyejaza na nuru na pempeni yake ilikuwa kama shamba na matunda mengi pa miti.

Mpadri Yoakimu alimuuliza: Hii bintu ninaona ni ninyi na namna gani uko huku?

-Mtawa Averkios alimujibu: Niko kwangu na walinipatia Baba wa mbingu kwa ajili ya wema na upenda-wanadamu mingi yake.

## 43. Malaika ya Mungu alisaidia maungamo ya mutawa moja

Kwa hii Skiti Mupya ya Kilima Takatifu aliishi mutawa moja aliyeitwa Kirilo, aliyekuja ku mwisho ya uzima yake ku mwaka 1965. Aliita mpadri ya roho yake Gabrieli juu ya kumuungama. Alikombana mpadri ya roho Gabrieli kumuungama, lakini mtawa Kirilo alimuwambia ya kama mu mbavu ya kushoto yake iliisha kulamata karatasi moja, lakini aliandika ninyi hakuna namna kuijua.

Alikwenda na mpadri ya roho mwingine na jina Haralambos, lakini na huyu hasikuweze kuungama mt. Kirilo. Kisha alimukaribia mpadri ya roho Neofitos pamoja na mpadri ya roho Gabrieli na walimuuliza:

-Mpadri Kirilo, unaona ninyi yulu ya mbavu yako?

Mugonjwa na muzee Kirilo alisema ya kama mu fasi ya kuume anaona wakijana wa wili na mavazi meupe, wenye waliokuwa wa Malaika na mu fasi ya kushoto walikuwa tayari kumunguruma ma shetani wengi; tena shetani moja aliisha kubeba komboshini ya mutawa Yosefu, aliyekuwa na huyu kule, na alicheza na mukila yake.

Mpadri ya roho Gabrieli alisema kwa Watawa wote kutoka inje ya chumba yake na aliuliza mtawa Kirilo kumuungama matendo yake yote ya uzima yake.

Wakati mugonjwa Kirilo alisema yoyote matendo yake, ile saa mpadri Gabrieli alimuuliza kama anaona tena hii karatasi pa mbavu yake. Mugonjwa alijibu ya kama ilikuwa tena hii karatasi yulu yake.

Mpadri ya roho kisha alisema kwa Kirilo kuuliza Malaika yake aliyekuwa kule karibu, kumwambia aliandika ninyi hii karatasi. Mutawa Kirilo alipindula kwa wa malaika wa wili na aliwaambia na ma sauti ili hasikusikie mpadri Gabrieli wala neno moja. Na Malaika alimujibu kwa hii lugha ingine. Ile saa mpadri Gabrieli aliweka Epitrahilion yake pa kichwa ya huyu mtawa Kirilo na alimuuliza alimwambia ninyi Malaika yake na hii karatasi aliandika ninyi? Na mutawa Kirilo alimwambia zambi wa wili, ili aliisha kusahabu yeye.

Mpadri ya roho, wakati alisikia na hii zambi ingine, alisoma sala ya usamehe. Kisha mutawa Kirilo alisema ya kama hii karatasi na hii zambi ililamata pa epitrahilion yake na hivi alitoa nafsi yake kwa mikono ya Mungu na alilala musingizi ya milele.

## 44. Historia toka uzima ya Mtakatifu Uaros

Mwanamuke moja aliyekuwa mutajiri na mweshimiwa mbele ya Mungu, aliitwa Kleopatra. Wakati Mushahindi Uaros alikufa kwa mateso mengi, huyu mwanamuke alikamata mwili yake na aliipeleka mu njimbo Palestini. Na, wakati ilisimamisha ufukuzo ya Kristu na Ndini Yake, huyu mwanamuke alijenga kanisa munene kwa jina ya yule mushahindi.

Huyu, basi, alikuwa na na mtoto moja wa pekee na pa huyu mtoto alitegemea kila kitumaini yake, kwa sababu bwana yake aliisha kufa ya zamani. Tena alituma makuta mengi kwa wakubwa ya inchi na aliwaambia kupatia ma cheo makubwa kwa mtoto yake ndani ya matembesho ya inchi yao.

Hii kanisa iliyeanza kuijenga aliisha na kisha aliita huyu mwanamuke wakubwa ya inchi na wa askofu ya Kanisa juu ya kufanya sala ya mwanzo. Walikuja na Watawa ya jangwa na waminifu ya ma fasi pempeni juu ya kutosha Mifupa ya Mtakatifu Uaros na kuweka ndani ya Kanisa yake mupya. Walifanya kila matayarisho na ma sala ya ile usiku yote. Huyu mwanamuke alichunga mwili ya Mt. Uaros pamoja na mwana wake na walimupeleka mu kanisa mupya na waliomba kwa Mutakatifu juu ya kuchunga na kulinzi mtoto yake.

Wakati iliisha Ibada ya Liturgia Takatifu, huyu mama Kleopatra alitayarisha chakula juu ya watu wote na ma chakula mazuri sana. Pamoja alimusaidia na mtoto yake, mwenye kwa ajili ya muchoko alipanda kivukutu ku mwili yake na magaribi ya ile siku alilaria pa kitanda mugonjwa. Karibu yake alimutulivu mama yake na alipugusha jashu yake. Lakini katikati ya ile usiku mtoto yake alipindula kichwa yake na alikufa mbele ya ma macho ya mama yake.

Wakati aliona hii jabo ya matata kabisa mama yake, alianguka chini na kizingu-zingu na bila kusema hata sauti moja. Kisha saa kidogo alirudia kwa mahasa yake na alilamuka mtoto yake pa mbavu yake alimupeleka ndani ya hii Kanisa mupya. Aliweka maiti yake ndani ya Altari takatifu. Alisimama mbele ya mwili ya mt. Uaros na, sawa huyu alikuwa muzima, alianza kumusema hivi:

Kazi ninyi kibaya nilifanya, ee Mushahindi ya Mungu na nilianguka kwa hii mateso ugumu? Misikuacha bwana yangu mu fasi ugeni na nilikuja kupeleka mwili yako hapa? Misikujenga hii kanisa mupya kwa ajili ya mapendo yako? Misikupatie uzima na nafsi yangu juu ya kusifu weye? Na niliomba ninyi juu ya hii matendo yangu? Niliongojea ninyi kisha hii matendo yangu? Nilipenda paka afya na wokovu ya mtoto yangu. Kintu ingine ninyi ilikuwa namna kupenda kuliko, paka mtoto yangu juu ya kunisaidia ku miaka uzee yangu? Lakini, ole kwangu mwenye mateso na sikitiko. Misikufurahi hata, kisha hii machoko yangu, kupindua nilijaza na uchungu, ewe Mushahindi ya Kristu!

Unipe, basi mtoto yangu mukongo ao uniue na mimi juu ya kuwa pamoja na mtoto yangu mimi mwenye mateso.

Vile aliria na maombolezo mingi na ma saa mingi. Kwa ajili ya muchioko na sikitiko alilala. Kwa ndoto yake aliona ya kama alionekana mbele yake mtoto yake na mavazi ya utukufu mingi na pempeni yake aliikaa mtakatifu Uaros. Alivaa na taji ya utukufu sawa hii taji alivaa na Mushahindi ya Kristu. Mushahindi alipindua na alimwambia:

-Juu ya ninyi, ewe mama muzuri, ukona sikitiko na unaikaa na unaria na unapika mwili yako na taabu inakula nguvu yako? Basi, hauone matukufu na masifu ngapi alipata mtoto yano? Hauone namna gani neema ya Mungu inaangazwa pempeni yake? Juu ya ninyi, basi, usipende kutosha hii taabu toka uso yako na usifurahi kama mama muzuri kwani unaona mtoto yako na utukufu kabaila? Basi, atakuja mtoto yako sasa karibu yako juu ya kumuona na macho yako na utamuona na utasikia ya kama aipaswe kufanya hivi na kuikaa kuria. Na alipindula kwa mtoto na alimwambia:

-Kuja tena karibu ya mama yako juu ya kuona muzuri furaha na utukufu ngapi ukonayo na hivi atatulivu, kwani anaria na ekona sikitiko mingi kwa roho yake.

Mtoto, hapana hasikumukaribia paka, lakini alikaribia Mtakatifu Uaros, alimubatia na alimuomba hapana kumwacha kukaribia mama yake, wala kwenda karibu yake. paka alipindula kwa mama yake na alimwambia:

-Uende muzuri, mama yangu. . . Uende kwa baraka ya Mungu. . . Uikaa mu nyumba yako na kimya. . . na simama kuria na kupiga mwili yako na kutosha ma nywele yako. . . kwa sababu, sawa vile unaona na macho yako, itakuwa bunya kugeuza hii uzima ya milele na furaha bila mwisho na kurudia mu uzima yenu ya mateso na zambi mingi.

Hii ma sauti alimuwambia mtoto yake. Mama yake, wakati alisikia hii ma sauti, aliomba kwa Mushahindi juu ya kubeba na huyu karibu yao juu ya kufurahi na huyu hii furaha ya milele. Na huyu Mtakatifu alimushauria kufata njia ya Mungu na pasopo mingi na hii njia itamuletea kwa wokovu ya nafsi yake. Wakati alimutulivu mt. Uaros na alimushauria muzuri, alitoka pamoja na mtoto yake.

Na huyu alilamuka mara moja na alishukuru  na kivukutu mingi Mungu na Mtakatifu yake, kwani walimustahili kuona hii ono. Kisha alibeba mwili ya mtoto yake na alimuweka karibu ya mwili ya Mtakatifu na alifanya sala  ya shukrani  ile usiku yote pamoja na wale waliokuwa kule ndani ya kanisa. Na asubui alifanya Liturgia takatifu na ma siku ingine aliendelea hivi.  Kisha ya kila Liturgia huyu mama Kleopatra aliwapatia na chakula. Tena aliwakaburia ma bintu yake yote na kabisa kwa wamaskini na huyu alivaa paka nguo moja na kila siku na usiku alikuwa karibu ya kanisa na alisafisha na alifanya kila kazi ya kanisa. Na hata nzuri alisafisha kwa saidio ya kifungo ya chakula na ma sala yake, na mtakatifu Uaros alikuja kwa kila Siku Kuu pamoja na mtoto yake na walimutulivu sana. Vile aliishi huyu mama Kleopatra tena miaka saba na kisha alifariki mwili yake, lakini na nafsi yake alipanda mbinguni pamoja na Watakatifu na mtoto mupendwa yake.

## 45. Faida toka ma Ibada ya Liturgia Takatifu na makumbusho ni ukubwa

Mwaminifu moja toka muji Smirni, aliyeitwa Dimitrios, wakati alisikia mwisho ya uzima yake, aliita mwana wake aliyeitwa Georgio, na alimuwambia ma jabo ma nani watafata. Alisuburia paka na huyu mtoto, kwa sababu paka huyu alipenda Mungu na alikuwa mweshimiwa mbele ya Mungu, lakini watoto wengine yake wa tatu na bibi yake waliishi uzima kibaya katika akili ya hii dunia. Huyu mtoto yake Georgios alitangaza kwa Mutawa Danieli, Mkubwa mpadri ya Kilima Takatifu toka nyumba wa Daniilei.

«Wakati baba yangu alifika ku mwisho ya uzima yake na  alifamia na ile siku ya mwisho yake, ile siku ya mwisho aliita mpadri moja mweshimiwa, aliyeitwa Dimitrios, mtu mufazili na mupole na alimwambia:

Mimi, mpadri ya roho yangu, leo ninakufa na ninakuomba kunisaidia kwa hii saa ya uhukumu, inapaswa kufanya ninyi? Mpadri, kwa sababu alijua uzima ya baba yangu, iliyekuwa katika boka ya Mungu na alikuwa tayari ya kuondoka, kwa sababu aliisha kufanya maungamo, Fumbo ya Mafuta Takatifu na Komonyo Takatifu mara mengi, alimwambia tena kufanya na hii tendo: «Kama iko namna kuhamuru watoto yako, alimwambia mpadri Dimitrios kwa baba yangu, kisha lufu yako kufanya mpadri moja ma Liturgia  Matakatifu makumi ine na kukumbuka jina yake.

Baba yangu alisikia sauti yake na alifurahi; aliniita na machozi na aliniomba kufanya mimi hii kazi na saidio ya mpadri moja.

Kisha ma saa wa wili, alikufa baba yangu na mara moja mimi niliita mpadri Dimitrios, bila kujua ya kama huyu mumoja aliisha kusema kwa baba yangu juu ya kufanya sisi Liturgia ya ma siku makumi ine. Mimi nilisema hivi kwa mpadri Dimitrios: Kwa sababu baba yangu alinipatia amri, kisha lufu yake, kufanya sisi Liturgia makumi ine, inje ya muji yetu, na kwa sababu weye unaishi inje ya muji yetu, ninakumba kufanya hii muchoko na kumaliza hii amri ya baba yangu na

mimi nitaripa juu ya hii muchoko yako na kila kintu ingine ya Kanisa mitairipa, Mpadri, wakati alisikia ma neno yangu, alinijibu na machozi pa macho yake. Mimi, Georgie mupendwa wangu, nilimwambia kwa baba yako juu ya kufanya Liturgia makumi ine na, ninapaswa mpaka mwisho ya uzima yangu kumukumbuka.

Mimi, kwa sababu nilijua heshima na boka ya Mungu ya huyu mpadri Dimitrios na ile sifa iliyekuwa na kwa baba yangu, nilimwambia nguvu kupokelea hii sauti na matakio yangu. Hivi alipokelea na alikwenda mu nyumba yake. Alisuburia pamopja na bibi na watoto yake wanawake na aliwaambia: Mimi, kwa sababu nitafanya ma Liturgia makumi ine moja kila siku juu ya pumziko ya huyu murafiki yangu bwana Dimitrios, nitambakia inje ya nyumba yetu, karibu ya kanisa ya Wa Mitume kumi na mbili na kule kila asubui nitafanya hii ma Liturgia ya ma siku makumi ine. .

Kweli huyu alifika mupaka liturgia ya makumi tatu na tisa na ilikuwa tena lazima ile siku mu Posho kufanya na ingine Liturgia ya mwisho, lakini ile usiku ilianza kuuma meno yake na alimbakia mpadri ile usiku mu nyumba yake. Bibi yake aliita mtu moja aliyetosha rino moja yake, kwani iliisha kuoza na hivi aliokolewa toka maumivu. Lakini, kwa sababu ilitosha na damu, alikamata naziri kumaliza ile Liturgia ya mwisho siku ingine asubui.

Lakini Georgios, kwa sababu hasikujue mambo ya umivu ya yule mpadri, ile usiku ya mwisho alitayarisha malipo ya huyu mpadri juu ya muchoko yake na alitaka kumupatia ile siku ya keshi, kisha mwisho ya ma Liturgia yote. Katikati ya usiku ya mu Posho, lakini, nililamuka kuomba kwa Mungu. Niliomba, lakini nilichoka; niliikaa pa kitanda na niliaanza kukumbuka ma fazila ya baba yangu na makosa yangu tangu kipimo ya udogo yangu. Tena niliwaza na akili yangu: «iko namna hii ma Liturgia makumi ine kusaidia nafsi moha ya mukristu aliyekufa ao Kanisa yetu anatwambia hivi kufanya juu ya kupata pumziko kidogo huu nafsi ya yule mukristu aliyekufa? Hivi niliwaza na huzuni ya roho na machozi na niliomba rehema ya Mungu. Kisha nilizania ya kama nililala na mara moja niliingia ndani ya kiwanja moja muziri kabisa bila misali na makiwanja ya hii dunia. Wakati nilikuwa kule, nilikisikia sikitiko iliye\ku ja toka mioyo yangu, kwani nilikuwa mwenye uchafu na misikukuwe mustahili kuingie kule. . Na ile wakati nilikuwa na hii huzuni ya roho, nilipata nguvu kwa mioyo yangu na nilisema, kwani Mungu alitaka kuniletea hapa, mara ingine upenda-wanadamu Yake alipenda kunirehema juu ya kutubu.

Vile nilisuburia na maungo yangu na kisha mara moja niliona nuru moja. Niliikaribia na niliona na ajabu ile pori pahali ilitoka arufu nzuri na utukufu na nuru mingi. Nilisema, o ngapi furaha na heri inaongojea wale watu wanaishi katika ma fazila ya Kristu mu dunia!

Kisha nilitembea kidogo na niliona nyumba moja kama nyumba ya mfalme muzuri sana. Nilikaribia na niliona ndani yake baba yangu Dimitrios, aliyevaa nguo na mwangaza na kujaza na moto. Aliniangalia na mapendo na wema mingi na upole na alinisema:

-Namna gani ulikuja hapa mtoto yangu?

-Mimi nilimujibu: Baba yangu, ninashangaa na mimi namna gani nilikuja hapa, kwani ninajua ya kama misina na mustahili. Lakini uniambie baba yangu: Namna gani uko huku na hii nyumba ya mwangaza iko ya mtu gani?

-Huyu na shagnilio mingi alinijibu: Wema ya Mwokozi wetu katika maombezi ya Mama wetu Mzazi-Mungu Bikira Maria, kwa mwenye nilikuwa, sawa vile unajua, heshima na utawa mingi, alinistahili kuingia leo ndani ya hii nyumba, lakini, kwa sababu muyengaji alitosha leo rino yake na bado kuisha ma siku makumi ine ya kuyenga hii nyumba; kwa hii mambo nitaingia kesho.

Wakati niliona na nilisikia mimi mwenye zambi hii ma sauti ya baba yangu, nilishangaa na nilijaza na machozi ma macjo yangu. Ile usiku yote nilimbakia bila kulala na nilishukuru na nilitukuza Mungu Mwema kamili. . . Siku ingine nilienda kwa mpadri Dimitrios na nilimupata kuikaa. Alinipokelea na furaha na alinisema:

-Tazama na mimi hapa sasa niliisha hii Liturgia ya mwisho na utukufu kwa Mungu niliisha ma Ibada ya ma Liturgia makumi ine.

Hii sauti yeye aliniambia kwani hasikutake kunisikitika, kwa sababi ilichelewa Liturgia moja siku moja. Ile saa mimi nilianza kutangaza kwa mpadri Dimitrios bile ma jabo ya ajabu niliona na, wakati nilifika mu historia juu ya kutosha rino yake na ya kama siku ingine itaisha ya kuyenga ile nyumba ya baba yangu na ya kama baba yangu ataingia ndani kesho, mpadri alijaza na ajabu na alipaza sauti na alinisema:

-Ndugu yangu mupendwa Georgie, mimi ni muyengaji ya ile nyumba. . .

Hii maono yote alisema mutawa mukubwa Danieli, mwenye alitembelea yule mpadri Dimitrios na alisikia toka masikio yake hii historia ya ajabu. Hii historia ilifanyika ku mwanzo 1920.

## 46. Ono na faida ya roho mingi ya Petro Mostratos

Mu Grekia aliishi mpadri moja ya roho mkubwa aliyeitwa Filotheos Zervakos. Huyu na baraka ya askofu yake alizunguluka ma fasi mengi ya kuachana na alihubiri na aliungama waminifu ya Kristu. Hii historia aliandika huyu mpadri Filotheos. Ni hii:

Ku mwaka 1917-1918 nilikwenda mu mukini Parikia na kule mwaminifu moja aliyeitwa Petro Mostratos aliniita mu nyumba yake. Alifanya maungamo huyu na bibi yake. Kisha bwana yake aliniambia hii historia:

«Mimi, mweshimiwa mpadri wangu, nilikuwa watoto wa wili, mwanaume na mwanamuke moja. Pamoja na bibi yangu tulikombana kufata watoto wetu mafundisho nzuri. wakati waliisha masomo ya mbili, tulikamata naziri kuwatuma mu kapitala Athina mu Masomo ya yulu kabisa. Binti yetu, aliyekuwa muloko ya miaka wa wili toka mwana wetu, alikuwa na akili mingi kupita ya mkubwa yake mu masomo. Tena alionyesha kuliko utawa, mapendo, imani kwa Mungu na ma fazila wengine. Wakati nilimwambia kwenda mu Masomo juu pia pamoja na ndugu yake mu kapitala Athina ya Grekia, huyu aliniambia:

-Baba wangu, mimi nilikufanya kwa mambo yote utii, lakini kwa hii matakio yako misitakufanye utii. Hii ma fundisho nilisikia ku masomo ya mbili inenea kwa mimi.

-Mimi nilimujibu: Ninataka, binti yangu, kutuma na weye mu Masomo ya yuluu pia juu ya kuwa mtu ya hekima mukubwa.

-Huyu alinijibu: Na mimi, baba wangu, ninazania ya kama fundisho kuliko ukubwa juu ya binti moja ni paka ya kuchunga ma fazila ya Mungu, kwani hivi Huyu anasema: «Heshimu baba yako na mama yako, siku zako zipate kuwa nyingi katika inchi Bwana Mungu wako anayokupa wewe». (Kutoka 20, 12). Nikusema sifa kwa binti moja ni kupenda wazazi wake, kuwasaidia kwa kipimo ya uzee yao, kama hawakuwa na mtoto mwingine sawa mweye, muliyechoka mingi kwa ajili yangu na, wakati nilikuwa ndani ya tumbo ya mama yangu, na, wakati nilikuwa mtoto mudogo na ksiha bintu mudogo na mpaka sasa. Hakuna namna kumiacha, kabisa ile wakati, pahali muko mweye wazee.

Mimi, alisema, baba yake, kwani niliona mapenzi nguvu yake, nilimwacha. Kila siku tuliona mapendo yake na utii na masubuko na zabihu yake ya kusaidia sisi na pamoja na bibi yangu tulifurahi sana na tulizania ya kama tulikuwa wenye heri, kwa sababu tulikuwa na binti moha mujaliwa neema ya Mungu na tulisahabu ya kama furaha na heri haina daima hapa mu uzima hii ya nyakati kidogo, lakini ni mu uzima ya milele.

Haikupitisha wakati mingi na aligonjwa binti yetu. Waganga walikamata naziri na walituwambia ya kama binti mupendwa wetu atakufa. Mara moja furaha yetu iligeuza na ilijaza roho yetu na taabu. Kwani nilipotea kila kitumaini ya waganga, nikimbilia kwa Mzazi-Mungu na Mtakatifu kamili Bikira Maria. Niliingia ndani ya kanisa yake, nilimuomba na machozi mingi kuokoa binti yangu toka lufu, ao kubeba mwana wangu na kuniacha binti yangu aliyekuwa

muzuri kuliko ya mwana wangu. . Mzazi-Mungu Maria hasikunitii na binti yangu alikufa. Wakati alikufa mimi na bibi yangu tulikuwa, bila hata utulivu kimoja. Kila siku tusikufanye kazi ingine, paka tuliria na tulilalamika sana.

Ya wakati ma siku kumi na tano nilimbakia pamoja na bibi yangu ndani ya nyumba yetu na tunaria sana. Kisha hii ma siku kumi na tano, nilienda mu kanisa juu ya kuwakisha kandila ya Mzazi-Mungu. Niliwakisha kandila na kisha, kwa sababu nilikumbuka ya kama niliomba ya Mzazi-Mungu kuokoa binti yangu, lakini huyu hasikunitii, mara moja nilizimisha kandila yake na nilimwabia na kisilani: «Mzazi-Mungu kwa sababu usikunitii juu ya kuokoa binti yangu; sasa na mimi nitazimisha kandila yako; Hivi nilifanya na nilirudia ku mulango yangu.

Wakati nililaria pa kitanda yangu, walikuja wa kijana wa wili na ma uso yao walikuwa na mwangaza mingi. Walinibeba, walinitosha ya nyumba yangu na tulitembea pamoja ndani ya kiwanja moja.

Kwani niliogopa, niliwauliza: Munanipeleka wapi?

Hawa wa malaika na uso kwa kisilani mingi walinijibu: Ee, usiwe asiyeamini. Juu ya ninyi usisadiki? Kuja na utasadiki. Tulitembea tena na tulifika ndani ya shamba moja muzuri sana, ambaye alifanana na paradizo. Katikati ya paradizo ilikuwa nyumba moja ukubwa sana na iliisha kuyengwa na zahabu yote ma fasi yake. Hawa wa malaika walinionyesha mulango moja na walinisema:

Ingia ndani toka hii mulango mu hii nyumba, na kule utaona binti yako.

Niliingia toka hii mulango na niliona chumba moja urefu sana. Ndani ya hii chumba walikuwa ma bikira ma binti ma elfu mingi, wenye waliikaaa pa ma kiti ya zahabu na ma fasi yao kuume na kushoto walikuwa ma taa ya kuwakisha. ma uso ya wa bikira waliangazwa kuliko ya jua na utukufu ya hii chumba na ma Kiti ya wa bikira binti hakuna namna ya kuisema. Nilianza kuangalia ma bikira ma binti na katikati yao niliona na binti yangu, aliyeikaa pa kiti ya nuru mingi, lakini ma taa yake waliisha kuzimisha. Wakati nilimuona, nilimufamia na nilikimbia mbiio karibu yake juu ya kumubatia na kumubusu. Lakini wakati nilikaribia na yeye aliniona, alisimama pa kiti yake na richo ukali aliniambia:

-Toka ya hapa; Namna gani ulipata nguvu na ulikuja hapa kuniuzi?

Alinitosha toka fasi yake na kisha yeye aliikaa pa kiti yake. Mimi nilianza kusikitika na kumwambia:

-Binti wangu, juu ya ninyi usinipokee: Usijue ngapi nilikupenda? Mimi niliomba kwa Mzazi-Mungu kukufa ndugu mkubwa yako juu ya kuishi weye juu ya kuwa karibu yangu daima na sasa weye unanifukuza?

-Simama, ananijibu, kusema hii ma sauti ya kama unanipenda, kwa sababu kama ulinipenda ilipaswa sasa kufurahi kwa hiiutukufu yangu, na sifa na heri yangu na hapana kusikitika. Ilipaswa kushukuru Mungu na Mzazi-Mungu Bikira Maria, wenye walinistahili hii heri na utukufu na hapana kutaabu.

Ile saa mimi nilimwambia: Binti wangu, juu ya ninyi ma taa ya wa binti wengine ni ya kuwakisha, lakini ma taa yako ni ya kuzimisha?

Huyu alinijibu: Weye na mama yangu mulizimisha hii ma taa yangu na, kama musitasimama kuria, musiseme ya kama mukona binti yenu.

Hii saa nilirudia kwa maungo yangu na nililamuka. Niliwaza makubwa matukufu ya Mungu, pahali niliona utukufu ya wa bikira na binti yangu na ya saa mingi nilikuwa na ajabu. Wakati nilisikia kidogo nzuri, niliita bibi yangu na nilimwambia ninyi wote niliona na yeye alipata utulivu mingi. Asubui nilikimbia mu Kanisa, nilianguka chini, mbele ya (ikona) picha ya Mzazi-Mungu na machozi mingi ya kutubu na furaha niliomba usamehe:

-Ee Mzazi-Mungu mwenye utulivu yangu na mulinzi yangu na waaminifu wote, unihurumie juu ya matendo yangu mbaya nilikufanya na nilikusema kwa ajili ya taabu mingi yangu.

Ninakushukuru mingi, ninakushukuru na nitakushukuru mupaka mwisho ya uzima yangu na nitawakisha kandila ya picha yako kila siku na usiku.

Nilirudia ku mulango, nilivaa manguo ya mazuri na nilitoka inje ya soko na nilitembea na furaha mingi ndani ya njia ile ni katikati ya muji. Wakati watu waliniona, walikuja kwangu mbio juu ya kunisalimia na kunisema salamu na uvumilia juu ya lufu ya binti yangu.

-Mimi niliwaajibu: Ninapokea salamu ya furaha na misipokee salamu ya taabu. Warafiki wengine yangu, walianza kusimanga katikati yao na kusema juu ya mimi: «Bwana petro kwa ajili ya sikitiko yake mingi, alipotesha akili yake na anapokee salamu ya furaha». Mimi niliwakaribia na niliwaambia:

-Hapana, misikupotee akili yangu. Mbele ya kuona alikuwa wapi binti yangu, kweli niliisha kupotea akili yangu, lakini sasa, kwani nilimuona ya kama anaishi na eko na utukufu mingi ya paradizo pamoja na kundi ya wabikira ma elfu mingi, ndani ya nyumba ya Bwana Yesu Kristu, nikona paka furaha na sifa. Ninapokea, basi, paka salimio ya furaha na hapana ya taabu. Nikona furaha kwa sababu mimi ni baba ya binti moja, ambaye ni bibi-arusi ya Mwana Arusi ya mbingu, nikusema Yesu Kristu.

## 47. Historia ya ajabu juu ya kutii kwa wazazi

Historia  juu ya muujiza moja ya matata sana juu ya utii mbele ya wazazi na heshima mbele ya Liturgia Takatifu.

Ile wakati alikuwa mfalme mu muji Konstantinopoli Theodosios Mkubwa ku mwaka (379-395), alikuwa kwa hii muji mtu moja mufazili na mutajiri ile wakati ya ujana yake na alikuwa na mwana moja aliyeitwa Theofilos. Lakini wakati alizeka, aliishi na usikini mingi na alisema kwa mwana wake:

-Mtoto yangu, tazama, unaona ya kama ni musikini sana na misina kintu juu ya maisha yetu. Basi, ninataka kuomba kwanifanyisia saidio moja juu ya kuokoa toka hii mateso yangu na mimi mutu ya bahati mbaya ile wakati ya uzee yangu na weye juu ya utii yako utastahiliwa ya wenye heri ya mbingu.

-Mwana wake alimujibu: Ee baba wangu, uniambie uwazo yako na mimi misitakataa kutii kwa amri yako.

Ile saa baba muzee yake alimuwambia: Mwenye heri Abrahamu alikuwa na mtoto moja na alienda kumuchinja; na huyu mwana mubarikiwa hasikurudie mukongo, lakini na kuti alipeleka na furaha na alifata baba yake bila boka. Vile fanya na weye mwana wangu mupendwa. Fata amri yangu na ninatumainia kwa Mungu mupenda-wanadamu ya kama weye hautataabu mingi.

-Basi, alisema Theofilos kwa baba yake: Unataka kuniua na mimi?

Yule baba yake alimujibu: hakuna namna kufanya hii kazi kibaya, mtoto yangu. Lakini fanya paka amri yangu paka moja juu ya kuuzisha weye kama mutumwa yangu na hivi nitaishi mu wakati ya uzee yangu. Vile misitazunguluka kama maskini na kuomba saidio ya watu wengine. Na Mungu juu ya hii wema yako atakupatia mali mingi kwa hii dunia na atapumzika nafsi yako mu fasi ya Abrahamu. Tena fanya na hii amri yangu ya mbili; Mbele ya kila kazi utafanya na amri ya mkubwa yako, kumbuku kila siku juu ya kwenda mu kanisa, mu Liturgia Takatifu na kisha uende mu kazi yako, kisha mwisho ya Ibada ya kanisa. Tena chunga heshima na utawa mingi mbele ya Mzazi-Mungu Bikira Maria. Kama utafanya hivi Bwana yesu atakuokoa toka hatari matata.

Mwana wake alimujibu: Sawa vile unataka baba wangu, fanya.

Siku ingine asubui baba yake, alimuitwa Yulianos, alimuuzisha mwana wake kwa mtu mukubwa ya nyumba ya mfalme aliyeitwa Konstnatinos. Huyu alimupenda Theofilos juu ya unyenyekevu, uzima ubikira, uso nzuri yake, hekima na mafundisho iliyejua na alimukuwa na mu meza ya kula pamoja naye.

Siku moja mkubwa yake Konstatinos alikwenda mu nyumba ya mfalme, lakini alisahabu kitabu yake, pahali alikuwa na karatasi ya mambo juu ya kusuburia na mfalme. Basi, alituma mutumwa wake Theofilos kwenda mbio kumuiletea. Kijana Theofilows alikimbia mbio mu nyumba yake. Aliingia mu nyumba ya mkubwa yake, alikamata mbio hii kitabu ya karatasi yake, lakini ile saa alikuwa pa kitanda bibi ya mkubwa yake pamoja na moja mutumwa mwingine na walifanya zambi ya mwili ya usharati. Huyu, kwa sababu alikimbia mbio ya kufanya kazi yake, hasikuwaone. Lakini wale watu mbaya waliwaza matendo mbaya kufanya. Wakati alirudia bwana wake ku mulago, alimwambia bibi yake: « Juu ya ninyi uliuza huyu mutumwa Theofilos? Juu ya kuja pa kitanda yangu na kufanya zambi ya usharati pamoja na mimi? Na, kama mimi misikuita mutumwa mwingine ya kunisaidia, ilikuwa namna huyu mutumwa Theofilos kutosha uzima safi na sifa yangu. Basi, kesho inapaswa kunirudisha sifa yangu; ninakujulisha ya kama kesho ninataka kichwa yake ndani ya mufuko moja. Misiweze kuishi ndani ya nyumba yetu pamoja na weye, kama utakataa kutimiza hii sauti yangu.

Wakati alisikia hii sauti ya bibi yake mkubwa Konstantinos alisirika sana kupingana ya huyu mutumwa yake Theofilos na alilaka kwa bibi yake ya kama atafanya mapenzi yake. Kesho alikutana mu nyumba ya mfalme pamoja na mkubwa mwingine ya mfalme na alimwambia: Kesho asubui nitakutumia mutumwa yangu moja na, wakati atakuja, utamukata kichwa yake na utaiweka ndani ya mufuku moja, utaifunga nzuri na utaniituma.

Mkubwa mwingine alimwambia: Mimi misipende kuhukumu mutu mona bila haki; kama wataichika watu wa watu ya kama huyu mtumwa ni mustahili ya kumuua, mitamuua.

Ile saa mkubwa Konstantinos, mbele ya watu wa tatu alisema hii mambo, yaka alifanya usharati na bibi yake na sasa inapaswa kumuua. Alisema hivi na kisha aliandika maneno ya lufu yake mu karatasi moja na alimupatia hii karatasi kwa mkubw mwingine juu ya kumuua.

Asubui, wakati ilikuja muchana, huyu mukubwa yake aliita mutumwa yake Theofilos na alimwambia: Uende` kwa mukubwa fulani na umuwambia ya kama mimi ninamusalimia na ninaongojea kunituma jibu yake.

Aliondoka huyu mutumwa musiyekosa mbele ya bibi ya mukubwa yake na alipita inje ya kanisa moja, pahali mpadri alifanya sala ya Liturgia. Aliingia ndani Theofilos na alimbakia mupaka mwisho ya Liturgia katika amri ya baba yake.

Yule mutumwa ambaye alifanya zambi ya usharati pamoja na bibi ya mukubwa, wakati aliona ya kama mutumwa Theofilos alichelewa sana, alisema kwa mukubwa yao Konstantinos: «Nitaenda mimi na ruhusa yako kuangalia juu ya ninyi anachelewa hii mambo. Mukubwa yake alimuwambia: «Uende».

Basi, alitembea mbio huyu mutumwa mwovu juu ya kubeba hii mufuko na ile kintu atamutupatia mkubwa mwingine. Aliingia mu nyumba ya yule mkubwa, alimusalia kwa jina ya mukubwa yake. Lakini kule kwa siri aliongojea askari moja, mwenye aliisha kubeba amri kuua huyu mutumwa ambaye ataingia ndani. Mara moja na upanga yake alikata kichwa ya huyu mutumwa mwovu na aliweka ndani ya mufuko moja. Kisha saa kidogo alifika na mutumwa Theofilos, mtu muzuri na bila kuwa mukosefu. Alimusalia mukubwa na huyu alimupatia mufuko hii. Mutumwa alikamata mufuko, bila kujua ndani ilikuwa kintu ninyi, alirudia kwa mukubwa yake. Watu wote walishangaa, lakini kabisa alishangaa bibi yake, kwa sababu huyu alituma Theofilos kumukata kichwa yake, lakini walikata kichwa ya yule mutumwa pamoja na mwenye alifanya zambi ya usharati.

Walimuuliza watu na mkubwa yake Konstastinos: «Unakamata ninyi ndani ya hii mufuko iliyetuletea? ».

Misijue, aliwajibu Theofilos. sawa vile uliniambia, mimi nilienda kule, nilisalimia mukubwa murafiki yako na yeye alinipatia hii mufuko, lakini kintu ninyi ni ndani misijue.

Watumishi yake walikamata hii mufuko, waliifugula na walishangaa, wakati waliona ndani kichwa ya yule mutumwa mwovu. Bibi ya mkubwa mwenye zambi, alishituka na alimbakia na

kinywa yake ya kufungwa, kwani asikuweze kusema sauti moja. Kisha wakati alipata kidogo nguvu, alisikia naziri wa haki ya Mungu. Na, kwani aliogopa juu hapana kupata hatari ingine toka Mungu juu ya hii tenzo kibaya yake, aliria na roho yake yote na alisema mbele ya watu wote hii uzulumu yake mukusema hivi:

Mimi, bwana na mkubwa yangu, ni bmtu mwenye zambi na mbaya, kwa sababu nilikuwa na sababu kukufa huyu mutumwa pamoja na mweye nilifanya zambi ya usharati ya miaka tatu na kipanda, lakini weye usikujue hii matendo mbaya yetu. Huyu mutumwa kijana ni mwenye safi na hasikufanya zambi pamoja na mimi ns mimi nilimuhukumu bila haki. Bwana ni wa haki na alipenda matendo ya haki na anapatia malipo kwa matendo ya kila mtu. «Basi, bwana na mkubwa yangu, unihurumie kwa ajili ya wema ya Mungu na ninakulaka ya kama misitafanya zambi wakati ingine tangu leo».

Ile saa mkubwa Konstantinos aliuliza huyu Theofilos kusema kweli, nikusema hali ya uzima yake na ma fazila yake. Ile saa yeye alimwambia uzima yake ya zamani na namna gani baba yake alimuuzisha juu ya maisha yake na alimushauria kuingia mu Misa mupaka mwisho ya Liturgia. Mukubwa yake, wakati alisikia hii uzima na ma fazila ayke, alimupenda sana na alimukwa na kama mwana wake pamoja mu meza na karibu yake. Na, mbele ya kufa aliandika yoyote uriti na mali yake kwa huyu Theofilos.

Kwa hivi, na sisi wa ndugu wapenzi wangu, inapaswa kuogopa Mungu na kuingia mu Misa kila wakati na kusimama na boka mupaka mwisho ya Liturgia sawa tunaona na hii ma macho yetu Bwana wetu Yesu Kristu, ambaye atatuhukumu ile siku ya matata ya mwisho ya dunia. Tena huyu anayetoka, bila mambo toka Kanisa, wakati inajifanya Ibada moja ao Liturgia Takatifu, anafanana na Yuda, aliyetoka ya Rabi Yesu Kristu Mwalimu yake na alienda kumutoa kwa WaKuhani ya Wa Ebrania Tena aipaswe mwaminifu moja kusuburia ao kusimanga ndani ya Kanisa.

## 48. Ninakushukuru sana mtoto wangu; ulinipumuzika

Kwa Monasteri moja ya Kilima Takatifu anayeitwa ya Mtakatifu Paulo Mutawa, aliishi mutawa moja. Mama yake kwa ajili ya uzee na malari alikufa. Kisha huyu mutawa, kwa sbaabu iko zwezo mu Kilima atkatifu kufanya watatwa ya wakati ma siku makumi ine kila siku komboskinion moja na kuomba kwa Mungu juu ya kupumzika mutumishi yake aliyekufa; nikusema hivi: «Bwana Yesu Kristu, Mwana wa Mungu, pumzika mutumishi yako fulani. Basi, huyu mutawa, kwa sababu alifamia mutawa mwingine toka Monasteri yake, aliyekuwa mtu mufazili na aliomba mingi na nguvu kwa Mungu alimuwambia: «Fanya, ndugu wangu, sala na komboshini juu ya kupumzika Mungu nafsi ya mama yangu».

Na kweli huyu alifanya sala kila siku komboskinion moja. Busiku ya ile siku ya makumi tatu na tisa, alikuja mama ya yule mutawa mbele yake na alimuwambia: «Ninakushukuru sana mtoto wangu; ulinipumuzika».

## 49. «Kristu alifufukuka wa padri. . .

Mara ingine ndani ya hii Monasteri ya Mtakatifu Mutawa Paulo ilifanyika na hii jabo. Ilikuwa Siku Kuu ya Ufufuo ya Bwana Yesu Kristu. Mpadri mkubwa alisema, kisha sala ya Ufufuo ya Kristu, kwa mutawa moja aliyeitwa Thomas: «uende padri Thomas, mu (Cimetiere) fasi ya wafu kusema kwa wapadri wenye kufa kule: «Kristu alifufuka». Mutawa Thomas, kwa sababu alikuwa mutu mupole na alifanya utii, bila shaka, alienda mbio kwa ile fasi walikuwa mifupa ya wapadri wenye wafu na alikamata na taa ya kuwakisha na aliwambia: «Ee wapadri wetu na wa ndugu wetu, Kristu alifufuka». Hii dakika mifupa yote walijitenga na kichwa-mufupa moja alinyanyua karibu kipimo ya metre moja na alisema: «Kweli alifufuka». Alirudia mutawa

Thomas na alimwambia hii mambo kwa mpadri Mkukubwa yake na kwa watawa ya Monasteri yake yote. Watu wote walitukuza Mungu na kabisa ma fazila na upole ya yule mutawa Thomas.

## 50. Walikuja Mzazi-Mungu na Mtakatifu Anastasia. . .

Ku mwaka 1993 alifariki mama Maria Horinos aliyekuwa toka Mukini Marmaras Neos ya Grekia-Halkidiki. waakti alikuwa na kipimo miaka 42. Namna gani aliisha uzima yake?

Huyu mama Maria alikuwa mwaminifu na alipenda Mungu na Kanisa. Wakati alikomea alifanya ndoa na bwana Othonas na walizala mtoto mwanaume na walimupatia jina kwa ubatizo Panayotis. Mama Maria aliogopa sana lufu, joo vile ya miaka mbili, mbele ya lufu yake, alionekana kwake Mzazi-Mungu Maria na alimupatia nguvu. Kwa ajili ya malari cancer alikuja ku mwisho ya uzima yake. Walimupeleka mu obitalo. Siku moja mama Maria, aliita bwana wake na alimuwambia: «Kuja pamoja na mtoto yetu ya kunisalimia, kwa sababu walikuja Mzazi-Mungu Maria na Mtakatifu Mutawa na Mushahindi Anastasia wa Roma na waliniambia ya kama watakuja kisha ma dakika kumi kunibeba». Na kweli, alisalimia watu ya jamaa yake na kisha ma dakika kumi alipanda nafsi yake mbinguni. Kisha lufu yake mwili yake ilikuwa teketeke, nikusema bile kukauka mupaka kuiweka ndani ya kaburi.

Utukufu kwa Mungu, kwa sababu anatuonyesha kwa sisi na wa ndugu ya dunia wenye ni watakatifu.

## 51. Mutawa Stefano toka Monasteri ya Mtakatifu Grigorio

Mutawa Stefano alizaliwa mu muji Pirgos ya Grekia ku mwaka 1873. Mu Monasteeri yake alikuja mu mwaka 1903 na alikufa mu mwaka 1935 na kipimo yake miaka 62. Mu Kitabu ya wale waliokufa tunasoma: «Huyu Mutawa alikuwa sawa moja mushahindi. Ya miaka mingi alitumika mu Monasteri yake. Tena alikuwa na na hii namna ya mwisho ya uzima yake. Mbele ya kufa aliona Walinzi Watakatifu wa tatu ya Monasteri yake, nikusema mt. Nikolao, mt. Grigorio na mt. mwanamuke Anastasia, wenye walimwambia ya kama kisha ma siku tano watakuja kumubeba, wakati itapika kengele ya kwanza, mbele ya sala ya magaribi. Huyu mutawa aliyemusaidia hii ma siku ya mwisho yake alisema: «Siku ya kwanza ya ile juma ya mwisho yake, walikuja ma roho mbaya - ma shetani, walimukaribia na walimushitaki. Mtawa muzee Stefano aliuliza musaidizi yake: «Wa nani hawa watu wenye makali na mbaya, wenye wanakuja kwangu? ». Siku ingine ya mbili walikuja wa malaika juu ya kumutulivu, lakini muzee Stefano hasikusikie walikuja wa nani na aliuliza musaidizi yake: «Hawa watoto wenye mazuri na inaangaza ma uso yao kama wa malaika ni wa nani?». Siku ya tatu aliona muzee Stefano Mtakatifu Paraskevi, kwa sababu alumushehima sana mu uzima yake na alikuwa na ikona yake mu chumba yake. Yule Mutakatifu alimukikiri ya kama ilikuwa mapenzi ya Mungu kupanda mbinguni sawa vile waliisha kumwambia Walinzi ya Monasteri yake. Siku ya ine aliona wa padri wote ya Monasteri yake ndani ya chumba yake na aliuliza musaidizi yake: «Hawa wa padri ni wa nani, padri Sofronie? ». Siku ya tano alitangaza kwa wapadri wengine ya kama inakaribia mwisho ya uzima yake na siku na saa gani ataondoka toka inchi yetu. Na kweli, wakati mutawa ya kanisa alipika kengele ya kwanza juu ya mwanzo ya Ibada ya magaribi, mutawa muzee Stefano aliacha hii uzima na alipanda na furaha na amani mingi mbinguni.

## 52. Sasa nilijiuhuru, sasa nilipata kimya, sasa nilipumuzika. . .

Kwa Monasteri ya Mtakatifu Grigorio aliishi na Mutawa Afksentios. Huyu alizaliwa ku mwaka 1892 mu Mukini Mandra ya Atiki ya Grekia. Mu uzima yake alikombana nguvu juu ya kuishi uzima moja takatifu na usafi. Alipenda kufanya kila kazi na kusaidia wa ndugu wake. Tena alipenda unyamaza juu ya kusema ma siku na saa yote sala ya Kristu: Bwana Yesu Kristu Mwana

wa Mungu unihurumie, mimi mwenye zambi». Kama aliishi katika baraka na neema ya Mungu tutaangalia ku mwisho ya uzima yake. Namna gani alifariki: Alifariki ndani ya nyumba ya wazee ya Monasteri ya Mt. Grigorio ku mwaka 1981, wakati alikuwa na kipimo yake miaka 89. Ile siku wa padri wote waliimba mu kanisa Sala ya Magaribi ya Siku Kuu ya Orthodoksia, mu Juma ya kwanza ya Kwarezima. Waliimba wimbo: Mwangaza upole (ilaron). . . wakati mutawa Afksentios aliacha nafsi yake kuluka mbinguni. Karibu yake waliikaa watawa wa wili wajana, wenye walisikia ya kama inje walikuja wakubwa watakatifu pamoja na ma punda yao, kwani watawa wa ndani walisikia makelele ya mwendo ya ma punda yao. Kisha mutawa moja aliona kutoka ya kinywa ya mutawa Afksentios nafsi yake, kama mwili muzima ya mutawa Afksentios, aliyesema paka na nafsi yake: Sasa nilijiuhuru, sasa nilipata kimya, sasa nilipumuzika. . . ». Na hivi alikufa.

Kisha juma moja huyu mutawa kijana alimuona mtawa Afksentios mu ndoto yake alimuuliza:

-Namna gani ulipita, padri Afksentie ma kundi ya ma shetani, kisha lufu yako? Ma shetani hawakukuuzi, kisha lufu ya mwili yako? ».

-Misikuwa na hata mambo moja. Paka shetani mudogo moja ya uzini alikuja mbele ya miguu yangu. Aliniona na boka na kisha alikimbia».

## 53. Mwisho takatifu ya Mwaminifu moja

Mu Monasteri ya Mtakatifu Grigorio aliishi na mutumishi moja mwaminifu, aliyeitwa Diogenis. Alikuwa toka Kisanga Lesvos ya Grekia na alitumika miaka mingi mu Kilima Takatifu na ma Monasteri ingine. Mbele ya mwisho yake walikuja ma roho maovu na ma uso ya ma ngurumbe na walimuogopa. Walimukokota, walifanya makelele na waliria. Kisha walifika ma shetani wa wili mbaya sana na mifupa na walikuwa na sego pa kicwa yao. Walimuangalia na mfano ukali. Kisha alikuja shetani moja mkubwa na murefu karibu na kipimo ma metre tatu na alisema kwa ma shetani wengine wadogo:

-Mumubebe huyu, hana uzima ingine. Juu ya ninyi munamuongojea?

-Hana tayari ndani ya ma karatasi yetu. Hana yetu, tusiweze kumubeba.

-Ma sauti ninyi munaniambia? Hii wakati mingi munafanya ninyi? Juu ya ninyi munachelewa kumutayarisha? (nikusema kumutupa mu zambi fulani).

-Ile saa ma shetani wadogo walimwambia ma sauti ya bure. Mukubwa yao alisirika na alianza kuwapika na aliwazambalisha yote. Kisha aliikaa huyu mbele ya huyu mwaminifu Diogenis ya ma dakika makumi tatu, bila kusema sauti kimoja. Kisha ma dakika kumi walikuja ma kundi ya wa shemasi na wa padri watukufu, wenye waliingia mu chumba ya Diogenis. Walipita pempeni yake. Walimubebelesha pa mbavu yake na alimwambia: Uko mutumishi yetu; uko mu kundi yetu. Fanya uvumilia na tutakuja, kisha ma siku tatu akubeba». Na kweli, kisha ma siku tatu mwaminifu muzuri Diogenis alipanda na nafsi yake mbinguni. Mbele ya kufa alipewa na Mwili na Damu ya Bwana Yesu Kristu.

Tena ninajua ya kama ku mwaka 1981 alikufa na mutumishi mwingine mu Kilima Takatifu ndani ya nyumba yake. Lakini watu wengine na watawa walisikia hii mambo kisha ma siku makumi ine. Jabo ya ajabu ni hii. Walipata mwili yake, bila kuharabika ao kuoza kisha ma siku makumi ine. Kupindua toka mwili yake ilitoshwa arufu moja nzuri. Huyu mwaminifu alikuwa mtu mtakatifu.

## 54. Wanakuja ma kundi yote ya watakatifu. . .

Mu Monasteri ya Mtakatifu Grigorio anaishi tena Mutawa Muzee Emanueli, ambaye alikuwa na dada moja mu dunia. Huyu aliitwa dada Vasilika na alimbakia bikira mupaka mwisho

ya uzima yake, kwa sababu alipenda kutoa uzima yote yake kwa uzima ubikira ya Mungu. Aliishi ndani ya nyumba yake ya Kisanga Lesvos, lakini aliishi, kama mutawa na alivaa manguo meushi. Alikuwa mushindani mukubwa, lakini alifuchama ma fazila na sindano yake ya Kristu. Asikuseme hata sauti moja kwa ndugu yake Emanueli, namna gani aliishi, hata kwa wa dada wake.

Ku mwaka 1959-60 walionekana kwa ndoto ya waminifu wengi Watakatifu Washahindi Rafaeli, Nikolaos na Irini, wenye walikufa katika mateso ya kuachana mu Kisanga Lesvos ku mwaka 1463. Hawa Watakatifu waliisha kumazikwa mu Monasteri yao, lakini ma karuri yao waliisha kuzibiria tangu ile mwaka walikufa na mateso. Na baraka ya Mungu walionekana mara ya kwanza ku mwaka 1960 na walisema kwa waminifu wengi kufika mu fasi ya ma kaburi yao juu ya kutosha mifupa takatifu yao.

Siku moja alionekana mpadri Mukubwa mtakatifu Rafaeli mbele ya dada Vasilika na alimwambia:

-Unataka, dada Vasilika kutosha Mifupa Takatifu ya mtakatifu mwanamuke Olimbia?

-Ndivyo, mtakatifu ya Mungu; haina lazima kuniuliza.

-Muzuri; uende na sema kwa mwaminifu Dukas kukuja hapa leo magaribi na ma bintu yake ya kuchibula ku ile fasi mimi nitakuwambia.

-Ee Mtakatifu ya Mungu, kama iko namna kesho, kwa sababu leo magaribi atachelewa, kwani kazi hii ni mingi.

-Hapana. utamwambia kukuja leo, kwa sababu kesho kwa hii fasi watumishi wengine wataanza kazi ingine ya kutupa matope ya ciment.

Kweli walienda ile siku magaribi. Alichibula bwana Dukas ku ile fasi mtakatifu Rafaeli alimwambia na mara moja walisikia bikelele moja. Ilikuwa kaburi ya mtakatifu Olimbia. Walitosha Mifupa yake na dada Vasilika alipeleka mu nyumba yake. Kichwa-mufupa yake ni mupaka sasa mu nyumba ya Mutawa Emanueli ya Monasteri ya Mtakatifu Grigorios.

Ile siku bwana Dukas alikwenda kuchibula walikuja naye na watu wa wili ya kumusaidia. Lakini walikataa kuamini ya kama Mtakatifu Rafaeli ni mtakatifu. Walisema ya kama alionekana mutumishi ya kanisa aliyeitwa Panayotis.

Ile usiku walisuburia na walikamata mpango kuchunga fasi moja, pahali alipaswa kupita Panayotis, juu ya kuangalia nani anaonekana Panayotis ao mtu mwingine. Moja aliikaa mu fasi moja na mwingine mu fasi ya ngambo ingine ya njia. Usiku alionekana katikati yao pa pepo mtakatifu Rafaeli. Aliwaita karibu yake na aliwaambia:

-Basi, mimi ni mutumishi panayotis, eee! Mimi misina Mtakatifu Rafaeli? Aliwapika na kofi moja kwa mtu moja na kofi ingine kwa mtu mwingine na watu kisha na machozi waliomba hurumia, mukusema hivi: «Utuhurumie, mtakatifu Rafaeli. Sasa tunakuamini ya kama usiwe Panayotis lakini uko kweli Mt. Rafaeli. Tangu ile siku wote wa wili walisadiki ya kama Mt. Rafaeli alifanya maonekano kila wakati. Hawa watu kila siku, asubui na magaribi, walikwenda kwa ile fasi alionekana mt. Rafaeli, nikusema walitembea saa moja kwa miguu, juu ya kuwakisha kandila moja mu ile fasi waliyenga chumba kidogo takatifu na walisujudu kule ma picha ya Watakatifu.

Dada Vasilika, alituwambia ndugu yake Mutawa Emanueli, aliiishi uzima nguvu kama mutawa. Karibu kila juma alifunga chakula na alikula paka antidoro, kisha mwisho ya Liturgia. Ndugu mukubwa yake alikuwa askofu na alimusaidia kwa kila kazi yake mu nyumba yake.

Mwisho ya uzima yake ilikuja mu Yanuarie ya mwaka 1965. Mzazi-Mungu Maria aliisha kumujulisha ya kama atamubeba mbinguni, kisha ma siku makumi ine. Ile siku ilitimizwa siku ya makumi ine. Wakati dada Vasilika alisikia waganga kumusema ya kama ni lazima kumupeleka mu obitalo huyu alikataa na alisema: «Hapana, hapana, mu obitalo, Mzazi-Mungu Mtakatifu kamili Maria atanibeba kisha saa kidogo. Vile aliisha kunisema. Saa yangu ilikuja». Mu ngambo ingine mbele ya kitanda yake, pahali aliisha kularisha ilikuwa fasi ya ma picha-Ikona ya

Watakatifu. Huyu Dada aliangalia daima ma Picha ya watakatifu. Mara moja na uso yake ya kujaza na furaha aliona kushuka karibu yake Watakatifu toka paradizo katika ma kundi yao. Ya kwanza walikuja wa Nabii, kisha wa Mitume, waShahindi, wa Askofu, Watawa, wa majeshi ya wa Malaika, kisha Mzazi-Mungu Bikira Maria na ku mwisho alikuja Yesu Kristu, ambaye alishuka na utukufu mingi na mwangaza ilijaza Uso yake.

Dada Vasilika alishituka na aliacha mara moja kutoka sauti moja wa ajabu toka kinywa yake, hivi: Aaaa! Mwipwa yake, mwanamuke Irini alimuuliza: «Shangazi yangu, ukona mambo ninyi? ».

-Irini, Irini, mtoto wangu alikuja Kristu kunibeba pamoja na ma Kundi yote ya Watakatifu wake. .

Wakati alisema hii ma sauti yake, Kristu alibeba nafsi yake na alipanda mbinguni, lakini kichwa yake ilinamisha pa mikono ya ndugu yake Mutawa Emanueli.

Mungu, kwa sababu alitaka kuonyesha kwa sisi utakaso yake, alifanya miujiza ya ajabu, wakati maiti ya dada Vasilika ilikuwa tena pa kitanda yake. Wakati alikufa mara moja ilikuja na ilisimama yulu ya mwili takatifu yake nguzo moja ya nuru, iliyekuwa yulu ya mwili yake 50 cm (kipande ya metre). Hii nguzo ya nuru ilikuwa pa mwili yake mupaka walimuweka ndani ya kaburi yake. Hii nguzo tena iliangaza na usiku na muchana ile fasi ilikuwa kaburi yake na watu wote walishangaa. Alilala musingizi ya wenye haki mu kipimo yake miaka 55, ku mwaka 1965.

Dada mwingine ya mutawa Emanueli aliitwa Persefoni. Na huyu aliishi kama mutawa, lakini hasikuvaa manguo na watawa. Aliishi uzima safi na ubikira na alimupenda sana Mungu na watoto yatima. Mbele ya usiku yake alisimama karibu yake usiku moja na huyu mutawa ndugu yake Emanueli aliyesema hivi: «Wakati nilimbakia karibu yake usiku moja, niliona ya kama alikuyaka lufu kama mtu lakini, bila nyama ku mwili yake, paka na squelette na alikamata kwa mukono yake upanga ileyeiko ya mavuno. Nilimuangalia na yeye aliniangalia, alisimama yulu ya mwili ya dada yangu na alinisema: «Kisha masiku tatu nitakuja kumubeba». Ile siku ilikuwa mukazi tatu. Mu Posho asubui kweli nafsi yake alipanda mbinguni. Mbele ya lufu yake alisema kwa sisi: « Bwana, Bwana Yesu Kristu wetu ananiongoje. . . Ninaende, ninaenda. . . ».

## 55. Hawa wanaofanya utii hawakufe. . . .

Mu Monasteri moja ya Kilima Takatifu ku mwaka 1918 ilifanyikwa jabo moja ya matata. Monasteri ilikuwa na mu fasi ya Makedonia, nikusema mbali na inje ya Kilima Takatifu ma kilometre 250 shamba moja munene na kule walitumika watawa toka Monasteri na watumishi wengi. Toka Monasteri ilikuwa namna kwenda Wapadri na mutubwi katika bahari kwa hii shamba. Ilikuwa wakati ya nvula na baridi ya mwaka moja na mpadri mukubwa ya hii Monasteri alilofa inje ya Kilima Takatifu. Mufwasi yake, mpadri Haralambos alikamata mpango kutuma watawa wa tatu mu ile Shamba iliyeitwa Vulchista, na mutubwi. Lakini wakati ilikuwa mubaya na mu bahari ilianza tufani na makelele ya maji yake.

Wale watawa walimwambia: Mpadri wetu, wakati ni mbaya na iko hatari ya kutembea mu bahari».

Yeye aliwajibu: Mwende, mufanye utii. Muko watawa inapaswa kutii.

Hawa Watawa kweli waliondoka. Lakini kidogo mbali ya Monasteri yao walikufa, ole, ndani ya bahari. Walisikia hii mambo ya taabu Watawa wote ya Monasteri yao na walisikitika mingi. Ile usiku mutawa moja, aliyeitwa Afksentios, mwenye jana magaribi aliisha kufa pamoja na wengine wa wili mu bahari, alikuja inje ya mulango ya nyumba ya mpadri Haralambos na alikokola mulango yake.

-Ni nani, alijibu ya ndani padri Haralambos.

-Niko mimi, mutawa Afksentios.

-Nani Afksentios? Mutawa Afksentios alikufa jana mu bahari.

-Mutawa Afksentios alimujibu: Hawa wanaofanya utii, hawakufe. . . .

Mpadri Haralambos, alishangaa. Kisha, kwani alikuwa na mpadri, alisimama kazi takatifu yake na tangu ile siku hasikufanya Liturgia na ma Ibada ingine.

## 56. Mtoto mwanamuke Konstantina alipanda mu Paradizo. . .

Mu Grekia iko muji moja inayeitwa Yanicha. Kule anaishi mupaka sasa jamaa moja.

Bwana anaitwa Polikarpos. Huyu na bibi yake walizala watoto wa wili: Mtoto mwanamume anayeitwa Theodoros na mwanamuke aliyeitwa Konstastina. Mtoto yao, mwanamuke Konstantina, wakati alikuwa na kipimo miaka 12 alipata malari nguvu, nikusema damu yake iliharabika na ilijifanya maji, nikusema alikwa na malari ya cancer.

Wazazi wake waliteswa ya wakati miaka wa wili juu ya kuokoa mtoto yao, lakini hakuna namna. Ilifika juma ya mwisho ya huyu binti yao. Alikuwa ndani ya obitalo na siku moja alisema kwa baba yake:

Baba yangu, kama wanakuja watu, wenye wanataka kuniona, angalia weye, kama ni watu wa Mungu na wanafata kanisa na uzima ya Mungu iko namna kuwaacha kunitembelea, lakini kama ni watu wenye zambi na pasipo imani na boka ya Mungu misipende kuja kunitembelea.

Baba yake alifanya utii kwa binti yake. Mbele ya lufu yake ma siku wili alifanya ulizo ingine ya ajabu kwa baba yake:

-Baba wangu, hapa ya muji yetu tukona ma kanisa ma ngapi?

-Ninazania tukona ma kanisa tano.

-Baba wangu, watu wa ngapi wanaikaa ndani ya muji yetu?

-Juu ya ninyi unaniuliza Konstantina? Lakini ninazania tuko karibu ma elfu makumi mbili na tano.

-Ninakuuliza, kwa sababu ninashangaa namna gani wanaingia hawa watu wote ndani ya ma kanisa tano.

-Mtoto yangu Konstantina, haujue ya kama hawaingie watu wote kila Siku ya Mungu na kila Siku Kuu mu Kanisa? -Aaa! Baba wangu, unajua hawa watu wanapotesha ninyi?

-Wanapotea ninyi, mtoto yangu?

-Kama walijua furaha ninyi na utukufu inawaongojea mu paradizo ilipaswa wote na haraka kuingi na ma kanisa ya Mungu.

-Namna gani unajua hii tangazo weye Konstantina?

Sasa, baba yangu nilirudia toka paradizo. Nafsi yangu alipanda mu mbingu na niliona ma fasi ya Watakatifu ya Mungu na nilifurahi sana.

-Nikusema, Konstantina, kama sasa atakuja Kristu na atakuambia: Kuja, Konstantina karibu yangu, weye utamufata?

-Mara moja, baba yangu, mara moja mitamufata. Na nitaongojea na furaha mingi kukuja hii saa.

Wakati ilifika saa ya lufu yake mtoto Konstantina alikuwa pa kitanda. Aliweka mukono yake pa kilari yake na alianza kusema kwa baba yake:

-Baba yangu, hapa iko, hapa iko na alitenga mukono yake yulu ya sigo yake.

Vile alitaka kuonyesha ya kama pole-pole inatoka ya mwili yake nafsi yake. Wakati aliweka mukono yake pa sigo yake alisema: «Baba wangu, muloko yangu Theodora ni mtoto muzuri; umusaidie mu uzima yake». Na mara moja alifunga ma macho yake. Kisha ma dakika tano aliingia shangazi ya huyu binti aliyekufa ndani ya nyumba yao. Mara moja alisema kwa ndugu yake:

-Ee Polikarpos, ninanunka ubani. Juu ya ninyi uliweka ubani sasa asubui? -Kuja, kuona. Misikuweke ubani.

Alishangaa na shangazi yake kwa sababu hii arufu ilitoka toka mwili ya mtoto Konstantina.

Niliuliza baba yake: namna gani aliishi mtoto yako mpaka kipimo ya miaka kumi na mbili yake?

-Binti yangu hasikujue njia ingine paka ya kwenda ku masomo, ku mulango na ku kanisa. Mara mingi mimi na bibi yangu tulimuwambia kukuja na sisi ya kutembelea wa rafiki wetu ao ku fanya mwendo moja mu bahari ao ma fasi ingine ya kuachana. Hakuna namna kutufata huyu mtoto yetu. Aliikaa mu nyumba na kule ao alisoma ma kitabu ya masomo yake, ao ma kitabu ya Mungu ao alifanya sala. Tena ma ile miaka yake hasikuniomba hata kintu moja, hata switi moja. Watoto wengine waliomba bintu ya kucheza na bintu ya masomo, lakini huyu binti Konstantina hasikuombe hata kintu moja. Vile, kwa sababu Mungu alimupenda, alimubeba karibu yake mu Paradizo. Alikufa ku mwaka 1982.

## 57. Ee Mungu wangu, uko wapi? Mtoto yangu anapotea. . .

Hii historia mutaisoma sasa alinisema mutawa Antonios toka Monasteri ya Mtakatifu Grigorio ya Kilima Takatifu, wakati tena alikuwa mu dunia, mbele ya kufanyika mutawa.

Mwaminifu moja aliishi mu muji Pirgos ya Grekia, alikuwa muganga na aliitwa Nikolaos. Alizala na bibi yake mtoto moja mwanaume, lakini huyu mtoto, wakati alikuwa na miaka tano alipata malari ya damu yake, nikusema cancer ya damu yake. Kila saidio ya watu ilikuwa ya bure na wazazi wake waliongojea lufu yake. Baba yake hasikukuwe mwaminifu nguvu, lakini mbele ya huitaji matata yake, alikimbilia  kwa Mungu, bila tena kujua namna gani atasuburia na Mungu.

Siku moja aliendа pa punda yake mu shamba yake, iliyekuwa mbali ya muji yake ma saa mbili na kipande. Mu njia aliwaza nani atamusaidia kwa mambo nguvu yake. Aliwaza mara ingine Mungu, lakini namna gani atamukutana, namna gani ataanza kumwambia? Ile wakati alitembea tena mu njia, hasikuweze kuvumilia. Alishuka chini ya punda, alinyanyua mikono yake yulu na nguvu yote ya roho yake alisema mbele ya Mungu na aliona mbingu:

-Mungu wangu, uko wapi? Mtoto yangu anapotea. . . . Unisaidie. Angalia umivu yangu, machozi yangu na unitaabu. Paka Weye sasa unaweza kunisaidia. . .

Alipanda na punda yake kilima moja, alifika mu fasi moja wazi na kule, o ya muujiza ya Mungu wetu! Aliona Yesu Kristu muzima mbele ya ma macho yake, aliyesimama pa pepo, karibu ma metre 200 yulu ya inchi. Alionekana ya kuvaa kama nguo mwangaza mingi na utukufu kabaila kabisa. Alimuona hata safi na hivi aliona na ma misipa ya mikono Yake. Aliangalia muganga Nikolaos ma dakika kidogo na kisha alimwambia na sauti nguvu:

-Usisikitike. Mtoto yako nitamupona.

Vile alisema na alikimbia.

Wakati aliona hii ono ya Bwana Yesu huyu muganga Nikolaos alikuja shetani na alimupanda ndani ya akili mawazo mbaya ya shaka mumusema: «Hii ono unaiona usiisadiki, ni tunda ya akili yako, kwa ajili ya taabu yako».

Muganga mbele ya kuichika kwa hii mawazo mbaya ya shetani, mara moja alikuja na haraka Bwana Yesu Kristu mara ya mbili na alimuwambia:

-Mimi ni Mungu wako na, namna gani nilikuambia, mtoto yako ataponyeshwa.

Kisha Bwana Yesu alikimbia na haraka.

Muganga aligeuza kazi yake. Hasikwende mu shamba, lakini alirudia ku mulango. Mama yake alimupokea na alimwambia:

-Kuja, mtoto yangu kuona mtoto mwanamuke yako, kwa sababu mbele ya saa kidogo alisikia muzuri na sasa anacheza pamoja na watoto wengine.

Aliingia muganga ndani ya nyumba yake na aliona hii mujiza. Mambo ya ajabu ni hii: Ya kama alistahiliwa kuona Uso ya Bwana wetu Yesu Kristu na kusikia toka kinywa takatifu yake:

-Usisikitike. Mtoto yako nitamupona.

## 58. Ah, mtoto yangu, hawa waganga tendo kibaya ninyi walinifanyisia!

Mu Monasteri ya Mtakatifu Grigorio anaishi tena mutawa muzee Emanueli, ambaye alinisema hii historia.

Mu fasi Plaka ya muji Athina ya Grekia aliishi jamaa moja. Bwana ya hii jamaa aliisha kufa na kisha walishi bibi yake na mtoto yake moja, aliyekuwa mwalimu ya masomo ya yulu pia.

Wakati moja alipata malari na ilikuja mwisho ya uzima yake, lakini waganga na namna ya kuachana walimukamata mu hii uzima na hawakumuache ya kufa katika amri ya mtoto yake, aliyemupanda mama yake. Kisha ma siku madogo alifariki mama yake na walimumazika mu Kazi moja magaribi, kisha Ufufuo ya Bwana Yesu kristu. Kisha ma siku kumi na tano alionekana huyu mama kwa ndoto ya mtoto yake na alimwambia:

-Ah, mtoto yangu, hawa waganga tendo kibaya ninyi walinifanyisia! Na dawa yao ya kuachana walinizibiria kukufa na mimi misikuweze kufuraha toka mafuraha ya paradizo, pahali niko sasa. Mweye hamujue namna gani inafurahi hapa nafsi yangu, kwa sababu ninaona utukufu ya Mungu na Watakatifu Wake! Nitaomba kwa Mungu kukuja na weye hapa mbio, lakini kama unapokea fundisho yake na unatimiza ma amri yake.

Ni kweli ya kama huyu mama aliishi uzima takatifu hapa na joo vile alipata ma baraka mengi mu paradizo.

## 59. Lufu mubaya ya mutawa moja

Mu Monasteri ya Mt. Dionisios ya Kilima Takatifu alikuwa mpadri mkubwa mtu moja aliyeitwa padri Haralambos. Huyu anasema hivi:

Wakati mimi niliishi pamoja na mpadri ya roho yangu Yosefu mu Skiti-Mukini Mupya ya Monasteri ya Mtakatifu Paulo, ilikuja wakati na alikufa mutawa moja. Huyu mu uzima yake, kisha Komonyo Takatifu, alikuwa na zwezo mbaya na likunywa vinyo mingi, lakinikisha alitapika vinyo pamoja na Mwili na Damu ya Kristu na hii ilikuwa kweli zambi mnene. Wakati alikufa sisi tulienda mu nyumba yake na tulimupata kufa chini ya kitanda yake. Ile usiku maiti yake ilikuwa mu nyumba yake, tukona sisi zwezo hapa mu Kilima Takatifu kusoma ma Zaburi ya Nabii Daudi. Basi, ile usiku nilisoma mimi ma Zaburi, lakini nilisikia boka na tetemeko ku mwili yangu. Nilisema hii mambo kwa mpadri ya roho yangu na yule aliniambia: «Huyu nafsi waliibeba ma shetani na wanakutetemeka kwa sababu sisi hatunana tena mamlaka kwa huu nafsi. Vile nilisikia na wakati nilifanya sala na komboskinion, kisha ma siku tatu, ma siku tisa na masiku makumi ine. Nilisikia tetemeko. Tena, wakati tulifanya ukumbusho yake kisha ma siku makumi ine, mimi nilifukiza na chetezo, lakini toka chetezo ilitoka arufu kibaya sana. Mpadri mkubwa yangu aliniambia: «Simama sala, hakuna faida kwa roho yake. Ma shetani waliweka ndani chetezo soufre juu ya kututeswa kwa simoko».

## 60. Askofu Grigorio

Mu Grekia iko fasi moja-Mitropolia, pahali mbele ya miaka 30 alikuwa askofu mtu moja mtakatifu aliyeitwa Grigorio. Tazama alituwambia ninyi juu ya mwisho yake mpadri mukubwa Hristodulos, ambaye ni sasa Igumeno mu Monasteri ya Kutlumusion ya Kilima Takatifu.

«Ndani ya nyumba yake alikuwa dada yake katika mwili, aliyeitwa Maria na mimi, lakini ile wakati nilikuwa shemasi yake. Mara moja nilimusikia kusema: «Kuja, ee Rabi wangu; anakuja Mfalme wetu. Tazama Mzazi-Mungu wetu. . . Muchefe juu ya kupita». Na sisi tulichofa kidogo mbali lakini bila kuona kintu moja ao mtu moja fulani. Kisha askofu Grigorio aliendela na alisema: «Tazama mt. Yoane Krisostomo, mtakatifu Grigorio. . . Yambo yenu. . . mwafu wako».

Kisha alisema: «Kujeni, kujeni watoto wapenzi wangu. . . Oh, Oh hawa watoto wa ngapi ni wazuri! ! Wanakuja, Maria dada yangu, leta ma switi kuwapatia kwa hawa watoto. . Kisha yeye alifugula mikono yake na alibebelesha hawa watoto, lakini sisi hatukuone watoto, paka tuliona mukono yake ile ilifugula. Dada yake aliniambia: «Rabi yetu alipotesha akili yake. Sasa tutafanya ninyi, kwa sababu malari yake ilifanyika kupita nguvu. . » Yule alimwambia: «Dada yangu, usitaabu; Utabeba malipo ya roho mingi toka Mungu wetu, kwa sababu ulinisaidia tangu kipimo yako udogo». Kisha alisema kwa mimi: «Wende mu nyumba ya watoto wenye yatima, kwa sababu wanakuongojea. Kisha kuja karibu yangu mara ingine». Lakini, mbele ya kuingia mu nyumba ya watoto, walinibeba singa (telefone) na waliniambia ya kama askofu yetu alifariki. . .

## 61. Askofu mtakatifu Nikolaos

Kisha askofu Grigorio walichakula Kanisa ya Grekia askofu mwingine aliyeitwa Nikolaos ku mwaka 1970. Huyu askofu alikuwa kweli mtakatifu. Ndani ya nyumba yake alikuwa kichwa-mufupa moja juu ya kukumbuka mwisho yake na kuria.

Alipata malari na ilipaswa kumupeleka mu Aglia ya muji Londino juu ya kumusaidia kwa afya yake. Lakini mbele ya ondoko yake alisema kwa mpadri Kristodulos: «Ee mpadri, mimi ninasikia ya kama misitarudie muzima hapa mu inchi yetu, kwa hivi beba Musalaba na Egolpion yangu, ile nilikobeka pa kilari yangu na pahali fasi utakuwa utanikumbuka.

Na kweli alienda askofu Nikolaos mu Aglia, lakini alikufa na kipimo yake miaka makumi ine na mbili (42) na walimupeleka mukongo na walimumazika mu Monasteri ya wanawake ya njimbo Evia. Kisha miaka wa wili mpadri Kristodulos, kwani ilipaswa kutoka na kuja mu Kilima Takatifu, alitakia kufanya Liturgia ya mwisho ndani ya hii Monasteri, pahali waliisha kumazika askofu Nikolaos. Mpadri Kristodulos alifanya sala ya usiku muzima pamoja na waminifu mengi. Katikati ya hii sala ya usiku mu fasi ya kuume ya Meza Takatifu ndani ya Altari Takatifu walisimama wa padri wa wili. Mimi, alisema mpadri Kristodulos niliwaza ya kama walikuwa wapadri toka Kilima Takatifu na kwa sababu waliomba na heshima na boka mingi, misikuwauzi, hata misikuwasalimia. Ile saa ilitoka toka chini ya Meza takatifu arufu nzuri sana. Iliisha Liturgia Takatifu na mimi nilikaburia kwa waminifu na kwa watawa wanawake antidoro. Kisha nilienda mu kaburi ya askofu Nikolaos kusoma sala ya Makumbusho yake. Kisha nilirudia na nilisema kwa mutawa mkubwa: Juu ya ninyi Muzee Mutawa uliacha na wapadri ya Kilima Takatifu waliondoka, bila kuwapatia kafe moja ao kusimama kidogo kuwafamia na mimi na kusuburia kidogo na hawa? ». Yule alishangaa na hasikujue kusema ninyi na alisema mtu moja katikati yetu hana muzuri; ekona malari. Tulisuburia naye juu ya ile arufu iliyetoka toka chini ya Meza takatifu. Kisha Mutawa mukubwa aliniambia ya kama chini ya Meza waliisha kuweka zamani kipande ya mifupa ya mtakatifu Arsenios na ninazania ya kama hii mufupa yake ilitosha hii arufu. Ile saa mpadri Kristodulos alielejea hii maono ya ajabu. Walikuwa askofu Nikolaos, aliyekufa mbele ya miaka wa wili na aliisha kumazikwa kule na mtakatifu Arsenios, kwa sababu ndani ya Altari ilikuwa kipande ya mifupa yake.

Wakati mpadri Kristodulos alienda kufanya sala ya ukumbusho ya askofu Nikolaos mu kaburi yake, yote fasi pempeni ya kaburi alitosha arufu.

Alisema kwa Mutawa mukubwa: «Juu ya ninyi mulimwanga hapa ma arufu? Haina muzuri. Watu watazania ya kama sisi tunataka kutakasa askofu.

Mutawa mwanamuke mukubwa alimujibu: Mbele ya ma siku tatu sisi tulisafisha marbre ya kaburi yake na sabuni na tusikuweke arufu hata kidogo. Hii arufu inatoka toka kaburi ya askofu wetu. Kisha ma siku kidogo walifugula ya saa kidogo kaburi yake na walishangaa. Mwili yake ni muzima ndani ya kaburi yake na inatosha arufu!! Mara ingine waliifunga.

Mpadri Kristodulos mu mwaka 1976 aliondoka toka mitropolia yake, ya Evia, pahali alikuwa askofu mtakatifu Nikolaos. Alikuja mu Kilima Takatifu na sasa ni mpadri mkubwa ya

Monasteri ya Kutlumusion. Ile miaka ya tatu ya kwanza, wakati alikuja mu Kilima takatifu, kila mu Posho Mkubwa alimutembelea askofu Nikolaos mu nyumba yake hapa mu Kilima Takatifu na walisuburia mambo ya kuachana. Tena askofu Nikolaos alimwambia: «Ninataka kunitosha toka kaburi yangu. Inenea, misipende kumbakia ndani wakati ingine». Mpadri Kristodulos alienda mu Athina kubeba ruhusa toka Makutano ya wa askofu wakubwa na wale walimwambia ya kama ni na haraka sasa kumutosha. Acha wakati ingine».

Ma fazila yake makubwa walikuwa: Unyenyekevu. Hasikupenda makuta na aliishi kama maskini sana. Alitembea na bilato ya kuharabika. Tena na kofya na ma nguo meushi yake walikuwa ya kuharabika. Alipenda sana watu na alifanya nguvu kuwasaidia. Kisha miaka filani huyu watamufamia kama Mutakatifu na sisi tutamushangilia ukumbusho yake. Utukufu kwa Mungu wetu.

## 62. Mtakatifu Efimia mu nyumba ya mutawa Paisios

Mu Kilima Takatifu aliishi mutawa moja mu jangwa aliyeitwa Paisios. Alikufa na utukufu mingi mu mwaka 1994. Wakati aliishi, usiku moja alikuja na alikokola mtu moja mulango ya nyumba yake ya jangwa.

Mutawa Muzee Paisios aliuliza ya ndani: Ni nani?

-Huyu alumujibu: Unifugule na nitakuambia niko nani.

-Misitakufugule, kama usitaniambie nani uko. Sema ya kwanza fundisho ya Imani yetu, nikusema Simvolo ya Imani Orthodokse.

-Huyu mugeni aliisema.

Mutawa Paisios alimwambia tena: Sema: «Baba yetu uliye mbingunii. . . » na wimbo ya Mzazi-Mungu: «Salamu Mzazi-Mungu Bikira Maria. . . ». Na huyu mugeni aliisema.

Kisha mpadri Paisios, bila shaka, alimufugula. Alishangaa, kwa sababu huyu mugeni alikuwa mwanamuke moja na wanawake inakatazwa kuingia ndani ya Mulima Takatifu.

Huyu mugeni alimwambia: Mimi niko Mtakatifu Efimia. Mungu alinituma juu ya kujulisha kwako ya kama juu ya hii mambo uliomba Kwake, itatimizwa. Ile saa Muzee Paisios alipika magoti mbele yake na alimuomba hurumia, kwa sababu alimuchelea inje ya mulango. Mtakatifu Efimia alimujibu ya kama hivi ilipaswa kufanya juu ya kupima kama huyu mugeni ni mtu ya Mungu ao ni roho ya shetani.

Kisha mpadri Paisios alifugula mulango ya kanisa mudogo yake na alimwambia kuingia ndani ya kubusu ma Ikona-picha ya Bwana Yesu. Kweli, huyu Mtakatifu aliingia, alibusu Ikona na kisha alitoka inje na alikimbia.

## 63. Mpadri mkubwa Markos ya Monasteri ya Mt. Dionisios

Mu Monasteri ya Mt. Dionisios aliishi mutawa moja aliyeitwa Markos. Huyu alikufa ku mwaka 1938 na kipimo yake miaka 92. Huyu alikuwa na mpadri na alifanya na Liturgia kila wakati. Alitumika nguvu na alisema na sala ya Mungu kila siku ya kuendelea. Alikula paka mara moja kila siku. Magaribi alifanya kifungo ya chakula.

Siku moja mbele ya lufu yake hasikuweze kupumuzika. Asubui, wakati alienda musaidizi yake kumuuliza namna gani alipita ile usiku iliyepita huyu alimwambia:

-Mtoto yangu, hii usiku juu ya ninyi walikuja hapa ma pusi yote? Kwa ajili ya makelele na ma sauti yao misikuweze kupumuzika.

Musaidizi yake alimujibu: Ee Muzee, hawakukuwa ma pusi, ilikuwa bintu beingine.

-Ma bintu ma nani walikuwa, mtoto yangu?

-Fanya uvumilia na utasikia.

Mpadri Markos, alisikia na kisha alinyamaza na alifanya paka sala na akili yake.

Siku ya tarehe 14 Yanuarie ilikuwa ya mwisho yake. Wakati alikufa nyumba yake ilijaza na arufu ya manukato nzuri sana. Alikuja na mpadri mkubwa yetu Gabrieli na alisema kwa watawa wengine juu ya ninyi waliweka ma harufu. Lakini watawa walimwambia ya kama hii harufu ilitoka toka mwili ya mpadri Markos. Ilimbaki hii harufu ya nyakati 30 dakika. Kisha walifanya wapadri wote maziko yake na walitukuza Mungu, kwa sababu hii jabo ya ajabu haikufanyikwa mara ingine ya wakati miaka makumi mbili

## 64. Kama unaomba, mpadri wangu, inakuja hapa ulimi moja ya nuru toka Mungu. . .

Toka Kitabu ya Mpadri mkubwa Yakobo, aliyeishi mu Monasteri ya Mtakatifu Daudi ya Kisanga Evia tunasoma hii jabo ya matata. Huyu mpadri mkubwa alikuwa mtu mtakatifu na alikufa mu mwaka 1992.

Kila siku alifanya Liturgia Takatifu na alikumbuka ma jina ya waminifu na wapdri wengi. Wakati siku moja asubui alifanya Ibada ya Matayarisho ya Litugia, nikusema Proskomidi mu lugha kigreki, katika zwezo yake alikumbuka na ma jina ya wale watawa waliishi zamani ndani ya Monasteri yake. Ile saa siku moja, wakati mpadri mkubwa Yakobo alikumbuka jina ya mutawa Agapios, mara moja alikuja huyu Agapios mbele yake na alimuwambia: «Mpadri wangu mimi niko ndani ya gehena, lakini, kama unaomba, inakuja hapa ulimi moja ya nuru toka Mungu na inanitulivu kidogo. . . ».

## 65. Jeshi ya wa malaika mu nyumba yake. . .

Mu muji Thesaloniki ya Grekia anaishi sasa dada moja anayeitwa Theodora. Huyu kwa ajili ya mapendo yake kwa Mungu anakataa kundowa. Anaishi pamoja na Bwana-Arusi Yesu Kristu katika uzima ya roho. Anatumika mu fasi moja kama mwandishi pamoja na watu wengine. Hawa watu wanashangaa na wanamuuliza: «Juu yaninyi, ee Theodora usipende kufanya ndoa na mwanaume moja?

Huyu anawajibu: Mimi nilifanya ndoa ya roho pamoja na Bwana wangu Yesu Kristu. Misipende kufanya ndoa na mwanaumke ya hii dunia.

Lakini hawa watu walimwambia: hatusikie, wakati unatwambia ya kama unaishi pamoja na Yesu Kristu. Namna gani ulifanya ndoa na Yesu Kristu?

Dada Theodora, kwa sababu alisikia hii maulizo mbaya kila siku waliingia ndani ya akili yake mawazo ya shaka na yeye kisha, alianza kuuliza maungo yake: «Ninaishi mimi pamoja na Yesu Kristu ao hapana? Namna gani nitajua ya kama uzima yangu inafata sheria na uzima ya Yesu Kristu?

Busiku moja alifanya sala ya usiku (Apodipnon Kidogo) na wakati alifika kwa somo ya hii sala: «Ewe Kristu Mungu unayesujudiwa na kutukuzwa wakati wowote. . . alionyesha furaha moja na ajabu moja ya ajabu kabisa wakati alifika mu somo: «utulindie kwa Malaika wako. . . ». mara moja ndani ya chumba yake, pahali ilikuwa giza, dada Theodora alisikia ya kama aliingia jeshi moja ya wa malaika wengi, wenye waliluka na walikelele na mabawa wao. Kisha hii jabo ya ajabu dada Theodora alisimama kuwaza kama iko karibu yake Yesu Kristu. Hana paka Yesu Kristu karibu yake, lakini jeshi muzima ya wa malaika yake.

## 66. Muujiza ya Mtakatifu Georgie mkubwa kwa mkubwa ya inchi ya Siria

Mu inchi Siria zamani aliishi mfalme moja aliyeitwa Umirimnis, aliyeikaa mu muji Diospoli ao mu jina ya wa muslima Ambli. Huyu mkubwa lituma mwipwa yake siku moja pamoja na wa askari wake juu ya kutengeneza mambo filani ku ile muji.

Ndani ya ilwe muji ilikuwa ya zamani kanisa mu jina ya mtakatifu Georgie mkubwa na wa muujiza. Wakati aliona hii kanisa ya mbali yule mkubwa mwipwa ya mfalme alihamuru watumwa wake kupeleka ma bintu yao ndani ya ile fasi ya kwanza ndani ya kanisa.

Basi, wakati walimaliza hii amri ya mkubwa yao watumishi wake, huyu mkubwa yao aliingia na yeye ndani ya ile fasi ya kanisa. Tena alihamuru kupeleka ndani ya kanisa na ma ngamia ma nyama yake, waliyekuwa kumi na mbili kwa kuwaangalia ya yuylu namna gani watakula.

Wapadri na watumishi ya ile kanisa walimwambia hapana kuikaa ndani ma nyama yake na kuweka ma bintu yao ndani ya kanisa, lakini huyu mutu mukafiri, aliyekuwa mugumu na mukali, hasikusikie ma sauti ya wapadri; tena aliwafokea ya kama atawalipiza, kama wataendelea kumuuzi.

Wakati watumishi walitimiza amri yake, ma nyama ma ngamia kumi na mbili, wakati waliingia ndani ya kanisa walikufa mara moja. Mukuona yule mukafiti hii tendo ya ajabu, alishangaa uwezo ya mtakatifu Georgie Mkubwa na alihamuru watumishi wake kutosha inje ya kanisa na inje ya lupago yake maiti ya ma nyama yote na kuwatupa mbali.

Wakati ilifanyikwa hii matendo yote, ilifika saa ya Matayarisho ya Liturgia Takatifu (Proskomidi). Kisha padri alikuwa tayari kutoa kwa Mungu na Bwana wetu zabihu usiyona damu. Yule mtu mukafiri aliangalia ya fasi moja yulu ya kanisa alifanya nini ndani ya kanisa na ndani ya Altari takatifu yule padri. Mungu Mwema na murahimu, alifugula ma macho ya nafsi ya yule mukafiri kwa kuona matendo ya ajabu na wa matata iliyefanyikwa pa Meza ya Matayarisho na kisha pa Meza ya Altari Takatifu.

Wakati alianza mpadri Ibada ya Matayarisho Takatifu (Proskomidi) aliona yule mukafiri kuchinja mpadri Mtoto moja aliyeikaa pa Sahani ya Meza ya Proskomidi. Aliona kweli mpadri kuchinja Huyu Mtoto na kumwanga Damu Yake ndani ya Kikombe takatifu, kukata Mwili yake kwa kipende-kipande na kuweka pa ile Sahani Takatifu.

Huyu mukafiri alisirika sana kupingana ya yule mpadri.

Wakati ilianza Ibada ya Liturgia Takatifu na ilikaribia saa juu ya kuimba waimbaji Wimbo ya Heruvikon, aliona yule mtu muslima mukafiri mkubwa ya kama mpadri alipeleka toka Mezaya Matayarisho (Proskomidi) hii Sahani Takatifu iliyejaza na vipande-vipande ya Mwili ya Huyu Mtoto na pamoja na Kikombe Takatifu, pahali ilikuwa ndani Damu ya Yule Mtoto aliipeleka pa Meza ya kati ya Altari Takatifu. Aliiweka pa Meza ya katikati na aliwafunika na kitambala moja takatifu.

Wakati ilifika wakati juu ya kupewa Waaminifu Mwili na Damu ya Kristu, aliona huyu mukafiri kubeba waminifu ya kweli kipande-kipande toka Mwili na Damu ya Huyu Mtoto yake. Mukuona hii materndo ya ajabu huyu muslima alishangaa na aliangalia na ajabu mingi.

Wakati mpadri aliisha Liturgia Takatifu, alibeba mikate ya Prosforo na aliipatia kwa mkubwa muslima. Mukuona hii mikate huyu muslima, alisema na namna ukali kwa mpadri mu lugha ya araba:

-Hii ni ninyi?

Mpadri alimujibu: Hii ni mikate mazuri na safi na toka hii mikate mimi nilibeba na nilifanya Liturgia yangu kwa Bwana wetu.

Muslima mkubwa na kisilani mingi na uchungu alimujibu: Ulibeba ya fasi wapi, ee mwenye uchafu, hii mikate na ulifanya Ibada yako? Mimi nilikuona namna gani ulichinja Mtoto moja na ulimwanga ndani ya Kikombe damu yake! Juu ya ninyi ulikata Mwili ya huyu Mtoto na uliweka vipande-vipande yake pa hii Sahani na kisha ulipatia kwa watu toka hii Mwili na Damu yake? Mimi, ee mwenye muwanji na mwenye buchafu, nilikuona kazi ninyi kibaya ulifanya.

Wakati alisikia hii ma sauti ya yule muslima mpadri alishangaa sana. Alianguka chini na mbele ya yule muslima, alikamata miguu yake na alimwambia: «Abarikiwe Mungu wetu aliyeumba mbingu na inchi yetu. Kwa sababu hii matendo uliyeona, mimi misikustahiliwa hata mara moja kuwaona. Ninasadiki kwa Mungu wangu ya kama weye uko mtu mkubwa, kwa sababu ulistahiliwa kuona hii Fumbo ya matata yetu na tena Mungu alikuandika mu kartasi ya wenye kuokolewa.

Huyu muslima alishangaa kwa hii ma sauti ya mpadri na alimujibu:

-haina vile sawa mimi niliona hii matenso yote.

Mpadri alimujibu: Ndivyo, ee bwana wangu, ni vile; Hivi ni ya kweli. Tunasadiki ya kama mukate na vinyo, ile sisi tunaitoa kwa Mungu ni ya kweli Mwili na damu ya Bwaana wetu yesu Kristu Mwana wa Mungu. Lakini hii maono uliiona, mimi misikustahiliwa kuiona hata mara moja mpaka sasa. Kristu ni mushuhuda yangu, ambaye atahukumu dunia nzima na haki Yake. Ninasadiki ya kama weye uko mtu mkubwa, kwa sababu Bwana na Mungu wetu alikustahili kuona hii ma Fumbo ya Kanisa yetu. Hii Fumbo ya ajabu waliona paka Wapadri wakubwa ya Kanisa yetu, wenye ni walimu wakubwa sawa Mt. Vasilios mkubwa, Grigorio Mutheologo na mwalimu ya dunia mzima Mt. Yoane Krisostomos, wenye walikuwa watumishi wenye stahili ya Kristu. Mimi, lakini, sawa vile nilikuwambia, kwani ni mtu mwenye zambi, misikustahiliwa kuona hii Fumdo ya ajabu. Paka kila mara ninaona mbela yangu mukate  na vinyo.

Wakati alisikia hii ma sauti ya mpadri huyu mukafiri muslima alishangaa tena, alinamisha chini kichwa yake na aliwaza ya saa mingi. Kisha, wakati alinyanyua yulu kichwa yake, alihamuru watumishi wake kuondoka. Kisha alisema kwa mpadri:

-Ninaona na ninajulisha ndani ya roho yangu ya kama imani ya wa Kristiani wa Orthodoksi ni ya kweli. Ole kwangu, kwa sababu uzima yangu yote niliipita kwa matendo ya bure, nikusema mu ndini wa uchafu ya wa muslima. lakini unibatize, kama ni mapenzi ya Mungu na mimi tangu sasa nitaabudu na namna kweli Bwana na Mungu wetu na mioyo yangu safi.

Ile saa mpadri alimujibu: Misiweze kufanya hii kazi, ee bwana wangu, kwa sababu weye uko mtu mukubwa sana na muyomba yako ni mfalme ya inchi ya Siria. Kama nitakubatiza, ninaogopa ya kama muyomba yako atabomoa ma kanisa yetu yote. lakini, kama unataka na moyo yako yote kubatizwa, utaondoka ya siri toka watu na watumishi wako na uende kwa patriarhi ya muji Yerusalema. Huyu atakubatiza.

Wakati alisema hii ma sauti mpadri, huyu muslima mkubwa alimusalimia na aliondoka. Alivaa nguo moja ya bure sana. Alilamuka usiku, aliondoka ya siri toka watu wake na alienda mu fasi ya Palestina, pahali ilikuwa ma fasi takatifu ya Bwana wetu Yesu Kristu. Aliingia mu nyumba ya Patriarhie, alipika magoti mbele ya mkubwa patriarhi na alimusema: «Ee padri mkubwa wangu na neema ya Mungu ninafata imani ya Kristu. Sasa ninapashwa kufanya ninyi juu ya kusaidia wokovu ya nafsi yangu?

Patriarhi mkubwa ya wa Kristiasni wa Orthodokse alimubatiza kwa Jina ya Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, kisha ma siku mnane na alimwambia: « Kama unataka kufanyika mukamilifu na kuokolewa, uende mu Monasteri ya Kilima Sinaya. Kule wanaishi watawa watakatifu. Pamoja na hawa utaikaa, utabeba alama ya Musalaba (Shima Ukubwa)ya Watawa na pamona nawao utastahiliwa uzima ya milele».

Wakati alisikia hii ma sauti ya Patriarhi huyu mtu, alikwenda mu Kilima Sinaya na furaha na utawa mingi. Alikwenda kwa Monasteri na alifanyika mutawa. Aliikaa kukle miaka tatu na alifunda ma zaburi ya Nabii Daudi. Wakati ilitimizwa miaka wa tatu, aliomba baraka ya mpadri mkubwa ya Monasteri juu ya kumwacha kutembea kwa yule mpadri aliyekuwa mu kanisa ya Mtakatifu Georgie ya muji Diospolis. Na kweli mpadri mkubwa alimwacha.

Wakati alikuja mu kanisa ya Mt. Georgie Mushahindi Mkubwa huyu mwaminidu, alianguka mbele ya miguu ya yule mpadri ya kanisa na alimwambia:

-Ee Mpadri mweshimiwa, unanifamia nani niko mimi?

-Mungu anakujua, mtoto wangu, ambaye anajua na anaangalia ma roho ya watu wote.

-Mimi niko mwipwa ya mfalme ya inchi Siria, ambaye nilikuwa mu fasi ya kwanza ya kansia yako hapa na niliona hii maono ya matata zaidi. Tazama sasa na neema ya Kristu na kwa maombi nguvu yako nilifanyika mukristu na mutawa. Lakini nikona na matakio ingine na kwa hivi nilikuja kwako. Kwa jina ya Kristu, usizaifu kunitimiza hii matakio yangu.

Mpadri, wakati alisikia hii ma sauti yake, alitukuza Mungu na alistaajabu, kwani aliona huyuy mtu aliyekuwa zamani kama imbwa ya pori sasa ni kondoo mupole ya Mungu.

Yule mutawa alimuwmbia: Ninatakia sana kuona Bwana wetu Yesu Kristu.

Mpadri alimujibu: Kama unatakia kuona Bwana wetu yesu Kristu, uende kwa muyomba yako mfalme ya Siria na kikiri mbele ya waale wa muslima wote ya kama Bwana wetu yesu Kristu ni Rabi na Muumba ya dunia nzima. Tena ya kama Yesu Kristu mbele ya miaka mengi anatawala pamoja na baba wake na ya kama alikuja kwa sisi na mwili katika Mama wake Bikira maria, alitenda miujiza ya ajabu, ya kama alisulubiwa kwa ajili yetu, alimazikwa na alifufuka kisha ma siku tatu na kisha ma siku makumi ine alipanda mbinguni na utukufu mingi na mara ingine atakuja kuhukumu watu wote wenye mzima na wenye kufa.

Alibeba ma sauti ya mpadri huyu mutawa kama silaha na alikwenda kwa muyomba yake. Wakati katikati ya usiku moja alifika mu nyumba ya mfalme a,iita na watu wa inchi Siria kuja kwake. Vile aliwaita: «Ee watu wote ya hii inchi, kujeni hapa kwani nikona kusema sauti moja ya ajabu».

Kwani ilikuwa usiku sauti yake ilikwenda ma fasi ya mbali mbali. Walilamuka watu wa muslima yote na walianza kuja na ma mishumaa ya kuwakisha kwa ile fasi juu ya kuona tendomoja ya ajabu. Wakati waliingia ndani ya ile nyumba na walimuona huyu mutawa,walimuulizakusikia ya mambo gani aliwaita. Huyu mutawa aliwaambia:

Kama mutanilaka ya kama mutanipatia makuta, nitamionyesha eko wapi mwipwa ya mfalme wenu, ambaye alitoka na eko mupotevu mpaka sasa.

Hawa walisema kwa mutawa: Kama utatuonyesha huyu eko wapi tutakupatia zahabu mingi.

-Mutawa aliwaambia: Twende pamoja kwa mfalme na mimi nitamiambia eko wapi mwipwa yake.

Wakati hawa wa muslima walisikia kusema hivi yule mutawa, walimubeba na walimupeleka kwa mfalme Umirimni na furaha mingi walimwambia ya kama huyu mutawa anajua eko wapi mwipwa yako.

Mfalme Umirimni aliuliza na lugha yake: Mwipwa yangu eko wapi?

-Mutawa alimujibu: Mimi niko mwipwa yako. Nilifanyika mukristu, ninasadiki kwa Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, Mungu mumoja. Tena ninasadiki kwa Bwana wetu Yesu Kristu, aliyekuja duniani na mwili toka Bikira Maria Mama wake. Huyu alifanya miujiza ya ajabu duniani hapa. Kisha alisulubiwa, alimazikwa, alifufuka na alipanda mbinguni na atakuja mara ingine kuhukumu watu wote ya dunia.

Wakati alisikia hii ma sauti huyu mfalme alimbakia na ajabu mingi na alisema kwa

mwipwa yake: mambo gani inafanyikwa kwa weye, ee mumbafu? Juu ya ninyi uliacha ndini yetu, ili tukonayo ya zamani na iliyetupatia utukufu na mali mingina sasa weye ulivaa hii manguo ya haya na uchafu na unatembea hapa? Kuja mara ingine kwa sisi, ukikiri Nabii wetu Mohameti, aliyetupatia mu kizazi yetu ma bintu mingi.

-Mutawa alimujibu: Ninyi bintu wote nilikuwa wakati nilikuwa muslima, walikuwa uriti na bintu ya shetani, lakini hii yote na mavazi ninavaa sasa ni utukufu na usharifu na kitumaini ya uzima wa milele. Ninahukumu na ninafiga ndini ya wa muslima na nabii yake ya uwongo ninamukana na ninamuhukumu, aliyeharabisha akili na imani yenu.

Wakati alisikia hii masauti ya mwipwa yake mfalme alionyesha mapendo kidogo kwa mwipwa yake na alimwambia: Simama, fuga kinywa yako na usichabula ndini yetu. Kisha alisema kwa watumishi wake: Mumukamate na mumutosheni huyu inje ya makutano yetu. Wakubwa wengine walisema kwa mfalme: Unauhuru huyu anayefiga na anahukumu ndini yetu na nabii mkubwa yetu? Huyu ni mustahili ya mateso mengi sana. Na sisi, basi, tutafanyika wa Kristiani na tutakataa imani ya wa babu wetu.

Wakati aliona hii fujo na mapinduzi yao mfalme alihamuru kumubamba na kufanya kila tendo wanataka. Ile saa walilamuka wakubwa wengine wote toka ma kiti yao, walipiga meno yao kupingana yake, walimubamba na walimukokota inje ya muji na walianza kumupika na maimbwe.

Huyu aliyekuwa zamani muslima na sasa mutawa mukristu na mushahindi aliita saidio kwa jina ya Bwana Yesu Kristu. Vile aliisha ukikiri yake na alikwenda kwa Kristu mupendwa wake.

Mwili takatifu yake ilimbakia chini ya maimbwe ma siku madogo. Yulu ya mwili yake ilikuja na ilimbakia yulu nyota moja mupaka asubui. Wa muslima, wenye waliona hii alama ya nyota walishangaa.

Kisha mfalme alihamuru wa Kristiani wadogo kwa kutosha na kupeleka mwili ya mtakatifu mutawa mu fasi ingine juu ya kumazika. Wakati wa Kristiani walimaliza amri ya mfalme, waliona ya kama mwili yake ilikuwa muzima na ilitosha harufu nzuri ya manukato. Walimumazika na sifa mingi na wimbo na wa padri wao na hivi alitukuzwa Bwana Yesu Kristu Mungu wetu.

## 67. Muujiza moja ya Mtakatifu Nikolaos

Ku muji kuibishevi ya Rusia aliishi jamaa moja: Mama na binti yake aliyeitwa Zoi (Uzima). Usiku ya tarehe 31 ya mwezi ya Desamba ya mwaka 1956 huyu binti Uzima aliita na marafiki wengine saba na wanaume wengine saba juu ya kucheza na kufurahi ile usiku. Ilikuwa wakati ya kwarezima kwa sababu Kanisa ya Rusia inafata Kalendari ya zamani na mama ya binti Zoi alimwambia hapana kutengeneza kazi ya chakula, kwani wejkona kwarezima, lakini binti yake hasikumutii. Ile usiku mama yake alikwenda mu Misa kuomba kwa Mungu.

Walikuja wale waliitwa kwa hii furaha, lakini bado kukuja muchumba mwanaume ya binti Zoi. Jina yake ilikuwa Nikolaos. Kila binti alikuwa na murafiki mwanaume yake, lakini binti zoi alimbakia bila murafiki muchumba yake. Mara moja, bila kuwaza mingi, alishuka Ikona ya Mtakatifu Nikolaos toka kibabashi ya nyumba yake na alisema mbele ya warafiki wake: Mimi sasa nitacheza pamoja na huyu Nikolaos, kwa sababu asikukuje muchumba yangu Nikolaos. Warafiki waake wengine walimushauria haipaswe kufanya hii kibego, lakini huyu aliwajibu: «Kama eko Mungu anaweza kunilipiza».

Alianza kucheza. Walianza kucheza na wa kijana wengine, lakini kisha maviringo yao mbili-tatu ilisikiwa bikelele nguvu ndani ya ile nyumba na mara moja mwangaza ilionekana kama umeme ndani ya ile usiku.

Furaha yao iligeuzwa kwa tetemeko. Walikimbia wote na tetemeko mingi. Paka binti Zoi alisimama bila kutenga na kukamata Ikona ya Mt. Nikolaos kwa mikono yake, iliyekuwa kulamata kwa kilari yake. Tena na huyu binti alisimama kama sanamu, kama marmbre. Waganga walikuja mara moja na hawakuweze kumusaidia juu ya kutenga toka fasi yake. Walimuweka sindano na dawa lakini hakuna kintu, kwa sababu ma sindano hakuna namna kuingia kwa meili yake, iliyekuwa kama mwamba. Walitaka kumupeleka mu obitalo, lakini hawakuweze kumupeleka toka fasi yake. Miguu yake walikuwa sawa kupingiliwa na misumari mu fasi yake ndani ya ile chumba. Lakini roha yake ilitumika! Binti Zoi alikuwa muzima. lakini hasikuweze wala kula wala kunywa kinywanji moja...

Wakati mama yake alirudi toka kanisa na aliona alifanyikwa mambo gani, alianguka chini na walimupeleka mu obitalo. Kisha ma siku kidogo walimutosha. Imani yake kwa wema ya Mungu, maombi yake ya nguvu juu ya kusamehe Mungu mtoto yake walileta uzima mara ingiune kwa mtoto yake.

Binti Zoi alisikia mara ingine na aliomba na machozi usamehe na saidio toka Mungu.

Ma siku ya kwanza ndani ya pempeni nyumba ya binti Zoi walikuja watu mengi, waliyekuja ya mbali kuangalia hii mambo ya ajabu ao waganga ao na watu ya roho. Lakini mbio-mbio nyumba walifungwa wakubwa ya inchi. Watu ya police walichunga inje kila ma saa mnane. Wa zamu wengine walishangaa, wakati walisikia ya ndani sauti ya zoi kupaza sauti. Tena karibu ya binti Zoi alisimama na mama yake, aliyefanya sala.

-Ee mama wangu, omba kwa Mungu! Omba, kwa sababu ninapotea kwa ajili ya ma zambi yangu! Omba kwa Mungu! Alimuwambia mtoto yake.

Hii mambo ya ajabu yote alisikia na patriarhi na walimuwambia kuomnba kwa afya ya binti Zoi. Patriarhi alijibu:

-Yule aliyemulipiza, huyu atamupona mara ingine.!

Ma siku madogo, mbele ya Siku Kuu ya Habari Njema ya Mzazi-Mungu alikaribia wazamu ya hii nyumba mpadri moja muzee mupole na mwema, ambaye aliwaambia kuwa wa zamu kumwacha kuingia ndani ya kuona binti Zoi. Wa zamu walikataa kumwacha ya kuingia. Huyu muzee alikuja na siku ingine asubui, lakini na wa zamu wengine hawakumuache. Siku ya tatu, pahali ilikuwa Siku Kuu ya habari Njema ya Mzazi-Mungu walimwacha. Hawa wa zamu walimusikia na mapendo ngapi aliuliza mtoto Zoi: « Basi, ulichoka kwa ajili ya hii usimamisho?».

Ilipita saa kidogo na, wakati wa zamu walitaka kumutosha huyu muzee inje, huyu hasikukuwe ndani ya hii nyumba...

Watu wote waliisha kusikia ya kama huyu muzee hasikukuwe mtu moja ya bure, lakini alikuwa Mtakatifu Nikolaos. Vile mtotoZoi alimbakia ya kusimama ma mwezi ine (128 ma siku), mupaka Siku Kuu ya Ufufuo ya Kristu, pahali ile mwaka ilikuwa mu tarehe 23 mwezi ya Ine (Aprilie) (Ku Kalendari upya ilikuwa mu tarehe 6 mwezi ya tano (Mai).

Ile usiku ya Ufufuo ya Bwana Yesu Kristu mtoto Zoi alianza kupaza sauti na kusema:

-Muombeni!

Wale wa zamu ya usiku waliogopa sana na walianza kumuuliza:

-Juu ya ninyti unapaza sauti nguvu?

-Mtoto Zoi aliwajibu: Ni mambo ya matata sana! Inchi yetu inajichoma! Mwombeni! Dunia mzima anapotea kwa ajili ya zambi yake!, mwombeni!

Tangu ile saa binti Zoi alirudia kwa nguvu ya mwili yake. Ku mwisho walimuweka pa kitanda, lakini huyu aliendelea kupaza sauti na kuita watu wote kwa sala mbele ya Mungu juu ya kuokolewa dunia kwa ajili ya zambi yake.

-Namna gani ulimbaki muzima mupaka sasa? Nani alikupatia chakula? Walimuuliza.

-Ma ndege kama hua walikuja na walinipatia nguvu, ilikuwa jibu yake. Toka hii jibu yake walisikia yote ya kama Mungu alimusamehe katika ufikisho ya Mtakatifu Nikolaos wa miujiza.

Hii matendo yote ya ajabu walifanya ajabu mingi kwa wale watu waliikaa ku muji Kuibishevina ma mugini ya pempeni. Watu wengi, kwa sababu walisikia ma sauti nguvu ya huyu mtoto Zoi juu ya kufanya maombi, walirudi kwa Mungu na walipata imani yao. *(Inapaswa kusema ya kama ile mwaka ilifanyikwa hii jabo mu Rusia ilikuwa parte ya Komuniste na ilikatazwa watu kuamini kwa Mungu).*

Watu walirudi mu Kanisa na kitubio ya kweli. Ninyi wote bado kuvaa musalaba, walianza kuvaa, lakini walijua ya kama ilikuwa boka kuwabamba na kuwapeleka mu buloko kwa ajili ya mavazi musalaba pa sigo yao.

Taifa muzima katika imani, boka na machozi aliomba usamehe ya zambi yake na alisema hii ma sauti ya motot Zoi: «Inchi yetu inajilugua; tunapotea kwa ajili ya zambi yetu~ Muombeni! Watu wanapotea kwa ajili ya mazulumu yao!

Siku ya tatu, kisha ufufuo ya Bwana Yesu, binti Zoi alitoka kwa Bwana Yesu, kisha usimamisho yake ya wakati ma siku 128 juu ya usamehe ya zambi yake yote. Roho Mtakatifu alimupatia nzuvu ile wakati ya mwezi ine juu ya kufufua na nafsi yake toka lufu ya zambi yake.

**MONASTERI YA MUTAKATIFU GRIGORIOS**
**KILIMA TAKATIFU**
**GREKIA**
**1998**